Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Tatu - Tarehe 16 Juni, 2014

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Bajeti Juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 Pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) Juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. CHRISTINA LISSU MUGHWAI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Na. 240

Ukosefu wa Hati Miliki

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Ukosefu wa Hatimiliki za Kimila Vijijini unasababisha migogoro mingi ya ardhi baina ya Kaya, Kijiji na Koo na kupelekea kutoweka kwa amani kwa wananchi kama inavyotokea huko Tarime.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haitoi Hati Miliki za Kimila kwa Wanavijiji wa Tarime?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupima Miji midogo ya Nyamongo, Sirari, Nyamwaga na Komaswa ili ijengwe kwa mpangilio mzuri?

(c) Je, kwa nini Serikali haiushirikishi Mgodi wa *North Mara* kupima Miji ya Nyamongo na Nyamwaga ambayo huhudumiwa na Mgodi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza, ni kweli kwamba mpaka sasa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime haijatoa Hatimiliki za Kimila kwa Wanavijiji. Hii ni kutokana na Halmashauri hiyo kutotimiza matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999 kuhusu uandaaji wa Hatimiliki za Kimila ambapo pamoja na masharti mengine, sharti mojawapo ni Kijiji kiwe kimepimwa na kupewa Hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ambayo ina jumla ya Vijiji 82 imeshaanza mchakato wa kukamilisha matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999, ambapo hadi sasa Vijiji 43 vimeshapatiwa vyeti vya ardhi na kati ya Vijiji hivyo, Vijiji 14 tayari vimeshaandaliwa hati zake. Taratibu zote zikishakamilika Halmashauri itaanza kutoa Hatimiliki za Kimila kwa Wanavijiji.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Halmashauri imetenga shilingi 3,656,050 kwa ajili ya kuandaa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu Miji ya Komaswa na Sirari, jumla ya Michoro 8 ya Mipango Miji yenye idadi ya viwanja 982 imeandaliwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji. Aidha, jumla ya Ramani za Upimaji 3 zenye jumla ya viwanja 158 vimeandaliwa na kuidhinishwa katika Mji wa Sirari.

Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi 121,017,530 kwa ajili ya upangaji na upimaji wa Miji midogo ya Sirari, Nyamongo, Nyamwaga na Komaswa.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, Serikali imekuwa ikishirikiana na mgodi wa *North Mara* toka mwaka 2006 ambapo Mgodi wa *North Mara* uligharamia *USD 59,943* kwa ajili ya uandaaji wa Mpango kabambe wa Mji wa Nyamongo *(Nyamongo Township Master Plan 2006 - 2026)*.

Aidha, kupitia Mfuko wa Dhamana wa Jamii ya *North Mara (North Mara Community Trust Fund)* mgodi wa *North Mara* umeonyesha nia ya kugharamia upimaji na utoaji wa hati katika Miji ya Nyamwaga, Nyangoto, na Kewanja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine!

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze Waziri kwa majibu aliyoyatoa lakini, Swali la kwanza anijibu utekelezaji wake utaanza lini?

Swali la pili, Waziri Mkuu alipotembelea Mji wa Sirari alitoa ahadi ya kuufanya Mji wa Sirari kuwa Mamlaka ya Mji mdogo. Yapata miaka mitatu imepita tangu mwaka 2011 mpaka sasa.

Ni lini Serikali, itatekeleza ahadi ya Waziri Mkuu ya kuufanya Mji wa Sirari kuwa Mamlaka ya Mji mdogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa. Mheshimiwa Mwanri, tafadhali!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuja hapa na faili lote la Wilaya nzima ile ya Tarime ya huku kwenye Mji na ile ya *District Council.* Ninayo *document* hapa inatoka *North Mara* rafiki yangu Nyangwine asiwe na wasiwasi na sisi kuhusu majibu tunayotoa hapa. Hapa wala asipite hivi akapita hivi na nini na kama kuna mtu mwingine anataka kuleta *information* yote ipo hapa.

Hizo dola 59,000 zililipwa kwa *UCLAS* kile Chuo cha Ardhi na anafahamu. Kazi hii imefanyika, michoro na kila kitu ninacho hapa kama hana tutakuja kupeana ili aweze kuona, kwa sababu hii ni *public information* na wala sio kitu cha kuficha ficha.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekwenda pale Sirari na mimi mwenyewe nimeenda kufuatilia hiki ambacho Waziri Mkuu alisema pale. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Sirari ukiacha inakwenda hivyo hivyo kesho ni ma-*squatter* pale. *He has a point*. Sisi tunajaribu kufuatilia jambo hili, ili kuhakikisha Miji hii inayosema yote hii inakuwa mamlaka ya Miji midogo kwa sababu ni maeneo ambayo yanakuwa haraka sana.

Kule kuna madini, kwa hiyo, wanakuwa kwa haraka sana. Mimi ninapenda kumpongeza Mbunge kwamba hili jambo ameliona na hili ndilo jambo ambalo Waziri Mkuu analisema, ndicho anachotaka kufanya pale. *(Makofi)*

Mji wa Sarai hatuwezi kuuacha hivyo unazagaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza hivyo na Ofisi yetu inaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu jambo hili.

Mwisho anasema ni lini sasa jambo hili litafanyika. Nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji na nimemwagiza mambo yafuatayo:

Akamilishe vitu vyote hivi anavyosema hapa. Hivi Vijiji anavyovisema hapa na maeneo haya anayoyasema hapa nataka nikwambie kilichotokea pale ni kwamba vile Vijiji ili vitoe Hati ya Kimila lazima vyenyewe viwe na Hati ya Kumiliki Ardhi. Vinginevyo, yeye ana *registration* wapo *registered* basi. Sasa hapa siwezi kuruhusu na wala sitaruhusu.

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tunaandikisha Kijiji kwa Hati za Kimila ndizo hizo zinakwenda Mahakamani unaskia zimekataliwa!

Lakini nataka nimthibitishie Mheshimiwa Chacha kwamba tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba Vijiji vyote alivyovitaja hapa, vyote vinapatiwa Hati zake kama zilivyoelekezwa.

NAIBU SPIKA: Tulibakize Swali hilo huko huko Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Leticia Nyerere, nilikuona!

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niulize Swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya Tarime ni sawa kabisa na migogoro inayoendelea Kwimba na hata Mwanza kwa ujumla. Migogoro ya Ardhi hii, kwa asilimia kubwa imesababishwa na wananchi kutokuielewa Sheria ya Ardhi na tumepoteza watu wengi Mkoani Mwanza kwa sababu watu wanachukua Sheria mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali sasa ipo tayari kutamka leo kwamba wataanza kuwaelimisha wananchi wote kuhusu Sheria ya Ardhi, ili tuweze kunusuru maisha ya wananchi wetu?

NAIBU SPIKA: Majibu ya Swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili la elimu, elimu ni afya. Watu wakipata elimu na kuelimishwa wanakuwa na afya ya ubongo. Hutapata matatizo, watu walielimika ama *Society* iliyoelimishwa haina matatizo, kwa sababu wanaelewa.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba kuna haja ya kutoa elimu. Lakini ipo haja pia, haya maeneo yanayozungumzwa hapa ni maeneo ambayo kidogo tunapotaka kuleta masuluhisho na Mheshimiwa Chacha Nyangwine anafahamu habari hii, tafrani inatokea tokea hivi. Kwa hiyo, hata kutoa elimu pale inakuwa ngumu.

Mimi nawaomba sana tutumia vyombo vipi, Serikali zetu za Vijiji, Mabaraza ya Madiwani, *Ward Development Committes* na hata Mashirika ya Dini yatumike hapa kuita amani, utulivu katika mambo yetu. Tunapozungumza jambo lolote, tuzungumze kwa kuelewana na kwa amani.

Badala ya kwamba kila wakati kila mtu yupo juu, *high high!* Matokeo yake unakuta hamwelewani na migogoro hii inaikuta iko mingi sana katika maeneo haya tunayozungumza.

Nakubaliana na mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja yakutoa elimu kwa ajili ya watu wote, ili waweze kuzijua hizi Sheria na taratibu za umilikaji wa ardhi.

NAIBU SPIKA: Tuendelea na suala linalifuata la Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa niaba yake Mheshimiwa endelea!

Na. 241

Maboresho Katika Hospitali ya Manyamanyama

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED (K.n.y. ESTER AMOS BULAYA aliuliza:-

Hospitali ya Manyamanyama imepewa hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya lakini hakuna vifaa muhimu kama Jenereta kwa ajili ya dharura na mashuka pia hayatoshelezi.

Je, ni lini sasa Serikali itafanya maboresho ya kuongeza vitu muhimu katika Hospitali ya Wilaya ya Bunda?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iliamua kupanua Kituo cha Afya cha Manyamanyama kuwa Hospitali ya Wilaya, ikiwa ni juhudi za makusudi za kuboresha huduma za afya Wilayani. Toka wakati huo Halmashauri imeendelea kutenga fedha kupitia vyanzo mbalimbali ili kuongeza majengo, maji, umeme na kuandaa watumishi wa afya wenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Manyamanyama kina jumla ya vitanda 110 ambapo kitanda kimoja kinatakiwa kuwa na mashuka 8 hivyo kufanya mashuka yanayohitajika kuwa 880, mashuka yaliyopo ni 279 hivyo kuna upungufu wa mashuka 601. Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 imetenga jumla ya sh.1,110,000/= kwa ajili ya ununuzi wa mashuka 74.

Kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi 6,600,000/= kwa ajili ya ununuzi wa mashuka 440.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Manyamanyama kinapata umeme kutoka kwenye gridi ya Taifa. Kwa sasa Kituo hiki hakina umeme wa dharura *(standby generator)*. Mwaka wa Fedha 2012/2013 Halmashauri ilitenga shilingi 10,000,000/= na mwaka 2013/2014 imetenga shilingi 20,000,000/= kwa ajili ya kujenga kibanda, kununua jenereta na kufunga. Kazi hizi zitagharimu shilingi milioni 30,000,000/=. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed Swali la nyongeza.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naibu Waziri haoni kama kuna tatizo kubwa la uchafu katika hiyo Hospitali ambayo imechaguliwa itakuwa Hospitali ya Wilaya, kuifanya ina hadhi ya kukosa mashuka na kusababisha chawa na kunguni kutokana na udhaifu wa mashuka kufuliwa kila mara?

Kwa hiyo, anasemaji kuhusu hiyo Hospitali kukimbiwa na wagonjwa, kuepuka magonjwa ya ngozi?

Swali la pili, Hospitali ya Kituo cha Afya ya Kirando inafanana sana na matatizo ya Kituo cha Afya cha huko Bunda na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kimezidiwa na wagonjwa na kina upungufu wa dawa. Tuliomba Serikali muda mrefu kupandisha hadhi iwe Hospitali kamili, lini Serikali sasa itaona kile Kituo kwa kuzidiwa wagonjwa iwe Hospitali kamili kutoa matatizo ya wagonjwa wote wanaokaa Kando Kando ya Ziwa Tanganyika?

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo kutoka Bunda hadi Kirando? Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa, Mheshimiwa Mwanri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili la Hospitali ya Manyamanyama, chawa, kunguni si kweli! Kwa maana hata Mbunge wake ambaye ni Steven Wassira yupo hapa na anasikia maneno haya. Kwa hiyo, sasa mimi nikikiri hapa kwamba ni kweli anachosema Mheshimiwa Keissy, mimi nadhani tu labda tutakwenda tutam-*expose* vizuri, Mheshimiwa!

Mimi ninayo barua hapa majibu haya yaliyotolewa hapa Mheshimiwa, yametolewa kwa misingi kwamba bado hiki ni Kituo cha Afya. Hizi takwimu ninazozitoa hapa zinakwenda kwa msingi wa Kituo cha Afya na hizi jitahada zinazofanyika hapa za mashuka na kila kitu nilichoeleza hapa, ukienda hizi hela zote zilizopangwa, kama ni kuwa na upungufu watakuwa na upungufu wa shuka 161 tu. Kwa sababu *requirement* yao ni mashuka 880. Kwa hiyo, hizi ndiyo *requirements* ya mashuka iliyopo pale na tume-*survey* hii tumekwenda kuiangalia.

Ninayo barua hapa na nitamwonyesha Mheshimiwa Keissy. Barua hii inatoka kwa *DMO* anamwandikia Waziri wa Afya akiomba sasa tupate kauli kamili ya kuifanya Hospitali hii iwe Hospitali kamili. Kwa taarifa tu, hawa wenzetu hapa wanatumia *Designated District Hospital (DDHO)* ambayo inaendeshwa na kanisa la K.K.K.T ndiyo wanayoitumia pale. Kwa hiyo, hicho anachokiona Mheshimiwa Keissy pale, hakiko hivyo kama anavyosema lakini nitam-*expose* nitakapotoka hapa.

Kwenye Hospitali hii ya Kirando, nimekwenda na mke wangu kuitembelea nikamwambia zungumza na kina mama wenzako kwa sababu kuna vitu vingine wakina mama huwezi sikiliza, nikamwambia asikilize halafu aniambie.

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed anafahamu kuna matatizo pale. Nikamwita Mganga Mkuu nikamwambia *arrest* hiyo *situation*, wale wanasaidiwa, wanasaidia na wenzetu wengine wanatoka majirani kutoka Congo, wanakwenda katika lile eneo. Tukamwita tuka-*arrest* hiyo *situation. (Makofi)*

Wale wanasaidiwa na kusaidia kuna wenzetu wanatoka majirani kutoka Congo na kwenda katika lile eneo. Tukamwita tuka-*arrest* hiyo *situation* lakini bado kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kuna tatizo pale na tumetoa maelekezo. Sasa mimi nitakaa na Mheshimiwa Keissy, niweze kujua kwamba tulipiga hatua gani. Pale mwanzo ilikwenda kama zimamoto hivi kwa kufanyika mambo makubwa.

Nataka nikuthibitishie kwamba hili eneo ni eneo ambalo tunalifahamu sisi kama TAMISEMI tutashughulikia ili tufanye kama Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed anavyotoka lifanyike.

NAIBU SPIKA: Tuendelea na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Mazingira, Swali linaulizwa na Mheshimiwa Rajabu Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole.

Na. 242

Juhudi za Kunusuru Mlima Kilimanjaro

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED aliuliza:-

Mlima Kilimanjaro ni kati ya maajabu makubwa duniani na moja kati ya alama kubwa tatu zitokazo na athari ya mabadiliko ya tabianchi.

(a) Je, Serikali ya Tanzania na Jumuiya za Kimataifa zimechukua hatua gani za kimkakati kunusuru mlima huo na maeneo ya vijiji jirani?

(b) Je tathmini inaonyesha ni kiasi gani cha theluji kilichiopungua kutokana na athari ya mabadiliko ya tabianchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole kuwa Mlima Kilimanjaro ni miongoni mwa maajabu ya dunia nani moja ya alama kubwa zinazoonyesha athari za mabadiliko ya tabianchi duniani.

Serikali na Jumuia za Kimataifa zimechukua hatua mbalimbali za kukabiliana Na uharibifu wa mazingira unaotiokana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kusaini/kuridhia mkataba wa mabadiliko wa tabianchi wa mwaka 1992 na Itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997 chini ya mkataba huu, kuandaa Sera, Sheria na mikakati mbalimbali. Hatua mahususi zilizochukuliwa ili kunusuru Mlima Kilimanjaro ni pamoja na:-

Kuendelea kuzibana nchi zinazoendelea kupunguza uzalishaji wa gesi joto duniani kwa asilimia 5.2 Mheshimiwa Naibu Spika naomba isomeke asilimia 5.2 badala 5.8 kupitia utekelezaji wa mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi na itifaki ya Kyoto.

Kutekelezwa kwa mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhi Mkoani Kilimanjaro chini ya Mpango Maalum wa Afrika kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Mradi huu unafadhiliwa na *UNDP* na ni wa kipindi cha miaka minne kuanzia 2011 – 2015 na una thamani ya dola za Kimerekani milioni tatu. Ofisi za mradi zipo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *KINAPA,* juhudi mbalimbali zinaendelea kufanywa za kupanda miti na kudhibiti uchomaji moto. Vile vile Uongozi wa Mkoa umezuia kabisa uvunaji wa miti ya mbao na kuni kutoka maeneo ya mlima isipokuwa kwa kibali maalum.

Pia kutoa elimu ya uhifadhi na utunzaji kwa wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro kwa kupitia Mpango wa Kupunguza uzalishaji wa Hewa Ukaa, *program* hii ilianza mwaka 2010.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na taarifa za Jopo la Wanasayansi wa mabadiliko ya tabinchi yaani *Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)* Mlima Kilimanjaro umepoteza takribani asilimia 80 ya theluji yake kuanzia mwaka 1912 kutokana na mabadiliko ya tabiachi. *(Makofi)*

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, na nmpongeze dada yangu kwa majibu yake mazuri ambayo kwa kweli ametueleza. Ila nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa sababu mradi huu wa maendeleo endelevu ya ardhi Mkoani Kilimanjaro unaishia mwaka 2015. Sasa nataka kujua baada ya ufadhili huu wa *UNDP* kumalizika mwakani.

Je, Serikali imejipangaje sasa ili kuweza kuendeleza maeneo hayo?

Lakini la pili ni kwamba Ofisi ya Mkoa wa Kilimanjaro au Mkoa umepiga marufuku kabisa ukataji pamoja na uchomaji moto wa miti katika Mlima ule, isipokuwa kwa kibali maalum.

Tunajua kwamba moja ya tatizo na udhaifu mkubwa tulio nao ni usimamizi katika uvunaji wa miti ndani ya nchi yetu.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba unapotoa mwanya wa baadhi ya watu kutoa vibali kwa ajili ya ukataji wa hii miti, hii asilimia ishirini *(20 per cent)* ambayo imebaki itaweza kuishia tu ndani ya miaka miwili au mitatu? Naomba majibu ya Serikali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Rajab kwa kuibua masuala haya ya mabadiliko ya tabianchi kama tunavyofahamu sasa hivi ndiyo tishio kubwa duniani linalokabili ustawi wa binadamu na maendeleo endelevu. Kwa hiyo, kadri tunavyoongea katika Bunge ndivyo tunavyoweza kujenga uelewa wa Watanzania na jamii juu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Sasa nikijibu maswali yake mawili kuwa mradi huu unaisha mwaka 2015 tumejipangaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimthibitie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunayo tayari *program* tumeandaa *concept paper* kwa ajili ya kuendeleza *phase two* ya mradi huu na wenzetu wa *UNDP* na *Global Environmental Facility* wako tayari kutusaidia.

Lakini pia ukisoma Bajeti yetu ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Mahenge, tayari pia zipo fedha za ndani kwa ajili ya kuhakikisha tunatunza na kulinda hifadhi ya mazingira hasa misitu katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Naipongeza sana Ofisi ya Mkoa wa Kilimanjaro, wao wenyewe katika Bajeti yao wameweka fungu kwa ajili ya kulinda hifadhi ya mazingira ya Mlima Kilimanjaro na Mikoa mingine kwa kweli waige. *(Makofi)*

Swali la pili, amesema kwa nini Ofisi ya Mkoa wa Kilimanjaro inaruhusu bado ukataji miti. Mheshimiwa Rajab katika Mikoa yote Mkoa ambao unetekeleza kwa dhati kulinda misitu na miti ni MKoa wa Kilimanjaro na wamefikia mpaka *stage* Kanisa la KKKT Kilimanjaro hawaruhusu mtoto apate ubarikio au kipaimarabila mzazi kuonyesha cheti kwamba amepanda miti 10. Kwa hiyo kwa kweli niwasifu sana. Miti kukatwa haikatazwi, lakini tunasema ukataji endelevu wa misitu na miti.

Lakini suala ulilouliza tunalifanyia kazi, kama unavyosema tunajenga *transparency* na *capacity* katika masuala ya uvunaji wa miti na misitu. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selasini najua nisipokupa nafasi kwa swali hili. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa sababu Mlima Kilimanjaro uko katika Jimbo langu. Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Mimi nina swali dogo tu ambalo linahusiana na ukataji na upandaji wa miti, pamoja na marufuku ambayo tumepigas kule Kilimanjaro ya kutaka miti ovyo, hususan iliyo katika Mlima Kilimanjaro. Hivi sasa Wazee ambao wamepanda miti yao miaka 20, 30 iliyopita na imeshakomaa nao wanakatwa kuvuna hiyo miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama za ujenzi na za kusomesha watoto wao. Serikali sijui mnasemaje kuhusu jambo hili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na hiyo changamoto imekuwa ikijitokeza katika maeneo mbalimbali na lengo letu ni kuhakikisha kwamba hatukati miti na misitu ovyo.

Ni kweli kuna wazee ambao wamepanda miti yao imeshakuwa ina miaka 20 wanakosa kibali. Lakini ndiyo maana tunasema uende utumie taratibu husika. Uanzie katika ngazi yako ya Kijiji kama ni kijiji katika Mtaa.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ameweka utaratibu ambapo mtu anaweza kuruhusiwa kukata msitu au mti. Lakini tunaangalia pia athari za ukataji wa huo mti au msitu utakuwa ni nini. Tunazungumzia suala la mabadiliko ya tabianchi. Kwa nchi yetu ya Tanzania tatizo kubwa linalosababisha kuongezeka kwa hiyo hewa ukaa ni kwa sababu tunakata miti ovyo, tuchoma misitu.

Kwa hiyo, lazima Mheshimiwa Selasini kidogo tuwe *very board*, tuwe kidogo wazito haturuhusu ovyo ovyo ukataji wa miti. Lakini naomba tuwashauri hao wazee wafuate taratibu. Wawasiliane na Ofisi zao za Serikali na nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kweli yuko makini sana katika suala la kulinda na kuhifadhi misitu. Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante nakushukuru sana na kwa kweli kila atakayepata kibali hicho basi aonyeshe amepanda miti 10 mipya. Wizara ya Ujenzi, tunaendelea swali la Engineer Athumani Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula.

Na. 243

Ujenzi wa Barabara kwa Njia ya Tozo

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA aliuliza:-

Nchi nyingi duniani zinatumia utaratibu wa ujenzi wa barabara kwa njia ya tozo (*Road Toll)* utaratibu uliopendekezwa kwa barabara ya Dar es Salaam hadi Chalinze kwa ubia na sekta binafsi (*PPP)*:-

(a) Je, Serikali imefanya uchunguzi wa kina kuona kama *PPP* inahitaji gerentii ya Serikali ili isipate hasara?

(b) Je, Serikali inafanya jitihada gani za kuanzisha Bodi mbalimbali nchini ili kutumia rasilimali mbalimbali zilizopo nchini ziweze kujenga barabara zetu badala ya kujenga kwa fedha taslimu?

(c) Je, utafiti wa kitaalam umefanywa ili kutoa ulinganifu wa namna mbalimbali za ujenzi huo, namna mbalimbali za ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kukuza uchumi wa nchi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) (b) na (c), kwa pamoja,m kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi yenye mafanikio inahitaji uthabiti a muundo wa kisheria *Legal Firm Work* Serikali ilianzisha Sera ya ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi mwaka 2009. Sheria ya ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi *PPP Act 2010* Kanuni ya ubia kati ya sekta umma na Sekta Binafsi *PPP Regulations,* mwaka *2011*na Kanuni za Manunuzi ya miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi

mwaka huo 2011 kwa kuzingatia Sheria nilizozitaja Wizara ya Ujenzi imeitangaza barabara ya Dar es Salaam-Chalinze ijengwe kwa njia ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwezo ulioko kati ya baadhi ya Taasisi za Umma na inatoa nafasi pale inapowezekana na kushirikiana na Taasii hizi katika ujenzi wa miundombinu ya umma.

Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inajenga daraja la Kigamboni kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *NSSF,* ambapo Serikali inachangia asilimia 40 na *NSSF* inachangia asilimia 60 ya gharama ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa moja kubwa ya utaratibu waSerikali na Sekta Binafsi kushirikiana katika kutekeleza miradi kwa pamoja ni nafasi unayopewa kila upande katika kutekeleza mradi. Sababu ya kuweka Sera, Sheria na Kanuni ni kuhakikisha tahadhari zinachukuliwa na hatua stahiki zinafuatwa kabla ya kuingia kwenye mikataba ya *PPP. (Makofi)*

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshmiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Lwenge. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara kwa njia ya tozo unahitaji mtu anaitwa *Transaction Advisor*. Huyu anakushauri uweke *guarantee* au usiweke *guaranteena* uweke *guarantee* kiasi gani ili Serikali isipate hasara. Sijui Serikali imefanya utartibu upi kuangalia kwamba wanashirikisha *TIB,* Benki yetu Kuu pamoja na huyo *Transaction Advisor?*

Swali dogo la pili Mheshimiwa Naibu Spika, Chalinze ni sehemu ambayo iko katikati, sasa sijui Wizara ya Ujenzi imeshirikiana kiasi gani na Wizara ya Uchukuzi ili kuangalia Bandari Kavu pale inajengwa ili nchi jirani za Malawi, Rwanda na Burundi, Zambia pamoja na Zimbabwe zinatumia fursa hii ya barabara hii ya tozo.

Je, kutakuwa na upungufu wa mizigo kwa kutumia injini na mabehewa ambayo mengi yananunuliwa sasa hivi kwa barabara ya tozo hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, najushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Mfutakamba, majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mhandisi Lwenge, Naibu Waziri Ujenzi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mfutakamba kwa sababu teknolojia hii ya kujenga mabarabara kwa ubia ni jambo jipya na ndiyo tunataka tulianze sasa hivi kwa miaka yote Serikali imekuwa inajenga barabara kwa kutumia fedha zake au za wafadhili.

Kwa hiyo ni jambo zuri ambalo naomba Waheshimiwa Wabunge walipokee kwamba sasa tuingize Sekta Binafsi isaidie tuweze kujenga mabarabara mengi zaidi yawe kwa kiwango cha lami.

Sasa suala la *transaction advisor* kwa sababu tunasema kwamba hili suala la kujenga barabara kwa njia ya kuingiza Sekta ya Binafsi ni jambo jipya. Ni kweli lazima tuwe na mtu ambaye ni mtaalam ambaye ana uzoefu na shughuli hizi na ndiyo maana hata huu mradi wa Dar es Salaam – Chalinze tumeshatangaza sasa hivi *expressional of interest* kwamba tumwajiri

transaction advisor ambaye atafanya kazi kwanza *feasibility study* kuweza kuona kwamba barabara hii tunayojenga na ile ambayo watu wengine wataendelea kutumia. Kwa sababu lazima uwe na njia mbadala.

Sasa hii ni njia ambayo tunataka tuipendekeze wawekezaji waweze kuona kwamba italipa katika muda ambao watu wameweka fedha zao na huyu *Transaction Advisor* kwa sababu ana uzoefu, atalinda ile fedha za mwekezaji zisipotee kwamba angalau amewekeza anapata na faida lakini pia wananchi watafaidika zaidi na pia tunalenga kwanza katika kuondoa msongamano wa Jiji la Dar es Salaam.

Masuala ya Bandari Kavu ni suala ambalo tutazingatia, tutashirikiana pamoja na Wizara ya Uchukuzi kuweza kuona maeneo ya Chalinze au maeneo mengine ya Mlandizi tuwe na maeneo ambayo mnaweza mkaweka Bandari Kavu. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na Serikali itafuatilia ushauri wake. *(Makofi)*

Na. 244

Wagonjwa Wanaoomba Msaada wa Matibabu Kupitia Vyombo vya Habari

MHE. ELIZABETH M. BATENGA aliuliza:-

Wizara ya Afya ndiyo yenye dhamana ya kulinda afya za wananchi kwa kutoa matibabu kwa watu wenye uwezo wa kifedha na wasio na uwezo huo, lakini ni jambo la kusikitisha ni kuona kwamba baadhi ya wananchi wanalazimika kuomba msaada wa fedha za matibabu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari kama vile *TV* na *Radio*.

Je, mwongozo wa Wizara unaelekeza kwamba kama mgonjwa hana uwezo wa kifedha hawezi kupatiwa matibabu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wapo wagonjwa ambao huenda kwenye vyombo vya habari ili kuiwezesha jamii na Serikali iweze kujua tatizo la kumsaidia.

Hata hivyo, Serikali inao utaratibu wa kuwatambua wagonjwa wasio na uwezo na kugharamia matibabu yao. Wagonjwa hao hutambuliwa katika Mtaa/Kijiji na kupewa barua ya msamaha utakaompa fursa ya kupatiwa matibabu hayo.

Aidha, upo mfumo wa rufaa kwa wagonjwa wote kuanzia ngazi ya Zahanati hadi hospitali ya Taifa na ikibidi rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi kwa gharama za Serikali kwa wasiokuwa na uwezo.

Vile vile Serikali inao utaratibu wa kutoa matibabu bure kwa akina mama wajawazito wanaojifungua, watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Wenye magonjwa sugu kama vile saratani, kifua kikuu, kisukari, UKIMWI na magonjwa ya akili, wengine wazee wenye umri zaidi ya miaka 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa rufaa unaposhindwa kumhudumia mgonjwa mapema baadhi ya wagonjwa wamekuwa wakitumia fursa ya vyombo habari ambavyo vimekuwa na mchango mkubwa wa kufanya tatizo la mgonjwa lijulikane kwa Serikali na jamii ili kulipatia ufumbuzi. Jamii na serikali imekuwa ikijitokeza na kuchangia fedha ambazo zimesaidia sana wagonjwa kwa matibabu ambayo wanahitaji.

Kutokana na uwezo mdogo wa kuwapeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi hivi sasa Serikali inajenga hospitali kubwa eneo la Mlonganzila ambayo ikikamilika itakuwa na uwezo wa kutoa huduma za afya ambazo kwa sasa wagonjwa wanalazimika kuzifuata nje ya nchi.

Serikali pia imeanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii yaani *CHF* ambapo Kaya na Familia inapata fursa ya kuchangia huduma ya afya kwa njia ya tele kwa tele au papo kwa papo. Kupitia utaratibu wa tele kwa tele Serikali huchangia fedha sawa na kiasi kilichokusanywa na Mfuko ambazo hutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Changamoto iliyopo ni idadi ndogo ya wananchi wanaojiunga na Mfuko huu hali ambayo huathiri ufanisi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri na Mikoa kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa *CHF* ili endapo Mtu binafsi au mwana kaya ameugua, Mfuko huu uwezo kusaidia gharama za matibabu.

Aidha Serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa rufaa ya matibabu katika ngazi zote ili wagonjwa wawezae kupata huduma ya matibabu bila matatizo. Jitihada hizi za Serikali zitasaidia kuimarisha huduma za afya kwa wagonjwa na kuondokana na utaratibu wa wagonjwa kuomba msaada wa matibabu katika vyombo vya habari.

MHE. ELIZABETH M. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini ningependa kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa hapa siyo kesi lakini iko mifano mingi ya wagonjwa wanaofukuzwa hospitalini, kwa sababu hawawezi kugharamia matibabu yanayotakiwa.

Kwa mfano operesheni au na vipimo. Lakini pia katika hospitali ambazo ziko mbali kwa mfano hospitali ya Ngara, Karagwe, Biharamulo, Mkoa mzima wa Kagera na mikoa mingine yote ya pembezoni. Wanapopewa rufaa kwenda hospitali za kwa mfano Muhimbili, Bugando na nyingine, hawapewi gharama za kusafiri kwenda kule na kusindikizwa kufika hospitali. Lakini wanaambiwa wajigharamie wenyewe.

Je, Serikali hapo ina mpango gani wa kurekebisha masuala haya?

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hapa yametolewa kwamba zipo huduma za kina mama wajawazito, wanaokwenda kujifunfgua, wanaotibiwa pamoja na Wazee. Lakini tunavyoona sisi labda mimi. Kwa mfano kwamba huduma hizi kwa kweli zinasua sua. Kwa mfano Wazee ukitembelea hospitali kwa mfano ile ya Kagera inayosemekana ni ya rufaa. Lakini unakuta wazee wamepanga foleni kwa muda mrefu sana, hawapati huduma ya haraka na ya kutosha na kuambiwa kwenda kununua dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri anasemaje hapo tufanyeje?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mama Batenga. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwanri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yanayosemwa hapa yana *certain assumption.* Kuna kitu *kinaitwa Community Health Fund (CHF)*. Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, atanisaiedia hapa.

Katika Halmashauri iliyoshiriki katika kuhamasisha huu Mfuko wa *CHF* na kupata Shilingi 250,000,000/=(Milioni mia mbili n hamsini) na CHF ikaongezea milioni mia mbili na hamsini zingine, jumla kuwa shilingi milioni mia tano (Sh. 500,000,000/=).

Nenda Rombo sasa hivi hutasikia hata siku mpoja haya matatizo yanayozungumzwa hapa. Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kwenye maeneo haya yanayozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara nimefika, unakaa kwenye mkutano wa hadhara unauliza hebu nyoosha mkono watu ambao wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii, hakuna. Unawezaje kutoa hizi huduma kama sisi hatujafanya kazi yetu ya kuhamasisha wananchi wajiunge na huu Mfuko. Mimi ninakiri anachokisema Mheshimiwa Batenga ni kweli. Mfuko wetu huu uwezo wake ni mdogo.

Sheria yetu ya Serikali inasema, wewe ukiweka mia mimi ninakuongezea mia. Mwananchi akienda na cheti pale, inaonyesha kwamba amelipia, yeye, mkewe na watoto wake wanne wenye umri usiozidi miaka kumi na nane, watapata huduma hiyo bure baada ya kulipia shilingi elfu kumi kama wameamua hivyo, hiyo haifanyiki. Sasa wanakwenda kwenye utaratibu wa papo kwa papo. Papo kwa papo ni ile huduma unayolipia Shilingiu elfu mbili saa hiyo. Uking'atwa na nyoka ghafla huna uwezo huo.

Duniani kote, watu wanaojua Bima ya Afya ni mtindo wa kisaasa wa kuishi hapa Duniani. Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani, moja ya eneo alilopata nalo matatizo ni hili la Bima ya Afya. Unamchukua mgonjwa Ngara kumpeleka Muhimbili, Jijini Dar es Salaam kama una uwezo unaobeba majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri mbele yako kuwa Halmashauri zetu zina upungufu mkubwa sana katika eneo hili ambalo Mheshimiwa Batenga anazungumza.

Tulienda Korogwe na Makamu wa Rais alifika pale na kutoa maelekezo. Hili linajibu swali la pili ambalo amesema kuhusu wazee. Tumesema kwamba orodha ya wazee wote katika kila Halmashauri ipatikane, na ifahamike.

Mkoa wa Tanga nimeshawaambia, nikimaliza hapa naenda Tanga ku-*check* watu wote waliojiunga na Mfuko wa Bima ya *Afya (CHF)* na kufungua Dirisha Maalum kwa ajili ya kazi hiyo.

Nataka nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri Mkuu na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuwaambia Wakurugenzi Watendaji huko waliko kuwa wakae chonjo. Hatuwezi kuruhusu kitu kama hiki kinachotokea hapa, madongo yanarushwa hapa kwa kitu ambacho ni dhahiri. Nimetoa mfano wa Wilaya ya Rombo kuonyesha kwamba ni kitu kinachowezekana kama tungefanya kama inavyotakiwa. Hili tatizo linalozungumzwa hapa halingekuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-*take note, ITV, TBC* na vyombo vingine vya Habari vimetusaidia sana. Unamwona mgonjwa pale na mguu wake anaumwa, umevimba na

kadhalika, ndicho anachotuambia hapa. Sisi kama Serikali tunachukua hatua na watu ambao wanaweza kusaidia nao wanasaidia pale.

Lakini dhana inayoonekana ni kwamba tumeshindwa kufanya kazi ile. Kazi ile katika hali ya kawaida ni kazi yetu sisi wote kama tungekuwa na uwezo kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kwamba nazungumzia suala ambalo ni *very sensitive*. Naomba unihurumie nisije nikasema hivi nikaonekana nimeharibu mambo. Jambo linalozungumzwa hapa ni la msingi sana. Sisi tunataka tutatue kabisa hili tatizo. Wakishaandikiwa pale Ngara kuwa wanatakiwa wapelekwe Muhimbili.

Muhimbili pale wakiandikiwa kwamba wanatakiwa wapelekwe India, wanatakiwa wapelekwe na Serikali, tena asindikizwe na *nurse* mpaka India. Suala hili tutamkumbusha Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na tutashirikiana naye kutekeleza kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na kukuthibitishia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sisi Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, kwa anayetaka papo kwa papo kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 ni shilingi 7,000/= kwa anayetaka usalama anatoa 10,000/= anapata bima ya afya ya mwaka mzima. Kwa hiyo, mtu anachagua ama 7 mara moja ama 10,000/= kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Twende kwenye chama ambacho hakijauliza swali kwa siku ya leo. Mheshimiwa Felix Mkosamali?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *ITV* imekuwa inaonesha watu ambao wana matatizo, kuliko *TBC* ambacho ndio chombo cha umma. Kwa nini *TBC* isipunguze matangazo ya *CCM* ambayo watu hata hawayahitaji iwe inatangaza watu hawa ambao wana matatizo kama *ITV? (Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, matangazo ya *CCM* yalitangazwa lini?

Hiyo naifuta mimi hiyo, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Habari? Mheshimiwa Nkamia?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuelewe, nilisema siku moja hapa kuna habari na hadithi. Chombo chochote cha habari kinatangaza habari, kama kuna chombo ambacho kinatangaza hadithi kama unavyosema Mheshimiwa Mkosamali, hilo ni jambo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niongeze tu kwamba, *TBC* wanafanya kazi kwa kufuata maadili ya taaluma ya uandishi wa habari; *ITV* wanafanya hivyo pia. Inawezekana kipindi ulichokiona wewe *ITV* ulikipenda zaidi. Pengine hakikukidhi maudhui ya habari. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tukubali majibu hayo, anayeongea ni mwanahabari, Mtaalamu kabisa.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale?

Na. 245

Kujenga Kituo cha Polisi – Tarafa ya Isangati

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Tarafa ya Isangati – Mbeya Vijijini, ina wakazi wapatao 100,000 lakini hawana Kituo hata kimoja cha Polisi na hulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 50 kufuata huduma hiyo wanapopata matatizo:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo kwenye Tarafa ya Isangati?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kutafiti maeneo mengine ya kupeleka huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza programu ya maboresho ya Jeshi la Polisi ambayo imeridhiwa na Serikali, Jeshi la Polisi lina mpango kabambe wa kusogeza huduma za ulinzi na usalama karibu na wananchi kwa kujenga angalao Kituo kimoja cha Polisi katika kila Tarafa kwa upande wa Tanzania Bara na Jimbo kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Utekelezaji wa mpango huu unategemea fedha zitakazotolewa na Serikali kwenye Bajeti ya kila mwaka. Pindi fedha zitakapopatikana Tarafa zote hizi zitajengewa Vituo vya Polisi na ikiwemo Tarafa ya Isangati.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linaendelea kubaini na kuyatambua maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kupelekewa miundombinu ya huduma ya ulinzi na usalama, ikiwemo kujenga vituo vya polisi katika maeneo hayo.

Aidha, napenda nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri za Miji na Wilaya na Wananchi kwa ujumla kushiriki katika ujenzi wa Vituo vya Polisi katika maeneo yanayohitaji huduma hiyo kama walivyohamasika kujenga Shule, Vituo vya Afya na kuchangia miradi ya maji.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la kujenga Kituo cha Isangati ni suala ambalo ni la muda mrefu, tangu Bunge lililopita. Lakini majibu ya Serikali karibu ni yaleyale yanafanana. Sasa sijajua kwamba, ni lini Serikali itakuwa na mpango maalum maana hii ilikuwa ni maombi maalum kwa ajili ya kujenga Kituo cha Usalama cha Polisi kule Tarafa ya Isangati?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nilikuwa naomba Waziri kama atakuwa tayari kwenda kufanya ziara katika eneo hilo, ili aweze kujionea hali halisi kwa nini wananchi wanatoka mbali wanasafiri muda mrefu kuja kutafuta huduma ya Polisi Mjini? Asante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, suala la ujenzi wa kituo hiki limekuwa la muda, lakini nafikiri sio sawa kwamba, hakuna kinachofanyika mpaka leo. Taarifa nilizonazo na ambazo Mheshimiwa Mbunge nina hakika anazo ni kwamba, kwenye Kata ya Ilembo tayari kiwanja kimepatikana na taratibu za kukipima na kutoa Hati zinaendelea. Baada ya kukamilisha taratibu hiyo tunaweza tena tukafikiria hatua nyingine ambayo inafuata ambayo itakuwa ni ujenzi.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge, aendelee kustahimili na kuusukuma huu mchakato wa kuhakikisha kwamba, Hati ya Kiwanja hiki inapatikana, ili tuwe kwenye mazingira bora ya kuweza kujenga Kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu ziara namwomba nimhakikishie kwamba, niko tayari na tupange mimi na yeye ratiba, ili tuende tukaangalie hili tatizo.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, niulize swali moja dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Chunya katika Mkoa wa Mbeya imechukua eneo takribani zaidi ya 49% na miundombinu yake ni mibovu. Na katika Wilaya hii kuna Wafugaji na Wachimba madini, lakini cha kushangaza Jeshi la Polisi lina gari moja tu na mahabusu yake hakuna, inabidi waende Mbeya Mjini kutumia mahabusu ya pale. Pale Chunya kuna mauaji, kuna vurugu katika Wafugaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe hapa tamko kuhusu Wilayah ii ya Chunya ambayo ni kubwa sana, lakini Jeshi la Polisi lina gari moja tu na mafuta ni matatizo? Nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze na nimshukuru kwamba, amelileta hili swali wakati ndio tunajadili Bajeti Kuu ya Serikali. Katika Bajeti ile kuna mapendekezo ya kupatiwa Jeshi la Polisi magari 777, nawashawishi Wabunge mwunge mkono jambo hilo liwezekane, ili Wilaya zote zipate magari, ikiwemo Wilaya ya Chunya. *(Makofi)*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na mkakati wa Serikali wa kujenga Vituo hivi vya Polisi pamoja na kushirikiana na wananchi, lakini kwa muda wa miaka miwili sasa mfululizo, Serikali imekuwa ikiahidi kuweza kukarabati Kituo cha Polisi cha Kengeja katika imbo la Mtambila, ambako Mheshimiwa Naibu Waziri alifika na akaahidi, ili kunusuru maisha ya Askari Polisi walioko katika Kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uniambie sasa mkakati wa kuwanusuru Askari wa Jeshi la Polisi, katika Kituo cha Kengeja umefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba nimjibu Mheshimiwa Masoud, swali lake la Nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimkiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa sababu, kila anapopata nafasi hili analiuliza na nilishamjibu. Jibu analo kwa kweli. Sasa anataka na leo nimjibu tena tu ni kwamba,

mimi mwenyewe nimekikagua Kituo cha Kengeja na kwa kweli kiko katika hali ambayo hata mimi ningekuwa Mbunge au si Mbunge ningekitetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati tulionao ni kuhakikisha kwamba, Kituo kile tunakifanyia ukarabati. Tulijaribu kutaka tufanye ukarabati katika mwaka huu unaoanza wa fedha, lakini fedha bado hazikuonekana kupatikana, lakini nimwahidi Mheshimiwa Masoud kwamba, tutachukua juhudi ya makusudi ya kuhakikisha kwamba, tunatafuta pesa mahali popote pale, ili katika ukarabati wa vituo na Kituo hiki cha Kengeja kiwemo, ili mimi na Mheshimiwa Masoud tuongee jambo jingine, *inshallah*. *(Makofi)*

Na. 246

Mashamba ya Mkonge – Tanga na Pangani

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Baadhi ya mashamba ya mkonge katika Wilaya ya Tanga na Pangani hayazalishi tena Mkonge ni mapori tu kwa sababu, yemetelekezwa kwa miaka mingi:-

Je, Serikali, ina mpango gani na mashamba hayo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa mitaji, matatizo ya uendeshaji na kushuka kwa bei ya mkonge katika soko la dunia, mashamba mengi ya mkonge yaliyokuwa yanamilikiwa na Mamlaka ya Mkonge Tanzania yakiwemo mashamba yaliyoko katika Wilaya za Tanga na Pangani yalishindwa kujiendesha kwa ufanisi.

Katika kushughulikia changamoto hizo, Serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* mwaka 1996 hadi 1999 ilibinafsisha mashamba hayo kwa wawekezaji binafsi, ili waweze kuyaendeleza kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baadhi ya Wawekezaji hao wakiwemo wawekezaji wa mashamba ya Marungu, Pongwe, Amboni na Kilimangwido, yaliyopo katika Wilaya za Pangani na Tanga walishindwa kuyaendeleza mashamba hayo na kuyatelekeza. Aidha, baadhi ya mashamba hayo yana migogoro ya umiliki iliyotokana na wamiliki hao kuchukua mikopo katika mabenki na kushindwa kurejesha mikopo yao, hivyo mashamba hayo kwa sasa yapo chini nya usimamizi wa mabenki kutokana na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa wananchi na baadhi ya mshamba kutelekezwa, Serikali inaendelea na mchakato wa kufuta Hatimiliki za mashamba yasiyoendelezwa, yakiwemo mashamba yaliyopo katika Wilaya za Tanga na Pangani, ili yapangiwe matumizi mengine ikiwemo kuyagawa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mkakati huo, Serikali kwa kushirikiana na mmiliki wa Shamba la Pongwe, tayari imeshabadilisha matumizi ya shamba hilo kwa kuligawa viwanja kwa wananchi.

Aidha, Serikali inaendelea kufuatilia wawekezaji wa mashamba mengine yaliyotelekezwa kwa lengo la kufahamu changamoto zinazowakabili, ili kuweza kutafuta wawekezaji wengine makini wa kuyaendeleza mashamba hayo au kubadilisha matumizi ya mashamba hayo na kuyakabidhi kwa Halmashauri za Wilaya na wananchi kwa ajili ya shughuli za kijamii na za makazi.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kuhusu hatma ya mashamba 10 ya Mkonge Mkoa wa Tanga na Mheshimiwa Waziri akajibu kuwa, ana-*good news* kwa watu wa Mkoa wa Tanga. Kuna mashamba 7 ya Mkonge ambayo Mheshimiwa Rais ameridhia ufutaji wa umiliki wake. Ningeomba kujua mashamba hayo saba ni yapi? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na mashamba hayo kuwa mapori kwa muda mrefu sana na kuwa kero kwa wananchi kama la Marungu, Kilimangwidu na wananchi wana matatizo sana kwa sababu ya ardhi hawana hata ya kulima.

Kwa hiyo, wananchi wamevamia mashamba yale wamejenga, wamelima. Naomba kujua, Serikali itawasaidiaje wananchi wakati wa ugawaji, nini hatma ya wananchi wale? Ahsante sana.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi hayupo, lakini mimi ninayo taarifa kwamba, tayari Wizara ya Ardhi imeshapeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais kuhusu kufuta Hatimiliki ya mashamba.

Baadhi ya mashamba ambayo tayari yameshawasilishwa ni mashamba 7 ya mkonge ya *Kihuhwi Sisal Estate, Sagula Sisal Estate, Lewa Sisal Estate, Bombwera Sisal Estate, Kwafungo Sisal Estate* na *Azimio Sisal Estate* na *Kilapula Sisal Estate*. Kama kuna orodha nyingine nitaomba tuwasiliane na Wizara ya Ardhi, ili tuweze kumpatia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali la pili, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi ni kwamba, kwa kweli, mashamba mengi yaliyotelekezwa haya mengi yameingia kwenye migogoro kutokana na wawekezaji hawa kushindwa na wengine wametumia Hati hizi kujipatia fedha na baadhi ya mashamba yameingia katika migogoro ya kwamba, sasa inakuwa vigumu kuwanyang'anya haraka haraka.

Kwa hiyo, hatua zinazochukuliwa na Serikali sasa ni kurejea mashamba haya, Wizara ya Ardhi itatumia Sheria za Ardhi kwa sababu, mashamba kama hayakutumika yameachwa kuwa mapori. Bado Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi au Serikali tunayo nafasi ya kuingilia na kubatilisha matumizi.

Kwa hiyo, tutawasaidia wananchi hawa. Nimeeleza kwamba, tutakachokifanya ni Halmashauri za Wilaya zikae na wale wananchi wajue wanataka kuyatumia kwa mipango gani, ili tuweze sasa kubatilisha Hati tuwakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo langu, wakati wa zoezi hili ningeomba sana sana wale ambao wanajipanga mara nyingi tunapofanya mambo haya, kujipanga kwa ajili ya

kuchukua maeneo haya, chonde chonde tukibatilisha haya mashamba na matumizi yake, wale wanaoomba waombe kwa ajili ya matumizi ya wananchi na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Na. 247

Kuweka Mnara wa Simu Kata ya Mwamagembe

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kuzishawishi Kampuni za simu kuweka mnara katika Kata ya Mwamagembe Wilayani Manyoni.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Kata hiyo yenye uchumi mzuri wa Kilimo cha Tumbaku na mazao ya misitu?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kupeleka huduma ya mawasiliano nchi nzima ikiwemo Kata ya Mwamagembe iliyo katika Wilaya ya Manyoni. Katika kufanikisha hilo pamoja na mambo mengine Serikali imekuwa inawahimiza watoa huduma za mawasiliano kupeleka huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini hasa yale maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara.

Vile vile Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote inatoa ruzuku kwa kampuni za simu kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali yenye shida za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Mgandu, Makanda, Sanza katika Wilaya ya Manyoni zilikuwa miongoni mwa Kata zilizoingizwa katika zabuni ya kwanza A iliyotolewa mwezi Februari mwaka huu 2014 kwa ajili ya kupatiwa huduma za mawasiliano.

Kata ya Mgandu ilipata mzabuni ambaye ni *TTCL* na Kata ya Makanda na Sanza zilipata mzabuni ambaye ni Kampuni ya *Vodacom* ambapo kazi ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba mwaka huu.

Aidha kata ya Mwamagembe katika Wilaya ya Manyoni inatarajiwa kuingizwa katika zabuni ya awamu ya pili inayotarajiwa kutangazwa katika mwaka ujao wa fedha yaani mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Lwanji na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuzihamasisha kampuni za simu kupeleka mawasiliano katika maeneo yote nchini na yenyewe itaendelea kufanya juhudi zake katika kuhakikisha kwamba maeneo yote yasiyo na mawasiliano yanapata mawasiliano. *(Makofi)*

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Mwaka wa fedha una miezi kumi na mbili na huu mwaka unaozungumza wa kuingiza zabuni wa kutangaza zabuni kwa ajili ya kupeleka mnara Mwamagembe unaanza mwezi ujao.

Sasa ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri awe *specific* ni lini hasa hii zabuni itatangazwa kwa ajili ya hatimaye waweze kuanza kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nilipenda kuuliza Serikali hapa kwamba hivi inatambua kwamba Mwamagembe ni Kata inayozalisha sana mazao ya misitu pamoja na mazao ya kilimo na hasa tumbaku. Wana uchumi mkubwa sana.

Sasa ningependa kuelewa sababu hasa inayofanya eneo lile liwe kisiwa kwa maana ya kupeleka mawasiliano maana toka Bunge la tisa nimeomba na Mawaziri wengi wamebadilishwa na ahadi hii imebaki ikiwa ni kitendawili.

Sasa ningependa kujua kwamba kuna hapa suala la ubaguzi lipo katika suala hili kwa sababu Kata ya Mitundu wameweka mnara, halafu wakaruka Mwamagembe wakaenda kuweka mbele, wakaweka Rungwa sasa hapa katikati hakuna mawasiliano na watu wana shughuli zao nyingi sana wanazozifanya lakini hawajasikilizwa mpaka leo.

Kwa hiyo mimi naomba leo Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze ni lini hasa mnara utapelekwa Mwamagembe ili watu hawa waweze kujikomboa na waweze kufanya biashara zao kwa uhakika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba na ni dhahiri na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba tumekutana mara kadhaa, amekuja Ofisini hapa Bungeni akifuatilia suala la mawasiliano kwenye Kata yake ya Mwamagembe.

Kwa hiyo, kwa wananchi wa Mwamagembe ambao wananisikiliza nataka niwahakikishie kwamba Mheshimiwa Mbunge wenu amekuwa analihangaikia sana hili tatizo sasa bahati mbaya huko nyuma kama unavyofahamu na Bunge lako kazi ya kupeleka mawasiliano.

Tulikuwa tunaipa sekta binafsi na makampuni haya yalikuwa na hiari ya kupeleka mawasiliano kokote wanakotaka na kule wasikotaka. Kutokana sasa na umuhimu wa mawasiliano kama miundombinu muhimu ya kukuza uchumi, Serikali imeamua sasa kulichukua jukumu hilo.

Kwa hiyo, ina uwezo wa kuamua sasa kwamba mawasiliano tupeleke wapi na kwa kipindi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda nimhakikishie sasa Mheshimiwa Mbunge kutokana na umuhimu mkubwa wa Kata ya Mwamagembe tutahakikisha kwamba mapema kabisa katika mwaka ujao wa fedha 92014/2015) katika zabuni za kwanza zitakazotangazwa katika mwaka ujao wa fedha kwenye mwezi wa nane basi Kata ya Mwamagembe itakuwepo.

Mimi binafsi nitahakikisha kwamba ujenzi unaharakishwa ili kilio cha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake kiishe. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nichukue swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge muda hauko upande wetu. Ni swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, linaloelekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Christowaja.

Na. 248

Sifa Zinazotakiwa Kwa Chuo Kutoa Mafunzo ya Shahada

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Jukumu la *NACTE* ni kusajili na kutoa ithibati kwa Vyuo vya Ufundi kote nchini.

Je, ili chuo kiweze kusajiliwa na kupewa ithibati ya kutoa Mafunzo ya Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu, kinatakiwa kuwa na sifa zipi?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo au Taasisi za Mafunzo ambazo sio Vyuo Vikuu vinasajiliwa na kupewa ithibati na Baraza la taifa la Elimu ya Ufundi *NACTE* kwa mujibu wa Sheria Namba Tisa ya Mwaka 1997 kifungu namba 5(1)(a),(b) na (e). Aidha chuo kinachokusudia mafunzo ya nguzo ya shahada kinatakiwa kuwasilisha maombi ya kutoa mafunzo hayo *NACTE* ambapo chuo kinachofuzu hupewa kibali kwa mujibu wa Kanuni zilizochapishwa kwenye tangazo la Serikali namba 155 la tarehe 10 Juni, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Chuo kiweze kutoa Mafunzo ya ngazi ya Shahada ni lazima kiwe na ithibati kamili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, mitaala inayokidhi vigezo vya *NACTE,* uwezo wa kubuni na kutayarisha *program* za mafunzo, mfumo thabiti, wa kudhibiti ubora wa mafunzo na shughuli za uendeshaji wa chuo, idara zenye sifa stahiki na uwezo wa kusimamia na kuendesha mafunzo, watumishi wenye sifa stahiki za taaluma na utaalamu na kuwa na sera na mipango ya utafiti.

Sifa nyingine ni kuwa na mfumo wa upandishwaji madaraja kwa Wakufunzi wanaozingatia uwezo wa kufundisha, kubuni na kufanya tafiti na kuchapisha taarifa za tafiti kwenye majarida ya kitaaluma ndani na nje ya chuo. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri na kutaja sifa ambazo chuo kinastahili kupata ithibati au kuruhusiwa kutoa shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu kama nilivyouliza, lakini kuna vyuo vingine au taasisi nyingine ambazo ziko chini ya *NACTE* ambazo sifa hizi zilizotajwa hazina.

Kwa mfano Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ambacho mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii tulikitembelea na kukuta kwamba chuo kile ile *top Management, Principle* ni mtu ambaye ana shahada mbili na ndiyo kwanza anasoma *Ph.D.* na wale *deputy* yule *ARC* wa *Academic Research and Consultancy* na yule mwingine ambaye anashughulika na mambo ya utawala na fedha ni watu ambao wana *Masters.*

Kisheria watu hawa hawaruhusiwi kuongoza chuo hiki kwa sababu baada ya kuuliza tuliambiwa kwamba anayetakiwa kuwa mkuu wa Chuo ni yule ambaye ni *Associate Professor* na wale *deputy* wawili ni wale ambao ni *Senior Lecturers* au wenye *Ph. D*. ni Madokta lakini kwa Serikali kuruhusu chuo hiki kutoa Shahada ya kwanza na *Post Graduate Diploma* na kuacha kutoa cheti au Stashahada kama ilivyokuwa Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo inaendekeza elimu duni na uongozi duni, tatizo ambalo litaigarimu nchi kwa miaka mingi ijayo? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Taasisi hiyo hiyo ya Tengeru mwanzo nimesema ilikuwa ikitoa *Certificate* na Stashahada, lakini sasa hivi imeachana na kutoa *Certificate* na Stashahada inatoa Shahada ya kwanza na *Post Graduate Diploma*.

Sasa naomba Waziri aniambie kwa Serikali kuendelea kuruhusu Taasisi nyingi kutoa Shahada na kuacha kutoa elimu ya ngazi hizi za chini, ambazo zinatoa watu au wafanyakazi ambao wanahitajika katika sehemu mbalimbali nchini.

Je, haioni kwamba inaziua hizi kada za kati ambazo tunazihitaji katika kuinua uchumi na kuleta maendeleo kwa kuruhusu watu wanaopata shahada tu peke yake?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kuhusu vigezo vya Mkuu wa Chuo. Katika chuo cha Tengeru hiki ni chuo ambacho ndani ya Bunge hili, Bunge lako limekipitisha kiweze kuwa na *autonomy* yake yenyewe na kimefanywa hivyo kwa sababu kinatimiza vigezo vile ambavyo vinawezesha chuo hiki kujiendesha chenyewe.

Chuo kina sifa stahiki za kitaaluma na vitendea kazi ambazo kinakipa uwezo wa kujiendesha chenyewe.

Sasa kama kuna mkuu ambaye hatimizi vigezo vile ambavyo vinatakiwa hili tutaliangalia kwa sababu haipaswi Bunge lipishe muswada ule kama chuo hiki hakitimizi vigezo hivi. Imani yangu ni kwamba Baraza la Elimu ya Ufundi *NACTE* limefanya kazi yake vya kutosha hadi kuweza kumshauri Waziri mwenye dhamana ili aweze kufikisha hapa Bungeni Muswada wa kutaka chuo kile kiwe kinajitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwamba kwa nini Serikali inaruhusu baadhi ya vyuo kutoa shahada badala ya kuendelea kutoa cheti na stashahada. Mwongozo wa ujumla kwa vyuo ambavyo vimepanda ngazi kadhaa nchini.

Kwa mfano Chuo kikuu cha Mbeya kilipotoka kwenye chuo cha Ufundi kuwa chuo kikuu maagizo ya Serikali ni kwamba wasiache kuendelea kutoa tuzo zile ambazo walikuwa wanazitoa mwanzo. Kwa mfano vyeti vile vya *FTC,* Diploma na kadhalika.

Pamoja na kwamba watakuwa wanatoa shahada zile za ngazi ya juu kama ambavyo sasa wameweza wamepata uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, havikatazwi na maelekezo ya jumla ya Serikali ni kwamba lazima waendelee na kutoa vyeti hivyo.

Tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunavyuo vyuo vingi zaidi vya kiufundi ambavyo vitatoa tuzo za ngazi ya chini ya shahada ili tuwe na wataalamu wanaohusika kama tunavyohitaji kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge maswali yetu yameisha kwa siku ya leo nawashukuru kwa ushirikiano. *So far,* sasa nitangaze kuhusu wageni tulio nao kwa siku ya leo nao ni kama hawa wafuatao.

Wageni wa Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mbunge wa Igalula ni Ndugu Nassir Ally, Katibu wa Umoja wa Vijana Wilaya ya Uyui Tabora. Pale ulipo Ndugu Nassor Ally, simama, Mheshimiwa Iddi Omari Mlenge, Katibu wa Mbunge Jimbo la Igalula unayeshughulikia uratibu karibu sana lakini Ndugu Haji Mlowezi Kihanga, Katibu wa Mbunge wa Siasa na uenezi karibuni sana.

Lakini pili tuna mgeni wa Mheshimiwa Joseph Selasini ambaye ni mtoto wake Ndugu Lisa Catherine Selasini, karibu sana Lisa baba anajitahidi sana kufanya kazi nzuri hapa Bungeni, wageni wa Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje Mheshimiwa Chibulunje ana wageni ambao ni wanafunzi arobaini (40) na walimu wao kutoka shule ya msingi Itiso Wilaya ya Chamwino. Wale wanafunzi wa Itiso, Chamwino simameni hapo mlipo natumaini watakuwa mahali Fulani.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya Mafunzo ni wanafunzi kumi na tano wa Shirika la Ndugu wa Fransisco Wakapuchini kutoka *Roman Catholic,* Nyumba ya Malezi iliyoko Miuji Dodoma, ahsanteni sana na karibuni sana hapa Bungeni.

Wanafunzi 40 na Walimu watatu kutoka *Mawenzi English Medium* Tarakea, Moshi karibuni sana wanangu, karibuni sana mmetoka Tarakea kule mwisho mpakani kabisa mpaka Dodoma mmesafiri safari ndefu nawaomba niwapongeze sana walimu na wanafunzi wote kutoka kule Tarakea. Mbunge wenu, Mheshimiwa Joseph Selasini, yuko hapa mnamwona anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni, karibuni sana wanafunzi kutoka Tarakea.

Wanachama 25 wa Klabu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tawi la Chuo Kikuu cha *St. John Tanzania* Dodoma. Wale wanafunzi wa kupambana na Rushwa kutoka *St. John* basi Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, unaona kazi ya APNAC inaendelea mpaka kwenye vyuo vikuu kwa sababu wewe ndiyo Mwenyekiti wa *APNAC* hapa karibuni sana endeleeni kupambana na kuzuia rushwa kuanzia kwenye ngazi ya Chuo Kikuu mliopo.

Naomba wasimame mabalozi 19 wa Maliasili na Utalii waliojitolea kutoka tawi la *UDOM* na Chuo cha Mipango ambao wanaongozwa na Mkurugunzi wao Mchungaji Clement Matwiga, karibuni sana.

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge tuna watoto 68 na walimu 6 (sita) kutoka Usharika wa KKKT Kanisa Kuu la Dodoma Mjini, ahsanteni sana watoto wazuri karibuni sana Bungeni, karibuni sana watoto na walimu wote kutoka Usharika wa KKKT. Tuna wageni vile vile kutoka KKKT Dodoma Mjini ambao ni Umoja wa Kina Mama 30 (thelathini) kutoka Kanisa Kuu, karibuni sana kina mama, karibuni sana Bungeni, Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatangazie matangazo mengine mawili. Moja linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club,* Mheshimiwa Iddi Azzan, ambaye kwa masikitiko makubwa anatangaza kwamba timu ya Bunge *Sports Club,* jana katika mchezo wa mpira wa miguu jana tarehe 15 Juni, 2014 timu ya Bunge *Sports Club* ilifungwa bao nne na upande wa Bunge *Sports Club* walijitahidi sana mabao yalikuwa mengi lakini wakafungwa haya machache sana manne na aliyeng'ara ni Mheshimiwa Amos Makalla.

Lakini kwa upande wa *netball* mpira wa mikono timu ya Waheshimiwa Wabunge ililipiza kisasi kwa kuwafunga bila huruma timu ya *NMB* jumla ya mabao 46 kwa sita na nyota wa

mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Grace Kiwelu. Tunawapongeza sana wachezaji wetu wa *netball*.

Waheshimiwa Wabun ge, Wachezaji wa *football* nilikuwa nawauliza hapa nini kimetokea wakasema kwamba ni kwa sababu ya kwenye kantini ya Bunge makongoro yamezidi sana siku hizi, sasa yapunguzwe kidogo, magoti yamejaa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Nkumba, Mwenyekiti wa Klabu ya Bunge ya Kulenga Shabaha, anaomba niwatangazie Wabunge kwamba tarehe 22 Juni, 2014 siku ya Jumapili, saa tatu kamili asubuhi, kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha katika Kambi ya Jeshi ya Makutupora.

Fomu za Ushiriki zinazungushwa humu Bungeni. Mheshimiwa Mbunge yoyote anayetaka kushiriki katika zoezi hilo anaombwa kuandika jina lake na kuthibitisha ushiriki wake tarehe 22 Juni, 2014 siku ya Jumapili kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha kule kwenye kambi yetu ya Jeshi ya JKT ya Makutupora na Waheshimiwa Wabunge ambao mnataka kuna fomu inazunguka mnaombwa mjiandikishe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao hamtaiona fomu mumwone Mheshimiwa Saidi Nkumba atawapatia na kwa wale ambao hawana kumbukumbu nzuri mpaka sasa Bingwa wa kulenga shabaha aliyepiga kwa shabaha kubwa kuliko wenginewote, kuliko Wabunge wengine wote, ni mimi mwenyewe nikifuatiwa na Mheshimiwa Saidi Nkumba, yeye akiwa namba mbili. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu tuendelee.

MISWADA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2014 *(The Finance Bill 2014)*

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Katibu. Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni *The Finance Bill 2014,* kwa hiyo, imeshasomwa hapa kwa mara ya kwanza. Nilisikia mtu anasema mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, Timu ya Bunge ya *Football* ni Timu ya Taifa. Juzi imefungwa mabao mawili kwa sababu mmechoka, leo mabao manne. Naomba mwongozo wako tujue ni nini tatizo? Inawezekana hawa mwalimu mzuri au hawana pesa na kama tutaona wana matatizo tuvunje hii timu tujenge mpya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mwongozo huu ni muhimu sana, sasa tumwite Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* atueleze kwa kifupi sana kwa nini *Bunge Sports Club* inatutia aibu Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. IDDI MOHAMED AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi. Niseme tu kwanza tukubali, kwenye mchezo wowote kuna kushinda, kushindwa ama

kutoka sare. Kwa hiyo, kufungwa ni moja ya matokeo ya mchezo huo. Timu ya Bunge iko vizuri, wale wanaokuja mazoezini wanajitahidi kufanya mazoezi. Tatizo kubwa ambalo tunalo, wala hatuna tatizo la pesa, kwa sababu sisi wenyewe Bunge tunazo pesa za kuendesha hiyo timu.

Kikubwa ambacho kinatukabili ni Waheshimiwa Wabunge wengi na wengi ambao ni vijana, hawapendi kuja mazoezini, hawataki kufanya mazoezi. Mara nyingi huwa wanajitokeza siku ya mechi tu na kulazimisha lazima wacheze na matokeo yake inakuwa ni kufungwa. Niseme kwa hali ambayo tunayo na majukumu makubwa ambayo tunayo, bado Timu ya Bunge inafanya vizuri ukiachilia mbali michezo hii miwili ambayo tumefungwa. Nashukuru. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Na mimi nakubaliana na kocha, Mheshimiwa Kombo, mabingwa wa Kombe la Dunia hivi sasa, Spain, juzi wamepigwa magoli matano na Uholanzi, haimanishi kwamba Spain ni timu mbovu hata kidogo. Kwa hiyo, katika mpira wa miguu mambo haya yanatokea. Katibu tunaendelea. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo tutaingia kwenye sehemu ya majadiliano kuhusiana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ya Bajeti, iliyotolewa wiki iliyopita, Siku ya Alhamisi. Kabla hatujaanza, kama ilivyo ada wataanza Wenyeviti wetu na Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba hiyo. Niwaambie tu kwamba, tumepata maombi ya watakaoshiriki katika majadiliano hayo kama 180 kutoka vyama vyote. Kwa maombi hayo, tumekaa kama ofisi tukaona kwa muda ambao tumejipangia, muda unatosha, kwa hiyo, hatutarajii maombi ya ziada. Tunategemea wale walioomba mpaka sasa ndiyo hao hao watakaochangia kwa siku hizi zilizopangwa.

Kwa hiyo, kutokana na fursa hiyo basi, hatutahitaji kulihoji Bunge, utaratibu utakuwa ni huu ufuatao; kwamba, kila mchangiaji sasa atakuwa na dakika kumi, badala ya dakika saba. Sasa tunarudi kwenye utaratibu wetu wa kawaida wa kikanuni, kwa saa za jioni badala ya Bunge kuanza saa 10.00, Bunge litaanza saa 11.00 na tutamaliza saa mbili kasorobo. Niwahakikishie Wabunge wote ambao wameomba kuchangia, mtapata nafasi kama mlivyoomba. *(Makofi)*

Kwa maelezo hayo, naomba sasa tuanze mjadala wetu kwa kuwasikiliza Kamati na Upinzani na tutaendelea na majina ya walioomba kadiri itakavyokuwa inatangazwa hapa mbele. Moja kwa moja, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/15, pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye Taarifa ya Kamati mwaka uliopita, Kamati ya Bajeti, pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kuisimamia Serikali, kwa kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi ya Serikali. Vilevile, Kamati hufanya uchambuzi wa hali halisi ya ukuaji wa Uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda, naomba Taarifa yote ya Kamati iingizwe katika kumbukumbu za *Hansard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa Bunge katika mchakato wa Bajeti, bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonesha utayari wa kupokea ushauri katika baadhi ya maeneo ambayo Kamati imekuwa ikitoa hususan eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya. Kamati inaona kuwa hii ni changamoto kubwa inayosababisha kutokuwepo kwa mabadiliko katika eneo muhimu la upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kuhusiana na mikakati ya kutekeleza bajeti kwa ufanisi na kuimarisha Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa masuala mbalimbali kuhusu mwenendo wa uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2013: Bunge lako Tukufu tayari limeshapokea taarifa kuhusu hali na mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14 kama ilivyowasilishwa tarehe 12 Juni, 2014 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa madhumuni makubwa ya Mpango wa Maendeleo ni kuongeza kasi ya maendeleo ili ifikapo mwaka 2025, nchi yetu iwe imetoka katika kundi la nchi maskini duniani na kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati *(Middle Income Country)*.

Kwa kuzingatia azma hiyo, Tanzania haina budi kuhakikisha inajenga uchumi wenye misingi imara na uwezo wa ushindani utakaoiwezesha kukabiliana na changamoto za maendeleo, kuweka mazingira wezeshi kwa mahitaji ya uwekezaji na mabadiliko ya utoaji huduma, masoko, biashara na teknolojia katika kanda na ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa, mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2010 – 2013 ni wa kuridhisha na umekua kwa wastani wa asilimia 6.8. Katika mwaka 2013 pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa kiwango cha asilimia 6.9 kwa mwaka 2012; asilimia 6.4 kwa mwaka 2011; na asilimia 7.0 kwa mwaka 2010. Ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka 2013, ulichangiwa zaidi na sekta ya mawasiliano ambayo ilikua kwa (22.8%); huduma za fedha (12.2%); viwanda na ujenzi (8.6%); biashara ya jumla na reja reja (8.3%); huduma (8.2%); na huduma za hoteli na migahawa (6.3%). Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu hazijafanya vizuri na wastani wa mchango wake katika Pato la taifa ulikuwa ni chini ya 4%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchumi mpana kukua kwa kasi ya kuridhisha kwa takribani miaka kumi mfululizo, umaskini miongoni mwa Wananchi wetu haupungui kwa kasi inayoridhisha kama ambavyo sensa ya mwaka 2012 inavyothibitisha. Hii inatokana na ukweli kwamba, sekta zinazobeba na kugusa maisha ya watu wasiopungua asilimia 75 ya Watanzania wote, yaani Kilimo, Mifugo na Uvuvi, hazikui kwa kasi inayotakiwa. Hii inatokana na Serikali kutowekeza vya kutosha katika sekta hizo pamoja na kuwepo kwa mwingiliano hafifu kati ya sekta zinazokua haraka na sekta hizo, yaani kilimo, mifugo na uvuvi, kuna *weak sectoral*

interlinkages na pia utekelezaji usio endelevu wa Sera na Programu mbalimbali zinazowekwa na Serikali kama vile KILIMO KWANZA na *ASDP* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viashiria vinavyoshawishi kuwepo ukweli kuwa familia zinazojishughulisha na kilimo, mifugo, uvuvi na misitu, ndizo zimeendelea kuwa maskini zaidi. Baadhi ya watafiti wanasema kuwa, pengo kati ya Wananchi wenye kipato cha juu na wenye kipato cha chini, limezidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya changamoto zinazokabili sekta hizi ni kutokuwepo kwa viwanda vya kuchakata mazao ili kuongeza thamani, masoko ya uhakika, bei yenye tija, upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na teknolojia sahihi na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina budi kuhakikisha kuwa shughuli zinazofanywa katika sekta hizi zinafanyika kwa tija na kuwaletea Wananchi manufaa na faida iliyo wazi na endelevu ili kupunguza umaskini haraka na kwa uhakika. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kuwekeza vya kutosha katika maeneo haya kwa asilimia kumi ya bajeti yake ya kila mwaka ili kuweza kupata ukuaji wa uchumi unaotazamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo baadhi ya nchi za Afrika zilizowekeza vya kutosha katika kilimo na kufanikiwa kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Kati ya mwaka 2003 na 2010, nchi za Burkina Faso, Ethiopia, Guinea, Malawi, Mali, Niger na Senegal, zimeweza kuwekeza kiasi cha asilimia kumi ya Bajeti zao katika kilimo. Nchi za Ghana, Madagascar na Zambia, zilifuatia kuwekeza kwa wastani wa asilimia tisa. Inakadiriwa kwamba, kutokana na mchango wa uwekezaji huu, nchi hizi zitaweza kupunguza umaskini uliokithiri kwa zaidi ya nusu ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii mtaiona katika makala iliyoandikwa na Mark Suzman wa Global Policy & Advocacy wa Bill & Melinda Gates aliyoitoa katika jukwaa la uchumi wa Afrika kule Abuja mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upatikanaji wa fursa za ajira nchini ni kubwa hasa kwa vijana. Ajira zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta ya Umma, hazitoshelezi kabisa katika kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili. Kwa mfano, nafasi za kazi 70 za Inspekta Wasaidizi katika Idara ya Uhamiaji zilizotangazwa, waliojitokeza kwenye usaili ni vijana 10,816! Hii ina maana kwamba, kila nafasi moja imeombwa na watu 155. Tatizo la ajira nchini linaendana pia na viwango vya umaskini, kama ambavyo Wananchi wengi maskini wamekuwa wakikimbilia mijini, ambako hali ya umaskini iko chini kuliko vijijini. Kwa mfano, Jijini Dar es Salaam, kulingana na takwimu zilizopo, linaongoza kwa kuwa na umaskini wa chini sana ikilinganishwa na miji mingine na vijijini. Hivyo, haishangazi kuona idadi ya Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ikiongezeka kwa kasi kubwa.

Tatizo la ajira litatatuliwa kwa kuishirikisha sekta binafsi kimkakati ili iweze kushirikiana na Sekta ya Umma, kuongeza uwekezaji kwenye sekta zinazohusisha Wananchi wengi kama nilivyobainisha hapo awali. Kubwa na la msingi zaidi ni kwa Serikali kuhakikisha kuwa, uchumi unakua kwa kasi zaidi ya asilimia nane kuliko ilivyo sasa; na ukuaji huo wa uchumi uwe endelevu kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi mfululizo . Hatua hiyo ndiyo itakayozalisha ajira nchini kwa kasi na kuongeza Pato la Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inaongelea mwenendo wa mfumko wa bei na thamani ya shilingi katika ibara ya 2.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2014, Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na deni la nje la sekta binafsi, lilifikia shilingi trilioni 30.56, ikilinganishwa na trilioni 23.67 Machi, 2013. Deni hili ni sawa na asilimia 57.47 ya Pato la Taifa kwa bei za sasa, ambalo ni shilingi

trilioni 53.17. Kati ya kiasi hicho, Deni la Serikali ni shilingi bilioni 26.8 na Deni la Sekta Binafsi la nje ni shilingi bilioni 3.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni hili, pamoja na Serikali kusema ni himilivu ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu hadi sasa na ni tishio kwa utengamavu wa uchumi jumla. Kamati inaona shaka kuhusiana na deni hili kutokuwa stahimilivu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Kuna madai mengi ya ndani ambayo hayajajumuishwa katika Deni la Taifa na taarifa zilizopo zinaonesha kuwa, madai hayo yanaendelea kuongezeka kutoka asilimia 0.5 ya Pato la Taifa mwaka 2012 hadi asilimia moja ya Pato la Taifa kwa mwaka 2013.

(ii) Uwiano uliopo wa Deni la Taifa na Pato la Taifa kiuchumi siyo wa kuridhisha. Ukubwa wa deni hili hauwiani na kiwango cha uzalishaji mali na ukuaji wa uchumi wa sasa wa asilimia 7.0 tu.

(iii) Udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma na ucheleweshaji wa uhakiki wa madai ya ndani. Taarifa ya Waziri wa Fedha ya nusu mwaka inaonesha kuwa, malimbikizo ya madai hayo hadi Desemba, 2013 yalikuwa yamefikia shilingi trilioni 2.09, ambayo ni asilimia nne ya Pato la Taifa. Kiwango hiki kinaaminika kuwa ndicho kiwango cha malimbikizo ya madai *(arrears*), kwa Serikali kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla kuhusiana na hali ya uchumi wa nchi: Kamati imebaini kuwa, bado kuna changamoto kubwa kwa Serikali ya kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa, mafanikio ya uchumi mpana yanafika vijijini, hususan katika kuongeza kipato cha Wananchi walio wengi na kupunguza umaskini wa kipato. Tutakapofanikiwa katika lengo hili, tutakuwa tunazungumzia ukuaji wa uchumi *(economic growth*), unaoenda sambamba na maendeleo ya kijamii na kiuchumi *(social-economic development*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kwamba, kama Taifa, bado hatujatumia vyema au kikamilifu, fursa zilizopo za kukuza uchumi wetu kupitia matumizi yenye tija na ufanisi wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 - 2015/16, unatoa mwongozo wa namna vipaumbele vya Taifa vitakavyotekelezwa ili kufungua fursa za ukuaji uchumi. Mwaka 2013/14 ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango huu katika mfululizo wa miaka mitano iliyopangwa katika Mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2013/14, ulilenga kutoa kipaumbele kwenye sekta zinazotekeleza miradi ya Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Miradi hiyo ni Kilimo, Uchukuzi, Nishati, Elimu, Maji na Fedha. Kwa kiasi fulani Kamati haijaridhika na hatua ya utekelezaji wa baadhi ya Miradi hiyo na sekta kama vile Maji, Fedha na Kilimo. Kutoridhishwa na utekelezaji huo kumetokana na ukweli kwamba, Miradi hiyo haikuwa imepelekewa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kutopelekwa kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza Miradi hiyo, imekuwa ni changamoto kubwa katika kuiwezesha Miradi hiyo kukamilika kwa wakati na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa maendeleo na pia kuchelewa kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepokea taarifa kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi hiyo ya kipaumbele na imeona kwamba ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kamati inashauri Serikali iendelee kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sekta hizo ili matokeo yake yaonekane katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jedwali Namba Moja la Taarifa, linaonesha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na kilichotolewa na Hazina katika baadhi ya mafungu hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu 2014. Jedwali hili linaonesha kuwa hadi Mei mwaka huu, yamepelekewa fedha za Hazina kwa kiwango kilicho chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mashauriano kati ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti na Serikali, Waziri wa Fedha alitoa taarifa Bungeni kwamba, shilingi bilioni 80 zitaongezwa Wizara ya Maji kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 kumalizika. Hadi taarifa hii inaandikwa, tayari shilingi bilioni 30 zimekwishatolewa. Tunaipongeza Serikali kwa hilo na ni matumaini ya Kamati kwamba, kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 50 kitatolewa kama Bunge lilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba Moja, Hazina haikuweza kutoa kiasi chote cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya sekta hizo kwa mwaka 2013/14. Kwa mfano, Kamati imeshangazwa kuona Idara mpya iliyoanzishwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, kutopokea fedha yoyote ya ndani, licha ya kwamba ilitengewa shilingi bilioni 4.964 ambayo ni sawa na asilimia 16.5 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa fungu hili. Kamati imeshindwa kuelewa iwapo mtekelezaji wa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo, hakupelekewa fedha za ndani kabisa isipokuwa za nje ambazo nazo zimetolewa asilimia 30 tu. Je, atawezaje kutekeleza majukumu yake ambayo kimsingi yapo katika mpango wa majaribio? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kuanzisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi, kwa kuunda kitengo maalum cha kufanya shughuli hiyo chini ya Ofisi ya Rais, *yaani Presidential Delivery Bureau (PDB)*. Utaratibu huu ni mzuri kama ukitekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha utaratibu wa *BRN* ili kuboresha utaratibu wa usimamizi wa utekelezaji wa miradi uliopo sasa. Kamati inapongeza hatua hii. Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na Kamati unaonesha kuwa, maeneo ya Matokeo Makubwa Sasa hayakupewa umuhimu uliostahili katika kupelekewa fedha kama Jedwali Namba Mbili la TAarifa yetu linavyoonesha. Mtalisoma ninyi wenyewe mtaona jinsi pesa zilivyopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, kutokupatikana kwa rasilimali fedha, kutaathiri sana utekelezaji wa Miradi na Programu zilizo chini ya *BRN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, iliandaa Sera na Mikakati ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, yaani *Public Private Partnership (PPP)* ya mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa malengo mazuri yalioainishwa katika Sera na Sheria ya Ubia huo, Kamati bado haijaridhishwa na ushiriki wa Serikali katika kutekeleza Miradi ya Ubia inayolenga kuimarisha ushirikiano huu. Hali hii imejidhihirisha katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo; mfano, uendelezaji wa Reli ya Kati, ukarabati na ujenzi wa bandari, Miradi ya Kufua Umeme, Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Ubalozi na Makazi ya Watumishi wa Balozi za nchi yetu zilizo nje ambayo mara nyingi, Bunge limekuwa likisisitiza utekelezaji wa Miradi hiyo kwa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haijaridhika na sababu inayotolewa mara kwa mara na Serikali kama kikwazo cha utekelezaji wa madhumuni na malengo ya Sera na Sheria ya *PPP*. Kutokana na Bajeti ya Serikali kuwa tegemezi, Kamati inaendelea kuishauri na kuitaka Serikali kuimarisha uhusiano na ushirikiano na sekta binafsi katika kuibua na kutekeleza miradi

mbalimbali ya ubia. Pamoja na tamko la Serikali juu ya azma ya kuanzisha Mfuko Maalum, Kamati ya Kitaifa na Kituo cha Miradi ya Ubia, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uwasilishwaji na kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya *Public Private Partnership,* ambao umesomwa mara ya kwanza katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba, ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni utaratibu ambao umeziwezesha nchi nyingi duniani kupiga hatua kimaendeleo na hivyo kuziwezesha nchi husika kukua haraka kiuchumi. Kama ilivyowahi kusemwa na Mchumi Mwanamaendeleo, Bwana Jefrey Sachs kuwa; "*The path to long-term development would only be achieved through private sector involvement and free market solutions*". Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba; "Maendeleo ya muda mrefu yanaweza tu kupatikana kwa njia ya ushiriki wa sekta binafsi na soko huru."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida zinazotokana na ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma, Kamati inatanabahisha kuwa Serikali ijitahidi kuwa makini kwa sababu yawezekana ukawepo upungufu utakaoweza kujitokeza hususan katika kuandaa mikataba ya miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti imetathmini kwa kina mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14. Mwenendo unaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, Serikali imekusanya shilingi bilioni 12,880 sawa na asilimia 70 ya mapato yote ya mwaka yaliyoidhinishwa na Bunge. Kiwango hiki cha ukusanyaji wa mapato si cha kuridhisha sana na Kamati inaona kwamba, sera za mapato kwa mwaka 2013/14 zimeshindwa kuleta mapato kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tunauona katika mwenendo wa mapato ya ndani. Malengo hayakufikiwa kwa sababu ya kutokufanya vizuri kwa baadhi ya vyanzo vya kodi. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 7,771.5, sawa na asilimia 75 ya makadirio; mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 425.5, sawa na asilimia 57 ya lengo; mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 252.8, sawa na asilimia 66 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3, inakisiwa kwamba, mpaka mwisho wa Mwaka wa Fedha 2013/2014, jumla ya nakisi ya Bajeti itafikia takribani shilingi trilioni 2.014, yaani mapato ambayo hayatapatikana katika Mwaka wa Fedha wa 2013/14. Wakati huo huo, bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/15 imeongezeka kwa asilimia 8.8, yaani trilioni 1.6, ikilinganishwa na bajeti ya mwaka huu wa fedha. Hii ina maana kwamba, pamoja na kuwa Serikali itapata mapato pungufu mwaka huu wa fedha, bado inajiaminisha kupata mapato mengi zaidi mwaka ujao wa fedha kufidia nakisi iliyojitokeza. Kamati inatarajia Serikali itatoa ufafanuzi kuhusu mipango madhubuti inayotoa uhakika wa kufikia malengo yaliyowekwa. Vinginevyo, hali hii inaweza kutafsiriwa kuwa bajeti ya mwaka ujao wa fedha tayari ina pengo la shilingi trilioni 3.6, yaani shilingi trilioni mbili ambazo hazikuweza kupatikana Mwaka wa Fedha 2013/2014 na shilingi trilioni 1.6 ambayo imeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waisome vizuri taarifa kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya misaada na mikopo inayosalia itapatikana kwa kiwango cha kuridhisha mpaka kufikia mwisho wa mwezi Juni, sehemu kubwa ya nakisi itatokana na mapato ya ndani, ambayo kwa makadirio ni shilingi trilioni 1.038.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Serikali yaliyohakikiwa mwaka 2013/14 ambayo hayakulipwa na hayakuingizwa kwenye Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2014/15, yanakadiriwa kufikia shilingi trilioni 1.3, sawa na asilimia 7.1. Ukijumlisha madeni haya ya shilingi trilioni 1.3 na pengo la shilingi trilioni 3.6 nililolielezea hapo awali, Bajeti ya mwaka ujao wa fedha ina pengo la shilingi trilioni 4.9, sawa na asilimia 24.68, karibia na asilimia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina mashaka kama sera hizi za mapato zitaweza kuleta mabadiliko ya mapato yanayokusudiwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/15. Kamati inashauri ni vyema Serikali ipitie upya sera zake ili kubaini kiini cha tatizo yaani; kwa nini vyanzo vya mapato havikufanya vizuri? Nini kitafanya vyanzo hivi vifanye vizuri zaidi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/15?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya kodi, bado kiwango hiki cha makusanyo si cha kujivunia sana. Katika Mwaka wa Fedha 2012/13, Kamati iliishauri Serikali kuharakisha kufanya tafiti zitakazowezesha kubaini vyanzo vipya vya mapato vitakavyowezesha Serikali kukusanya mapato zaidi kwa kutumia rasilimali tulizonazo. Hatua hii ilitarajiwa kupunguza utegemezi wa bajeti.

Kamati inasikitika kuona kuwa Serikali kupitia Bajeti yake, imeshindwa kuleta vyanzo vipya ambavyo vingeweza kutekelezwa katika mwaka huu na ujao wa fedha. Vilevile Kamati haijaridhishwa na kasi ya kufanyiwa kazi kwa vyanzo vilivyopendekezwa katika Taarifa ya Kamati ya Spika ya Mapato, ijulikanayo kwa jina maarufu *Chenge I*. Baadhi ya vyanzo vipya vya mapato vya kodi ambavyo Kamati inaamini vinaweza kuingizia serikali mapato mengi mara moja ni pamoja na uvuvi wa bahari kuu; kupiga mnada vitalu vya misitu na vya uwindaji wa kitalii; kupiga mnada masafa ya mawasiliano; kodi za majengo na kadhalika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako unaishia ishia malizia tafadhali.

ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni saa moja!

NAIBU SPIKA: Endelea tulikuwa tunaweka sawa,

ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Kamati inashangazwa na sababu inayotolewa na Serikali kwamba, hatuwezi kukusanya mapato hayo hadi hapo Serikali itakapojenga bandari maalum ya uvuvi, yaani *fish port;* wakati kwa taarifa rasmi za Serikali zilizotolewa Bungeni, Serikali inapoteza takribani Dola za Marekani milioni 222, sawa na Shilingi bilioni 372,960. Kamati inahoji, hadi hapo tutakapojenga bandari maalum ya uvuvi, tutakuwa tumepoteza mapato kiasi gani? Kamati inahimiza mapendekezo yaliyotolewa kwenye Taarifa ya *Chenge 1* yatekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inaelezea kwa kirefu suala zima la maduhuli, ibara ya 4.1. Kwa sababu ya muda sitaweza kuyasoma hayo. Ibara ya 4.1.2 inaelezea misaada na mikopo ambayo nchi yetu inapata, naomba myasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, tuna kila sababu nchi yetu kujikwamua kutoka kwenye utegemezi kwa kuangalia namna ambavyo baadhi ya nchi ambazo miaka ya 50 iliyopita tulikuwa sawa kimaendeleo; mfano Korea Kusini ambayo imefuzu kutoka kuwa nchi tegemezi na kuwa nchi iliyoendelea. Nchi hiyo na nyingine nyingi kama

Malaysia, zilitumia aina tofauti za mifumo ya kimaendeleo kama vile uchumi wa soko na mikakati ya ajira, *job creating strategies,* ambazo zimewawezesha kufika walipo sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo tu sekunde.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba, hotuba ambayo anaisoma Mwenyekiti bado hamjapata nakala zake kutokana na tatizo la uchapishaji. Wanafanya juhudi ya hali ya juu kabisa kuhakikisha mnapata muda si mrefu ujao.

Naomba tuendelee kumsikiliza Mwenyekiti wetu.

ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tu kufikia malengo yetu ya kimaendeleo kama tutasimamia misingi iliyo imara. Ninukuu maneno ya Bwana Kofi Annan, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alisema" *"The determination of Africans, and genuine partnership between Africa and the rest of the World, is the basis for growth and development."* Tafsiri yake isiyorasmi ni kwamba; "'Uamuzi wa Waafrika wenyewe na ubia wa kweli kati ya Afrika na maeneo mengine ya Dunia, ndiyo msingi wa ukuaji wa uchumi na maendeleo. "

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno hayo yanatuongoza tu katika kuhakikisha kwamba, tunatumia misaada tunayopata vizuri ili kujiendeleza kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini kama ambavyo sehemu ya malengo ya misaada hiyo inavyoonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya ndani na mikopo yenye masharti ya kibiashara. Mtajisomewa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la mwenendo wa matumizi. Matumizi ya Serikali kwa ujumla bado ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti. Kamati imebaini kuwa matumizi ya Serikali yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kwamba ni makubwa kuliko mapato. Hali hii imechangiwa na kutokuwepo kwa nidhamu katika matumizi, hali ambayo imejidhihirisha zaidi katika upande wa manunuzi. Pamoja na kuanza kutumika kwa Sheria mpya ya Manunuzi ya Mwaka 2011, bado manunuzi mengi yamekuwa yakifanyika bila tija. Mfano, manunuzi ya dharura yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, ambayo hayakupata kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali. Manunuzi hayo yalikuwa na gharama ya Dola za Kimarekani 810,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutosimamia kwa umakini matumizi ya Serikali lilisababisha bajeti ya mwaka 2013/14 kuanza na deni, yaani *expenditure float* ya shillingi billion 611.4, ambayo ni matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/13, lakini hayakulipwa mwaka huo na deni hili halikuingizwa kwenye bajeti ya 2013/14. Hali hii inatarajiwa pia kujitokeza tena kwa kiwango kikubwa zaidi kwenye bajeti ijayo ya mwaka 2014/15. Malimbikizo ya madai hayo hadi Desemba, 2013 yalikuwa yamefikia shilingi trilioni 2.09, ambayo ni asilimia nne ya Pato la Taifa. Tatizo hili ni lazima litafutiwe dawa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yaliyobainika kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha kwenye baadhi ya Miradi ni pamoja na utekelezaji wa Miradi chini ya kiwango; Miradi kukabidhiwa bila kukamilika; Miradi kutumia fedha zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa; taasisi kubadili bei za Mikataba ya Miradi; na baadhi ya Miradi iliyokamilika kutotumika kutoa huduma kwa walengwa kama ilivyopangwa. Yote hayo yapo katika taarifa mtakazoziona kwenye taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/14 utekelezaji wa bajeti katika baadhi ya mafungu, ulifanyika kinyume na matarajio ya Serikali. Yapo baadhi ya mafungu ambayo hayakutengewa fedha, lakini walipewa fedha nje ya bajeti za fungu husika. Hali hii ilisababisha baadhi ya mafungu ambayo yalikuwa yametengewa fedha, kutopelekewa fedha kama walivyopangiwa. Mafungu ambayo yalipokea fedha nje ya bajeti za Mafungu hayo yameoneshwa katika Jedwali Namba Tano ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mafungu hayo yalitumia fedha za ziada kiasi cha shilingi bilioni 115.81, ambayo ni sawa na asilimia 10.3 ya jumla ya fedha ambayo iliidhinishwa. Mtaziona ni Wizara zipi zinazohusika kwenye taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 jumla ya shilingi trilioni 2.735 zilitengwa kwa ajili ya kugharimia Deni la Taifa. Hata hivyo, kiasi cha shilingi trilioni 3.341 zilitumika katika mwaka huo kugharimia deni hilo. Ugharimiaji wa deni hilo katika mwaka huo ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 606 ambalo halikuwa kwenye Bajeti ya Serikali. Hata hivyo, ongezeko hilo ni pungufu kidogo ya ongezeko lililotumika katika Mwaka wa Fedha 2011/12 ambalo lilikuwa shilingi Bilioni 624. Kamati hairidhishwi na utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la malimbikizo ya madeni katika Wizara na Idara za Serikali. Katika hali ya kawaida, inatazamiwa kwamba Wizara na Idara za Serikali zitatumia fedha kulingana na bajeti iliyopangwa. Hata hivyo, hali hii imekuwa haitekelezeki kwa sababu mbalimbali zikiwemo ucheleweshwaji katika upatikanaji wa fedha za Bajeti. Endapo Wizara na Idara zitaendelea kutumia huduma, ama kulazimika kufanya hivyo bila kulipia, hali hii hutengeneza deni ambalo kama fedha za mwaka husika hazitatolewa, deni hilo huathiri bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa madai hayo yataachiwa mafungu husika yaingie nayo katika mwaka wa fedha ujao kama madeni. Suala hili linaendelea kuathiri bajeti ya mwaka husika na hivyo kuwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti. Kwa maana nyingine ni kwamba, bajeti zetu mwaka hadi mwaka zimekuwa zikitumika kwa kiasi kikubwa kulipa madeni badala ya kutekeleza mipango iliyopangwa katika mwaka husika. Matokeo yake ni miradi mingi kutokamilika kwa wakati, lakini pia kuiongezea Serikali gharama pale ambapo Miradi iliyopangwa kutekelezwa kuchelewa kukamilika au kutokamilika kabisa. Katika eneo hili, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa Serikali kuzitaka Wizara na Idara za Serikali kuwa na kasma ya kulipia madeni yao kutoka katika mafungu yao ili kuondokana na utaratibu wa kuyaficha madeni hayo na kuacha yalipwe kwa kutumia bajeti ya mwaka wa fedha unaofuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililogusa hisia za Wajumbe wa Kamati kuhusu matumizi ni kwenye Balozi zetu zilizopo nje ya nchi. Ofisi hizi huendesha shughuli zake kwa kujitegemea na kasma zake husimamiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2012/13, baadhi ya Balozi zilitumia fedha zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge. Kati ya Balozi 32, Balozi 16 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, zilionesha kutumia fedha nje ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge ambacho ni Shilingi bilioni 6.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2014/15, Sura ya Bajeti: Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 19,853.3 kutoka vyanzo mbalimbali na kwa mahitaji yaliyoainishwa. Jedwali Namba Sita katika Taarifa ya Kamati limetoa sura halisi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15, Kamati imebaini kuwa lipo tatizo la kimsingi tokea siku ya kwanza bajeti hiyo itkapoanza kutekelezwa, ambalo ni mapato yote ya ndani ni shilingi trilioni 12.44; matumizi yote ya kawaida

ni shilingi trilioni 13.408; mapato ambayo Serikali itakusanya ni asilimia 63.3 tu ya Bajeti yote ya Serikali; nakisi ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 968, nakisi hii haijumuishi *expenditure float* ya wastani wa shilingi bilioni 611; mikopo na misaada ya kibajeti inahitajika kulipia sehemu ya matumizi ya kawaida ya Bajeti ya Serikali; Bajeti ya Maendeleo ni shilingi trilioni 6.445; nakisi hiyo inazibwa na mikopo ya ndani, mikopo ya nje na misaada ya miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika uchambuzi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 imebaini pia kuwa kuna tatizo la kimsingi kutokea siku ya kwanza Bajeti inapoanza kutekelezwa kwenye upande wa matumizi kama ifuatavyo:-

Moja, Deni la Taifa ni shilingi trilioni 4.354 sawa na asilimia 21.93 ya bajeti yote; mishahara ni shilingi trilioni 5.317 sawa na asilimia 26.78 ya bajeti yote; Matumizi Mengineyo, yaani *OC* ni shilingi trilioni 3.735 sawa na asilimia 18.82 ya bajeti yote; Jumla ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi trilioni 13.408 sawa na asilimia 67.54 ya Bajeti yote; Misaada na mikopo ya kimaendeleo ni shilingi bilioni 2,019.4 sawa na asilimia 10.2ya bajeti yote; Misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 922.2 sawa na asilimia 4.6 ya bajeti yote; Mikopo ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 1,745 sawa na asilimia 8.79 ya bajeti yote; Mifuko ya pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 274.1 sawa na asilimia 1.38 ya bajeti yote na Miradi ya Maendeleo imetengewa shilingi trilioni 6.445 sawa na asilimia 32.46 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ingependa Serikali itoe mchanganuo wa kuonesha kiasi halisi cha misaada na mikopo ya kibajeti itakayopokelewa ili kuweka bayana takwimu hizo zinazoeleza kwamba, misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 922,168 na Mikopo na Misaada ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 1,745.3 bila kuchanganua kiasi cha misaada na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia kwa makini sura ya bajeti, utaona kwamba, makadirio ya makusanyo ya ndani ya shilingi trilioni 12.44 hayatoshi kugharimia mahitaji ya mishahara ya trilioni 5.317, Deni la Taifa trilioni 4.354 na matumizi yasiyoepukika trilioni 3.063, ambayo kwa ujumla yanatupa kiasi cha shilingi trilioni 12.734. Hivyo, makusanyo yetu ya ndani ya kodi ni pungufu kwa shilingi trilioni 0.294.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati Kuhusu Baadhi ya Hatua za Kodi Zinazopendekezwa na Serikali kwa mwaka ujao wa fedha ziko katika Ibara ya Sita ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina kuhusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15, yafuatayo ni maoni na ushauri wa jumla wa Kamati ya Bajeti:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuahidi kwamba, itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati pamoja na Bunge lako kuhusu usimamizi na nidhamu ya matumizi, bado hakuna mabadiliko ya kuonesha ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu kwamba umezingatiwa. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, ushauri ilioutoa wakati wa kuchambua na kupitia Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2013/14, yaani mwaka huu wa fedha, ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ushauri wa Bunge lako Tukufu juu ya matumizi yasiyokuwa ya lazima, Serikali ilianzisha Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu kwa madhumuni ya kuimarisha kaguzi za ndani katika Wizara, Idara na Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati za Bunge wakati zikichambua mapato na matumizi ya Serikali, hazikuona mabadiliko yoyote katika kudhibiti mapato na matumizi ya Serikiali. Aidha, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inadhihirisha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha siku nyingi cha Wabunge kuhusiana na hatua ya kupunguza baadhi ya misamaha ya kodi ambayo haina tija. Pamoja na lengo zuri la Serikali la kupunguza misamaha ya kodi hatua kwa hatua hadi kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua hizo bila kuathiri hatua nyingine za kusimamia uwekezaji nchini kama ilivyoelezwa na Serikali yenyewe kupitia Hotuba ya Waziri Mkuu wakati anawasilisha makadirio na matumizi ya ofisi yake, ukurasa wa 26, aya ya 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa *CAG* unaonesha kuwa Serikali imeendelea kukopa kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kutekeleza Miradi na mahitaji mbalimbali. Hata hivyo, kiasi kinachorejeshwa na Serikali ni kidogo sana. Ikumbukwe kwamba, fedha za mifuko ni za Wanachama wa Mifuko husika, hivyo kutorejeshwa kwa wakati kwa fedha hizo, kutasababisha Mifuko husika kushindwa kulipa pensheni kwa Wanachama wake watakaokuwa wanastaafu kwa kiwango wanachostahili. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 Mifuko hii ilikuwa ikiidai Serikali takribani shilingi trilioni tatu. Kamati inaihimiza Serikali kuweka utaratibu endelevu wa kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *PSPF,* Serikali inadaiwa kiasi cha shilingi trilioni 3.3 ikiwa ni malimbikizo ya pensheni ya Wanachama hadi kufikia Juni, 1999. Serikali imekuwa ikilipa shilingi bilioni 50 kila mwaka, ambacho ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na kiasi inachodaiwa. Kamati inaishauri Serikali itumie utaratibu wa malipo kwa fedha taslimu na hati fungani ili kuokoa Mfuko na hatari ya kufilisika. Aidha, Kamati inatambua kuwa, Serikali imekuwa ikichangia asilimia 15 ya mshahara wa mtumishi kwenye Mfuko wa *PSPF*. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa, kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na mzigo ambao Mfuko utabeba baada ya mtumishi kustaafu. Hivyo, Kamati inashauri Serikali iongeze kiwango cha mchango kwa Watumishi wa Serikali kufikia asilimia 20 na kufanya jumla ya mchango wa Wanachama kuwa asilimia 25 ya mshahara wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali katika mwaka 2013/14 umebaini kuwepo kwa madeni makubwa katika baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma. Mfano, Wizara ya Ujenzi ambayo imekuwa ikitekeleza Miradi ya Ujenzi wa Barabara bila kuwalipa wakandarasi kwa wakati kwa kuzingatia mikataba yao na hivyo kujikuta ikianza kila mwaka wa fedha ikiwa na malimbikizo ya makubwa ya madeni. *(Makofi)*

Hali hii imesababisha Wizara hii kutumia bajeti yake ya mwaka unaofuata kulipia madeni ya mwaka uliopita badala ya kutekeleza Miradi iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika. Kamati inashauri Serikali itoe agizo kwa Maafisa Masuuli wote, kulipa madai ya wazabuni kwa wakati ili kuepuka kuzalisha madeni ambayo yanaigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha na kusababisha hasara kwa wakandarasi kwa kuwapunguzia uwezo wa mitaji yao. *(Makofi)*

Kwa madeni ya Wizara na Taasisi ikiwemo *TANESCO* ambayo yamelimbikizwa hadi sasa, Kamati inashauri Hazina iyafanyie uhakiki na madai hayo na kuweka utaratibu wa kuyalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15 uliofanywa na Kamati, umeonesha kwamba mzigo wa matumizi ni mkubwa mno ikilinganishwa na vyanzo vya mapato vilivyopendekezwa.

Nadhani, Serikali imekosa ubunifu na haitaki kupokea ushauri kuhusiana na vyanzo vipya vya mapato, kwa kuwa imekuja na vyanzo vilevile vya kitamaduni vilivyozoeleka, wakati kuna vyanzo vingine vingi; pombe, sigara, soda, juisi. *(Makofi)*

Vyanzo hivi ni pamoja na vilivyopendekezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaoendelea kutekelezwa na Serikali, mapendekezo yaliyotokana na Maabara ya *BRN,* mapendekezo yaliyotolewa na Ripoti ya *Chenge I,* pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yenyewe. Kamati inaendelea kuhimiza Serikali kufanyia kazi mapendekezo na ushauri uliotolewa ili kupunguza nakisi ya bajeti na mzigo kwa walipa kodi wale wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, Washirika wa Maendeleo wamekuwa wakichangia takribani asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali. Mwelekeo walionao hivi sasa ni wa kuhama kutoka katika kuchangia Bajeti ya Serikali ya kila mwaka na kwenda kuchangia katika miradi ya kisekta yenye sura ya uwekezaji na kibiashara. Kwa kutambua kuwa Bajeti ya Serikali bado ni tegemezi kwa kiasi kikubwa, Kamati inashauri Serikali kujiandaa kupokea utaratibu huo mpya kwa kuhakikisha kwamba, inaainisha Miradi muhimu ambayo itakuwa na matokeo makubwa ili iweze kutekelezwa mara moja kupitia utaratibu huo kwa lengo la kupata matokeo makubwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu wetu wa bajeti husubiri Serikali ikusanye mapato kwanza ndiyo yasambazwe kwa watekelezaji, huchelewesha sana utekelezaji wa miradi na bajeti husika. Kamati inaishauri Serikali kufikiria kwa umakini na uharaka ushauri kwamba, kuanzia mwaka ujao wa fedha, Serikali ianzishe utaratibu wa kukopa ama kuazima fedha toka vyanzo mbalimbali nafuu za kutekeleza bajeti ya serikali kwa kiwango cha kufikia walau robo moja, yaani shilingi trilioni tano ya bajeti yote ya mwaka ya Serikali. Utaratibu huu huitwa *capital budget,* badala ya utaratibu wa *cash budget*, ambao umetumika kwa muda mrefu sasa wakati ulitakiwa kuwa mpango wa mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuharakisha kuletwa Bungeni, Sheria ya Bajeti itakayofanya kazi sambamba na Sheria mpya ya Manunuzi ili kudhibiti matumizi mabaya kinyume na sheria na kanuni kwa nia ya kuweka nidhamu katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Serikali kutazama upya ufanisi wa utoaji maamuzi stahiki kwa muda. Hali hii inaligharimu sana Taifa letu, mifano iko mingi tu, tusipofanya maamuzi kwa wakati ni gharama kubwa. Muda ni mali, Waswahili wanasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi wetu unatakiwa ushuke na uwafikie Wananchi walio wengi kuliko ilivyo sasa. Tunahitaji maono, dhamira ba ubunifu kuweza kufanikisha lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti umeonesha kwamba, bajeti imejaribu kugusa watu wa chini lakini katika mfumo ambao kwa namna fulani unaonekana kuwa na changamoto. Ni dhahiri kuwa, mapendekezo ya mfumo wa kodi na tozo mbalimbali zilizoainishwa zinaonesha nia ya Serikali katika kuongeza mapato, lakini baadhi ya mapendekezo hayo yana ugumu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15 kwa kiasi cha Shilingi trilioni moja nukta sita, ikilinganishwa na Bajeti ya Serikali inayomalizika mwaka huu, linatia mashaka iwapo malengo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi yatawiana. Panahitaji nidhamu ya hali ya juu ya utendaji ili kuweza kufikia malengo haya kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hiin kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru kwa dhati, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya (MB), Naibu Mawaziri wake; Mheshimiwa Adam Kigoma Malima (MB), Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba (MB), kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati. Namshukuru pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano

na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (MB) kwa kushirikiana vyema na Kamati. *(Makofi)*

Nawashukuru pia Wataalam wote kutoka Hazina na Tume ya Mipango, ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia pia fursa hii kukuhakikishia wewe na Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania kwa ujumla kwamba, kazi iliyokuwa mbele ya Kamati haikuwa rahisi, ilikuwa ngumu sana ukizingatia kuwa Kamati hii ni mpya. Kamati imefanya kazi kwa kujituma kwa muda mrefu mfululizo bila kupumzika. Ninapenda kuchukua fursa hii pia, kumshukuru Katibu wa Bunge letu, Dkt. Thomas Kashililah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa Mbise na Makatibu wa Kamati hiyo; Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto na Michael Kadebe, kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa hii na naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

Taarifa ya Kamati ya Bajeti Kama Ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2013 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2014/2015 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2013/14 NA MAPENDEKEZO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/15 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye taarifa ya Kamati mwaka uliopita, Kamati ya Bajeti, pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kuisimamia Serikali kwa kujikita zaidi kwenye kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi ya Serikali. Vile vile, Kamati hufanya uchambuzi wa hali halisi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa Bunge katika mchakato wa Bajeti, bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonesha utayari wa kupokea ushauri katika baadhi ya maeneo ambayo Kamati imekuwa ikitoa hususan eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya. Kamati inaona kuwa hii ni changamoto kubwa inayosababisha kutokuwepo kwa mabadiliko katika eneo muhimu la upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kuhusiana na mikakati ya kutekeleza bajeti kwa ufanisi na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI KUHUSU MWENENDO WA UCHUMI KWA MWAKA WA FEDHA 2013

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu tayari limeshapokea taarifa kuhusu hali na mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14 kama ilivyowasilishwa tarehe 12 Juni, 2014 na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa madhumuni makubwa ya Mpango wa Maendeleo ni kuongeza kasi ya maendeleo ili ifikapo mwaka 2025 nchi iwe imetoka katika kundi la nchi maskini duniani na kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati *(middle income country)*. Kwa kuzingatia azma hiyo, Tanzania haina budi kuhakikisha inajenga uchumi wenye misingi imara na uwezo wa ushindani utakaoiwezesha kukabiliana na changamoto za maendeleo, kuweka mazingira wezeshi kwa mahitaji ya uwekezaji na mabadiliko ya utoaji huduma, masoko, biashara na teknolojia katika kanda na ulimwengu kwa ujumla**.**

2.1 Ukuaji wa Uchumi na Kuondoa Umasikini

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2010 – 2013 ni wa kuridhisha na umekua kwa wastani wa asilimia 6.8. Katika mwaka 2013 pato halisi la Taifa (GDP) lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa kiwango cha asilimia 6.9 kwa mwaka 2012 ; asilimia 6.4 kwa mwaka 2011; na asilimia 7.0 kwa mwaka 2010. Ukuaji wa pato la Taifa kwa mwaka 2013, ulichangiwa zaidi na sekta ya mawasiliano (22.8%) ; huduma za fedha (12.2%) ; viwanda na ujenzi (8.6%) biashara ya jumla na reja reja (8.3%);huduma (8.2%) na huduma za Hoteli na Migahawa (6.3%). Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu hazijafanya vizuri na wastani wa mchango wake katika Pato la taifa ulikuwa ni chini ya 4%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchumi mpana kukua kwa kasi ya kuridhisha kwa takribani miaka kumi mfululizo, umasikini miongoni mwa wananchi wetu haupungui kwa kasi inayoridhisha kama ambavyo sensa ya Mwaka 2012 inavyothibitisha. Hii inatokana na ukweli kwamba sekta zinazobeba na kugusa maisha ya watu wasiopungua asilimia 75 ya watanzania wote, yaani **Kilimo, Mifugo** na **Uvuvi** hazikui kwa kasi inayotakiwa. Hii inatokana na Serikali kutowekeza vya kutosha katika sekta hizo pamoja na kuwepo kwa muingiliano hafifu kati ya sekta zinazokua haraka na zile zinazokua polepole (*weak sectoral interlinkages*) na pia utekelezaji usio endelevu wa Sera na programu mbalimbali zinazowekwa na Serikali kama vile **KILIMO KWANZA** na **ASDP** na kadharika.

Mheshimiwa Spika, Kuna viashiria vinavyoshawishi kuwepo ukweli kuwa familia zinazojishughulisha na kilimo, mifugo, uvuvi na misitu, ndizo zimeendelea kuwa maskini zaidi. Baadhi ya watafiti wanasema kuwa pengo kati ya wananchi wenye kipato cha juu na wenye kipato cha chini limezidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya changamoto zinazokabili sekta hizi ni kutokuwepo kwa viwanda vya kuchakata mazao ili kuongeza thamani, masoko ya uhakika, bei yenye tija, upatikanaji wa pembejeo na teknolojia sahihi na ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina budi kuhakikisha kuwa shughuli zinazofanywa katika sekta hizi zinafanyika kwa tija na zinawaletea Wananchi manufaa na faida iliyo wazi na endelevu ili kupunguza umasikini haraka na kwa uhakika. Hivyo Serikali ina wajibu wa kuwekeza vya kutosha katika maeneo haya (asilimia 10 ya bajeti) ili kuweza kupata ukuaji wa uchumi unaotazamiwa.

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya nchi za Afrika zilizowekeza vya kutosha katika kilimo na kufanikiwa kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Kati ya mwaka 2003 na 2010, Burkina Faso, Ethiopia, Guinea, Malawi, Mali, Niger na Senegal ziliweza kuwekeza kiasi cha asilimia 10 ya Bajeti zao katika kilimo. Nchi za Ghana, Madagascar na Zambia zilifuatia kwa kuwekeza kwa wastani wa asilimia 9. Inakadiriwa kwamba, kutokana na mchango wa uwekezaji huu, nchi hizi zitaweza kupunguza umaskini uliokithiri kwa zaidi ya nusu ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika tatizo la upatikanaji wa **fursa za ajira** nchini ni kubwa hasa kwa vijana. Ajira zinazotolewa na serikali pamoja na sekta ya umma hazitoshelezi kabisa katika kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili. Kwa mfano nafasi za kazi 70 za inspekta wasaidizi katika Idara ya Uhamiaji zilitangazwa, waliojitokeza kwenye usahili ni vijana 10,816! Hii ina maana kwamba kila nafasi moja imeombwa na watu 155. Tatizo la ajira nchini linaendana pia na viwango vya umasikini, kama ambavyo wananchi wengi masikini wamekuwa wakikimbilia mijini, ambako hali ya umasikini iko chini kuliko vijijini. Kwa mfano, Jiji la Dar es Salaam kulingana na takwimu, linaongoza kwa kuwa na umasikini wa chini sana ikilinganishwa na miji mingine na vijijini . Hivyo, haishangazi kuona kuwa idadi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa. Tatizo la ajira litatatuliwa kwa kuishirikisha sekta binafsi kimkakati ili iweze kushirikiana na sekta ya umma, kuongeza uwekezaji kwenye sekta zinazohusisha wananchi wengi kama nilivyobainisha hapo awali. Kubwa na la msingi zaidi ni kwa Serikali kuhakikisha kuwa uchumi unakua kwa kasi zaidi ya asilimia 8 kuliko ilivyo sasa na ukuaji huo wa uchumi uwe endelevu kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi mfululizo . Hatua hiyo ndiyo itakayozalisha ajira nchini kwa kasi na kuongeza Pato la Mtanzania.

2.2 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei na thamani ya shilingi

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mfumuko wa bei umepungua na umeendelea kuwa tarakimu moja toka asilimia 9.8 Machi, 2013 hadi asilimia 6.1 Machi 2014. Hii imetokana na juhudi za Serikali kusimamia mfumuko wa bei ya chakula hasa kwa upande wa bidhaa za mchele, ngano na mahindi.Mfumuko wa bei umeshuka pia kutokana na utaratibu wa Benki Kuu kupunguza mzunguko (ama ujazo) wa fedha nchini ama kwenye uchumi. Kamati inashauri jitihada za kudhibiti mfumuko wa bei ziendelezwe kwa namna ambayo haitaathiri ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi 2013/14; thamani ya shilingi katika soko la mabenki imeendelea kushuka ukilinganisha na Dola ya Kimarekani. Wastani umeonesha kuwa thamani ya shilingi kwa dola za kimarekani ilishuka kutoka shilingi 1,598.8 mwezi Machi, 2013 hadi hadi shilingi 1,634.3 mwezi Machi, 2014. Siku ya ljumaa tarehe 12 Juni, thamani ya Dola moja ya Kimarekani ilipanda kufikia shilingi 1683.52. Hii imetokana pamoja na mambo mengine, na kuongezeka kwa mahitaji ya nchi kwa bidhaa toka nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali izidi kuimarisha udhibiti wa soko la fedha za kigeni.

2.3 Deni la Taifa:

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Machi 2014 Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na deni la nje la sekta binafsi lilifikia shilingi trilioni 30.56 ikilinganishwa na trilioni 23.67 Machi 2013. Deni hili ni sawa na asilimia 57.47 ya Pato la Taifa (kwa bei za sasa) ambalo ni shilingi trilioni 53.17. Kati ya

kiasi hicho, Deni la Serikali ni shilingi bilioni 26,832 na Deni la Sekta Binafsi la nje ni shilingi bilioni 3,730.6.

Mheshimiwa Spika, deni hili, pamoja na Serikali kusema ni himilivu ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu hadi sasa na ni tishio kwa utengamavu wa uchumi jumla. Kamati inaona shaka kuhusiana na deni hili kutokuwa stahimilivu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(iv) Kuna madai mengi ya ndani ambayo hayajajumuishwa katika deni la Taifa na taarifa zilizopo zinaonesha kuwa madai hayo yanaendelea kuongezeka kutoka 0.5% ya pato la Taifa mwaka 2012 hadi 1% ya pato la Taifa mwaka 2013.

(v) Uwiano uliopo wa Deni la Taifa na pato la Taifa kiuchumi siyo wa kuridhisha. Ukubwa wa deni hili hauwiani na kiwango cha uzalishaji mali na ukuaji wa uchumi wa sasa wa asilimia 7.0.

(vi) Udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma na ucheleweshaji wa uhakiki wa madai ya ndani. Taarifa ya Waziri wa Fedha ya nusu mwaka inaonyesha kuwa malimbikizo ya madai hayo hadi Desemba 2013 yalikuwa yamefikia **shilingi trillion 2.09**, ambayo ni asilimia 4 ya Pato la Taifa. Kiwango hiki kinaaminika kuwa ndicho kiwango cha malimbikizo ya madai *(arrears*) kwa Serikali kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishatoa maelezo mazuri ya kuweza kukabiliana na madeni haya (soma MKUKUTA II, Ripoti ya CAG ya 2012/13), hata hivyo utekelezaji wake bado siyo wa vitendo na hivyo kubaki nadharia tu.

2.4 Mwenendo wa viwango vya riba na mikopo:

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viwango vya riba katika huduma mbalimbali za Benki na Taasisi za Fedha umeendelea kutokuwa wa kuridhisha na hivyo kuendelea kuathiri ukuaji wa uchumi. Takwimu zinaonesha kuwa, hadi mwezi Februari, 2014 wastani wa riba za mikopo zilikuwa asilimia 15.96 kutoka wastani wa asilimia 15.61 kwa mwaka 2013 kwa kipindi kama hicho. Riba za kuweka zimeimarika kwa asilimia 0.06 kutoka asilimia 11.50 kwa mwaka 2013 hadi asilimia 11.56 kwa mwaka 2014. Aidha, uwiano wa riba za kukopa na kuweka (*interest rate spread*) umepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.56 kutoka wastani wa asilimia 2.70 kwa mwaka ulioishia Februari, 2013.
Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa sekta binafsi, mikopo imeendelea kukua kwa asilimia 16.1. Hadi mwezi Februari 2014 kiasi cha shilingi bilioni 10,625.6 kilikuwa kimetolewa kama mikopo. Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo na kukua kwa kasi zaidi ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ni sekta ya ujenzi (asilimia 14.3), biashara (asilimia 14.1), mawasiliano na uchukuzi (asilimia 12.6), kilimo (asilimia 11.2) na uzalishaji wa viwandani (asilimia 9.8).

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha Mikopo inapatikana kwa sekta binafsi na inaendelea kuongezeka. Hata hivyo Kamati inaona kiwango hiki cha ukuaji kimekuwa ni kidogo kwa sababu sekta za kilimo na viwanda vidogo na vya kati vimekuwa havihudumiwi ipasavyo na taasisi za fedha (mabenki) kutokana na sababu kwamba havikidhi masharti ya kukopeshwa. Hali hii ikiendelea hatutaweza kujikwamua katika kuondoa umaskini wa kipato, kuongeza ajira mpya na kupunguza mzigo wa utegemezi katika kaya na hivyo kusababisha kudumaa kwa maendeleo ya kiuchumi.

2.5 Uuzaji, uagiziaji wa bidhaa na huduma nje:

Mheshimiwa Spika, uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje umekuwa mkubwa kuliko uuzaji. Urari wa biashara unaonyesha kuwa nakisi ina mwenendo wa kuongezeka. Hali hii ina mchango

mkubwa katika kudumaza uzalishaji na kuathiri thamani ya shilingi yetu na uchumi wa nchi kwa ujumla.

2.6 Ushauri wa jumla kuhusiana na hali ya uchumi wa nchi

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taswira hii ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2013 na Mwelekeo wake, Kamati imebaini kuwa bado kuna changamoto kubwa kwa Serikali kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa mafanikio ya uchumi mpana yanafika vijijini, hususan katika kuongeza kipato cha wananchi walio wengi na kupunguza umaskini wa kipato. Tutakapofanikiwa katika lengo hili, tutakuwa tunazungumzia ukuaji wa uchumi (*economic growth*) unaoenda sambamba na maendeleo ya jamii na kiuchumi (socio-*economic development*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba kama Taifa, bado hatujatumia vema au kikamilifu fursa zilizopo kikamilifu kukuza uchumi wetu kupitia matumizi yenye tija na ufanisi wa rasilimali zetu.

3.0 MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA

3.1 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2013/2014

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 -2015/16 unatoa mwongozo wa namna vipaumbele vya Taifa vitakavyotekelezwa ili kufungua fursa za ukuaji uchumi. Mwaka 2013/14 ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango huo katika mfululizo wa miaka mitano iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/14 ulilenga kutoa kipaumbele kwenye sekta zinazotekeleza miradi ya **Matokeo Makubwa Sasa** (MMS ama BRN). Miradi hiyo ni Kilimo, Uchukuzi, Nishati, Elimu, Maji na Fedha. Kwa kiasi fulani Kamati haijaridhika na hatua ya utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo na sekta kama vile Maji, Fedha na Kilimo. Kutoridhishwa na utekelezaji huo kumetokana na ukweli kwamba miradi hiyo haikuwa imepelekewa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kutopelekwa kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kumekuwa ni changamoto kubwa katika kuiwezesha miradi hiyo kukamilika kwa wakati na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa maendeleo na pia kuchelewa kufikia Malengo ya Maendeleo ya Millennia (Millenium Developemnt Goals).

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea taarifa kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ya kipaumbele, na imeona kwamba ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kamati inashauri Serikali iendelee kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sekta hizo ili matokeo yake yaonekane katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, Jedwali lifuatalo linaonesha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na kilichotolewa na Hazina katika baadhi ya mafungu hadi kufikia mwezi Mei 2014.

Jedwali Na.1: Namna Mafungu yalivyopokea fedha hadi mwezi Mei, 2014

Angalizo:Jedwali hili linaonyesha kuwa mafungu mengi hadi Mei 2014 yamepelekewa fedha na Hazina kwa kiwango chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mashauriano kati ya Kamati ya kudumu ya Bajeti na Serikali, Waziri wa Fedha alitoa taarifa Bungeni kwamba shilingi bilioni 80 zitaongezwa Wizara ya Maji kabla ya mwaka wa fedha 2013/2014 kumalizika. Hadi taarifa hii inaandikwa, tayari shilingi bilioni 30 zilikwishatolewa. Ni matumaini ya Kamati kwamba kiasi kilichobaki kitatolewa kama Bunge lilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 1 Hazina haikuweza kutoa kiasi chote cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya sekta hizo kwa mwaka 2013/14. Kwa mfano, Kamati imeshangazwa kuona Idara mpya iliyoanzishwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa **kutopokea fedha yoyote ya ndani licha ya kwamba ilitengewa shilingi bilioni 4.964 ambayo ni sawa na aslimia 16.57 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa fungu hili.** Kamati imeshindwa kuelewa iwapo mtekelezaji wa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi hakupelekewa fedha za ndani kabisa isipokuwa za nje ambazo nazo zimetolewa asilimia 33 tu, **je atawezaje kutekeleza majukumu yake ambayo kimsingi yapo katika mpango wa majaribio?**

3.2 Mfumo wa Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kuanzisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi kwa kuunda kitengo maalum cha kufanya shughuli hiyo chini ya Ofisi ya Rais *(Presidential Delivery Bureau-PDB)*. Utaratibu huu ni mzuri kama ukitekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha utaratibu wa BRN ili kuboresha utaratibu wa usimamizi wa utekelezaji wa miradi uliopo sasa. Kamati inapongeza hatua hii. Hata hivyo uchunguzi

uliofanywa na Kamati unaonesha kuwa maeneo ya Matokeo Makubwa Sasa hayakupewa umuhimu uliostahili katika kupelekewa fedha kama jedwali Na. 2 linavyoonyesha.

Jedwali Na. 2: Mahitaji ya Rasilimali na Nakisi ya bajeti kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa mwaka 2013/2014 (Tshs Milioni)

Chanzo: *Rapid Budget Analysis 2013, synoptic note*.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kutokupatikana kwa rasilimali fedha kutaathiri sana utekelezaji wa miradi na programu zilizo chini ya BRN.

3.3 Ushiriki wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iliandaa Sera na mikakati ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership-PPP*) ya mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na. 18 ya mwaka 2010 na Kanuni za utekelezaji wa Sheria hii za mwaka 2011. Aidha, kwa kutambua kuwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni njia muafaka inayoweza kutatua matatizo yanayotokana na ukosefu wa fedha, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa rasilimali za umma kwa ufanisi, Serikali imeandaa mfumo mpya wa kubuni, kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa malengo mazuri yalioanishwa katika sera na sheria ya ubia huo, Kamati bado haijaridhishwa na ushiriki wa Serikali katika kutekeleza miradi ya ubia inayolenga kuimarisha ushirikiano huu. Hali hii imejidhihirisha katika baadhi ya miradi ya maendeleo mfano uendelezaji wa reli ya kati, ukarabati na ujenzi wa bandari, miradi ya kufua umeme, miradi ya ujenzi wa Ofisi za Ubalozi na makazi ya watumishi wa balozi hizo nje ya nchi n.k ambayo mara zote Bunge limekuwa likisisitiza utekelezaji wa miradi hiyo kwa ubia baina ya sekta hizi mbili**.**

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhika na sababu inayotolewa mara kwa mara na Serikali kama kikwazo cha utekelezaji wa madhumuni na malengo ya sera na sheria ya PPP. Kutokana na Bajeti ya Serikali kuwa tegemezi, Kamati inaendelea kuishauri na kuitaka Serikali kuimarisha

uhusiano na ushirikiano na sekta binafsi katika kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya ubia. Pamoja na tamko la Serikali juu ya azma ya kuanzisha **Mfuko Maalum, Kamati ya kitaifa na kituo cha miradi ya ubia**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uwasilishwaji na kupitishwa kwa mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya *Public Private Partnership* ambao umesomwa mara ya kwanza katika Mkutano huu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba**,** ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni utaratibu ambao umeziwezesha nchi nyingi duniani kupiga hatua kimaendeleo na hivyo kuziwezesha nchi husika kukua haraka kiuchumi. Kama ilivyowahi kuelezwa na Mchumi na Mwana maendeleo, Bw. Jefrey Sachs kuwa ***"the path to long-term development would only be achieved through private sector involvement and free market solutions"***. Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba: **"Maendeleo ya muda mrefu yanaweza tu kupatikana kwa njia ya ushiriki wa sekta binafsi na soko huria."**

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zinazotokana na ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma**,** Kamati inatanabahisha kuwa Serikali isipokuwa makini, yapo mapungufu yanayoweza kujitokeza hususan kama Serikali haitakuwa makini katika kuandaa mikataba.

4.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2013/

4.1 Mwenendo wa Mapato

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imetathmini kwa kina mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14. Mwenendo unaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili 2014, Serikali imekusanya shilingi bilioni 12,882 sawa na asilimia 70 ya mapato yote ya mwaka yaliyoidhinishwa na Bunge. Kiwango hiki cha ukusanyaji wa mapato si cha kuridhisha na Kamati inaona kwamba sera za mapato kwa mwaka 2013/14 zimeshindwa kuleta mapato kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tunauona katika mwenendo wa mapato ya ndani. Malengo hayakufikiwa kwa sababu ya kutokufanya vizuri kwa baadhi ya vyanzo vya kodi. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Fedha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 7,771.5 sawa na asilimia 75 ya makadirio; mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 425.5 sawa na asilimia 57 ya lengo; mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 252.8 sawa na asilimia 66 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kuwa, hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni mwaka huu, makusanyo ya mapato yanayotokana na kodi yatafikia asilimia 93 ya lengo. Hii ina maana kwamba nakisi ya makusanyo itakuwa **asilimia 7 sawa na shilingi bilioni 728**. Kwa uelewa huo, Kamati imefanya makadirio ya nakisi kwa vyanzo vingine vya mapato ya ndani hadi itakapofikia mwisho wa mwaka wa fedha kwa kuzingatia mwenendo wa miezi kumi hadi sasa, kwa sharti kwamba mwenendo huo wa makusanyo utaendelea kuwa kama ulivyo sasa. Matazamio ya mwenendo wa mapato hadi mwisho wa mwaka yameoneshwa kwenye jedwali Na. 3 ya Taarifa hii.

Jedwali Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Mapato hadi kufikia Juni, 2014.

Chanzo: Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa fedha 2014/15
Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.3, inakisiwa kwamba mpaka mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya nakisi ya **Bajeti itafikia takribani shilingi trilioni 2.014**, **yaani mapato ambayo hayatapatikana katika mwaka wa fedha wa 2013/14. Wakati huo huo, bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2014/15 imeongezeka kwa asilimia 8.8 (trilioni 1.6) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2013/2014. Hii ina maana kwamba pamoja na kuwa Serikali itapata mapato pungufu mwaka huu wa fedha, bado inajiaminisha kupata mapato mengi zaidi mwaka huu wa fedha kufidia nakisi iliyojitokeza**. Kamati inatarajia Serikali itatoa ufafanuzi kuhusu mipango madhubuti inayotoa uhakika wa kufikia malengo yaliyowekwa. **Vinginevyo, hali hii inaweza kutafsiriwa kuwa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 tayari ina pengo la shilingi trilioni 3.6, yaani shilingi trilioni 2 ambazo hazikuweza kupatikana mwaka wa fedha 2013/2014 na trilioni 1.6 ambayo imeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana.**

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya misaada na mikopo iliyosalia itapatikana kwa kiwango cha kuridhisha mpaka kufikia mwisho wa mwezi Juni**,** sehemu kubwa ya nakisi itatokana na mapato ya ndani, ambayo kwa makadirio ni **shilingi trilioni 1.038.**

Mheshimiwa Spika, madeni ya Serikali yaliyohakikiwa mwaka 2013/14 ambayo hayakulipwa na hayakuingizwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2014/15 yanakadiriwa kufikia **shilingi trilioni 1.3** (sawa na **asilimia 7.1**). Ukijumlisha madeni haya ya **shilingi trilioni 1.3** na pengo la **shilingi trilioni 3.6** lililoelezwa hapo juu, Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 ina pengo la **shilingi trilioni 4.9, sawa na asilimia 24.68, karibia na asilimia 25.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inamashaka kama sera hizi za mapato zitaweza kuleta mabadiliko ya mapato yanayokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2014/15. Kamati inashauri ni vema Serikali

ipitie upya sera zake ili kubaini kiini cha tatizo yaani; Kwanini vyanzo vya mapato havikufanya vizuri? Nini kitafanya vyanzo hivi vifanye vizuri zaidi kwa mwaka wa fedha wa 2014/15?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya kodi, bado kiwango hiki cha makusanyo si cha kujivunia sana. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Kamati iliishauri Serikali kuharakisha kufanya tafiti zitakazowezesha kubaini vyanzo vipya vya mapato vitakavyowezesha Serikali kukusanya mapato zaidi kwa kutumia rasilimali tulizonazo. Hatua hii ilitarajiwa kupunguza utegemezi wa bajeti.

Kamati inasikitika kuona kuwa Serikali kupitia Bajeti yake imeshindwa kuleta vyanzo vipya ambavyo vingeweza kutekelezwa katika mwaka huu na ujao wa fedha. Vile vile Kamati haijaridhishwa na kasi ya kufanyiwa kazi kwa vyanzo vilivyopendekezwa katika taarifa ya Kamati ya Spika ya Mapato ijulikanayo kama **Chenge I**. Baadhi ya vyanzo vipya vya kodi ambavyo Kamati inaamini vinaweza kuingizia serikali mapato mengi mara moja ni pamoja na: **uvuvi wa bahari kuu**; **kupiga mnada vitalu vya misitu na vya uwindaji wa kitalii; kupiga mnada masafa ya mawasiliano**; **kodi za majengo** n.k.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi wa Bahari Kuu, Kamati inashangazwa na sababu inayotolewa na Serikali kwamba hatuwezi kukusanya mapato hayo hadi hapo Serikali itakapojenga bandari maalum ya uvuvi (*fish port*) wakati kwa taarifa rasmi za serikali zilizotolewa Bungeni**, Serikali inapoteza takribani Dola za Marekani milioni 222 sawa na Shilingi bilioni 372,960.** Kamati inahoji, hadi hapo tutakapojenga bandari maalum ya uvuvi, tutakuwa tumepoteza mapato kiasi gani? **Kamati inahimiza mapendekezo yaliyotolewa kwenye Chenge 1 yatekelezwe**.

4.1.1 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijaweza kufanya vizuri sana katika makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi. Kwa muda sasa baadhi ya Wizara, Idara na wakala mbalimbali wa Serikali hazijaweza kukusanya maduhuli kiasi cha kufikia malengo waliyowekewa. Zaidi ya robo tatu ya Wizara, Idara na wakala za Serikali hazikuweza kufikia malengo ya makusanyo kwa asilimia 50 hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya Wizara ambazo sehemu ya bajeti yake inategemea makusanyo ya maduhuli. Kutofanya vizuri katika ukusanyajii wa maduhuli husika kuna athari ya moja kwa moja katika bajeti zao. Baadhi ya Wizara na Idara hizo ni kama vile **Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Maliasili na utalii, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto**.

Mheshimiwa Spika, angalizo la Kamati kwa Serikali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli linatokana na ukweli kwamba maduhuli ni sehemu ya mchango wa bajeti ya Serikali. Udhaifu uliojionesha katika eneo hili unachangiwa kwa kiasi kikubwa na Wizara na Taasisi zinazokusanya maduhuli kutotimiza malengo yake ipasavyo na hivyo kupunguza mapato ya Serikali. Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo katika uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli, ambapo malengo ya maduhuli hayazingatii hali halisi ya ukusanyaji kwa kufanywa malengo makubwa sana ama madogo sana ikilinganishwa na uwezo wa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka viwango halisia na kusimamia ukusanyaji wa maduhuli hayo kama Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 inavyoelekeza. Aidha, Kamati inarejea wito wake kwa maafisa masuuli kuhakikisha kwamba jukumu la kukusanya maduhuli

waliyopangiwa linapewa kipaumbele kama majukumu mengine ili Serikali ipate mapato stahiki. Ni wakati sasa kwa Serikali kuanza kuchukua hatua stahiki kwa mashirika na Taasisi za Serikali ambazo zinashindwa kukusanya maduhuli kama inavyotakiwa. Aidha, Kamati inaomba Bunge lipewe matokeo ya utafiti wa eneo maduhuli uliokuwa ukifanywa na Wizara ya Fedha kwa madhumuni ya kuboresha makusanyo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya mabadiliko ya sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 148 na Sheria ya Wakala wa Serikali sura 245 ili kuweka sharti la wakala na Taasisi za Serikali kuwasilisha Hazina kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi badala ya mapato ya ziada. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, kwani imepelekea mashirika haya kuchangia zaidi katika mfuko mkuu wa Serikali.

4.1.2 Misaada na Mikopo

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika nchi yetu ni miongoni mwa nchi zinazoendelea duniani. Mbali na mapato ya ndani, Bajeti ya Serikali hutegemea misaada na mikopo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Fedha, wafadhili wamejitahidi kutekeleza ahadi zao. Hata hivyo kwa upande wa fedha za miradi, mwenendo wa utoaji wa fedha hizo umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka kutokana na Serikali kutotimiza mchango wake katika miradi hiyo. Katika mwaka wa fedha 2013/14 ambapo Serikali imeanza kutekeleza program yake kabambe wa tekeleza kwa **Matokeo Mkubwa Sasa**, hali ya kusuasua kwa utoaji wa fedha imeendelea kuonekana. Hali hii ya sintofahamu inaifanya Kamati kuangalia utaratibu mwingine unaoweza kutumiwa na wafadhili katika kugharamia miradi ya maendeleo. Kikubwa hapa ni kuhakikisha utaratibu utakaotumiwa uwe wa manufaa kwa nchi na uzingatie sheria na taratibu, hususani katika uingizaji wa vitendea kazi na malighafi ambazo hazipatikani nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaungana na Serikali kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo katika kuchangia Sehemu ya bajeti yetu. Hata hivyo, ili kuwafanya washiriki wetu waweze kukamilisha ahadi zao kikamilifu na kwa wakati, Serikali izingatie kutekeleza makubaliano na ahadi zake za kibajeti hususani kwenye bajeti ya maendeleo katika kila mradi. Hatua hii itasaidia katika kuimarisha uwezo wetu wa ukusanyaji wa mapato ambayo yatasaidia kutekeleza miradi ya kiuchumi ambayo itaiingizia nchi mapato. Kwa kufanya hivyo, nchi itakuwa imejiweka katika hatua nzuri ya kupunguza utegemezi wa bajeti. Msisitizo wa Kamati katika eneo hili ni kwamba, makusanyo yaelekezwe zaidi kwenye kugharamia na kutekeleza miradi ya maendeleo na sio matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa tuna kila sababu nchi yetu kujikwamua kutoka kwenye utegemezi kwa kuangalia namna ambavyo baadhi ya nchi ambazo miaka ya 50 tulikuwa sawa kimaendeleo; mfano Korea Kusini ambayo imefuzu kutoka kuwa nchi tegemezi na kuwa nchi iliyoendelea. Nchi hiyo na nyingine nyingi, zilitumia aina tofauti za mifumo ya kimaendeleo kama vile uchumi wa soko *(market-based*) na mikakati ya ajira *(job creating strategies)* ambazo zimewawezesha kufika walipo sasa.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tu kufikia malengo yetu ya kimaendeleo kama tutasimamia misingi iliyo imara. Ninukuu maneno ya Bw. Kofi Annan aliyesema:-

> *"The determination of Africans, and genuine partnership between Africa and the rest of the world, is the basis for growth and development."*
> Tafsiri yake isiyorasmi ni kwamba "*'Uamuzi wa Waafrika wenyewe, na ubia wa kweli kati ya Afrika na maeneo mengine ya dunia, ndiyo msingi wa ukuaji wa uchumi na maendeleo."*

Mheshimiwa Spika, maneno hayo yanatuongoza tu katika kuhakikisha kwamba tunatumia misaada vizuri ili kujiendeleza kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini kama ambavyo sehemu ya malengo ya misaada hiyo yanavyoonesha.

4.1.3 Mikopo ya ndani na mikopo yenye masharti ya kibiashara

Mheshimiwa Spika,Kamati yangu inatambua jitihada za Serikali katika kutafuta fedha maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo pamoja na kulipia madeni. Pamoja na ukweli kwamba mikopo ya masharti ya kibiashara ina riba kubwa ikilinganishwa na ile isiyo ya kibiashara, mikopo hii ndiyo iliyo na uhakika na uharaka katika upatikanaji wake. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili, 2014 Serikali ilikopa shilingi bilioni 1,803.9 kutoka soko la ndani ambapo kiasi cha shilingi bilioni 690.6 ni kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba mikopo yote (yaani mikopo nafuu na mikopo yenye masharti ya kibiashara) ielekezwe katika miradi ya maendeleo ili iweze kuleta tija badala ya fedha hizo kutumika kwa matumizi ya kawaida. Tujikumbushe mfano rahisi wa **Mpango wa Marshal** ulipokuwa unaanzishwa mwaka 1947, ambapo nchi nyingi za Ulaya ziliamua kuanza kupokea misaada kutoka vyanzo tofauti. Katika hali hiyo Benki ya Dunia ikaona kuwa inakabiliwa na ushindani na hivyo kuamua kubadili mwelekeo wake kwa nchi zisizokuwa za Ulaya. Hadi kufikia mwaka 1968, mikopo yake ilikuwa inatengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha mapato, kama vile bandari, mifumo ya barabara, na mitambo, ambayo ilikuwa ikizalisha mapato ya kutosha ili kuziwezesha nchi zinazokopa kulipa mkopo kupitia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya nchi ambazo zimefanikiwa kwa kutumia utaratibu huu. Tanzania tunachelewa wapi kuamua kufuata njia walizofuata wenzetu? Wakati wa kubadilika ni sasa, tukiendelea kusubiri muda hautusubiri, idadi ya watu inazidi kuongezeka na mahitaji, matatizo na changamoto pia vitazidi kuongezeka.

4.1.4 Maoni ya Kamati kuhusu makusanyo yaliyotokana na Hatua za Kodi zilizopendekezwa na Serikali kwa mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Serikali ilifanya marekebisho katika maeneo 22 ya mfumo wa kodi, yaliyotarajia kuiingizia Serikali kiasi cha shilingi milioni 970,516.0 katika kipindi cha Julai hadi April 2014. Kati ya maeneo hayo 22 ni maeneo 11 tu ndio yaliweza kukusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 70, maeneo 9 yalikusanya mapato kwa kiwango cha chini ya asilimia 70. Wakati huo huo maeneo 3 hayakukusanya mapato yoyote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoridhika na ukusanyaji wa kodi kwa ujumla, hususan katika kipindi cha mwaka 2013/14, Kamati ilifarijika na hatua ya ukusanyaji wa kodi katika maeneo matano yafuatayo:-

Jedwali Na. 4: Makusanyo yaliyopatikana hadi April, 2014 kutokana na marekebisho ya viwango vya kodi

Chanzo: Wizara ya Fedha, 2014

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato kwa maeneo tajwa hapo juu kumesaidia Serikali kupata mapato ambayo kimsingi yasingeweza kupatikana kama marekebisho hayo yasingefanyika. Eneo la kodi zilizokusanywa kwa magari chakavu ambalo limewezesha Serikali kukusanya mapato kwa asilimia 320, limeonyesha kufanya vizuri na limeashiria ni kwa jinsi gani ushuru wa bidhaa zinazokataliwa *(reject goods)* unavyoweza kuleta matunda kwa baadhi ya maeneo. Pamoja na kwamba ushuru wa bidhaa umefanya vizuri katika eneo hilo la ukusanyaji wa mapato kutokana na magari chakavu, athari yake itaonekana kwa jamii kwa kuwa inasababisha uchafuzi wa hali ya hewa na kushusha kipato cha mwananchi wa kawaida ambaye hupoteza kiasi kikubwa cha fedha kwenye kununua vipuri.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa wa Serikali kufikiria kushusha viwango vya kodi kwa magari mapya ili kuwezesha wananchi kununua magari hayo na hivyo kuondokana na athari zitokanazo na matumizi ya magari chakavu kama vile uchafuzi wa mazingira na ununuzi wa vipuri mara kwa mara. Pamoja na hayo Kamati ina taarifa kwamba hatua ya serikali kuongeza kodi kwa magari yenye umri wa zaidi wa miaka 10 ili kupunguza uingizaji wake, wauzaji walishusha zaidi bei ili yaendelee kuwa nafuu kwa wanunuzi wa Tanzania, ikizingatiwa pia kuwa Tanzania ni mnunuzi pekee wa magari yenye umri mkubwa katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa kodi zilizokunywa kutokana na ushuru wa mafuta ya taa na dizeli, ni eneo jipya kabisa na limeweza kuonyesha kufanya vizuri pia. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba maeneo hayo na mengine ambayo hayakufanya vizuri yakiwekewa msukumo zaidi katika ufuatiliaji yataiwezesha Serikali kukusanya mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kodi zilizotakiwa kutozwa baada ya kuondoa misamaha ya kodi kwenye sukari, mchele na ngano hakuna kodi yoyote iliyokusanywa kutoka katika bidhaa hizo. Hali hii imesababisha matarajio ya Serikali kutofikiwa kabisa. Hata hivyo, Kamati imeshindwa kuamini kama ni kweli bidhaa hizo hazikuingizwa nchini katika kipindi hicho kutokana na kuwepo kwa malalamiko kuhusu uwepo wa bidhaa hizo hususan sukari ambayo imezagaa kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo, Kamati inaamini kuwa

bidhaa hizo zimeingizwa nchini kwa njia ya ujanja bila kutozwa kodi na hivyo kuisababishia Serikali hasara ya ukosefu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maghala yanayohifadhi bidhaa hizo, ili kubaini tarehe zilipoingizwa bidhaa hizo na kama zililipiwa kodi. Aidha, Serikali iimarishe ulinzi kwenye mipaka yake, pamoja na ukaguzi wa bidhaa bandarini ili kuepusha uingizaji wa bidhaa nchini bila kulipiwa ushuru.

4.2 MWENENDO WA MATUMIZI

4.2.1 Matumizi ya Serikali kwa ujumla

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Serikali bado ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti. Kamati imebaini kuwa matumizi ya Serikali yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kwamba ni makubwa kuliko mapato. Hali hii imechangiwa na kutokuwepo kwa nidhamu katika matumizi, hali ambayo imejidhihirisha zaidi katika upande wa manunuzi.

Pamoja na kuanza kutumika kwa Sheria mpya ya Manunuzi ya mwaka 2011, bado manunuzi mengi yamekuwa yakifanyika bila tija. Mfano manunuzi ya dharula yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania ambayo hayakupata kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali2.Manunuzi hayo yalikuwa na gharama ya **Dola za Kimarekani 810,000**.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutosimamia kwa umakini matumizi ya serikali ulisababisha bajeti ya mwaka 2013/14 kuanza na deni ***(expenditure float)*** la shillingi **billion 611.4** ambayo ni matumizi ya mwaka wa fedha 2012/13 lakini hayakulipwa mwaka huo na deni hili halikuingizwa kwenye bajeti ya 2013/14.

Hali hii inatarajiwa pia kujitokeza tena kwa kiwango kikubwa zaidi kwenye bajeti ijayo ya mwaka 2014/15. Malimbikizo ya madai hayo hadi Desemba 2013 yalikuwa yamefikia **shilingi trillion 2.093**, ambayo ni asilimia 4 ya pato la taifa. Tatizo hili ni lazima litafutiwe dawa haraka.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyobainika kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha kwenye baadhi ya miradi ni pamoja na: utekelezaji wa miradi chini ya kiwango; miradi kukabidhiwa bila kukamilika; miradi kutumia fedha zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa; taasisi kubadili bei za mikataba ya miradi; na baadhi ya miradi iliyokamilika kutotumika kutoa huduma kwa walengwa kama ilivyopangwa4**.** Pia utoaji fedha kwenda kwenye miradi haukuzingatia vipaumbele vilivyowekwa, kukubalika na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 utekelezaji wa bajeti katika baadhi ya mafungu ulifanyika kinyume na matarajio ya Serikali. Yapo baadhi ya mafungu ambayo hayakutengewa fedha lakini walipewa fedha nje ya bajeti za fungu husika. Hali hii ilisababisha baadhi ya mafungu ambayo yalikuwa yametengewa fedha kutopelekewa fedha kama

walivyopangiwa. Mafungu ambayo yalipokea fedha nje ya bajeti za Mafungu hayo yameoneshwa katika Jedwali Na.5 ya Taarifa hii**:**
Jedwali Na.5: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na zile zilizotumika kwa baadhi ya Mafungu kwa mwaka 2013/14

Chanzo: Wizara ya Fedha,2014
Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mafungu hayo yalitumia fedha za ziada kiasi cha shilingi **bilioni 115.81** ambacho ni sawa na **asilimia 10.3** ya jumla ya fedha ambayo iliidhinishwa kwa mafungu hayo katika mwaka wa fedha 2013/14.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha matumizi ya ziada kimetumika ndani ya miezi tisa ya utekelezaji wa Bajeti. Kutokana na Jedwali Na. 5 ni dhahiri kuwa bajeti za mafungu hayo ziliandaliwa bila kuzingatia mahitaji halisi kwenye mafungu hayo isipokuwa kwa mafungu ya **Fungu 28 – Jeshi la Polisi** na **Fungu 38 – Ngome** ambayo yaliomba fedha za nyongeza wakati wa kupitisha bajeti zao lakini Hazina walishindwa kuridhia kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa Fungu kama vile **Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi** ambalo katika kipindi hicho limetumia fedha za ziada ambazo zingeweza kuwa bajeti ya Wizara mbili, limekuwa miaka yote likitumia bajeti zaidi ya ile iliyoidhinishwa na Bunge. Kamati inauliza je, **ni miaka yote Wizara hii inashindwa kuweka viwango halisi na sahihi vya shughuli zao**?

Mheshimiwa Spika, angalizo la Kamati kuhusiana na matumizi hayo nje ya bajeti halimaainishi kwamba mahitaji hayo yasingegharamiwa, bali ni msisitizo kuhusu umuhimu wa uandaaji wa bajeti halisia *(realistic budget)* na nidhamu ya matumizi. Lakini pia linaikumbusha Serikali kuhusu ushauri ilioutoa mwaka jana kuhusiana na usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti, ambapo Kamati iliishauri Serikali kabla ya kuhaulisha *(reallocate)* fedha kutoka fungu moja kwenda jingine iwasiliane na Kamati ya Bajeti katika msingi ule ule wa mashauriano baina ya Bunge na Serikali ili kuhakikisha nidhamu ya bajeti inazingatiwa**.**

Mheshimiwa Spika, iwapo maafisa Masuuli watashindwa kuweka viwango vya mahitaji yao kibajeti kuwa halisia, na iwapo Hazina itashindwa kuridhia fedha ambazo zinaombwa kama nyongeza kwa mafungu wakati wa kufanya mashauriano na Kamati ya Bajeti basi, matumizi nje ya bajeti halisia yatastahili kudhibitiwa kwa kuanzisha sheria ya bajeti.

4.2.2 Deni la Taifa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi **trilioni 2.735** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia deni la Taifa. Hata hivyo, kiasi cha shilingi **trilioni 3.341** zilitumika katika mwaka huo kugharamia deni hilo. Ugharamiaji wa deni hilo katika mwaka huo ni sawa na ongezeko la shilingi **bilioni 606** ambalo halikuwa kwenye bajeti. Hata hivyo, ongezeko hilo ni pungufu kidogo ya ongezeko lililotumika katika mwaka wa fedha 2011/12 ambalo lilikuwa shilingi **Bilioni 624**. **Kamati hairidhishwi na utaratibu huu**.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya CAG5, imebaini kuwa uhakiki wa mseto wa Deni la Taifa umebaini akaunti saba (7) za wafadhili wanaodai Serikali zenye thamani ya **Sh. 1.247 trilioni** ambazo hazikufanyiwa malipo yoyote tokea mwaka 1998**.** Maelezo yaliyotolewa kuhusu akaunti hizo ni kwamba, malipo yake yamesimama kwa sababu mazungumzo kati ya Serikali na wafadhili yanaendelea kwa nia ya kuipatia Serikali nafuu ya madeni na hata pengine kuyafuta kabisa. Pamoja na kutolewa kwa maelezo hayo, hakuna vielelezo vyovyote vilivyotolewa kuthibisha kuwepo kwa mazungumzo hayo. Hali hii inaonesha kutokuwepo kwa uwajibikaji kuhusiana na madeni yetu.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa hadi kufikia Machi, 2014 lilikuwa limefikia shilingi **trilioni 30.563** ikilinganishwa na shilingi **trilioni 23.67** mwezi Machi, 2013. Pamoja na sababu zilizotolewa na Serikali6, **Kamati hairidhishwa na usimamizi wa deni hilo kwa ujumla. Pia Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa Idara ya Usimamizi wa Deni la Taifa**.

4.2.3 Malimbikizo ya Madai (watumishi na wazabuni)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la malimbikizo ya madeni katika Wizara na Idara za Serikali. Katika hali ya kawaida, inatazamiwa kwamba Wizara na Idara za Serikali zitatumia fedha kulingana na bajeti iliyopangwa. Hata hivyo, hali hii imekuwa haitekelezeki kwa sababu mbalimbali zikiwemo ucheleweshwaji katika upatikanaji wa fedha za Bajeti. Endapo Wizara na

Idara zitaendelea kutumia huduma, ama kulazimika kufanya hivyo bila kulipia, hali hii hutengeneza deni ambalo kama fedha za mwaka husika zisipotolewa, deni hilo huathiri bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa madai hayo yataachiwa mafungu husika yaingie nayo katika mwaka wa fedha ujao. Suala hili linaendelea kuathiri bajeti ya mwaka husika na hivyo kuwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti. Kwa maana nyingine ni **kwamba bajeti zetu mwaka hadi mwaka zimekuwa zikitumika kwa kiasi kikubwa kulipa madeni badala ya kutekeleza mipango iliyopangwa katika mwaka husika**. Matokeo yake ni kutokamilika kwa wakati kwa miradi mingi lakini pia kuiongezea Serikali gharama pale ambapo miradi iliyopangwa kutekelezwa kuchelewa kukamilika au kutokamilika kabisa. **Katika eneo hili Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa Serikali kuzitaka wizara na Idara za Serikali kuwa na kasma ya kulipia madeni yao kutoka katika mafungu yao ili kuondokana na utaratibu wa kuyaficha madeni hayo na kuacha yalipwe kwa kutumia bajeti ya mwaka wa fedha unaofuta**.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine lililogusa hisia za wajumbe kuhusu matumizi ni kwenye Balozi zetu zilizopo nje ya nchi. Ofisi hizi huendesha shughuli zake kwa kujitegemea na kasma zake husimamiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kamati imebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2012/13 baadhi ya balozi zilitumia fedha zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge. Kati ya balozi 32, balozi 16 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, zilionesha kutumia fedha nje ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge ambacho ni **Shilingi bilioni 6,227,749,594** kwa malipo ya mishahara kwa watumishi waliostaafu7 ya shilingi milioni 575.47 yaliyohusisha balozi tatu; baadhi ya watumishi kukaa zaidi ya muda wa mikataba yao ya miaka minne.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba baadhi ya Balozi zetu zimekuwa zikilalamika kuhusu ukarabati wa balozi zao lakini inashangaza kuona kwamba zinakua miongoni mwa zinazokuwa na matumizi makubwa zaidi ya kiwango wanachoidhinishiwa na Bunge. Mfano ubalozi wa Maputo ni miongoni mwa Balozi ambazo zinahitaji ukarabati katika ofisi zake na waliwasilisha maombi ya fedha za nyongeza kwa ajili ya ukarabati. Katika mwaka wa fedha, 2012/13 Ubalozi huo umetumia kiasi cha shilingi 117,400,068 nje ya bajeti iliyotengwa. Pamoja na kwamba maelezo kuhusu matumizi hayo hayakuwekwa bayana katika ripoti ya CAG, Kamati inashauri kuwa matumizi yote yanayofanyika nje ya bajeti iliyotengwa yawekwe bayana, na maafisa masuuli wazingatie kufanya matumizi yanayoendana na bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kidiplomasia hasa sekta ya uchumi, Kamati inashauri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuzingatia ushauri uliotolewa na CAG kuhusu kuanzisha mfuko katika Fungu lake kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii. Kwa kutambua kuwa Kamati imekuwa ikiihimiza Serikali kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato, katika eneo hili Kamati inaona kwamba suala hili litakuwa kichocheo katika kukusanya mapato yatakayosaidia katika kugharamia mahitaji ya balozi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imepokea taarifa kuhusuiana na kushindwa kufikia makubaliano kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii NSSF na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu ujenzi wa majengo ya balozi zilizo nje ya nchi.

Moja ya jukumu la Bodi ya Wadhamini ya Mifuko ya Jamii ni kuhakikisha kwamba mtaji unaongezeka kupitia faida zitokanazo na uwekezaji kwenye vitega uchumi mbalimbali ikiwepo milki *(real estate)*. Hivyo, ubia baina ya Serikali na Mifuko hiyo una faida kwa pande zote mbili, kwamba Serikali itapata miundo mbinu inayohitaji kwa ajili ya ofisi na makazi ya watumishi wa balozi zake pamoja na kodi itakayolipwa kutokana na faida, na mifuko husika itapata faida na hivyo kuongeza mtaji wao.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha mazungumzo baina ya mifuko ya hifadhi jamii na Wizara ya Mambo ya nje ili kukamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba za watumishi katika balozi zetu za Nairobi na Maputo.

Kukamilika kwa ujenzi wa majengo hayo kutaipunguzia serikali mzigo wa kodi ya pango na itapata fedha za ziada kuhudumia balozi zetu zilizo kwenye nchi nyingine. Aidha, Serikali iharakishe kulipa deni lililobakia kwa Serikali ya New Zealand iliyotuuzia jengo nchini Ufaransa.

5.0 BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2014/15

5.1 Sura ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi bilioni 19,853.3** kutoka vyanzo mbalimbali na kwa mahitaji yaliyoainishwa. Jedwali Na 6 (pie chart) katika Taarifa ya Kamati limetoa sura halisi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15 kama linavyosomeka:-
Jedwali Na.6. Sura halisi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15

5.2 Mapato ya Ndani

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 Kamati imebaini kuwa lipo tatizo la kimsingi tokea siku ya kwanza bajeti hiyo inapoanza kutekelezwa, ambalo ni kwamba:

- Mapato yote ya ndani ni **shilingi trillion 12.44**;
- matumizi yote ya kawaida ni **shilingi trillion 13.408**;
- Mapato ambayo Serikali itakusanya ni **asilimia 63.3** tu ya bajeti yote;
- Nakisi ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 968**;
- Nakisi hii haijumuishi *expenditure float* (wastani wa **shilingi bilioni 611**8)
- Mikopo na Misaada ya kibajeti inahitajika kulipia sehemu ya matumizi ya kawaida
- Bajeti ya maendeleo ni **shilingi trilioni 6.445**

· Nakisi hiyo inazibwa na mikopo ya ndani, mikopo ya nje na misaada ya miradi ya maendeleo

5.3 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 imebaini pia kuwa kuna tatizo la kimsingi kutokea siku ya kwanza Bajeti inapoanza kutekelezwa kwenye upande wa matumizi kama ifuatavyo;

· Deni la taifa ni **shilingi trilioni 4.354** (21.93% ya bajeti yote)

· Mishahara ni **shilingi trilioni 5.317** (26.78% ya bajeti yote)

· Matumizi mengineyo (OC) ni **shilingi trilioni 3.735** (18.82% ya bajeti yote)

· Jumla ya **Matumizi ya Kawaida** ni shilingi **trilioni 13.408** (**67.54%** ya Bajeti yote)

· Misaada na mikopo ya kimaendeleo ni **shilingi bilioni 2,019.4** (***10.2%*** *ya bajeti yote*)

· Misaada na mikopo ya kibajeti ni **shilingi bilioni 922.2** *(**4.6%** ya bajeti yote*)

· Mikopo ya Miradi ya maendeleo ni **shilingi bilioni 1,745** (**8.79%** ya bajeti yote)

· Mifuko ya pamoja ya Kisekta ni **shilingi bilioni 274.1** *(**1.38%** ya bajeti yote*)
·**Miradi ya Maendeleo** imetengewa shilingi **trilioni 6.445** (**32.46%** ya bajeti yote)

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa Serikali itoe mchanganuo wa kuonesha kiasi halisi cha misaada na mikopo ya kibajeti itakayopokelewa ili kuweka bayana takwimu hizo zinazoeleza kwamba misaada na mikopo ya kibajeti ni **shilingi bilioni 922,168**, na Mikopo na Misaada ya Miradi ya Maendelo ni shilingi **bilioni 1,745.39** bila kuchanganua kiasi cha misaada na mikopo.

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia kwa makini sura ya bajeti, utaona kwamba makadirio ya makusanyo ya ndani ya **shilingi trilioni 12.44** hayatoshi kugharamia mahitaji ya Mishahara **(trilioni 5.317)**, Deni la Taifa **(trilioni 4.354)** na Matumizi yasiyoepukika **(Trilioni 3.063)** ambayo kwa ujumla yanatupa kiasi cha **shilingi trilioni 12.734.** Hivyo makusanyo yetu ya ndani ya kodi ni pungufu kwa **shilingi trilioni 0.294.**

6.0 MAONI YA KAMATI KUHUSU BAADHI YA HATUA ZA KODI ZINAZOPENDEKEZWA NA SERIKALI KWA MWAKA 2014/15

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri maelezo yaliyotangulia, Kamati ya bajeti inaipongeza Serikali kwa kufanya maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato kwa kurekebisha sheria takribani 13 ambazo zitapelekea kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kuweza kuhudumia wananchi ipasavyo na kufikia malengo ya kiuchumi katika mwaka wa fedha wa 2014/15. Pamoja na hatua hizo nzuri za Serikali, Kamati ya Bajeti inatoa maoni katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kodi ya zuio ya asilimia 15 kwenye ada wanayolipwa wakurugenzi wa bodi kila mwisho wa mwaka iangaliwe upya kwa kuwa, Kodi ya zuio (WHT) kwa washauri binafsi ni asilimia 5 kwa kila mwisho wa mwaka.

(ii) Kwa upande wa kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Kamati haijaridhika na punguzo hili, hivyo inashauri Serikali kupunguza kiwango hiki hadi kufikia tarakimu moja (single digit) kwa mwaka ujao wa fedha.

(iii) Viwango vya ongezeko la kodi kwa wafanyabiashara wadogo kwa mapato ghafi yanayozidi shilingi milioni 4 kwa mwaka na yasiyozidi milioni 7.5 kwa mwaka kutoka asilimia 2 hadi 4 kwa mauzo kwa wenye kumbukumbu za mauzo; na kwa kuongeza kutoka laki 1 hadi shilingi laki 2 kwa wasikuwa na kumbukumbu za mauzo. Viwango hivi ni mara mbili ya viwango vya awali. Kamati ina maoni kuwa viwango hivi vitakatisha tamaa wafanyabiashara wadogo wanaolipa kodi na hivyo kutafuta mbinu za kukwepa kulipa kodi, na wale ambao bado hawajajiandikisha hawatajiandikisha kamwe na hivyo kusababisha Serikali kuokosa hata kile kidogo kilichotegemewa kupatikana. Kwa msingi huo Kamati inashauri:-

(a) Serikali kupunguza kodi iliyopendekezwa ifikie asilimia 3 badala ya 4 kwa wafanyabiashara waliosajiliwa. Kodi kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa ibakie shilingi laki moja.

(b) Mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo wadogo yaboreshwe ili kuvutia wafanyabiashara wadogo wadogo kujitokeza na kusajiliwa.

(iv) Kubadilisha ukomo wa umri wa magari yasiyo ya uzalishaji (non-utility vehicles) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia 25 hivi sasa kutoka miaka kumi na zaidi kwenda miaka minane. Kamati inatambua kuwa nia ya Serikali ni kulinda mazingira ya nchi yetu, kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa magari na kupunguza ajali. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuwa na sera mahsusi ya kodi itakayohamasisha wananchi kununua magari mapya badala ya chakavu kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwa magari mapya.

(v) Kuhusu Kurekebisha viwango maalum (specific rates) vya Ushuru wa Bidhaa zisizokuwa za mafuta (Non-petroleum products) kwa asilimia 10; vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali, n.k. Kwa kuzingatia kuwa vinywaji baridi ni sehemu ya mahitaji muhimu ya binadamu, Kamati inashauri kuwa pendekezo la ongezeko la asilimia 10 kwa bidhaa hizo liondolewe. Aidha, kuhusu bidhaa za Sigara kutozwa Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 25 ili kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku (Framework Convention on Tobacco Control) wa Shirika la Afya Duniani, Kamati inaona kuwa kila mwaka kodi katika bidhaa hizi zinaongezeka na kulalamikiwa na wananchi. Ni vema Serikali ikatambua kuwa uvutaji wa sigara na hata unywaji pombe kwa baadhi ya watu hauwezi kuzuiwa/kupunguzwa kwa bei kubwa. Baadhi ya watu, hasa walio katika vipato vya chini, wataendelea kunywa na kuvuta kwa sababu mbalimbali kama vile *addiction* na msongo wa mawazo matokeo yake ni kuendelea kuongeza umasikini zaidi kwa na familia zao hasa kwa wale wa vipato vya chini. Hali kadhalika, kama hali itaendekea kuwa hivi kila mwaka kuna hatari ya Serikali kupoteza wawekezaji katika sekta hizo.

(vi) Ni muhimu kuzingatia kuwa ushuru wa leseni haupaswi kuwa kama chanzo cha mapato tu bali pia ni utambulisho na nyenzo ya kuwezesha kuanzisha, kuendeleza na kukuza biashara na hivyo kupanua wigo wa kodi. Kamati inashauri kuwa, Serikali iangalie vizuri marekebisho ya viwango vya ushuru wa leseni za biashara inayotegemea kutoza.

(vii) kwa upande wa sheria ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni muhimu kujua hali halisi ya Tanzania katika aina mbalimbali za ushuru uliopunguzwa na kama kwa kupunguzwa kwa viwango vya ushuru huu kwa muda uliotajwa (mfano mwaka mmoja zaidi) wazalishaji wa Tanzania wanajiandaa au wanaandaliwa vipi kuweza kuwa kuumudu ushindani.

7.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina kuhusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15, yafuatayo ni maoni na ushauri wa jumla wa Kamati ya Bajeti:-

7.1 Nidhamu ya matumizi ya fedha za umma

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Serikali kuahidi kwamba itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati kuhusu usimamizi na nidhamu ya matumizi bado hakuna mabadiliko ya kuonesha ushauri wa Kamati na Bunge lako tukufu kwamba umezingatiwa. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba ushauri iliyotoa wakati wa kuchambua na kupitia Bajeti ya serikali ya mwaka 2013/14 ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ushauri wa Bunge lako tukufu juu ya matumizi yasiyokuwa ya lazima, Serikali ilianzisha Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu kwa madhumuni ya kuimarisha kaguzi za ndani katika wizara, idara na taasisi, sekretariati za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati za Bunge wakati zikichambua mapato na matumizi ya Serikali hazikuona mabadiliko yoyote katika kudhibiti mapato na matumizi ya Serikiali. Aidha taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinadhihirisha hili.

7.2 Misamaha ya Kodi

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha siku nyingi cha Wabunge kuhusiana na hatua ya kupunguza baadhi ya misamaha ya kodi ambayo haina tija. Pamoja na lengo zuri la Serikali la kupunguza misamaha ya kodi kwa hatua kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua hizo bila kuathiri hatua nyingine za kuhamasisha uwekezaji nchini kama ilivyoelezwa na Serikali10.

7.3 Madeni ya Mifuko ya Pensheni

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya CAG unaonesha kuwa Serikali imeendelea kukopa kutoka kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya kutekeleza miradi na mahitaji mbalimbali. Hata hivyo, kiasi kinachorejeshwa na Serikali ni kidogo sana. Ikumbukwe kwamba, fedha za mifuko ni za wanachama wa mifuko husika, hivyo kutorejeshwa kwa wakati kwa fedha hizo kutasababisha mifuko husika kushindwa kulipa pensheni kwa wanachama wake watakaokuwa wanastaafu kwa kiwango wanachostahili. **Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 Mifuko hii ilikuwa ikiidai Serikali takribani zaidi ya shilingi trilioni 3. Kamati inahimiza Serikali kuweka utaratibu endelevu wa kulipa madeni hayo**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa PSPF Serikali inadaiwa kiasi cha **shilingi trilioni 3.3** ikiwa ni malimbikizo ya pensheni ya wanachama hadi kufikia Juni 1999. Serikali imekuwa ikilipa **shilingi bilioni 50** kila mwaka ambacho ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na kiasi inachodaiwa. Kamati inashauri Serikali itumie utaratibu wa malipo kwa fedha taslimu na hati fungani ili kuokoa mfuko na hatari ya kufilisika. Aidha, Kamati inatambua kuwa Serikali imekuwa ikichangia asilimia 15 ya mshahara wa mtumishi kwenye mfuko wa PSPF, hata hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na mzigo ambao Mfuko utabeba baada ya mtumishi kustaafu. Hivyo, Kamati inashauri Serikali iongeze kiwango cha michango kwa watumishi wa Serikali kufikia asilimia 20 ili kufanya jumla ya mchango wa wanachama kuwa asilimia 25 ya mshahara wake.

7.4 Madeni makubwa ya Serikali

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2013/14 umebaini kuwepo kwa madeni makubwa katika baadhi ya Wizara na taasisi za umma. Mfano Wizara ya Ujenzi ambayo

imekuwa ikitekeleza miradi ya ujenzi wa barabara bila kuwalipa wakandarisi kwa wakati kwa kuzingatia mikataba yao na hivyo kujikuta ikianza kila mwaka wa fedha ikiwa na malimbikizo ya makubwa ya madeni. Hali hii imesababisha Wizara hii kutumia bajeti yake ya mwaka unaofuata kulipia madeni ya mwaka uliopita badala ya kutekeleza iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika *(current FY)*. Kamati inashauri Serikali itoe agizo kwa maafisa Masuuli wote kulipa madai ya wazabuni kwa wakati ili kuepuka kuzalisha madeni ambayo yanaigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha na kusababisha hasara kwa wakandarasi kwa kuwapunguzia uwezo wa mitaji yao. Kwa madeni ya wizara na taasisi ikiwemo TANESCO ambayo yamelimbikizwa hadi sasa Kamati inashauri Hazina iyafanyie uhakiki na madai hayo kuyalipa mapema.

7.5 Vyanzo vipya vya mapato

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15 uliofanywa na Kamati umeonesha kwamba mzigo wa matumizi ni mkubwa mno ikilinganishwa na vyanzo vya mapato vilivyopendekezwa. Serikali imekosa ubunifu na haitaki kupokea ushauri kuhusiana na vyanzo vipya vya mapato, kwa kuwa imekuja na vyanzo vile vile vya kitamaduni vilivyozoeleka wakati kuna vyanzo vingine vingi. Vyanzo hivi ni pamoja na vilivyopendekezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaoendelea, Mapendekezo ya Maabara ya BRN na Kamati ya **Chenge I** pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti. Kamati inaendelea kuhimiza Serikali kufanyia kazi mapendekezo na ushauri uliotolewa ili **kupunguza nakisi ya bajeti na mzigo kwa walipa kodi wale wale**.

7.6 Mchango wa washirika wa Maendeleo katika bajeti ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wamekuwa wakichangia takribani asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali. Mwelekeo walionao hivi sasa ni wa kuhama kutoka kuchangia katika mfuko wa pamoja wa bajeti na kwenda kuchangia katika miradi ya kisekta yenye sura ya kibiashara. Kwa kutambua kuwa Bajeti ya Serikali bado ni tegemezi kwa kiasi kikubwa, Kamati inashauri Serikali kujiandaa kupokea utaratibu huo mpya kwa kuhakisha kwamba inaainisha miradi muhimu ambayo itakuwa na matokeo makubwa ili iweze kutekelezwa mara moja kupitia utaratibu huo kwa lengo la kupata matokeo makubwa sasa.

7.7 Uagizaji wa bidhaa kwa pamoja *(Bulk procurement)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa uagizaji wa pamoja katika sekta ya mafuta umekuwa na mafanikio makubwa, Kamati inashauri utaratibu huu utumike kwa bidhaa nyingine zinazotoka nje kama vile sukari, mchele na saruji n.k zinazoingizwa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika,kwa kuwa utaratibu wa bajeti kusubiri serikali ikusanye mapato kwanza ndiyo yasambazwe kwa watekelezaji huchelewesha sana utekelezwaji wa miradi na bajeti husika, Kamati inaishauri Serikali kufikiria kwa umakini na uharaka ushauri kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2014/15 Serikali ianzishe utaratibu kukopa ama 'kuazima' fedha toka vyanzo mbalimbali nafuu za kutekeleza bajeti ya serikali kwa kiwango cha kufikia walau robo moja, yaani **shilingi trillion 5** ya bajeti ya mwaka. Utaratibu huu huitwa ***capital budget*** badala ya utaratibu wa ***cash budget***, ambao umetumika kwa muda mrefu sasa wakati ulitakiwa kuwa mpango wa mpito.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa kuharakishwa kuletwa Bungeni **sheria ya bajeti itakayofanya kazi sambamba na sheria 'mpya' ya manunuzi** ili kudhibiti matumizi mabaya kinyume na sheria na kanuni kwa nia ya kuweka nidhamu katika utekelezaji wa bajeti ya serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Serikali kutazama upya ufanisi wa utoaji maamuzi stahili kwa muda. Hali hii inaligharimu sana taifa letu. Mifano iko mingi.

8.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi wetu unatakiwa ushuke na uwafikie wananchi waliowengi kuliko ilivyo hivi sasa. Yanahitajika maono, dhamira na ubunifu kuweza kufanikisha lengo hili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti umeonesha kwamba bajeti imejaribu kugusa watu wa chini lakini katika mfumo ambao kwa namna fulani unaonekana kuwa na changamoto. Ni dhahiri kuwa mapendekzo ya mifumo ya kodi na tozo mbalimbali zilizoainishwa zinaonesha nia ya serikali katika kutaka kuongeza mapato lakini baadhi ya mapendekezo hayo yana ugumu ndani yake.
Mheshimiwa Spika,ongezeko la Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/15 kwa kiasi cha **shilingi trilioni 1.605**, ikilinganishwa na Bajeti ya Serikali inayomalizika ya mwaka 2013/14 ongezeko hili linatia mashaka iwapo malengo ya ukusanyaji na matumizi yatafanikiwa. Inahitajika nidhamu kubwa ya utendaji ili kuweza kufikia malengo haya kwa upande wa Serikali.

9.0 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Saada Mkuya, Mb, Naibu Waziri wake Mhe. Adam K. Malima, Mb na Mhe. Mwigulu L. Nchemba, Mb kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Namshukuru pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Mahusiano na Uratibu Mhe. Stephen Wassira , Mb kwa kushirikiana vyema na Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Hazina na Tume ya Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Andrew J. Chenge, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dr Festus B. Limbu, Mb -Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Amour, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dr. Cyril Chami, Mb - "
5. Mhe. John M. Cheyo, Mb - "
6. Mhe. Mansoor Hiran, Mb - "
7. Mhe. Josephat Kandege, Mb - "
8. Mhe. Christina M. Lissu, Mb - "
9. Mhe James Mbatia, Mb - "
10. Mhe. Godfrey W. Mgimwa, Mb - "
11. Mhe Assumpter Mshama, Mb - "
12. Mhe. Dkt. Goodluck J. Ole-Medeye, Mb - "
13. Mhe. Hamad Rashid, Mb - "
14. Mhe. Kidawa Saleh, Mb - "
15. Mhe. Joseph Selasini, Mb - "
16. Mhe. Saleh Pamba, Mb - "
17. Mhe Beatrice Shelukindo,Mb - "
18. Mhe Ritha Mlaki, Mb - "
19. Mhe Peter Serukamba, Mb - "

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukuhakishia wewe, Bunge lako Tukufu, na Watanzania kwa ujumla kwamba kazi iliyokuwa mbele yetu haikuwa rahisi, ilikuwa ngumu sana, ukizingatia kuwa Kamati hii ni mpya. Kamati imefanya kazi kwa kujituma, kwa muda mrefu mfululizo bila kupumzika. Ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa D. Mbise na Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto na Michael Kadebe kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Andrew J. Chenge, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
16 Juni, 2014

NAIBU SPIKA: Naomba tumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa Hotuba yake, yeye pamoja na Kamati yake ya Bajeti, kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kipindi chote ambacho tumekuwa hapa Bungeni. Wamekuwa wakikutana bila kuchoka, kwa muda mrefu sana wakitusaidia kuweka sawa sawa masuala mazima ya bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya muda si mrefu sana tuaanza uchangiaji kama nilivyosema mwanzoni, lakini nawaomba sana mtakaokuwa mnachangia, ni vizuri mkaipitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mahusiano na Uratibu, ambayo inaendana na masuala ya mipango ya nchi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/15; lakini vilevile mkaipitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayohusu Bajeti; na pia mkaipitia Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili kuona uchambuzi wake umekuwaje.

Baada ya Mwenyekiti wa Bajeti kumpa saa moja, Upinzani nao wanayo saa moja ya kuweza kutoa maoni yao kuhusiana na suala lililo mbele yetu. Kwa hiyo, moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Esther Matiko, ambaye yeye atakuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya upinzani, akiwasilisha Bungeni, Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/15. Mheshimiwa Esther Matiko; karibu sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Esther Matiko, hajawahi kusoma maoni mbele hapa, karibu sana, unazo dakika ishirini.

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Fedha kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. ESTHER N. MATIKO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/15, kwa mujibu wa Kanuni ya 105(8) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu). *(Makofi)*

Kipekee, napenda kuishukuru familia yangu, mume wangu mpendwa na watoto wangu, kwa kunitia moyo katika kazi zangu za Kibunge na Kichama. Aidha, nawashukuru Wananchi wote wa Mkoa wa Mara hususan wa Wilaya ya Tarime, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Hotuba hii inukuliwe na *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/15 ni Sehemu ya Nne ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16) kama ulivyopitishwa na Bunge hili na pia ni Sehemu ya Kwanza ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Dira 2025 imeundwa na nguzo kuu tano ambazo ni kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; kuweka mazingira ya amani, usalama na umoja; kujenga utawala bora; kuwepo jamii iliyoelimika vyema na kujifunza kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya msingi ni kwa kiasi gani Serikali ya CCM imefanikisha utekelezaji wa nguzo ya kwanza ya Dira 2025, ambayo ni kuboresha hali ya maisha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unasema wazi kuwa, Sera ya Matumizi haioneshi msisitizo maalum wa kupunguza matumizi yaendane na makusanyo ya ndani. Aidha, lile lengo la kutumia asilimia 22 ya makusanyo ya ndani kwa matumizi ya kawaida limeshindikana kabisa.

Kwa mwaka wa fedha 2014/15 makusanyo ya ndani ni shilingi trilioni 12.17 na matumizi ya kawaida inaonesha kuwa ni shilingi trilioni 13.408. Aidha, hili linajidhihirisha wazi katika Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kama kweli Serikali inataka kufikia Malengo ya Milenia, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia matakwa ya mpango katika matumizi kwenye Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda Wananchi wafahamu kwamba, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya 2014/15 yaliyoletwa na Serikali ili yajadiliwe na Bunge hili ni ya nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Kwa maneno mengine ni kwamba, imebaki miaka miwili tu kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda pia kuwajulisha Wananchi kwamba, wakati imebaki miaka miwili tu kwa Serikali kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, umebaki mwaka mmoja tu kwa upande wa CCM kukamilisha utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM ya Mwaka 2005 inasema, naomba kunukuu: "Kukuza uchumi kwa kiwango cha zaidi ya asilimia kumi kwa mwaka ifikapo 2010 kutoka ukuaji

wa sasa wa asilimia sita nukta saba. Pia Kuanza kupunguza umaskini kwa watu wetu kwa namna iliyo dhahiri." Haya yalikuwa ni malengo ya kufikia mwaka 2010, ambapo hadi sasa uchumi haujafikia asilimia kumi, pia asilimia zaidi ya 28.8 ya Watazania wote wanaishi chini ya mstari wa umaskini *(below the poverty line),* kwa takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2012, hii ni sawa na Watanzania takribani milioni 12 wanaishi *below the poverty line*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti, Serikali haijafanikiwa kuwa na bajeti yenye uhalisia wa kupunguza umaskini wa Watanzania, kwani Bajeti inayolenga kupunguza umaskini ni ile ambayo inalenga kupunguza mzigo wa kodi kwa Wananchi, ambayo inalenga kutoa ajira nyingi kwa Wananchi, ni ile ambayo inakuza uwekezaji hasa wa ndani, ni ile inayomfanya Mtanzania aweze kuweka akiba *(savings),* ni ile ambayo inalenga kuinua maisha ya walio wengi ambao wako vijijini, ni ile inayolenga uchumi umilikiwe na Watanzania na ni ile inayolenga kukuza ujasiriamali na ile inayokuza ulaji *(increased consumption)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bajeti zote tangu tuanze utekelezaji wa Mpango wa Taifa, pia utekelezaji wa ilani ya CCM, na kwa kuwa sisi wote tunayo nia ya kuwaondoa Watanzania katika umaskini, ni kwa vipi sasa Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa mipango yote inaendana na sera zetu za bajeti ili tuweze kuoanisha mipango na utekelezaji wake? Kama wataalamu tunao, rasilimali tunazo, na kama kweli tunayo nia ni kwa vipi tunashindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali iliambie Bunge lako nini kikwazo cha kutekeleza mpango wa maendeleo au ni hila za CCM kuwafanya Watanzania waendelee kuwa maskini kwa maslahi yao ya kisiasa? Ni vyema bila kujali itikadi zetu, tuungane pamoja kwa nia ya kuwatoa Watanzania katika umasikini mkubwa, kwani ni ukweli kwamba hawatakiwi kuwa katika umasikini huu, ukilinganisha na utajiri wa nchi hii ulivyokuwa mkubwa. Hali hiihaikubaliki, inabidi sasa tuanze kufikiria kutanzua kitendawili hiki kwa kuwa nchi tajiri sana, tuna rasilimali nyingi sana na watu wake ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sura ya Tisa, Ibara ya 212 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010, inasema kwamba; Chama cha Mapinduzi katika miaka mitano ijayo (2010 - 2015), kinaelekeza nguvu kubwa katika kutimiza lengo la msingi la Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, kwa kuendeleza jitihada za ujenzi wa uchumi wa kisasa na Taifa linalojitegemea. Katika kuzingatia jukumu hilo, Ilani ya CCM ya 2010 hadi 2015, inatangaza nia ya modenaizesheni ya uchumi. Kwa maana ya modenaizesheni ya uchumi ndiyo njia ya uhakika itakayobadili na kuleta mapinduzi katika uchumi wa nchi, kujenga msingi wa uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda, kuondoa umaskini wa Wananchi wetu kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Wananchi wapime na kufanya tathmini wenyewe juu ya mambo yafuatayo; je, miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa Upande wa Serikali na miaka minne ya Utekelezaji wa Mpango huo huo kwa upande wa CCM imeleta mabadiliko katika maisha yao kama ilivyokusudiwa kwenye Mpango huu na Ilani yao ya Chama cha Mapinduzi?

Je, ni kweli kwamba mkakati wa CCM wa kufanya Mapinduzi ya Uchumi (modenaizesheni ya uchumi), uliotangazwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 umefanikiwa? Je, ni kweli kwamba msingi wa Uchumi wa Tanzania unaongozwa na viwanda kama CCM ilivyoahidi kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya 2010?

Je, ni kweli kwamba umaskini wa Wananchi umepungua zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama CCM ilivyoahidi kupunguza umaskini kwa Wananchi na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania?

Je, ni kweli kwamba sasa hivi Tanzania ina uwezo zaidi wa kujitegemea kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo CCM iliahidi kwamba kabla ya 2015 Tanzania itakuwa na uchumi imara na hivyo kujitegemea?

Je, hali ya ajira hasa kwa vijana ni bora zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo Serikali ya CCM iliahidi kutoa ajira ili kupunguza umaskini wa kipato?

Je, ni kweli kwamba ugumu wa maisha kwa Wananchi umepungua zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo Serikali ya CCM ilivyoahidi?

Je, bajeti za Serikali kwa miaka minne iliyopita imeweza kuondoa tatizo la umasikini kwa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/15 ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao nao ni sehemu ya kwanza kati ya sehemu tatu za mipango ya nchi kufikia maendeleo ya mwaka 2025. Lengo la ujumla la sehemu ya kwanza ya Dira ya 2025 ni kutoa fursa ili hazina ya rasilimali za nchi zitumike ipasavyo kwa kuweka mazingira wezeshi na kutanua wigo wa ukuaji wa uchumi ili maskini waweze kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kurudia kauli ambayo tumekuwa tukiieleza Serikali kuwa Mpango mzuri haupimwi kwa vigezo vya jinsi Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kilivyopangwa vizuri, maneno mazuri yaliyomo katika hotuba hiyo au nadharia ya malengo ya kisiasa yanavyonyumbuliwa katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utengaji wa asilimia kati ya 25 na 30 ya bajeti kuanzia mwaka 2012 hadi sasa kwa matumizi ya maendeleo ni kwenda kinyume cha Mpango wa Maendeleo, ambao umeeleza vyema kwamba, utekelezaji wa sehemu ya kwanza ya mpango wa miaka mitano, Serikali itenge si chini ya asilimia 35 kila mwaka kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango mzuri wa Maendeleo kimsingi ni takwimu ya jinsi tarakimu za mapato na matumizi zilivyopangwa na utekelezaji wake. Kinyume na hapo, Mpango uliowekwa vizuri kwenye Hotuba bila ya kuwepo kwa mkakati wa utekelezaji wa Mpango huo ni kazi bure. Kwa sababu hiyo, Hotuba ya Kambi Rasmi kwa mwaka huu, inajikita katika uchambuzi wa takwimu mbalimbali zilizomo katika Mpango uliopita na Mpango wa mwaka huu wa fedha ili kuonesha kwa jinsi gani Mpango unaoletwa na Serikali usivyokuwa na mashiko katika utekelezaji wake; kwani fedha za utekelezaji ndiyo kigezo kikuu cha kutuonesha tutokako, tulipo na wapi tunakokwenda kama nchi. Aidha, kigezo hiki ndicho pia kinaonesha kama vipaumbele vyetu viko sahihi, kama tunasimamia fedha na rasilimali zetu vizuri, kama tunachukua hatua wakati mwafaka ili kudhibiti ubadhirifu, wizi na ufisadi au la tunaendelea kuwa kama ni *business as usual.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2013/14: Kitendo cha kutenga asilimia 30 ya bejeti toka mwaka 2012 hadi mwaka huu, kama fedha za maendeleo, ni kinyume na matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kifungu cha 4.5.1, ambacho kinasisitiza kutenga si chini ya asilimia 35 ya Bajeti Kuu. Upungufu huu maana yake ni kwamba, tuko nyuma sana katika kufikia Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa mara nyingine, kukusanya mitaji ya ndani kutoka kwa Watanzania wenyewe kwani Miradi mingi ni kwa ajili ya maendeleo yetu na hili linaondoa dhana nzima ya uchumi inayoitwa *the tragedy of the common.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali wa Maendeleo kwa Mwaka 2013/14 ulikuwa ni kuzingatia vipaumbele vilevile vya Mpango wa Miaka Mitano ambavyo ni Miundombinu, Kilimo, Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani, maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi, na mwisho ilikuwa ni uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa za Serikali zinaonesha kuwa, kumekuwepo na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha unaoishia mwezi Juni. Jambo la ajabu ni kwamba, takwimu za Wizara ya Fedha zinaonesha kwamba, utekeleza wa bajeti kwa fedha za maendeleo kwa fedha za ndani hadi mwezi Mei, fedha zilizotolewa ni asilimia 52.2 tu na fedha za nje ni asilimia 39.6 tu na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo zilizopatikana kuwa asilimia 46 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona taarifa za serikali zinajaa hadaa kwa Wananchi kwa kuwasilisha takwimu na tathmini zisizo halisi na zenye kudanganya Umma. Kwa ujumla, taarifa hizi zinalenga kuonesha aidha mafanikio makubwa yamefikiwa na Serikali katika kutoa huduma kwa jamii au kuonesha kukamilisha Miradi ya Maendeleo kwa kiasi kikubwa huku uhalisia ukiwa ni tofauti kabisa na yanayoandikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Utekelezaji Miradi ya Maendeleo ya Mwaka 2013/14, ukurasa wa nane, inaonekana kuwa katika Sekta ya Kilimo mafanikio mengi yamepatikana kwa kutaja mambo yasiyopimika na hasa yasiyo na uhusiano na vipimo vya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Sekta ya Kilimo hupimwa kwa kuangalia mambo yafuatayo: Uzalishaji katika mazao ya kilimo, mchango wa uzalishaji huo wa kilimo kwenye Pato la Taifa, upatikanaji wa masoko kwa mazao ya kilimo, bei ya mazao kulingana na faida kwa wakulima na kufikika kwa masoko, lishe na uhakika wa chakula kwa familia na Taifa unaotokana na mafanikio ya uzalishaji, maboresho ya mbinu na pembejeo za uzalishaji katika sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Taarifa za serikali zinaongelea mambo tofauti na ambayo yanawahadaa Wananchi kufikiria kuna mafanikio ambayo kwenye uhalisia hayapo. Hivi sasa tunashuhudia kuendelea kudorora kwa mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa, ambapo sasa ni 4.3 tu ikilinganishwa hata na ile asilimia 4.6 ya mwaka 2008. Ieleweke kwamba, licha ya kilimo kuwa nguzo muhimu katika uchumi wetu na kwamba Watanzania takribani asilimia 80 wanategemea kilimo katika kuendesha shughuli zao za maendeleo, sekta hii ndiyo inachangia mchango mdogo zaidi kwa sekta zilizobakia ukiachia uvuvi nao ambao unahujumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya Bajeti ya Maendeleo kwenye Sekta ya Kilimo, kwa miaka kati ya 2010/11 hadi 2013/14, imekuwa inakwenda kwenye Idara ya Maendeleo ya Mazao na kufuatiwa iliyokuwa Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi. Ni kweli kwamba, Idara zote hizi ni muhimu, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kama fedha hizo zingelikuwa zinaingizwa moja kwa moja kwenye Benki ya Kilimo na wakulima kukopa, ni dhahiri kilimo kingekuwa na tija zaidi kuliko ilivyosasa kwani thamani ya fedha hizo kwenye kilimo haionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kilimo ndiyo Sekta Kiongozi katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni na kubwa zaidi, ndiyo Sekta inayoongoza kwa kutoa ajira. Hivyo basi, ili kukifanya kilimo kuwa na tija zaidi, badala ya kuweka motisha za kikodi kuwaleta wawekezaji kutoka nje ili kuwekeza kwenye kilimo; Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo la muhimu kwa kuweka mpango wa kutoa mikopo, kuiwezesha Benki ya Kilimo kufanya kazi na kuwafikia wakulima wengi zaidi; hivyo, uwekezaji katika kilimo ukafanywa na Wananchi wenyewe na faida itakayopatikana itarudi humu humu nchini tofauti na kama uwekezaji utafanywa na wageni. Hili ni muhimu sana kwani kutakuwa na *concept* nzima ya *multiplier effect* kama uwekezaji katika kilimo utajikita hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imesema hapo awali kuwa, fedha nyingi zinazowekezwa kwenye sekta ya mazao kama zitawekwa kwenye Benki ya Kilimo, ni dhahiri fedha hizo zitatumika kwa tija zaidi na zuri zaidi zitarudi katika mzunguko wa kukopesha. Aidha, kwa njia hii ni dhahiri ajira zitaongezeka maradufu na itapunguza wimbi la vijana kuhamia mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, mkakati wowote ambao uhahusu uwekezaji katika kilimo, hauhusu wakulima wadogo na wakati, maana yake ni kwamba, wakulima wadogo wataendelea kuwa ni Manamba katika Mashamba Makubwa ya Wawekezaji, ambao ndiyo Mpango wa Serikali ya CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba mpango huu utaendeleza mtindo wa kuwapora wananchi ardhi na kuwamilikisha wageni, jambo hili siyo haki na linapingwa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, tulielezwa kwamba Sekta ya Elimu ambako vigezo vya ukuaji mafanikio ya Elimu vimeachwa huku Serikali ikizungumzia mambo ya utekelezaji tu. Vigezo vya mafanikio ya elimu ni pamoja na ubora wa elimu, ufaulu wa wanafunzi ikiwa ni pamoja na kuwa na ujuzi wa kumudu matakwa ya kiwango kilichofikiwa na idadi ya wahitimu ikilinganishwa na mahitaji ya soko, watoto waliopo, walioandikishwa na waliomaliza mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tungeweza kuongelea mafanikio kwa kuondoa kero, lakini taarifa hii kwa maana taarifa ya Serikali hata kero za Walimu, ukosefu wa madawati na miundombinu mingine haijazungumziwa kabisa. Hii pia ninaendelea kusema ni kuwahadaa wananchi na kulidanganya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu sasa inayotolewa kwenye shule za Serikali, itaendelea kuwa duni sababu ya uwekezaji mdogo unaofanywa kutokana na ukweli kwamba Sera, Sheria na Kanuni zilizowekwa ili kuendeleza elimu hazifuatwi, badala yake vigezo hivyo vimewekezwa kwenye Shule Binafsi tu. Mfano mzuri, ni pale Sera inaposema kuwa, Shule haitasajiliwa hadi iwe vyoo, viwanja vya michezo, maabara na kadhalika, lakini tumeendelea kuona Shule ngapi za Kata zilizoanzishwa bila kuwepo kwa matakwa haya ya Kisheria.

Huu ni udhaifu unaotokana na ukweli kwamba, Serikali inamiliki shule, inasimamia shule, inatunga mitaala, inatunga mitihani, ni kwa vipi Serikali iwe kama mchezaji, mchezeshaji na msimamizi wa michezo. Ni lazima Serikali ikubali kubakia na jukumu la kusimamia ubora wa elimu na kuruhusu uendeshwaji kuchukuliwa na chombo kingine ambacho kitakuwa kimeundwa. Vinginevyo tutabaki kulalamika miaka yote, kuwa *output* ya elimu hailingani na *input* inayowekwa katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda muafaka sasa Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kubadili usimamizi wa Sekta ya Elimu kwa Serikali kuwa msimamiaji wa ubora wa elimu tu,

na siyo mtoaji wa elimu, kwani kufanya hivyo inaua dhana ya ushindani, baina ya watoaji wa elimu na huu ni upofu wa wataalam wetu na washauri wetu katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na mjadala mkubwa kwamba Mashule na Vyuo Binafsi zinatoza karo kubwa kiasi kwamba wananchi wenye vipato vya chini, hawawezi kusomesha watoto wao kwenye shule hizo. Hoja ya Msingi ni kwa nini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizo binafsi zinakumbwa na ubaguzi ule ule wa Serikali, ambao shule hizo zinatakiwa kulipa kodi kadhaa na ili shule hizo ziendelee kuwepo ni lazima wapandishe karo kwa wanafunzi na hapo ndipo ughali unapoonekana wazi na kodi hizo zifuatazo ni kama, shule binafsi zinatoza:-

(i) *Corporation Tax*

(ii) Value Added Tax

(iii) Skill and Development Levy

(iv) Land Rent na kuna

(v) Local Government Taxes kama:-

(a) Propety Tax.

(b) City Service levies.

(c) Tax for sign board.

(d) Fire Brigade Inspection Fees na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Nishati, Serikali ilikuwa na lengo kuwafikisha umeme wananchi kwa asilimia 80. Asilimia 30 ya wananchi kwa maana ya watumiaji 150,000, ifikapo Julai. Huku Wizara ikiripoti wananchi 70,000 tu. Taarifa ya Serikali zinapingana na zilizokuwa zikipigiwa chapuo na Katibu Mkuu wa CCM, zikidai kwamba asilimia 36 ya wananchi hadi mwezi Julai, 2014 walikuwa wameunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ikumbukwe kwamba tarehe 12 Juni, 2014, wakati Waziri wa Mipango anawasilisha, alisema kwamba, wananchi 133,931 ndio waliounganishwa tu. Hii pia inaendelea kudhihirishwa kwamba, kwa kipindi cha miezi miwili tu wangewezaje kuunganisha wananchi 68,931, iwapo kwa kipindi cha miezi tisa waliunganisha 70,000 tu. Napenda kujua zaidi ya hapo ni kuwa hali halisi iliyopo kwa wananchi na vilio kwa vijiji ni kutofikishiwa nishati huku baadhi ya vijiji vikiwa vimeunganishwa kwa wakaazi wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimesikia kengele ya kwanza, naomba kwenda moja kwa moja kwenye hitimisho na kama nilivyosema awali, ningependa hotuba yangu iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Real Estate Regulatory Authorities,* katika ushauri wetu wa Bajeti ya Mpango iliyopita tulisema Serikali kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Sekta, kwani fedha nyingi zinapotea kwa kodi ya majengo na kodi ya ardhi, *(Property Tax and Land Rent),* hazikusanywi ipasavyo, hivyo kuikosesha Serikali mapato ambayo yangeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni dhahiri kodi itakusanywa kulingana na ardhi iliyopo katika miji na majiji, *(land value depend on location)*. Ni kweli kwamba tumekuwa tukikosa mapato mengi sana kutokana na kukosekana kwa mdhibiti katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; Tanzania ni nchi yenye wachumi wazuri, waliobobea na ukweli ni kwamba, nchi jirani zimekuwa zikikopi mipango yake kwa kutumia Wataalam wetu. Ni kweli kwamba Mipango ya hao Watalaam wa Mipango na Wataalam wetu, wameendelea kuliko sisi. Hoja kubwa ya kujiuliza ni kwa nini kama mipango mizuri, tunayo na Wataalam tunao, mambo hayaendi kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la msingi hapa ni kuwa nchi zilizoendelea, uchumi ndiyo unatakiwa kuongozoa mfumo wa siasa. Lakini kwetu sisi, siasa ndiyo inayooongoza mfumo wa uchumi kwa maana mipango yetu inapangwa kwa kuangalia zaidi matakwa ya kisiasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujikita zaidi kwenye kutekeleza mpango na siyo kwenda kwenye matakwa ya viongozi wa kisiasa kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, ni aibu kubwa kwa nchi makini na tajiri kama Tanzania kuendelea kupangisha ofisi kwa ajili ya Mabalozi wake Nje ya Nchi, wakati nchi inamiliki viwanja katika Mataifa hayo. Serikali pia imeendelea kupanga nyumba za watumishi na maafisa kwa gharama za juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika hilo ni kwa vipi mfano, nchi makini kama Tanzania ilivyo, inaweza kuuza nyumba za watumishi wake hasa Madaktari na kuwapatia viwanja vya kujenga nyumba zao katika maeneo ya mbali na sehemu wanazofanyia kazi huku tukijua umuhimu wa Sekta ya Afya. Hii ndiyo mipango ya Serikali ya CCM na ni wizi wa viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hujuma hizi kwa Taifa zinazofanywa na Mawaziri waliopewa dhamana ya kusimaia rasilimai za Watanzania, lakini wanashindwa. Kambi Rasmi ya Upinzani, inawataka Mawaziri wahusika wajipime kama kweli bado wanafaa kuendelea kuwa watumishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira tatanishi kama haya, ni lini kweli tunaweza tukajitapa kuwa tutafikia malengo ya Milenia wakati bado tunaendelea kuona ufisadi ukitawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona bado ninao muda, naomba nizungumzie kipengele kingine kuhusu kukuza uchumi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukuza Uchumi Vijiini *(Rural Growth)* ni kipaumbele cha mwanzo kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka kadhaa iliyopita. Kitaendelea kuwa kipaumbele chetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa, kama mkakati utawekwa kwa kila Halmashauri za Vijiji za kutengeneza mazingira ya kutoa ajira rasmi zipatazo mia tano (500) kwa

mfano, kila mwaka basi zitakuwa zimepiga hatu kukabiliana na wimbi kubwa la vijana kukimbilia mijini kwa kutafuta ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mazingira ya vijijini yanatofautiana, kwa kuwa rasilimali zilizopo katika maeneo mbalimbali ya Wilaya nayo pia yanatofautiana, pia kati ya Wilaya na Wilaya. Hivyo basi, Serikali inatakiwa kuweka viwango mkakati yaani *(threshold)* kwa maendeleo tunayotakiwa kufikia kwa kila Wilaya, kulingana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya …

NAIBU SPIKA: Ahsante. Malizia sasa Mheshimiwa Esther.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI – OFISI YA RAIS MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Esther Matiko, japo ni mara ya kwanza kusoma hapa, lakini umejitahidi umefanya vizuri sana, tunakushukuru sana dada yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyo ni Mheshimiwa Esther Matiko, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Taarifa ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2014/2015, alikuwa anamvaa kaka yake Mheshimiwa Stephen Wasira, wote wawili hawa wanatoka Mkoa wa Mara. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Ni shemeji yake.

NAIBU SPIKA: Ni shemeji. Aaa, alikuwa anapambana na shemeji yake.

Taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 kama Ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE. ESTHER NICHOLAS MATIKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA MWAKA 2014/2015

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 105 (8) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2013)

1. UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru mwenyezi mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya bunge hili kutoa maoni ya kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kuniamini na kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi ya Rais- Mahusiano na Uratibu. Kipekee naishukuru familia yangu (Mume wangu na watoto wangu wapendwa) kwa kinitia moyo katika kazi zangu za kibunge na kichama. Aidha wananchi wote wa Mkoa wa Mara hususani wa Wilaya ya Tarime kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika,Mpango huu wa maendeleo wa mwaka 2014/15 ni sehemu ya nne ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) kama ulivyopitishwa na Bunge hili, na pia ni sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa Dira ya maendeleo ya Taifa ya 2025. Dira 2025 imeundwa na nguzo kuu tano ambazo ni: (i)Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani,usalama na umoja (iii) Kujenga utawala bora (iv) Kuwepo jamii iliyoelimika vyema na inayojifunza, na (v) Kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Hoja ya msingi ni kwa kiasi gani Serikali ya CCM imefanikisha utekelezaji wa nguzo ya kwanza ya Dira 2025, ambayo ni kuboresha hali ya maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Mpango wa maendeleo wa miaka mitano unasema wazi kuwa sera ya matumizi haioneshi msisitizo maalum wa kupunguza matumizi ili yaendane na makusanyo ya ndani. Aidha lile lengo la kutumia asilimia 22 ya makusanyo ya ndani kwa matumizi ya kawaida limeshindikana kabisa[1]. Kwa sasa mwaka wa fedha 2014/15 makusanyo ya ndani ni shilingi trilioni 12.178 na matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 13.408. Aidha, hili linajidhihirisha wazi katika taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, njia ya kubana matumizi kwa kuondoa udhaifu wa kukarabati barabara mara kwa mara, kuwa na kipindi maalum cha kukarabati barabara mara baada ya kukabidhiwa kwa Serikali nalo nitatizo kubwa linalotumia mabilioni ya fedha za walipa kodi. Taarifa ya Mpango wa miaka mitano inaonesha kwamba kwa mujibu wa makadirio ya benki ya dunia kiasi cha dola za kimarekani bilioni 2.4 kwa mwaka zinatumika kukarabati barabara katika bara la Afrika. Na hili kwa ushauri wao lingeweza kuepukwa kama kungekuwa na kipindi maalum cha ukaratabati ***"timely preventive maintenance"*** na pia kuna mapungufu kadhaa yanayoendana na udhaifu wa Serikali kushindwa kuwa makini. Kama vile kushindwa kukusanya kodi, kuwa na watumishi wengi wasiokuwa na tija[2] n.k

Mheshimiwa Spika, Kama kweli Serikali inataka kufikia malengo ya millenia, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia matakwa ya mpango katika matumizi kwenye miradi ya maendeleo.

1 Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano-
2 Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano 4.5.1- (ii)

Mheshimiwa Spika, Kama kweli Serikali inataka kufikia malengo ya millenia, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia matakwa ya mpango katika matumizi kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda wananchi wafahamu kwamba Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya 2014/15 yaliyoletwa na Serikali ili yajadiliwe na Bunge hili ni ya nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Kwa maneno mengine ni kwamba imebaki miaka miwili tu kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda pia kuwajulisha wananchi kwamba wakati imebaki miaka miwili tu kwa Serikali kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, umebaki mwaka mmoja tu kwa upande wa Chama cha Mapinduzi kukamilisha utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 inasema nanukuu "***Kukuza uchumi kwa kiwango cha zaidi ya asilimia kumi (10%) kwa mwaka ifikapo 2010 kutoka ukuaji wa sasa wa asilimia sita nukta saba (6.7%)***" Pia **"*Kuanza kupunguza umaskini wa watu wetu kwa namna iliyo dhahiri*"**, haya yalikuwa ni malengo ya kufikia mwaka 2010, ambapo hadi sasa uchumi haujafikia asilimia 10, pia Asilimia 28.1 ya Watazania wote wanaishi chini ya mstari wa umaskini (below poverty line kwa takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2012), hii ni sawa na Watanzania milioni 12.

Mheshimiwa Spika,Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti serikali haijafanikiwa kuwa na bajeti yenye uhalisia wa kupunguza umaskini wa watanzania, kwani Bajeti inayolenga kupunguza umaskini ni ile ambayo inalenga *kupunguza mzigo wa kodi kwa wananchi*, ni ile ambayo *inatengeneza ajira nyingi*, ni ile ambayo inakuza *uwekezaji hasa wa ndani*, ni ile inayomfanya *Mtanzania aweze kuweka akiba (savings)*, ni ile ambayo inalenga kuinua maisha ya walio wengi ambao wako vijijini, ile inayolenga *uchumi umilikiwe na Watanzania*, ile inayolenga *kukuza ujasiriamali* na ile *inayokuza ulaji* (increased consumption).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti zote tangu tuanze utekelezaji wa mpango wa taifa, pia utekelezaji wa ilani ya CCM, na kwa kuwa sisi sote tunayo nia ya kuwaondoa watanzania katika umaskini, ni kwa vipi sasa serikali imejipanga kuhakiki mipango yetu inaendana na sera zetu za bajeti ili tuweze kuoanisha mipango na utekelezaji wake? Kama wataalamu tunao, rasilimali tunazo, nia tunayo, ni kwa vipi tunashindwa?

Mheshimiwa Spika, Ni vema sasa serikali iliambie bunge lako nini kikwazo cha kutekeleza mpango wa maendeleo? Au ni hila za CCM kuwafanya watanzania waendelee kuwa maskini kwa maslahi ya kisiasa? Vema bila kujali itikadi zetu tuungane pamoja kwa nia ya kuwatoa watanzania katika umasikini mkubwa kwani ni ukweli kwamba hawatakiwi kuwa huko kutokana na utajiri wa nchi hii ulivyokuwa mkubwa. Hali hii haikubaliki kabisa. Inabidi tutanzue kitendawili hiki cha kuwa nchi tajiri sana kwa wingi wa rasilimali ila watu wake ni masikini.

Aidha, Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sura ya Tisa (9) Ibara ya 212 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 inasema kwamba:

"Chama Cha Mapinduzi katika miaka mitano ijayo,(yaani 2010 - 2015) kinaelekeza nguvu kubwa katikakutimiza lengo la msingi la Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 kwa kuendeleza jitihada za ujenzi wa uchumi wa kisasa na taifa linalojitegemea. Katika kuzingatia jukumu hilo Ilani hii ya CCM ya 2010 hadi 2015 inatangaza nia ya modenaizesheni ya uchumi. Modenaizesheni ya uchumi ndiyo njia ya uhakika itakayobadili na kuleta mapinduzi katika uchumi wa nchi, kujenga msingi wauchumi wa kati unaoongozwa na viwanda, kuondoa umasikini wa wananchi wetu kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitegemea……..."
Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka wananchi wapime na kufanya tathmini wenyewe juu ya mambo yafuatayo:

i. Miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa Upande wa Serikali na Miaka Minne ya Utekelezaji wa Mpango huo huo kwa upande wa CCM imeleta mabadiliko katika maisha yao kama ilivyokusudiwa na mpango huu?

ii. Je, ni kweli kwamba Mkakati wa CCM wa kufanya mapinduzi ya Uchumi (Modenizationi ya uchumi) uliotangazwa na ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2010 umefanikiwa?

iii. Je, ni kweli kwamba msingi wa uchumi wa Tanzania unaongozwa na viwanda kama CCM ilivyoahidi kwenye ilani yake ya uchaguzi ya 2010?

iv. Je, ni kweli kwamba umasikini wa wananchi umepungua zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama CCM ilivyoahidi kupunguza umasikini kwa wananchi na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania?

v. Je, ni kweli kwamba sasa hivi Tanzania ina uwezo zaidi wa kujitegemea kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo CCM iliahidi kwamba kabla ya 2015 Tanzania itakuwa na uchumi imara na hivyo kujitegemea?

vi. Je ni kweli kwamba hali ya ajira hasa kwa vijana ni bora zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo Serikali ya CCM ilivyoahidi kutoa ajira ili kupunguza umasikini wa kipato?

vii. Je, ni kweli kwamba ugumu wa maisha umepungua zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo Serikali ya CCM ilivyoahidi kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania?

viii. Je, bajeti za Serikali kwa miaka minne iliyopita zimeweza kuondoa tatizo la umasikini kwa watanzania?

Mheshimiwa Spika, Mpango wa maendeleo wa mwaka 2014/15 ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ambao nao ni sehemu ya Kwanza kati ya sehemu tatu za mipango ya nchi ili kufikia dira ya maendeleo ya mwaka 2025. Lengo la ujumla la sehemu ya kwanza ya dira ya 2025 ni "**kutoa fursa ili hazina ya raslimali za nchi zitumike ipasavyo kwa kuweka mazingira wezeshi na kutanua wigo wa ukuaji wa uchumi ili watu maskini waweze kukua kiuchumi**".

Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kurudia kauli ambayo tumekuwa tukiieleza Serikali kuwa Mpango mzuri haupimwi kwa vigezo vya jinsi Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kilivyopangwa vizuri, maneno mazuri yaliyomo katika hotuba hiyo, au nadharia ya malengo ya kisiasa yanavyonyumbuliwa katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, utengaji wa asilimia kati ya 25 na 30 ya bajeti kuanzia mwaka 2012 hadi sasa kwa matumizi ya maendeleo ni kwenda kinyume cha Mpango wa maendeleo[3] ambao umeeleza vyema kwamba kwa utekelezaji wa sehemu ya kwanza ya mpango wa miaka mitano Serikali itenge si chini ya asilimia 35 kila mwaka kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mpango mzuri wa Maendeleo kimsingi ni takwimu ya jinsi tarakimu za mapato na matumizi zilivyopangwa na utekelezaji wake. Kinyume na hapo mpango uliowekwa vizuri kwenye hotuba bila ya kuwepo kwa mkakati wa utekelezaji wa mpango huo ni kazi bure. Kwa sababu hiyo hotuba ya Kambi Rasmi kwa mwaka huu, inajikita katika uchambuzi wa takwimu mbalimbali zilizomo katika mpango uliopita na mpango wa mwaka huu wa fedha

3Mpango wa Mandeleo wa miaka 5- ibala ya 4.5 – **(Guidelines for Expenditure Probity)**
ili kuonyesha kwa jinsi gani Mpango unaoletwa na Serikali usivyokuwa na mashiko katika utekelezaji wake. Kwani fedha za utekelezaji ndio kigezo kikuu cha kutuonesha tutokako, tulipo na wapi tunakokwenda kama nchi.

Aidha Kigezo hiki ndicho pia kinaonyesha kama vipaumbele vyetu viko sahihi, kama tunasimamia fedha na rasilimali zetu vizuri, kama tunachukua hatua wakati mwafaka ili kudhibiti ubadhirifu, wizi na ufisadi au ni business as usual?

2. HALI YA UCHUMI WA TAIFA

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hali ya uchumi inaonesha kuwa Pato la Taifa katika mwaka 2013 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 kwa mwaka 2012. Shughuli ndogo ambazo zilikua kwa kasi kubwa katika mwaka 2013 ni pamoja na mawasiliano asilimia 22.8; ujenzi asilimia 8.6; biashara ya jumla na rejareja asilimia 8.3; na hoteli na migahawa asilimia 6.3. Kwa upande mwingine ukuaji wa sekta ya kilimo ulibaki kama ilivyokuwa mwaka 2012 wa asilimia 4.3. Hii ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli ndogo za mazao kutoka asilimia 4.7 mwaka 2012 hadi asilimia 4.5 mwaka 2013.

Aidha, **Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ndogo ya mifugo na uwindaji ya asilimia 3.1 hadi 3.8 na misitu kutoka asilimia 2.4 hadi 3.3. Pia shughuli zingine ambazo ukuaji wake ulipungua katika mwaka 2013 ni bidhaa za viwandani asilimia 8.2 hadi 7.7; umeme na gesi asilimia 6.0 hadi 4.4; uchukuzi asilimia 7.1 hadi 6.2; na uvuvi asilimia 2.9 hadi 2.2.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Tanzania Bara kwa Mwaka 2011/12 unaonesha kuwa ***"Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa mtu mmoja kwa mwezi ni Shilingi za Tanzania 36,482/= na Kiwango cha Umaskini wa Chakula kwa mwezi kwa mtu mzima ni Shilingi za Tanzania 26,085/=. Kwa kutumia takwimu hizi, matokeo yanaonesha kuwa zaidi ya robo (asilimia 28.2) ya watu wote waishio Tanzania Bara wako chini ya mstari wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi na asilimia 9.7 ya watu wote wapo chini ya mstari wa umaskini wa chakula[4]".***

2.1. MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu, inayo wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sera za fedha na sheria zinazohusu mashirika ya fedha na benki. Jukumu hili huambatana na wajibu wa kudhibiti mfumuko wa bei (inflation), ambalo wizara imejitahidi kulitekeleza.
Hata hivyo, Wizara imeshindwa kusimamia viwango vya riba vinavyotozwa na mabenki pamoja na taasisi za fedha. Wakati mfumuko wa bei umeshuka toka asilimia 19.8 Disemba 2011 na kufikia asilimia 6 mwezi Machi 2014, viwango vya riba katika mabenki na asasi za fedha vimeendelea kuwa vya juu.

Mheshimiwa Spika, riba halisi '(***real interest rate***)' ambayo inakadiriwa kama tofauti ya '***nominal interest rate'*** na ***'inflation rate'*** hivi sasa ni kati ya asilimia 12 – 18. Hakuna shughuli ya kiuchumi ya kawaida unayoweza kuifanya na kuweza kulipa riba za juu kiasi hiki.

Mwananchi wa kawaida akiweka akiba yake analipwa riba '(saving deposit rate)' ya asilimia 3 wakati mfumko wa bei wa sasa ni asilimia 6. Hata wakati mfumko wa bei ulipokuwa asilimia 19.8 riba aliyolipwa mwananchi wa kawaida anayeweka akiba ilikuwa asilimia 2.9. Mabenki yetu hayampi mwananchi wa kawaida motisha wa kuweka akiba bali yanambana mjasiriamali kwa kumtoza riba kubwa.

Mheshimiwa Spika, Riba katika benki na asasi za fedha imeendelea kuwa juu, mojawapo ya sababu ya kiwango hiki kuwa juu ni Serikali kuwa mmoja wa wakopaji wakubwa kutoka katika mabenki na asasi za fedha za hapa nchini. Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania iliyotolewa mwezi Machi 2014 imeainisha kuwa Serikali imekopa kutoka kwenye vyanzo vya

ndani zaidi ya shilingi Trilioni moja katika kipindi cha Mwezi Machi 2013 hadi Machi 2014. Hali hii imesababisha ushindani usio wa haki baina ya serikali na wananchi wanaokopa katika mabenki hayo (crowding effect). Anayeumia kwa hali hii ya ushindani na serikali ni mkopaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, ukopaji wa serikali kama ulivyoelezwa hapo juu unachangia kufanya riba ziwe za juu. Riba inayolipwa na serikali kwa 'Treasury Bills' ya mwaka mmoja mpaka mwezi Disemba 2013 ilikuwa asilimia 15.63. Kwa mabenki mengi kuwekeza kwenye hatifungani za serikali '(treasury bills and bonds)' kuna faida kubwa ya uhakika ambapo kumkopesha mjasiriamali wa kawaida kuna 'risk' kubwa ya kutolipwa.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwepo na mabenki mengi mfumo wetu wa fedha haufanyi kazi ya kukusanya akiba kwa wingi na kuiwekeza kwa wajasiriamali wandani ili kukuza uchumi na kuongeza ajira. (Mfumo wa riba upo kwenye Quarterly Economic Report of March 2014 ya Benki Kuu Table 3.13).

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa riba za benki kutaongeza fursa za kukopa na kusaidia wananchi kukuza mitaji. Hali hii itasaidia ongezeko la ajira ambalo ni tatizo kubwa sana nchini, kukua kwa uchumi wa taifa, idadi ya walipa kodi itaongezeka na ustawi wa wananchi utaimarika.

3. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2013/14

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kutenga asilimia 30 ya bajeti toka mwaka 2012 hadi mwaka huu kama fedha za maendeleo, na hili ni kwenda kinyume na matakwa ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano, kifungu cha 4.5.1 ambacho kinasisitiza kutenga si chini ya asilimia 35 ya bajeti kuu. Mapungufu haya maana yake ni kwamba tuko nyuma sana katika kufikia malengo ya millenia.
Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa mara nyingine kukusanya mitaji ya ndani kutoka kwa watanzania wenyewe kwani miradi mingi ni kwa ajili ya maendeleo yetu na hili linaondoa dhana nzima ya uchumi inayoitwa ***"tragedy of the common"***

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14 ulikuwa ni kuzingatia vipaumbele vile vile vya mpango wa miaka mitano ambavyo ni:

a. *Miundombinu, b. Kilimo, c. Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani, d. Maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi, na mwisho ni e. Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.*

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Serikali zinaonesha kuwa kumekuwepo na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mpango kwa mwaka wa fedha unaoishia mwezi juni, lakini jambo la ajabu ni kwamba takwimu za wizara ya fedha zinaonesha kwamba utekeleza wa bajeti kwa fedha za maendeleo kwa fedha za ndani hadi mwezi Mei fedha zilizotolewa ni asilimia 52.2 na fedha za

nje ni asilimia 39.6 tu. Na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo zilizopatikana kuwa asilimia 46.2 tu.

Mheshimiwa Spika, Hoja ya msingi hapa kama sekta za kipaumbele kwa mujibu wa mpango zimepewa fedha ambayo haikidhi kuleta matokeo ambayo yalitarajiwa katika mpango wa miaka mitano pamoja na dira ya maendeleo ya mwaka 2025. Ufuatao ni mgawo wa fedha za maendeleo kama zilivyotolewa na Hazina.

Chanzo: Taarifa ya Waziri wa Fedha-

Mheshimiwa Spika, Inasikitisha kuona taarifa za serikali zinajaa hadaa kwa wananchi kwa kuwasilisha takwimu na tathmini zisizo halisi na zenye kudanganya umma. Kwa ujumla taarifa hizi ama zinalenga kuonyesha mafanikio makubwa yamefikiwa na serikali katika kutoa huduma kwa jamii au kuonesha kukamilisha miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa huku uhalisia ukiwa ni tofauti kabisa na yanayoandikwa.

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo ya mwaka 2013/14 (uk.8) inaonekana kuwa katika sekta ya kilimo mafanikio mengi yamepatikana kwa kutaja mambo yasiyopimika na haswa yasiyo na uhusiano na vipimo vya mafanikio.

a. KILIMO

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya sekta ya kilimo hupimwa kwa kuangalia mambo yafuatayo:

- Uzalishaji katika mazao ya kilimo na mchango wa uzalishaji huo wa kilimo kwenye pato la Taifa
- Upatikanaji wa masoko kwa mazao ya kilimo, bei ya mazao kulingana na faida kwa wakulima na kufikika kwa masoko;
- Lishe na uhakika wa chakula kwa familia na Taifa unaotokana na mafanikio ya uzalishaji; na
- Maboresho ya mbinu na pembejeo za uzalishaji katika sekta.

Mheshimiwa Spika, Lakini ukiangalia taarifa za serikali zinaongelea mambo tofauti na ambayo yanawahadaa wananchi kufikiria kuna mafanikio ambayo kwenye uhalisia hayapo. Hivi sasa tunashuhudia kuendelea kudorola mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa ambapo sasa ni 4.3 ikilinganishwa na 4.6 mwaka 2008. Ieleweke kwamba licha ya kilimo kuwa nguzo muhimu katika uchumi wetu na kwamba watanzania takribani asilimia 80 wanategemea kilimo katika kuendesha shughuli zao za maendeleo, sekta hii ndio inachangia mchango mdogo zaidi kwa sekta zote zilizobakia ukiachia Uvuvi unaohujumiwa, ambapo viwanda na Ujenzi vinachangia 7.5% huku sekta ya Huduma ikichangia 8.2%.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya kilimo kwa miaka kati ya 2010/11 hadi 2013/14 imekuwa inakwenda kwenye idara ya maendeleo ya mazao na kufuatiwa iliyokuwa idara ya Umwagiliaji na huduma za ufundi. Ni kweli kwamba idara zote hizi ni muhimu, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kama fedha hizo zingelikuwa zinaingizwa moja kwa moja kwenye benki ya kilimo na wakulima kukopa ni dhahiri kilimo kingekuwa na tija zaidi kuliko ilivyosasa kwani thamani ya fedha hizo kwenye kilimo haionekani.

Mheshimiwa Spika, Kilimo ndiyo sekta kiongozi katika kuliingizia taifa fedha za kigeni na kubwa zaidi ndiyo sekta inayoongoza kwa kutoa ajira. Hivyo basi ili kukifanya kilimo kuwa na tija zaidi badala ya kuweka motisha za kikodi kuwaleta wawekezaji kutoka nje ili kuwekeza kwenye kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo bora kwa kuweka mpango wa kutoa mikopo kwa kuiwezesha benki ya kilimo kufanya kazi na kuwafikia wakulima wengi zaidi na hivyo uwekezaji katika kilimo ukafanywa na wananchi wenyewe na faida itakayopatikana itarudi humu nchini tofauti na kama uwekezaji utafanywa na wageni. Hili ni muhimu sana kwani kutakuwa na ***"multiplier effect***"kama uwekezaji katika kilimo utajikita hapa hapa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imesema hapo awali kuwa fedha nyingi zinazowekwa kwenye sekta ya mazao kama zitawekwa kwenye benki ya kilimo ni dhahiri fedha hizo zitatumika kwa tija zaidi na nzuri zaidi zitarudi na kuingia tena kwenye mzunguko wa kukopesha. Aidha, kwa njia hii ni dhahiri ajira zitaongezeka mara dufu na itapunguza wimbi la vijana kuhamia mijini.

Mheshimiwa Spika, Aidha, mkakati wowote ambao unahusu uwekezaji katika kilimo ambao hauhusu wakulima wadogo na wa kati maana yake ni kwamba bado wakulima wadogo wataendelea kuwa ni manamba katika mashamba makubwa ya wawekezaji ambao ndio mpango wa Serikali ya CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba mpango huu utaendeleza mtindo wa kuwapora ardhi wananchi na kuwamilikisha wageni. Jambo hili siyo haki na linapingwa kwa nguvu zote.

b. ELIMU

Mheshimiwa Spika, Vivyo hivyo kwenye sekta ya elimu ambako vigezo vya ukuaji na mafanikio ya elimu vimeachwa huku serikali ikizungumzia mambo ya utekelezaji tu. Vigezo vya mafanikio ya elimu ni pamoja na Ubora wa Elimu, Ufaulu wa Wanafunzi ikiwa ni pamoja na kuwa na ujuzi wa kumudu matakwa ya kiwango walichofikia, idadi ya wahitimu ikilinganishwa na mahitaji ya soko, watoto waliopo, walioandikishwa na waliomaliza mafunzo. Hata hivyo tungeliweza kuongelea mafanikio kwa kuondoa kero, lakini taarifa hii hata kero za walimu na ukosefu wa madawati hazizungumzwi. Hii ni kuwahadaa wananchi na kulidanganya bunge.

Mheshimiwa Spika, Elimu yetu hasa inayotolewa kwenye shule za Serikali itaendelea kuwa duni sababu ya uwekezaji mdogo unaofanyika kutokana na ukweli kwamba, sera, sheria na kanuni zilizowekwa ili kuiendeleza elimu serikali haizifuati, badala yake vigezo hivyo vinawekwa kwenye shule binafsi. Mfano mzuri ni pale sera inaposema kuwa shule haitasajliwa hadi iwe na vyoo, viwanja vya michezo, maabara n.k

Mheshimiwa Spika, Ni shule ngapi za kata zinaanzishwa bila ya kuwepo kwa matakwa hayo ya kisheria? Huu ni udhaifu unaotokana na ukweli kwamba, Serikali inamiliki shule, inasimamia shule inatunga mitaala, inatunga mitihani ni kwa vipi serikali iwe kama mchezaji, mchezeshaji na msimamizi wa mchezo. Ni lazima serikali ikubali kubakia na jukumu la kusimamia ubora wa elimu na kuruhusu uendeshaji wa elimu kuchukuliwa na chombo kingine, vinginevyo tutabaki kulalamika miaka yote kuwa ***"out put ya elimu ailingani na in put inayowekwa katika elimu"***

Mheshimiwa Spika, Ni muda mwafaka sasa Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadili usimamizi wa Sekta ya elimu kwa serikali kuwa msimamiaji wa ubora wa elimu na sio mtoaji wa elimu, kwani kufanya hivyo inaua dhana ya ushindani baina ya watoaji wa elimu. Huu ni upofu wa wataalam wetu au washauri wetu katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mjadala mkubwa kwamba mashule na vyuo binafsi zinatoza karo kubwa kiasi kwamba wananchi wenye kipato cha chini hawawezi kusomesha watoto wao kwenye shule hizo. Hoja ya msingi ni kwanini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Spika, shule hizo binafsi zinakumbwa na ubaguzi ule ule wa Serikali ambapo shule hizo zinatakiwa kulipa kodi kadhaa na ili shule hizo ziendelee kuwepo ni lazima wapandishe karo kwa wanafunzi, na hapo ndipo ughali unapoonekana wazi. Kodi hizo ni zifuatao:

1. Corporation tax
2. Value Added TAX
3. Skills & Development Levy
4. Land Rent
5. Local Government taxes:
    a. Property tax
    b. City Service levies
    c. Tax for sign board
6. Fire brigade Inspection fees
7. Work permit fee for teachers (Wanaotoka nje kwa ajili ya masomo ya sayansi).

c. SEKTA YA NISHATI

Mheshimiwa Spika, Katika sekta ya nishati serikali ilikuwa na lengo la kuwafikishia umeme asilimia 30 ya wananchi kwa kuwaunganishia umeme watumiaji 150,000 ifikapo Julai 2014. Huku wizara ikiripoti kuwaunganishia umeme wananchi 70,002 tu, taarifa ya serikali zinazopigiwa chapuo na

Katibu Mkuu wa CCM zinadai kuwafikia asilimia 36 ya wananchi kabla hata ya Julai 2014. Na ili kuona kwamba serikali imepanga kwa makusudi kabisa kuwahadaa wananchi kupitia takwimu ni pale mhe Steven Wassira katika taarifa yake ya mpango mwezi Aprili aliainisha wananchi 70,002 tu ndio waliounganishiwa umeme kati ya July 2013 na Aprili 2014(nah ii ni kwa kipindi cha miezi 9),lakini kwenye hotuba yake ya 12 Juni 2014 ameainisha kuwa ni wananchi 138,931 wameunganishiwa umeme, hii inaonyesha ongezeko la wananchi 68,931 ndani ya miezi miwili tu? Huu ni uongo wa wazi kwa wananchi na Bunge hili huku wakijua kuwa taarifa hizi hazina ukweli wowote. Zaidi ya hapo ni kuwa hali halisi iliyopo kwa wananchi ni vilio kwa vijiji kutofikiwa na nishati hiyo huku baadhi ya vijiji vikiwa wameunganishiwa wakaazi wachache tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa bajeti ya Kaya iliyotolewa mwaka huu inasema, ***"Matokeo yameonesha kuwa mwaka 2011/12 asilimia 18 ya kaya za Tanzania Bara zinaishi katika nyumba zilizounganishwa na umeme wa gridi ya Taifa. Hili ni ongezeko la asilimia 6 ukilinganisha na matokeo ya mwaka 2007. Nyumba nyingi Maeneo Mengine ya Mjini zimeunganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa kuliko Maeneo ya Vijijini. Utafiti huu pia umebaini asilimia 68 ya kaya zilizopo Dar es Salaam na asilimia 36 katika Maeneo Mengine ya Mjini zimeunganishwa katika gridi ya Taifa. Aidha, takribani asilimia 4 ya kaya za Maeneo ya Vijijini ndizo zilizounganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa[5]".***

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaitaka Serikali ilieleze Bunge na wananchi, kama ni ukweli kwamba asilimia zaidi ya 75 ya watanzania wanaishi vijijini na kwa mujibu wa tafiti hizo za idara ya taifa ya takwimu kuwa ni asilimia 4 tu ya wananchi waishio vijijini ndio waliounganishwa kwa gridi ya Taifa. Je hizo asilimia 36 za maeneo ya mijini ndio zinazoongelewa na waheshimiwa wanaowakilisha wananchi waishio vijijini?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani itakuwa haijatenda haki kama haitaomba kupatiwa majibu katika sakata zima la IPTL, PAP na ESCROW akaunti. Hivyo basi kwa niaba ya wananchi inahoji yafuatayo:

1. ***Kosa la kwanza IPTL haikuweza kukamilisha mradi wake 1995 kwenye kipindi cha dharula na badala yake ikakamilisha mwaka 1998. Baada ya kumaliza mwaka1998 IPTL ililalamikiwa na tanesco ICSID kwamba imekuza gharama za uwekezaji na hivyo kukuza gharama za umeme. Mwaka 2001 uamuzi wa ICSID ukatoka ikabainika ni kweli IPTL ilikuza gharama kwa kiasi cha dola 27milioni. Serikali ilikuwa na haki ya kupewa fedha zilizokuwa zimelipwa kama capacity charge.***

2. ***Mwaka 2002 IPTL ikaanza kuiuzia umeme Tanesco lakini mwaka 2004 Tanesco ikabaini kuwa IPTL ilidanganya kuhusu mtaji. IPTL ilisema 30% ya mtaji ilikuwa nao kama equity sawa na dola 36milion ambayo ni shilingi bilioni 36 na kwamba 70% ilikopa. Lakini baada ya ukaguzi ikabainika kuwa IPTL haikuweka dola 36milion kama equity bali dola 50 ambapo kwa exchange rate ya wakati huo ya 1:1000, dola50 ilikuwa sawa na Tsh elfu 50 ambazo hata fundi baiskeli angeweza kuwekeza.***

3. ***Kutokana na kasoro hiyo Tanesco ikataka gharama ya umeme (tarrif) ishuke kwa sababu bei ilizingatia equity ya tshs bilioni 36 kumbe ni tsh 50000. Mabishano yakaendelea mpaka 2006. Mwaka 2006 Serikali na Tanesco ikashinikiza ifunguliwe akaunt maalumu (escrow) ili malipo yawekwe huko mpaka mgogoro utapokwisha kuhusu bei sahihi ndipo pesa hiyo igawanywe kwa kuzingatia bei sahihi baina ya pande mbili ndio maana ilikuwa kosa kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda kusema pesa yote ya escrow eti ni ya IPTL kabla ya uamuzi kuhusu bei haujafikiwa.***

4. ***Mwaka 2008 IPTL iliposhindwa kujiendesha ikawekwa chini ya receivership chini ya RITA ambapo ni RITA ikawa inasimamia gharama za uendeshaji. Mwaka 2013 September ikatoka hukumu ya mahakama kuu chini ya Jaji Utamwa ilojichanganya baada ya VIP mwenye 30% kushtaki na kutaka IPTL iondolewe chini ya receivership na mali zote za IPTL ipewe kampuni ya PAP ya singasinga anaitwa Sethi.***

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze watanzania ni kwanini ilifungua ESCROW ACCOUNT kama ilikuwa ni haki kwa IPTL kulipwa capacity charge hiyo?Na kama kulikuwa na uhalali wa kufunguliwa kwa hiyo akaunti ni kwanini sasa fedha zote zimelipwa na Serikali kukosa hata shilingi?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya nishati hasa gesi imekuwa ndio tegemeo la kuitoa nchi yetu katika hali ya umasikini tuliyonayo kwa sasa na kutusukuma hatua kadhaa mbele. Jambo hili linawezekana ikiwa kutakuwepo na ubunifu wa mkakati makini na sio mkakati wa kutegemea wawekezaji toka nje kwani mind set za watawala zimelalia huko, na hawaamini kabisa kama watanzania wazawa wanaweza kuwekeza katika sekta hii ya gesi.

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa gesi ya kupikia majumbani imekuwa inapanda kila kukicha na fedha za kigeni zinazotumika kuagiza gesi hiyo nje ya nchi ni nyingi sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo la busara kama gesi asili inachakatwa na kujazwa kwenye mitungi kwa ajili ya matumizi ya majumbani badala ya kutegemea mpango wa TPDC wa kusambaza gesi kwa njia ya mabomba kama mfumo wa maji ulivyo. Uwekezaji huu unaweza kutuchukua miaka 20 ijayo hadi wananchi kuona manufaa ya nchi kuwa na gesi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa jambo hili linawezekana kabisa na watanzania wanaweza kuwekeza katika viwanda vya ku-"compress gas" na kuiweka kwenye liquid form na kuijaza kwenye mitungi na kuisambaza kama ambavyo soda au bia zinasambazwa kwa watumiaji. Mfumo huu utaokoa mabilioni ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza gesi ya kutumia majumbani na pia utasaidia kuokoa mazingira yanayoharibika kutokana na ukataji wa mkaa unaotishia maeneo mengi ya nchi yetu kugeuka jangwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa uwekezaji wa aina hii hauhitaji mtaji kutoka nje, bali wananchi kwa wingi wao wanaweza kutoa mtaji huu na wao wakawa ni wanahisa katika uwekezaji huu, kianachotakiwa ni ubunifu wa jinsi ya kuwashirikisha wananchi katika uwekezaji huu. Faida itabaki hapa hapa nchini kinyume na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Katika sekta ya maji, taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo inaonesha kuwa serikali imefanikiwa kuongeza kasi ya kuwafikishia huduma za maji safi wananchi kutoka 300,000 hadi 500,000 hadi watu 2,390,000 kwa miezi sita tu ya utekelezaji bajeti ya 2013/14. Hii haijalishi kuwa wizara hii hadi kufikia Juni 2014 ilipowasilisha taarifa yake ya utekelezaji bajeti na kuomba bajeti ya 2014/15 ilikuwa imepatiwa jumla ya 27% tu ya bajeti. Hii maana yake ni kwamba kwa kipindi cha miaka zaidi ya hamsini ya uhuru watu waliopatiwa maji safi na salama vijijini ni 500,000 lakini kwa miezi sita tu idadi hiyo imeongezeka kwa takriban asilimia 260 na kufikia watu 2,390,000. Kwa hali ya kawaida ni nani anaweza amini miujiza hii?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu utekelezaji wa jumla wa miradi ya maendeleo kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka 5, taarifa ya serikali inaonesha kati ya miradi 80 iliyopangwa kutekelezwa, hadi Aprili 2014 (huu ukiwa ni mwaka wanne wa utekelezaji mpango) HAKUNA hata mradi mmoja uliokamilika. Kati yake miradi 13 inaendelea vizuri huku minne mingine ikiwa ya kuridhisha, na iliyobaki 63 ikiwa katika hali isiyoridhisha na au imekwama. Iwapo utekelezaji huu ungewekwa kwenye GREDI za ufaulu wa kielimu ungekuwa kama ifuatavyo:

Division I = 0;

Division II = 13;

Division III = 4;

Division IV = 51; na

Division 0 = 12

Je, malengo ya mpango ya 2025 yatafikiwa kwa utekelezaji wenye tathimini (evaluation) ya kufeli kama nilivyoinisha kwenye gredi za ufaulu.

Mheshimiwa Spika, Mwaka huu wa fedha wa 2014/15, mwaka wa mwisho wa utekelezaji Mpango huu, serikali imeomba jumla ya TShs 5.445 Trilioni kutekeleza ukamilishaji miradi hiyo huku kukiwa na uhakika kabisa kuwa haiwezi kukamilisha ahadi hizi hewa.

Eneo jengine la hadaa ni pale serikali inaposhindwa kuwaeleza wananchi na Bunge sababu za kushindwa kwake. Kwa mfano miradi wa Ujenzi ya barabara za Dumila – Kilosa na ule wa Dumila – Turiani imekwama kwa zaidi ya mwaka sasa huku matuta yake yakiota majani na wakandarasi kulalamikia malipo. Hakuna mahala popote kwenye taarifa hizi serikali inaelezea utekelezaji miradi hii. Miradi kama hii ipo mingi nchini ambayo hutekelezwa kimyakimya na au kutelekezwa kwa miaka kadhaa bila ukamilishaji na kuwaacha wananchi kwenye dhiki zaidi kuliko awali.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni kichocheo kimojawapo cha kukuza uchumi na pia chanzo kikuu cha mapato kama kitatumika vyema. Serikali kwa makusudi imeshindwa kukusanya kodi ya ardhi kwa nyumba nyingi zilizopo maeneo ya mijini na badala yake imekuwa ikitumia fedha nyingi kwenda kupima maeneo ambayo wamiliki wake hata hawalipi kodi. Ina kadiriwa kwamba karibu asilimia kati ya 30 na 60 ya nyumba za mijini hazina hati jambo linalopelekea kupoteza mapato ya kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaitaka Serikali kuondoa ukiritimba usiokuwa na maana na kupunguza gharama za utoaji wa hati za nyumba na viwanja na ikibidi hati zitolewe na wananchi walipie taratibu huku wakilipa kodi ya ardhi. Tunaamini jambo hili liko ndani ya uwezo wa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia hali halisi iliyopo kwa wananchi na yale yaliyoandikwa kwenye nyaraka za Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, sababu zifuatazo ndizo zimepelekea hali hiyo:

1. Tunapanga maendeleo yetu kwa kutegemea misaada au uwezeshaji toka kwa wahisani (Misaada na mikopo 30% +)

2. Tunapanga mipango ambayo hatuwezi kuitekeleza. Miradi mingi inachukua muda zaidi ya muda pangwa na hivyo kuongeza gharama.

3. Miradi mingi ya maendeleo haina uhalisia wa malengo/mahitaji ya jamii lengwa (Miradi inakuwa si shirikishi na hivyo utekelezaji wake hauhusishi wananchi).

4. Serikali haijatekeleza vipaumbele ilivyoviweka (Yaani kupanga bajeti yake kulingana na maazimio iliyoridhia).

5. Serikali kushindwa kutoa fedha za maendeleo hata zile zilizopangwa kwenye bajeti yake, kupeleka kiasi ambacho sicho kilichopangwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

6. Miradi mingi inayokamilika kutokidhi viwango, jambo linalosababisha ukarabati wa mara kwa mara kwa muda mfupi.

4. UWEKEZAJI WA PAMOJA KATI YA SERIKALI NA SEKTA BINAFSI

Mheshimiwa Spika, Serikali inakosa fedha za kuendesha miradi mikubwa ya maendeleo, aidha kwa kuwadharau wananchi inadhani wenye mitaji ni lazima watoke nje ya nchi. Hili ni kosa kubwa sana.
Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uwekezaji ya Taifa-NICOL iliundwa na wazawa kwa ubunifu wao wakazunguka nchi nzima kukusanya mtaji kwa watanzania na walifanikiwa mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kufanya uwekezaji. Hoja ni kwanini Serikali inashindwa kuwaamini watanzania kuwa wawekezaji katika miradi mbalimbali ambayo ni dhahiri fedha za wananchi zinaweza kurudi haraka? Miradi kama ya reli ambayo mzigo wa kutoka na kurudi DRC ni wa uhakika, hivyo mtaji kurudi kwa wanahisa ni haraka. Miradi ya Umeme kwa kutumia maji ya mto Rufiji (Stiglers Gorge). Mtaji wa Kufufua shirika la Ndege la Tanzania, wakati tuna makampuni mengi ya wazawa yanayojihusisha na utalii (Tour Operators) na Taasisi zinazojihusisha na Utalii zilizo chini ya Serikali kama TANAPA, na NGORONGORO CONSERVATION AUTHORITY.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali imechoka kwa kukosa ubunifu wa jinsi ya kupata mtaji toka ndani ya nchi wakati kuna sheria ya PPP inayoruhusu uwekezaji wa pamoja na Sekta binafsi ambayo ni wananchi. Tunarudia tena WAZAWA WANA FEDHA ZA KUTOSHA KUENDESHA NCHI YAO BADALA YA KILA KUKICHA KUKIMBILIA NJE.

5. TAKWIMU

Mheshimiwa Spika, Takwimu ndio hitajio la kwanza katika kupanga mipango na katika kufanya tathmini ya mipango yako. Hivyo basi katika mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umasikini tumekuwa tukipatiwa takwimu zinazoonesha kuwa katika yale malengo mbalimbali ya kupunguza umasikini tuko katika hatua bora na ya kujivunia. Mfano taarifa ya Mkukuta ilikuwa inaonesha kuwa lile lengo la kuwapatia wananchi maji safi na salama kwa mwaka 2009 ilikwishafikia asilimia 57.8, lakini baada ya kupitia upya ikagundulika kwamba ni asilimia 40 tu. Hii maana yake nini? Hii ni hadaa kwa wananchi na wadau wa maendeleo kwa kutaka kuficha madhaifu au ni kutumia takwimu zisizo sahihi jambo ambalo linapelekea kupanga mipango ambayo haina uhalisia na kutunga sera ambazo haziwezi kututoa katika umasikini tulionao japokuwa fedha zipo lakini matumizi hayaendani na hali halisi.

6. MICHEZO NA SANAA

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipendekeza uendelezaji wa sekta ya michezo kama mojawapo ya vyanzo vya mapato nchini. Umuhimu wa

Serikali katika kuwekeza kwenye michezo, ni pamoja na kuongeza mapato, kutoa nafasi za ajira na pia katika kudumisha amani na utamaduni wa Mtanzania.

Shabaha kubwa ya uendelezaji wa viwanja vya michezo nchini ni katika kuijengea Serikali uwezo wa kukusanya mapato zaidi. Hii inawezekana kwa Serikali kuwekeza katika viwanja vya michezo vilivyopo ambavyo vimehodhiwa na chama tawala. Baadhi ya Viwanja vyenye uwezo wa kuliongezea taifa mapato makubwa ikiwa vitaendelezwa ni pamoja na uwanja wa Samora-Iringa, Sheikh Amri Abeid- Arusha, CCM Kirumba –Mwanza, Sokoine-Mbeya na Jamhuri-Dodoma. Kwa uchambuzi wa kina, viwanja hivyo vya michezo vimejengwa katika maeneo muhimu kishabaha, ambayo yana uwezo wa kuingizia taifa mapato kutokana na mwamko wa wananchi hasa katika michezo.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa kisasa wa Benjamin Mkapa maarufu kama uwanja wa Taifa ambao ulijengwa kwa kushirikiana na Serikali ya China kwa thamani ya Shilingi Bilioni 56.4, umeweza kuiongezea Serikali mapato kwa kiasi kikubwa kutokana na makusanyo yanayotokana na mechi za mpira wa miguu pekee. Kwa mujibu wa aliyekuwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mhe. Amos Makalla wakati akijibu swali Bungeni Aprili 2013, alieleza kuwa tangu Uwanja wa Taifa uanze kutumika mwezi Agosti, 2007 hadi kufikia mwezi Februari mwaka 2013, ulikuwa umeingiza shilingi 1,533,697,666 kwa makusanyo yanayopitia Wizara ya Habari, Vijana, Tamaduni na Michezo ambazo hizo ni nje ya mapato yanayokusanywa kupitia kodi ya ongezeko la thamani (VAT) yanayowasilishwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF).
Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa uwanja huu wa kisasa umeendelea kutumika kwa ajili ya michezo na matamasha mbalimbali, ukusanyaji wake wa mapato haujaridhisha kutokana na kutokuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato hali inayochangia ukusanyaji hafifu wa mapato na mianya ya ubadhirifu unaotokana na kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa kiteknolojia.

Kambi rasmi ya Upinzani, inapendekeza yafuatayo yafanyike ili kuweza kutumia sekta ya michezo kwa kupitia ujenzi wa viwanja vya kisasa vya michezo nchini na kuongeza ukusanyaji wa mapato;

Mosi, kuvirejesha viwanja vyote vya michezo vilivyohodhiwa na Chama cha Mapinduzi kwa Serikali ili viwe mali ya umma kama ambavyo viliwahi kuwa chini ya Baba wa Taifa.

Pili, kuviendeleza viwanja hivi kwa kuingia ubia na makampuni makubwa ya uwekezaji ama na nchi wahisani ili kurejesha hadhi ya viwanja vitakavyoendana na mahitaji ya kisasa ya viwango na ubora wa viwanja vya michezo.

Tatu, kuhakikisha kuwa uwanja wa Taifa hautumiki katika michezo ya aina yoyote bila ya mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ili kuzuia ubadhirifu wa mapato katika mechi mbalimbali unaofanywa na watendaji wasiowaaminifu.

Nne, kupunguza misamaha ya kodi katika makampuni makubwa na kwa walipa kodi wakubwa na fedha hizo zitumike kuboresha baadhi ya viwanja ili kuinua uchumi na kutoa fursa za ajira zitakazotokana na uwekezaji wa viwanja nchini.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta misamaha ya kodi ambayo kwa mwaka 2013/2014 ilifikia trilioni 1.5, ambapo kwa gharama ya shilingi bilioni 56.4 zilizotumika

kujenga uwanja wa taifa , misamaha hiyo ya kodi ya trilioni 11.5 zingeweza kujenga viwanja 27 vya kisasa nchini, 25 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara na viwanja viwili vya kisasa Zanzibar.

6.1. UENDELEZAJI WA SEKTA YA SANAA NCHINI

Mheshimiwa Spika, lengo la kuendeleza sanaa nchini ni kuongeza nafasi za ajira pamoja na kuongeza vipato ili kukuza uchumi nchini. Sanaa ikipewa kipaumble pamoja na kurasimishwa ina uwezo wa kuliongezea taifa mapato yatokanayo na kazi za wasanii kama ilivyo kwa soko la filamu nchini Nigeria. Mwanzoni mwa mwaka huu, Nigeria imetangazwa kuwa ndilo Taifa lenye uchumi mkubwa barani Africa na kuipita Afrika Kusini. Pato Ghafi la Ndani (Gross Domestic Product 'GDP') la Nigeria limefikia Dola Billion 509 huku lile la Afrika ya Kusini likifikia Dola Bilioni 322. Kwa mujibu wa Idara ya Takwimu ya Nigeria, Nigeria imekuwa Taifa lenye uchumi mkubwa Afrika baada ya wanauchumi wa nchi hiyo kuziongeza sekta za Mawasiliano na Filamu (Nollywood) kwenye takwimu.

Ni dhahiri kuwa soko la Filamu la Nigeria linatoa mchango mkubwa mno katika ukuaji wa uchumi wa nchi hiyo. Kabla ya hapo Nigeria ilionekana kama taifa linalotegemea zaidi uuzaji wa mafuta na ilikadiriwa kuwa pato la mafuta lilichangia asilimia 32 kwenye GDP lakini ripoti ya wanauchumi hivi karibuni imeonesha sasa pato la mafuta huchangia Asilimia 15 tu ya pato ghafi la ndani. Nollywood ndiyo sekta ya pili kwa kutoa ajira katika nchi ya Nigeria baada ya sekta ya kilimo, na mchango wake kwa Taifa ni mkubwa sana kwani ina thamani ya Naira bilioni 853.9 (Dola za Marekani bilioni 5.1). Hii ni ishara ya jinsi gani sekta ya filamu inavyoweza kukuza na kubadili uchumi wa nchi yoyote, kwa njia ya utoaji wa ajira kama itachukuliwa kwa umakini mkubwa. Matokeo ya kukubalika kwa sinema pia huwafanya watayarishaji wa sinema, waigizaji na watendaji wengine kuwa na heshima kwenye jamii na hata kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa sekta ya filamu ikiwa ni mojawapo ya kazi za sanaa ina umuhimu mkubwa katika kubadilisha sera za kiuchumi kuliko sasa ambapo Serikali inawatumia wasanii wa filamu kama daraja lao la kutimiza malengo ya kisiasa na si katika kuiboresha tasnia nzima ili kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Mojawapo ya mafanikio ambayo Serikali ya CCM imekua ikiyafanya wimbo ni pamoja na kulinda haki za wasanii na kazi zao, wakati huo huo Serikali hii imeshindwa kuandaa Sera ya Sanaa itakayorasimisha sekta hii katika mfumo wa kiuchumi. Aidha, Serikali haina takwimu za uhalisia wala utafiti wowote uliofanywa kuijua nguvu ya soko la sanaa nchini, hakuna miundombinu ya soko la sanaa, wala thamani ya mchango wa sekta hii katika uchumi wa taifa hautambuliwi ipasavyo. Kukosekana kwa hayo yote ni dhahiri kuwa kazi za sanaa hazilindwi, hazikuzwi, hazitangazwi, hazitambuliki na wala hazipewi umuhimu unaostahili kama ambavyo sekta iliyo rasmi inavyopaswa kuwa. Serikali imeshindwa kuitilia maanani, kuchukua hatua stahiki, kutoa takwimu halisi za mchango wa sekta hii kwenye uchumi wa taifa pamoja na ukuaji wa kasi wa sekta hii hali inayosababisha ishindwe kupata pato halisi linalotokana na sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Shughuli nyingi zinafanyika kiholela bila wahusika kuwa na hakimiliki na sehemu kubwa ya mchango wake kwa pato la taifa haijarekodiwa katika vitabu vya mapato vya taifa. Hii inaonesha kuwa mchango wa sekta hii katika pato la taifa ni mkubwa zaidi kuliko takwimu zinavyoonyesha. Ili kama Taifa, tuweze kupiga hatua na kuimarisha sekta ya hakimiliki ni lazima sasa serikali iache porojo za kuwaongopea wasanii kuwa wanautambua mchango wao, bali ielekeze nguvu kuhakikisha kuwa sera madhubuti za kusimamia sekta ya sanaa nchini zinatungwa pamoja na sheria na kanuni zinazostahiki ili kuboresha uendeshaji wa sekta hii nchini. Uwepo wa sera bora zitachochea maendeleo ya kisekta, mazingira ya ubunifu yenye ushindani na salama ambayo serikali itayatumia kuendeleza sekta hii na kutambua thamani ya kazi za ubunifu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya hakimiliki nchini mwaka 2009 ilichangia kiasi cha Sh676 bilioni sawa na asilimia 4.6 ya Pato la Taifa (GDP), likiwa ni zaidi katika uchumi wa taifa kuliko sekta ya hoteli, migahawa na madini. Taarifa hiyo ambayo imetolewa hivi karibuni kwa lugha ya Kiingereza ikiwa na jina: 'The Economic Contribution of Copyright-Based Industries' kwa mwaka 2012, imebainisha kwamba sekta ya madini imechangia asilimia 2.6 ya GDP wakati hoteli na migahawa imechangia asilimia 4.5, sekta ya hakimiliki imefanya vyema. Pia sekta hii imeajiri watu wengi zaidi ya wale walioajiriwa na sekta ya afya na ustawi wa jamii, fedha, majumba ya kukodisha, huduma za biashara, ujenzi, usafirishaji, mawasiliano, madini, umeme, gesi na sekta ya maji. Mchango wa sekta ya hakimiliki kwa malipo ya wafanyakazi, ulikuwa Sh 80.474 bilioni sawa na asilimia 5.

Aidha, nchi kadhaa ambazo sasa zimeendelea zilikuwa na uchumi sawa na Tanganyika (sasa Tanzania) wakati tukipata uhuru mwaka 1961, nchi hizo ni pamoja na Singapore, Korea Kusini, Thailand, Malaysia na kadhalika, ila kilichowafanya kutuacha kimaendeleo na kupata maendeleo ya haraka ni ulinzi na uendelezaji wa Miliki Bunifu katika kazi za sanaa. Leo hii Korea Kusini imekuwa ni Taifa kubwa na lenye mchango katika kazi za sanaa Barani Asia kwa sababu tu ya kulitambua kundi la wasanii na kuweka mazingira mazuri ya ulinzi wa Miliki Bunifu kiasi cha kubatizwa jina la Marekani ya Asia. Korea imefanikiwa sana kueneza utamaduni wake katika nchi zingine za Asia, na walitumia fursa ya mtikisiko wa kiuchumi uliozikumba nchi za Asia mwaka 1997, ambapo wao waliamua kuwekeza katika sanaa na utamaduni kwa lengo la kuzalisha na kuuza nje kama bidhaa. Hata Rais wa wakati huo, Kim Dae-jung, alipenda kujiita Rais wa Utamaduni na alianzisha mradi huo na kutenga dola za Kimarekani milioni 148.5. Leo hii, Tanzania inashindwa nini katika kuirasimisha sanaa ambayo CCM inaitumia kujipatia kura?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaelekeza nguvu zake za kuhakikisha kuwa muswada wa Sera ya sanaa unaletwa Bungeni ili kufanikisha utungaji wa Sheria na Kanuni utakaongoza kazi mbalimbali za sanaa nchini ili kuweza kuongeza fursa za ajira na ukusanyaji wa mapato kwa taifa zima kwa ujumla.

7. MAENEO YA KIPAUMBELE KATIKA MWAKA WA 2014/15

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mpango huu umeainisha maeneo ya kitaifa ya kimkakati kwa mwaka wa 2014/15 ambayo ni miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, huduma za fedha na utalii huku maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi yakiwa ni elimu/mafunzo ya ufundi, afya na ustawi wa jamii, mifugo na uvuvi, misitu na wanyamapori ,madini, ardhi, nyumba na makazi, usafiri wa anga, hali ya hewa, biashara na masoko, ushirikiano wa kikanda na kimataifa, utawala bora, vitambulisho vya taifa, sensa ya watu na makazi, kazi na ajira pamoja na mazingira.

8. REAL ESTATE REGULATORY AUTHORITY

Mheshimiwa Spika, katika ushauri wetu kwa bajeti ya mpango iliyopita tuliitaka Serikali kuanzisha mamlaka ya kudhibiti sekta hii kwani fedha nyingi za kodi ya majengo na kodi ya ardhi (Property tax and Land Rent) hazikusanywi na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa mamlaka hii ni dhahiri kodi itakusanywa kulingana na ardhi ilipo katika miji na majiji (land value depend on location). Ni ukweli kwamba tumekuwa tukikosa mapato mengi sana kutokana na kukosekana kwa mdhibiti katika sekta hii ya ardhi yenye majengo.

9. KUKUZA UCHUMI VIJIJINI (Rural growth)

Mheshimiwa Spika, kukuza uchumi vijiji ni kipaumbele cha kwanza kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka kadhaa iliyopita na kitaendelea kuwa kipaumbele chetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa kama mkatakati utawekwa kwa kila Halmashauri za vijijiji za kutengeneza mazingira ya kutoa ajira rasmi zipatazo mia tano kila mwaka basi zitakuwa zimepiga hatua kukabiliana na wimbi kubwa la vijana kukimbilia mijini kwa ajili ya kutafuta ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mazingira ya vijijini yanatofautiana na kwa kuwa rasilimali zilizo katika maeneo ya wilaya za vijijini zinatafoutiana pia kati ya wilaya na wilaya, hivyo basi Serikali kuu inatakiwa kuweka kiwango mkakati (threshold) cha maendeleo kinachotakiwa kufikiwa na kila Wilaya kulingana na fedha zilizotengwa kwa ajili kukuza uchumi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii, mabadiliko ya kimaendeleo yataonekana zaidi kuanzisha mifuko ya uwezeshaji ambayo wanafaikaji ni wale waishio mijini zaidi na kwa upande wa wilayani ni wale wenye uwezo tayari.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imeainisha maeneo yafuatayo kama vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo:

1. Kukuza Uchumi Vijijini
2. Miundombinu na Usafiri wa anga
3. Ardhi, Nyumba na Makaazi
4. Elimu na Afya
5. Michezo na Sanaa

10. UGHARAMIAJI WA MPANGO

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa serikali kwa mwaka 2014/2015 ni dira ya kuakisi mpango wa kibajeti kwa mwaka 2014/2015, na ili kuweza kutekeleza mpango kwa ufanisi ni dhahiri kuwepo kwa umuhimu wa kubainisha vyanzo vya mapato vya uhakika ambavyo vitawezesha kugharimia miradi ya maendeleo inayokusudiwa, kuna haja ya serikali sasa kutafakari kwa kina na kuona kazi kubwa inayofanywa na kambi rasmi ya upinzani bungeni kuishauri serikali juu ya uongezaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti kila mwaka inaweza kuijengea heshma nchi yetu na pia kuboresha huduma kwa wananchi wake na si kwa kutegemea mapato ya nje ambayo yameendelea kuidhoofisha nchi yetu mbele ya uso wa dunia kwa kuwa taifa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inapendekeza kukusanya mapato ya ndani 25% ya GDP ili kuweza kuendesha miradi yetu wenyewe. Uwezo wa makusanyo hadi kufikia hapo tunao, kwanza ni kupambana na makampuni makubwa ya kimataifa ili yalipe kodi stahiki na kuacha ujanja wa kukwepa kodi, kuondoa misamaha ya kodi na kuzuia upoteaji mapato ya ndani, Kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi wa kada zote kulipa kodi kwa kuwawekea mazingira wezeshi na aminisho ya matumizi ya kodi zao. Ni dhahiri kuwa mapato ya ndani yaweza kutekeleza vipaumbele vyetu ili kukabiliana na matatizo tuliyoainisha.

Mheshimiwa Spika, katika miaka kadhaa kambi rasmi ya upinzani bungeni kwa nia njema ya kuijenga nchi yetu ilipendekeza mambo kadhaa ili kuweza kuongeza mapato ya serikali na

moja ya mambo yaliyopendekezwa ni kuhakikisha kwamba serikali inakusanya kodi kwa kiwango cha asilimia 30 kama 'ongezeko la mtaji' ('capital gains') kutokana na mauziano ya Kampuni yoyote ambayo mali zake zipo Tanzania. Je, utekelezaji wa ushauri huo umefika wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja ya pato la Taifa kama wenzetu wa Uganda na Kenya. Serikali ilikubaliana na pendekezo hili kwa maneno lakini imeshindwa kulitekeleza licha ya kutoa ahadi za kufanya hivyo kila mwaka. Hivi sasa misamaha ya kodi imefikia asilimia 4.1 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, bajeti mbadala itatoa mgawanyo wa fedha kwa vipaumbele hivyo katika utekelezaji wake.

11. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenye wachumi wazuri na waliobobea na ukweli ni kwamba nchi jirani zimekuwa zikipanga mipango yake kwa kutumia wataalam wetu. Ni ukweli kwamba mipango ya hao wanaotumia mipango na wataalam wetu wameendelea kuliko sisi. Hoja kubwa ya kujiuliza ni kwanini kama mipango mizuri tunayo na wataalam tunao mambo hayaonekani kuwa yanasonga mbele?

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi hapa ni kuwa nchi zilizoendelea uchumi ndio unatakiwa kuongoza mfumo wa siasa, lakini kwetu sisi siasa ndio inaongoza mfumo wa uchumi kwa maana mipango yetu inapangwa kwa kuangalia zaidi matakwa ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujikita zaidi kwenye kutekeleza mpango na sio kwenda kwa matakwa ya viongozi wa kisiasa kama inavyofanya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, ni aibu kubwa kwa nchi makini na tajiri kama Tanzania kuendelea kupangisha ofisi kwa ajili ya mabalozi wake nje ya nchi wakati nchi inamiliki viwanja katika mataifa hayo, Serikali pia imeendelea kupanga nyumba za watumishi na maofisi kwa gharama za juu. Aidha, katika hilo ni kwa vipi nchi makini inauza nyumba za watumishi wake hasa madaktari na kuwapatia viwanja vya kujenga nyumba zao maeneo ya mbali na sehemu wanazotolea huduma. Hii ndiyo mipango ya Serikali ya CCM au ni wizi wa viongozi Serikali? Hujuma hizi kwa taifa zinazofanywa na Mawaziri waliopewa dhamana ya kusimamia raslimali za watanzania lakini wanashindwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Mawaziri wahusika wajipime kama kweli bado wanafaa kuendelea kuwa watumishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira tatanishi kama haya ni lini tunaweza kujitapa kuwa tunafikia malengo ya milenia?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Esther Nicholas Matiko(Mb)
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-
Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu
16.06.2014

NAIBU SPIKA: Tunao wageni wa Mheshimiwa Ezekiah Chibulunje kutoka kule Itiso, ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Itiso, wapatao 40 wakiwa na Walimu wao, walikuwa hawapo asubuhi nilipowatambulisha, nawaomba wasimame pale walipo wanafunzi waliotoka Itiso. Karibuni sana wanafunzi wa Itiso na Walimu, karibuni hapa Bungeni, mjifunze mambo yanavoendelea, Mbunge wenu Mheshimiwa Chibulunje anajitahidi, anafanya kazi vizuri sana hapa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wahehimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na michango yetu. Kabla sijamwita Mheshimiwa Mbatia, nilimwona Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed. Mheshimiwa Ally Kessy, unaweza ukasimama hapo ulipo. Mheshimiwa Ally Kessy amepiga *suit* leo. *(Makofi)*

Sasa ni mabadiliko makubwa, niliona niwajulishe Waheshimiwa Wabunge, sijui kuna nini leo, Mheshimiwa Ally Kessy, ameamua kubadilisha viwango. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed alisimama na kuonekana Bungeni)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Kessy, tunakushukuru unaweza ukakaa tu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Kwa Waheshimiwa wengine basi natoa wito na sisi tubadilike kidogo, tuelekee huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa James Mbatia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani upande wa Wizara ya Fedha, nakuomba sasa ukaribie, utoe hotuba yako na tumekupangia dakika 40. Karibu sana Mheshimiwa Mbatia!

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ni siku ya Mtoto wa Afrika, napenda niwatakie watoto wote wa Tanzania na Afrika nzima, Heri ya Siku ya Mtoto wa Afrika na urithi pekee tunaoweza kuwapatia watoto wetu ni elimu bora. Kwa namna ya pekee niwatakie watoto wangu Janeth, Joyce na Andrew, heri ya siku ya mtoto wa Afrika na Mama yao Catherine tunaendelea kushirikiana kuwalea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatia maoni haya kwa mujibu wa Kanuni ya 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na siha njema ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Makadiiro ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda tena kumshukuru Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli katika Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai kuwa Naibu Waziri Kivuli katika Wizara hii. Aidha, shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Christina Lissu, Naibu Waziri katika Wizara hii, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri Vivuli, kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani na viongozi wenzangu kutoka katika Vyama vya CHADEMA, *CUF* na *NCCR*-Mageuzi, kwa ushauri na maoni yao yaliyofanikisha kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sera za Bajeti ya mwaka 2013/2014. Sera ya Mapato. Serikali ilikusudia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 18.249, kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Hadi tarehe 30 Aprili, 2014 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi trilioni 12.882. Makusanyo hayo yanadhihirisha nakisi ya shilingi bilioni 5.475, ambayo ni sawa na asilimia 30 ya Bajeti ya Mwaka 2013/2014. Kwa hiyo, katika miezi miwili iliyobaki ni dhahiri nakisi hii haitaweza kufikiwa. Huu ni uthibitisho wa kushindwa kwa Serikali kusimamia vizuri mapato na kwa mujibu wa Kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, ilikusudia kutumia shilingi bilioni 5,645 kwenye matumizi ya maendeleo na shilingi bilioni 12,604 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2014, jumla ya shilingi bilioni 3,115 ziliidhinishwa na kutolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na Makadirio ya shilingi bilioni 5,645. Kiasi hiki ni sawa na wastani wa asilimia 55 tu ya Bajeti hiyo ya maendeleo. Hata hivyo, matumizi ya kawaida yaliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 13,034.7, sawa na asilimia 71 ya Makadirio ya Mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi zilizowasilishwa Bungeni, kipaumbele cha Serikali kinaonekana kuwekwa zaidi kwenye matumizi ya kawaida ya Serikali, kuliko matumizi ya maendeleo. Hali hii imekuwa ikirudia mara kwa mara kwa Serikali yetu, kuweka kipaumbele kwenye matumizi ya kawaida na kushindwa kuweka kipaumbele kwenye Miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilipendekeza, yako mengi, yako kwenye hotuba yangu, lakini nitasema machache, kwamba **kufuatia** shilingi bilioni 619.8, kuongezwa kwenye deni la Taifa. Serikali ilishauriwa pia kutenganisha deni halisi la Taifa na matumizi mengine yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza Fungu hili la deni la Taifa na Mafungu mengine yatenganishwe na mengine yaingizwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Mpaka sasa Serikali haijatoa taarifa rasmi ya uekelezaji fasaha wa mapendekezo hayo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani, ilipendekeza kiwango cha kodi ya Mapato, (*Pay As you Earn)*, kishuke kutoka asilimia 14, iliyokuwepo wakati huo, ili iweze ikafikia tarakimu moja ya asilimia tisa na kuwa kodi hiyo itozwe kwa mtu anayepata mshahara unaozidi shilingi 250,000/=. Pendekezo hili lilifanyiwa kazi kwa kushusha hadi asilimia 12 kwenye Bajeti ya mwaka 2014, lakini pendekezo hili, halijatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia ilipendekeza kwa Serikali, iache kuchukua mikopo yenye masharti ya kibiashara, badala yake vyanzo vya mapato, vilipendekezwa ili kuondokana na adha ya madeni ya ndani na ya nje. Pendekezo hili halijazingatiwa kwa sababu Bajeti ya mwaka 2014/2015, imeendelea kuonesha dira ya Serikali kukopa fedha kwa kiwango cha riba za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulipendekeza kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Mtwara, (Mtwara *University for Petroleum Studies),* ili kutayarisha wataalam wa kutosha wa Sekta ya Mafuta na Gesi na kuliandaa Taifa kuwa na wtaalam katika maeneo hayo na hivyo Taifa kuweza kutumia utajiri wa mafuta na gesi uliopo katika nchi yetu. Pendekezo hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulipendekeza kuanzishwa kwa Pensheni ya Uzeeni kwa Wazee wote wa nchi yetu wenye umri wa zaidi ya miaka 60, kwa kuwa walitumikia Taifa hili kwa

uadilifu, uaminifu na uzalendo mkubwa. Serikali mpaka sasa haijaweza kutekeleza pendekezo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza pia kushushwa kwa tozo ya kuendeleza *study (Skill Development Levy)* kutoka asilimia sita ya sasa mpaka asilimia nne. Katika pendekezo hili, tulishauri Serikali, waajiri wote walipe kodi hii ikiwemo Serikali na Mashirika ya Umma. Serikali ilichukua pendekezo hili, kwenye mapendekezo yake ya Bajeti ya mwaka 2013/2014, lakini bila kuhusisha Mwajiri Mkuu yaani Serikali. Ni vema kodi hii ilipwe na waajiri wote nchini ili ishuke kwa asilimia iliyo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa limeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa kasi kubwa sana, hali ambayo inatishia ustawi wa Taifa kama halitasimamiwa kwa umakini na haraka. Hotuba ya Waziri wa Fedha, inaonesha kwamba hadi kufikia Machi, 2014, deni la Taifa lilifikia shilingi Trilioni 30.563, ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 23.674 katika mwezi Machi, 2013. Hili ni ongezeko la takriban shilingi trilioni saba, ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 29 ya deni la Taifa kwa kipindi cha mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ongezeko la mikopo la takriban shilingi trilioni saba kwa mwaka mmoja tu, halijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. Ongezeko hili la takriban shilingi trilioni saba, ni sawa na Bajeti nzima, *full Budget* ya mwaka 2008/2009, ambayo ilikuwa ni shilingi trilioni 6.8. Ikumbukwe kuwa mwaka 2008/2009, ni miaka mitano tu iliyopita, ukopaji wa namna hii unatishia uchumi na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu na hotuba za Bajeti za miaka iliyopita za Mawaziri wa Fedha, Deni la Taifa limeongezeka kwa kasi kutoka shilingi trilioni 9.3 mwaka 2007/2008, hadi shilingi trilioni 30.6 mwaka 2013/20014. Hii ni wazi kuwa deni liliongezeka kwa kiasi cha shilingi trilioni 21.3. Serikali imelipa shilingi trilioni nne na kufanya fedha zilizokopwa kuwa jumla ya shilingi trilioni 25.3 katika kipindi hicho cha miaka saba tu. Huu ni ukopaji hatarishi kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya deni hili kuwa hatarishi kwa uchumi wa Taifa, Serikali bado inatajaria kuongeza deni hilo kwa kukopa shilingi trilioni 4.3 kama ilivyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeonesha kushindwa kulipa deni hilo kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato, badala yake imekuwa ikikopa ili kulipa deni. Mfano, hotuba ya bajeti ya mwaka 2014/2015 imeonesha kuwa katika shilingi trilioni 1.8 zilizokopwa katika soko la ndani, zaidi ya shilingi trilioni 1.1 zilitumika kulipa madeni ya hati fungani wakati shilingi trilioni 0.69 tu tuziliwekwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kiashiria cha karibu sana kwa Serikali kufilisika. Kukopa mikopo ya kibiashara yenye riba kubwa ili kulipa mikopo yenye riba ndogo au kwa uendeshaji wa kawaida wa Serikali au Taasisi zake ni kiashiria cha kutosha kuainisha maamuzi yasiyo na uelewa wa kawaida sana wa utawala na usimamizi wa fedha. Mikopo ya kibiashara hutafutwa kwa matumizi ya uwekezaji kwenye sekta ya maendeleo na siyo ya ulaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchumi unaokua kwa wastani wa asilimia kati 6.5 na saba kwa mwaka, ni vigumu sana kuweza kulipa deni la Taifa linalokua kwa wastani wa asilimia kati ya 15 na 30 kwa mwaka. Bila kuwa na vyanzo vipya vya mapato au kusamehewa deni hili itakuwa vigumu sana kuweza kulipa deni hilo kikamilifu. Hii ni kwa sababu uwiano wa ukuaji wa uchumi hauendani na kasi ya ukuaji wa deni hata kidogo. Pamoja na upungufu wote huu,

Serikali imeendelea kujitapa kuwa inakopesheka na hivyo kuashiria kutokuwepo na hofu yoyote ya kukopa huku kwa ukopaji wa kiholela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha zaidi ni kuwa, sehemu kubwa ya mikopo hii inakopwa katika soko la ndani. Hali hii imekuwa ikileta ushindani mkubwa kwa wananchi na wajasiriamali wanaotaka kukopa ili kukuza mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa mengi duniani yanakopa na yana madeni makubwa. Suala la msingi la kutofautisha nchi moja na nyingine ni kasi ya kukua kwa deni husika na matumizi ya mkopo huo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza na kutaka majibu kutoka kwa Serikali, matumizi ya fedha zilizokopwa na nchi yetu ndani ya miaka saba ni yapi na yameleta maendeleo kiasi gani kwa Taifa *(value for money)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa bei za soko kuhusu trekta moja ambazo Serikali imeziidhinisha kuwa ziuzwe hapa nchini kwa ajili ya kilimo kupitia mradi wa Taifa wa Kilimo Kwanza, ni wastani wa shilingi milioni 30 kwa trekta moja lenye ubora wa hali ya juu. Endapo fedha zilizokopwa kwa miaka saba, shilingi trilioni 25.3, zingetumika kuweka kipaumbele katika kilimo na kununua matrekta ya kisasa yenye ubora wa hali ya juu, ni dhahiri Serikali ilikuwa na uwezo wa kununua matrekta 843,333.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kata tulizonazo hapa Tanzania takribani (3000), Matrekta hayo yangeweza kugawiwa kwa kila Kata kupata trekta 281. Hakika kama hili lingetendeka, Taifa letu lingekuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa kuzalisha chakula duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo fedha zilizokopwa kwa kipindi cha miaka saba zingetumiwa katika sekta ya elimu, kila mwanafunzi anayesoma hapa nchini yaani kuanzia shule ya msingi hadi Chuo kikuu, angeweza kutengewa milioni mbili na laki tatu (shilingi milioni 2.318) kwa ajili ya shule. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za sasa kuwa asilimia 23 ya Watanzania wote, ambao ni takriban wanafunzi 10,350,000 wako katika shule za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa Bunge lako Tukufu litunge Sheria ya Bajeti haraka iwezekanavyo ili iweze kudhibiti ukopaji na matumizi ya mikopo ya Serikali. Vile vile tunapendekeza kuwa, katika sheria hiyo iwe lazima kwa Serikali kupata kibali kutoka katika Bunge lako Tukufu kabla ya kuweza kukopa kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/2015, matarajio ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni:-

(i) Sera ya mapato na matumizi ya serikali *(fiscal policy)* ambayo inalenga kukidhi mahitaji ya muda mfupi, wa kati na yale ya muda mrefu na yenye mikakati mahususi ya kukuza uchumi wetu.

(ii) Bajeti inayotoa kipaumbele kwa sekta ambazo ndio kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi, ajira na hatimaye kupunguza umaskini. Sekta kama vile elimu, kilimo, nishati, miundominu na utalii.

(iii) Bajeti inayoainisha bayana mikakati madhubuti ya kuzuia matumizi ya anasa, ubadhirifu na rushwa katika manunuzi ya umma.

(iv) Bajeti ambayo inaonesha mikakati maalum ya kuongeza wigo wa walipa kodi kutoka idadi ndogo iliyopo hivi sasa.

(v) Bajeti ambayo inahimiza utekelezaji kwa vitendo, Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

(vi) Mikakati endelevu wa kuratibu na kupunguza ukuaji wa sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za mapato mwaka 2014/2015; Serikali imefanya mabadiliko katika sera zake za kuongeza vyanzo vya mapato na kuondoa baadhi ya mikakati ya mwaka uliopita ikiwemo ile ambayo iliyoanza kutumika mwaka wa fedha wa 2013/14. Kwa mfano:-

(i) Kuongeza kiwango cha kutozwa kodi kwa wafanyabishara wadogo wadogo, ambao wengi ni wale wasio rasmi kutoka asilimia moja hadi asilimia mbili ya mapato ghafi ya kati ya shilingi 4,000,000/= hadi 7,500,000/= kwa mwaka. Hatua hii ya Serikali itasababisha wafanyabishara wadogo wadogo, kukwepa kulipa kodi na hivyo kudumaza ukuaji wa biashara ndogo ndogo ambazo ni chanzo kimojawapo cha uhakika cha ajira nchini.

(ii) Kufuta misamaha ya kodi ya zuio kwa ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakaazi. Ni hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba misamaha ya kodi isiyo na tija ya ukuaji wa uchumi ifutwe, lakini utekelezaji wake lazima uzingatie sekta na sekta. Kufuta msamaha wa kodi ya zuio kwa wanaokodisha ndege kutaathiri sana sekta ya usafiri wa anga na utalii kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii bado iko chini kibiashara, ikilinganishwa na baadhi ya nchi za wenzetu katika Kanda ya Afrika Mashariki na nchi za SADC (Mfano, Kenya, Rwanda, Afrika Kusini na kadhalika). Hakuna shirika la ndege hapa Tanzania lenye uwezo wa kununua ndege mpya za kisasa, ndege zilizo nyingi ni za kukodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa msamaha huu itabidi nauli za ndege zipande kwa mfano hivi sasa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma nauli hiyo ni sawa na kutoka Dar es Salaam kwenda Dubai na hivyo kuathiri ukuaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kwa upande mwingine Serikali inaendelea kwa kasi kubwa ya kujenga viwanja vya ndege hapa nchini kwa upande mwingine inaua sekta ya anga. Mfano, mwezi uliopita, jirani zetu wa Kenya wametangaza mikakati madhubuti ya kukuza utalii wa ndani na wa nje, ukiwemo wa kupunguza ushuru wa kutua uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta kwa asilimia 40. Hii ni hatua kubwa ya ushindani katika sekta ya Utalii, ukizingatia kwamba Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa vivutio vya utalii duniani na kwa sasa *GDP* yetu kutoka Utalii ni 17.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya sera ambayo hayazingatii ukuaji wa biashara. Kwa mfano, tangu tumepata uhuru kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, bajeti yetu imekuwa ikitegemea mapato ya soda, sigara, bia na sasa juisi na chibuku. Ni vema hatua hii ikaangaliwa kwa mapana yake kwani inaongeza athari kwenye afya za Watanzania, hasa wale wa kipato cha chini na hili analijua sana Mbunge wa Rombo Mheshimiwa Joseph Selasini inavyoathiri wanaume kwenye Jimbo lake katika nguvu za uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hakuna msisitizo wa dhati *(affirmative action)* wa kufufua viwanda vya vidogo vidogo yaani *textile* na ngozi *(leather)* ambavyo vingelipewa unafuu wa kodi katika nyanja mbalimbali za uwezekezaji katika sekta hizi.

Badiliko linalopendekezwa katika aya ya 95 ni kwamba, ('Taasisi za kidini kwa waajiriwa wake ambao ni mahsusi kwa kuendesha ibada tu'. Tunaomba ufafanuzi wa kina wa kusudio hili, kwani taasisi za kidini zilizo nyingi zimekuwa zikifanya kazi nzuri ya kutoa huduma muhimu za kukuza Utu wa Binadamu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Matumizi; ili bajeti iweze kutekelezwa kwa ufanisi ni lazima ioneshe madeni yatakayoingia nayo katika mwaka mpya wa fedha na namna ambavyo madeni hayo yatalipwa. Katika hotuba ya bajeti kwa mwaka 2014/2015, Serikali imelieleza Bunge lako Tukufu namna ambavyo sekta mbalimbali za maendeleo zitagawiwa fedha, lakini hatujaelezwa juu ya madeni ya kila sekta yenye jumla ya zaidi ya shilingi trilioni mbili ambayo hayakulipwa katika bajeti ya 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mengine ni matumizi ya anasa ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kubwa. Karibu viongozi wote wa ngazi za Wakurungezi, Makamishna, Makatibu Wakuu na Mawaziri wananunua na kutumia magari ya anasa ya kifahari yaani *Toyota Landcruiser V8* (licha ya kuwa thamani ya kila gari moja la aina hiyo ni zaidi ya shilingi milioni 280, pia gharama ya kuyaendesha ni ya ghali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa bajeti umeelezwa vizuri na Waziri Kivuli wa masuala ya Bajeti. Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao sasa umefikia miaka minne ya utekelezaji wake, malengo muhimu ya mpango huu ni kukuza uchumi wa nchi, ambao kama Taifa tulijiwekea malengo ya kukua hadi kufikia asilimia nane kwa mwaka *(8% GDP growth per annum*) ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha malengo ya mpango wa miaka mitano yaani mwaka 2011/2012 mpaka 2015/2016, lengo ni kufikia asilimia kumi (10%) ya pato la Taifa kwa kila mwaka, kuanzia mwaka 2016 mpaka mwaka 2025 - Dira ya Maendeleo ya Taifa. Ukisoma mpango wa Serikali utaona upo uwezekano wa kufikia lengo, lakini ukisoma utekelezaji wake ni tofauti na malengo ya mipango wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lililo dhahiri kwa viongozi walio wengi, hufanya matumizi ya anasa na kulipana posho kubwa, wakati wananchi walio wengi hawapati huduma muhimu? Tunatakiwa kujiuliza, je, kwa mwenendo tunaokwenda nao malengo haya yatafikiwa? Swali hili ni la msingi tukizingatia kwamba Mpango huu wa Miaka Mitano ni sehemu ya Dira ya Taifa ya 2025, ambayo inalenga kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye kipato cha kati yaani kufikia Dola 3,000 ifikapo 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha zaidi ya miaka 50 cha utekelezaji wa bajeti Serikali, inayoongozwa na CCM, haijafanikiwa kuwa na bajeti yenye uhalisia wa kupunguza umaskini wa Watanzania, kwani Bajeti inayolenga kupunguza umaskini inatakiwa iwe ni ile ambayo inayolenga kupunguza mzigo wa kodi kwa wananchi,ni ile ambayo inatengeneza ajira nyingi kwa wananchi wake, ni ile ambayo inakuza uwekezaji hasa wa ndani, ni ile inayomfanya *Mtanzania* aweze kuweka akiba,ni ile ambayo inalenga kuinua maisha ya walio wengi ambao wako Vijijini ni ile inayolenga uchumi wa nchi umilikiwe kwa asilimia iliyo kubwa na wananchi wake, ni ile inayolenga kukuza ujasiriamali na ni ile inayokuza ulaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta na ajira kwa Vijana; kwa muda mrefu sasa suala la ajira kwa vijana limejadiliwa katika Bunge hili Tukufu, lakini halijapatiwa bajeti ya kutosha. Ni jambo lililo wazi kwamba litaendelea kuwa ni tatizo kwa la Taifa na hatimae kuwa ni bomu linalosubiriwa kulipuka wakati wowote. Upo umuhimu wa kulitafutia ufumbuzi wa kibajeti jambo hili kwani vijana ndiyo rasilimali kazi kuu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vipaumbele vya Taifa; mtavisoma vyote katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti mbadala ya Upinzani; Bajeti Mbadala ya Upinzani 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua uwepo wa vyanzo vingi vya mapato kwa Taifa kama vile kodi, gharama za leseni na vibali mbalimbali, tozo na ushuru kwenye huduma mbalimbali zitolewazo na Serikali pamoja na asasi zake. Katika mapato yatokanayo na kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo:-

(i) Asasi zote zinazokusanya mapato ya Serikali ziongezewe uwezo kwa kuwekeza mfumo wa kisasa utakaosaidia fedha zote zinazokusanywa kuwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

(ii) Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* iboreshwe zaidi.

(iii) Bodi ya Rufaa za Kodi pamoja na Baraza la Rufaa za Kodi nchini ziboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato yasiyotokana na kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza:-

(a) Ukanda wa uwekezaji kwa ajili ya kukuza bidhaa na kuuza nje ya nchi uboreshwe.

(b) Kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na wamiliki wa majengo na ardhi.

(c) Kuboresha makusanyo ya mapato katika maliasili za Taifa kama vile madini, misitu na bahari kuu.

(d) Kuboresha ufanisi wa bandari ili bandari itumike kama kituo kikuu cha kuingizia bidhaa kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa taarifa zinaonesha kuwa Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali kuongeza mapato, bado zipo fursa nyingi za kuongeza mapato ya Serikali ambazo hazijafanyiwa kazi. Hali hii imepelekea kushindwa kukusanya mapato yanayokusudiwa na hivyo kufanya tushindwe kutekeleza bajeti kwa mapato yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mapya ya kuongeza mapato; kodi kwa sekta isiyo rasmi; wachimbaji wa madini, maelezo yake yako katika hotuba yangu; mapato ya kodi ya ardhi na maliasili, mauzo ya mazao ya misitu, uvuvi, mapato ya uwindaji wa kitalii, mrabaha wa wa madini yaani *loyalties*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kulingana na taarifa za Kamati ya Taifa ya Tanzania *Extractive Industry Transparency Initiative (TEITI)*, mbinu chafu na usiri ni miongoni mwa mambo yanayogubika sekta ya uchimbaji madini. *TEITI* imeweka wazi pia kuwa kuna tofauti kubwa kati ya mipango ya viwango vinavyoripotiwa kulipwa na Makampuni ya Madini na zile za Serikali kama mrabaha, huku makampuni yakionesha yanalipa fedha nyingi kuliko Serikali inavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ya kodi kuna Taasisi za Kibiashara za Serikali nimeziorodhesha zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari zetu Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar zikiendeshwa kwa mradi wa ubia yaani *Public Private Partenership"- PPP* zinaweza

kuongeza mapato na hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 1.8 kwa mujibu wa taarifa za Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato Mbadala; Kudhibiti ukwepaji Kodi na udanganyifu trilioni 1.831; Kuongeza ufanisi wa *TRA* bilioni 708; Kudhibiti Misamaha ya kodi trilioni 1.386; Kuongeza ufanisi Bandari ya Dar es Salaam kwa 50% trilioni 1.44;, Pesa – Fasta, tozo la 15% kwenye faida ya Wakala wa Makampuni bilioni 268.8; Tozo ya 1% mpya tunayopendekeza ya manunuzi yote ya nje na tozo ya 0.5% ya mauzo yote ya nje itatengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Reli yaani *Special Railways Development Levy* tutapata bilioni 226.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mrabaha wa 5% kwenye uvuvi wa samaki katika bahari kuu mwaka huu ni meli 68 zimepewa leseni. Ukichukua Mrahaba kwa 5% wa *Tuna Fish* kilo moja ni kati ya Dola tano na Dola saba, unachukua Dola tano utapata zaidi ya bilioni 14.025; Marekebisho ya kodi sekta ya misitu bilioni 240.416 na jumla ya vyanzo mbadala ni Trilioni 6.154.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Bajeti, Mapato. Mapato ya ndani asilimia 84, sawa na shilingi trilioni 18.372. Mapato ya kdi yanayokusanywa na *TRA* shilingi trilioni 17.272; Mapato yasiyo ya kodi shilingi 1.099; Mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 458.4; Mikopo na misaada ya kibajeti shilingi 922; Mikopo na Misaada ya miradi ya maendeleo ikijumuisha *MCT* shilingi trilioni 2.019. Jumla ya misaada na mikopo ya nje ni shilingi trilioni 2.941. Jumla ya mapato yote ni sh. 21,772, 867,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida asilimia 57.33 sawa na shilingi trilioni 12.482; Deni la Taifa asilimia 19 sawasawa na shilingi 4.152; Mishahara asilimia 27 sawa na shilingi trilioni 6.037; matumizi mengineyo asilimia 10.5 sawa na shilingi trilioni 2.292; Wizara shilingi trilioni 1.876; Mikoa shilingi bilioni 45.853; Halmashauri shilingi bilioni 366.829; matumizi ya maendeleo asilimia 42.6 sawa na shilingi trilioni 9.29; fedha za ndani shilingi trilioni 6.38 na fedha za nje shilingi trilioni 2.941. Jumla ya matumizi yote ni sh. 21,772, 867,000,000. Limeoneshwa jedwali la ulinganisho kati ya bajeti ya Serikali na ile inayopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa mapato ya fedha za Maendeleo, kukuza uchumi vijijini *(rural growth)* asilimia 35.3, kwenye maendeleo sawa na shilingi trilioni 3.279; Miundombinu na usafiri wa anga asilimia 17.8 sawa na shilingi 1.653; Ardhi, Nyumba na Makazi asilimia 12 sawa na shilingi trilioni 1.17; Huduma za Jamii kama vile Elimu na Afya, shilingi trilioni 2.564; Michezo na Sanaa asilimia sita sawa na shilingi bilioni 622 na hii ninayoisoma ni tofauti na yale ya kawaida, haya ni ya maendeleo. Jumla kwenye maendeleo ni shilingi trilioni 9.29.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, hatua zinazochukuliwa za kufanya mabadiliko katika kukuza utu wa binadamu, ni lazima viongozi wawe na nyenzo kuu ya Maarifa (elimu na uzoefu). Bila ya maarifa na uzoefu, utakuwa ni ubabaishaji tu. Uaminifu na uadilifu kwetu sisi Wabunge ni muhimu sana ili tuweze kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni msingi mkuu wa kanuni ya demokrasia ulimwenguni kuwa, sheria zote na mamlaka za kusimamia na kutoza kodi zizingatie uwakilishi wa wananchi ambao ndio walipa kodi. Serikali yetu inaendeshwa kwa ridhaa ya Watanzania ambao tumekubali kuchangia matumizi ya Serikali kwa kulipa kodi. Walipa kodi watashiriki mchakato mzima kama wanaridhika kwamba hakuna hila katika mabadiliko. Mabadiliko yoyote yatafanikiwa tu, ikiwa nia na lengo ni kupanua uhuru wa raia na kulinda utu wao. Adui namba moja wa mabadiliko endelevu ni unafiki na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia hekima na busara wewe, Spika, Wenyeviti wa Bunge na Katibu wa Bunge kwa dhamana mliyopewa ya kulitumikia, kulisimamia na kuliongoza Bunge hili Tukufu. Aidha, nawashukuru wote walioshiriki katika kuandaa maoni haya ya hotuba kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha. Tunakushukuru sana kwa mawasilisho yako kuhusiana na hotuba ya bajeti na maoni ya Kambi nzima ya Upinzani, tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa John Chenge; Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa James Mbatia, sasa tunaelekea kwenye uchangiaji kama nilivyosema mwanzo, ambapo wachangiaji tuna dakika kumi kumi. Bado dakika 10 si nyingi, lakini ukijipanga vizuri ukajielekeza kwenye hoja, unaweza ukazitumia vizuri. Tutapata wachache kwa asubuhi hii na jioni tutaendelea kama tulivyosema asubuhi ambapo tutaanza saa kumi na moja kamili jioni.

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Amour na Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine ajiandae. Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili nami niseme machache juu ya hotuba yetu ya Wizara ya Fedha ama hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka sisi kama Wabunge tumekuwa tukiishauri Serikali, lakini nimekuja kugundua, pamoja na kwamba tumekuwa tukiikosoa, bado Serikali yaani ni kama tunaionea, maana yake hawawezi, yaani ni sawa na mtoto wa miaka 10 kumbebesha mzigo wa kilo 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeanza tu na ushauri kwamba, Taifa lolote haliwezi kuendelea bila ku-*invest* kwenye tafiti *(research)*, kwa sababu kinachoonekana hapa ni kwamba, Serikali haijui matatizo ya wananchi, wanasimuliwa tu. Ndiyo maana hata watu wanaowaagiza waende wakafanye hizo *research* ni wale ambao wanawapa shilingi milioni 100 wanakwenda wana-*cook data* zote. Sasa mwisho wa siku ukifuata zile *data* ndiyo matokeo yake haya, bajeti za hovyo kabisa ambazo hazitekelezeki. Haya ndiyo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ni lazima jambo la kwanza mu-*invest* kwenye *research* (muwekeze) kwenye tafiti ya kila tatizo, nafikiri baada ya hapo ndiyo tunaweza tukawasaidia, lakini kinyume na hapo tutakuwa tunawaonea tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili bajeti; bajeti ya pombe, soda, sigara, juisi, ambayo miaka yote ndiyo imebaki kuwa hiyo hiyo. Tumekuwa tukilalamika, lakini watu hawasikii, maana yake hawana namna yoyote, hawana ubunifu wowote nje ya huu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda kwenye mapendekezo, ushauri na maswali, leo ndiyo najikita zaidi huko. Moja, ukipitia taarifa ya Mashirika ya Fedha Duniani *(IMF* na *World*

bank) ya mwaka 2011 inasema wanaopaswa kulipa kodi kwa Tanzania ni milioni 13.5; *IMF* wanasema Watanzania tuna walipa kodi milioni 13.5, wanaolipa kodi sasa Tanzania ni milioni 2.5, milioni 11 hawalipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya taarifa hiyo hiyo ya *IMF* inasema Wakenya milioni 12.5 wanatakiwa walipe kodi, wanaolipa kodi Kenya ni milioni 9.5. Hapa tatizo siyo vyanzo vya mapato, wala bajeti ndogo, tatizo ni uzembe kwenye Serikali kwenye kukusanya mapato. Hatuwezi kuendelea kulea watu katika mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, leo nawapa *data* tu. Ukipitia tu taarifa ya Wizara ya Fedha ya China mapato yatokanayo na uagizaji wa bidhaa kutoka China tu, taarifa ya mwaka jana tu mwaka 2013 Juni, Tanzania tumeagiza vitu vya kawaida kutoka China, ondoa magari, pikipiki na vitu vingine, vitu vile vya kawaida tu *tooth picks*, sijui vile vya masikioni, sijui nini, vyenye thamani ya dola bilioni 3.1 sawasawa na shilingi trilioni 5.115. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani shilingi trilioni tano na bilioni 150 zimetoka Tanzania zimekwenda China, kasome ripoti ya kodi ya *TRA* hamna kitu. Unajiuliza taarifa hizi, sasa sisi tume- *export* nini kwenda China? Tume- *export* bidhaa za thamani ya shilingi milioni 600. Hii taarifa iko kwenye Wizara ya Fedha ya China, halafu unasingizia, unakuja na bajeti kama hizi hazieleweki, hazina miguu wala nini! *(Makofi)*

Ukipitia taarifa za hawa hawa watu wa *TRA* uagizaji wa magari, pikipiki, unaweza ukashangaa, lakini nchi haina hata kiwanda tu cha kutengenezea *bolt* tu, *tube*, tairi tu, maana yake hata *spare* zenyewe *used* tunaagiza huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa haliwezi kwenda katika mfumo huu, unakuja na bajeti za stahili hii. Leo tena unakuja unasema unazuia watu wanaoagiza magari, badala ya miaka 10 iende miaka nane wakati hata taarifa zenyewe hizi huna hata *bolt* moja unayotengeneza. *What do you expect* kutoka kwenye hivi? Ingieni kwenye ubia na kampuni kama *Toyota, Nissan* waje watengeneze *spare* hapa hapa nchini. Sasa tunaagiza *spare used* (chakavu) kutoka huko huko Japan! Jamani huwa tunajaribu kuwashauri, lakini tunashindwa ni namna gani mtaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, unajua usiwe unasingizia kila siku mapato madogo hatuna vyanzo. Taifa hili leo, nchi yetu hii Tanzania tuna Mashirika ya Serikali; kwa mfano *National Housing* pekee, ukichukua thamani ya majengo ya *National Housing* pekee, nina hakika mnaweza kupata mapato yanayoweza kusaidia hili Taifa. Mapato ambayo yanaweza kusomesha, yakaenda kwenye afya, REA na kwingineko. Sasa wewe ni sawasawa uko nyumbani, una ng'ombe, una mtoto anasoma shule halafu unasema nimekosa ada. Wewe kipaumbele chako ni kipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *this is wonderful*! Ndiyo hili Taifa lilivyo. Unajua nilikuwa nasoma kitu kimoja kwenye *facebook* wanasema sisi ni watu wa tatu kwa akili ndogo duniani, bado naifanyia utafiti, kwani nina wasiwasi na hili! *This is a shame! (Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde huo utafiti ni wa kufuta kabisa. *(Kicheko)*

MHE. DAVID E. SILINDE: Sawa!

NAIBU SPIKA: Endelea kuchangia.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mashirika kama *TPDC* ndiyo wamiliki wa leseni za vitalu vyote. Ugunduzi wa gesi ambao tunao mpaka siku hii ya leo, tuna

karibu *cubic feet trillion 46.7* ndiyo ambazo zimegunduliwa mpaka sasa hivi. Thamani ya ujumla wa huu ugunduzi wa hii gesi iliyopo ni trilioni 1200, thamani yake. Tukiondoa mambo ya *exploration* na nini, gharama halisi ya mwisho ambayo sisi kama Taifa tunaweza tukapata ni trilioni 400, hiyo ni bajeti ya miaka mingapi? Hawana mapato, wanalalamika, wanalia. Sasa matokeo yake ni nini? Ndiyo Rais anakuja kuzindua tamasha la uzalendo, uzalendo unanunuliwa? *(Makofi/Kicheko)*

Unasoma gazeti la Mwananchi unaona pale *stadium*, sijui *PTA* watu 10,000 wanaomba ajira 700 tu.

MBUNGE FULANI: 70.

MHE. DAVID E. SILINDE: Ajira 70; watu 10,000 mkutano wa hadhara! Nyie washauri wa Rais *I wish* mngemshauri Rais aende akasikilize wale watu 10,000 wanaotafuta ajira 70, tunadanganya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo katika Taifa hili; barabara zote anazojisifu Mheshimiwa Magufuli, haitekelezwi kwa wakati. Mradi mmoja wa barabara, unasaini leo barabara, inakuja kujengwa baada ya miaka mitano. Tunalipa riba, tunalipa *penalt*, madeni matupu, Watanzania hawaambiwi, tunapeleka wapi Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambia angepatikana Rais mmoja fyatu, anaweza kujenga hii nchi. Unachukua tu bajeti ya mwaka mmoja unaingiza kwenye maji, maji yanaonekana na watu wanapata maji. Sasa matokeo yake unakuta miradi, maeneo kama Tunduma kule ambako sisi tunaingiza mapato makubwa, tunachangia Taifa fedha nyingi *almost* bilioni tatu kila mwaka, hamtupi chochote, ubinafsi tu mnachukua zile fedha mnapeleka kwenu na kwenyewe kule wanazila tu, hamna lolote wanalolifanya! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utakwenda kweli na bajeti ya namna hii! Twende kweli na bajeti ya namna hii, tutakwenda mbele? Ahadi za Rais zinatekelezeka? Si tunawadanganya wananchi! Tumeshindwa, kama tumeshindwa tu kwenye jambo la ajira na kila mwaka zaidi ya wanafunzi 40,000 wanatoka kwenye vyuo vikuu, sijazungumzia kwenye *certificate*, *diploma* wala ngazi za chini kabisa. Wanafunzi 40,000, *this is shame! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bajeti haina kitu chochote cha maana ambacho imekifanya. Sasa nawashauri vilevile mkitaka mapato yaongezeke, wekezeni kwenye ngazi ya Halmashauri.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde, malizia.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana.

Baada ya Mheshimiwa Silinde kama nilivyosema ni Mheshimiwa Amina Abdallah Amour!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nitaanza na madeni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeagiza madeni yote yapelekwe Hazina ili yafanyiwe uhakiki na baadaye yafanyiwe malipo. Hii ni hatua nzuri, lakini kuna jambo moja ambalo linadhoofisha; kuna tetesi zinasemekana kuwa baadhi ya madeni haya mnapohakiki, mnaona ni ya kubuni na mengine yalishalipwa. Hii si kama Wizara inakosea, lakini wanafanya makusudi na nyie hatua mnayoichukua ni kuyafuta tu. Kwa hiyo, naiomba Wizara baada ya kufuta madeni haya ambayo ni ya kubuni, siyo madeni ya kweli, wahusika wote muwachukulie hatua za kinidhamu, siyo muwaachie tu kwa kuyafuta, haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye ukomo wa magari chakavu. Ukomo wa magari chakavu ulikuwa ni kuanzia miaka 10 na kuendelea, sasa hivi ni miaka nane na kuendelea. Hii ni hatua nzuri, lakini sababu mliyoisema kuwa ni uharibifu wa mazingira na la pili ajali, lakini na magari mapya pia yanasababisha ajali na ndiyo nyingi kuliko hayo chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, ikiwa kuna uharibifu wa mazingira, barabara ni mbovu. Ukitazama foleni za magari zimejaa njiani nazo husababisha ajali, je, hizi mtazifanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye majina kwenye *plate numbers* za magari. Miaka miwili iliyopita mliweka ada ya majina kwenye *plate numbers* za magari kwa shilingi milioni tano (5,000,000/=) kwa muda wa miaka mitatu kwa kila anayetaka kuweka jina kwenye *plate* ya gari, lakini kwenye kitabu chako Mheshimiwa Waziri sijaona sehemu uliyoandika matokeo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwuliza Mheshimiwa Waziri, je, wamepata mapato yale waliyokusudia? Kama hawajapata sasa nawashauri badala ya kuweka milioni tano (5,000,000/=) waweke shilingi milioni mbili au moja (2,000,000/= au 1,000,000/=). Jambo lingine wanaweza kuwaambia hata hizi pikipiki kwa sababu jambo hilo ni la hiari siyo la lazima, watu wenye pikipiki kama na wao wakitaka kuweka majina kwenye *plate numbers* wawafanyie japo kwa laki moja (100,000/=) na hii itasaidia kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja kwenye fedha za maendeleo. Mwaka huu tunaoendelea nao ambao utamalizika kesho kutwa walitenga shilingi trilioni 5.4 kwa ajili ya maendeleo, lakini hawajaweza kuzifikia. Mwaka huu wanatenga shilingi trilioni 6.4 kwa ajili ya maendeleo, hii ni hatua nzuri, lakini swali ninalotaka kuwauliza ni kwamba, watawezaje kufikia shilingi trilioni 6.4 ikiwa vyanzo vya mapato ni hivyo hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Kamati ya Mheshimiwa Chenge kama tulivyosema tumeleta mapendekezo ya vyanzo vipya vya mapato na kila siku tunawaambia kuna hii Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu, lakini Serikali hamtaki kusikia, mnatwambia mnaifanyia kazi, huu ni mwaka wa pili, niwaulizeni Serikali hii kazi au utafiti huu mtaumaliza lini ili Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu ianze kufanya kazi na kuweza kukusanya mapato kwa ajili ya bajeti yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine za *EFD*. Pamoja na Serikali kutoa elimu na kukutana na wafanyabiashara, lakini bado wafanyabiashara hawataki kusikia. Sasa ikiwa mtafanya mabavu hatutofika, kwa hivyo, nawashauri Serikali bado mrudi kwa wafanyabiashara mkae pamoja na mje na maamuzi ya pamoja. Labda nyie mnasema kwa sababu hawataki kulipa watakuwa wanaiba, lakini hamjapata hasa kiini cha kukataa kutumia mashine hizi. Kwa hiyo, nikuombeni Serikali mrudi chini, mzungumze tena na wafanyabiashara badala ya kutumia mabavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja tena kwenye ukuaji wa uchumi. Kila siku tunasikia hapa kila mwaka ukuaji wa uchumi umekua, uchumi umekua. Sasa leo nataka kuiuliza Serikali sitaki kupoteza muda wa kueleza mengi kwa nini umaskini unakua, unazidi kila siku. Ukuaji huu wa uchumi kwa nini haufikii kwenye mifuko ya maskini na wao wakajua kama uchumi umekua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea nakuja kidogo maana yake nimechangia sana kwenye Kamati ya Bajeti, sasa hivi naboresha boresha tu. Nikija kwenye misamaha ya kodi, naipongeza Serikali kwa kusema itapunguza misamaha ya kodi, lakini pia natoa agizo au msisitizo kwa Serikali, hatua hii iende kidogo kidogo, sio iende haraka vupu mnakuja kwenye pato la Taifa la asilimia moja, kwani mkienda hivyo tunaweza tukakosa uwekezaji. Lazima kazi hii muifanye kwa uangalifu, hatua kwa hatua, kidogo kidogo, muanze moja mpaka tutafikia hilo pato la Taifa la kufikia asilimia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kidogo hapa nitagusia tatizo la ajira. Kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri bado hajawawezesha vijana kupata ajira ya kutosha, vijana wako wengi, vijana wengi wamemaliza kusoma wako wengine waliofikia *form two*, wengine *form four,* wengine wamefikia vyuo vikuu, lakini utakavyowaona njiani wanavyohangaika humjui aliyesoma na wala humjui asiyesoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iwawezeshe hawa vijana waweze kupata kibarua, vijana ni Taifa leo na la kesho si la kesho tu na leo pia. Tunawahitaji hawa vijana bila ya vijana hakuna maendeleo kwenye nchi yoyote na hakuna ushindi wa chama chochote bila ya kukubaliwa na kijana. Kwa hivyo, naomba tuwawezeshe hawa vijana ili mwaka 2015 na sisi *CUF* tuchukue ushindi. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Amour kwa mchango wako. Sasa Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine!

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Taifa kwa mwaka 2014/2015. Nianze kwanza kwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo kinaifanya hasa katika kuboresha miundombinu na mambo mengine na katika Jimbo langu la Tarime wamejitahidi sana ingawa kuna matatizo kidogo kidogo, lakini nawapongeza kwa juhudi hizo na nawapa pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kabisa kwamba ni dhahiri kwamba, haya mambo yote ili yawezekane vizuri na tufanye kazi vizuri suala la amani katika nchi yetu ni la msingi sana. Hivyo naisisitiza Serikali pamoja na kwamba kila mtu anatakiwa asimamie amani katika nchi yetu Serikali ya Chama cha Mapinduzi bado ina dhamana ya kulinda amani kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba nimjibu mchangiaji aliyetangulia rafiki yangu Mheshimiwa Silinde, amesema kwamba uwezo wa Watanzania kuwa na akili ni wa tatu kutoka mwisho. Hilo si kweli, huo ni utafiti wa *facebook* na naomba utafiti wa *facebook* Bwana Silinde uufanyie kazi. Kuna tofauti kati ya kufikiri na kuwa na akili. Kila mmoja ana akili isipokuwa uwezo wa kufikiri ndio tunatofautiana, nafikiri uchukue hiyo kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika nchi yetu tufahamu kwamba ili tuweze kuendelea tunahitaji kabisa tufikiri na sio kwamba tukae tunabishana, kila mmoja anahitajika

atimize wajibu wake, ni wajibu wa hata wa kila Mbunge kushauri Serikali na Serikali itasikiliza, lakini sio kutoa *data* ambazo zingine ni za uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo napenda kusisitiza katika bajeti hii katika Wilaya yangu ya Tarime naomba ikamilishe miradi ya sekta ya madini ihakikishe kwamba inawasaidia wananchi wa Tarime, lakini vile vile maji na ujenzi wa barabara kutoka Nyamwaga mpaka Mto Mara, umeme wa *REA*, elimu pamoja na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha msingi ni kwamba, ikumbukwe kabisa kwamba. ili tuweze kufanya maendeleo makubwa sana kule Tarime. nasisitiza kwamba tupime ardhi ya kule Tarime ili kila mwananchi apate eneo lake alimiliki na aweze kupata mikopo ya kufanyia maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi nasema kwamba, Serikali ijitahidi sana kubana matumizi. Sana sana Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 ifanyiwe marekebisho kwa sababu hii sheria inapelekea vitu vinanunuliwa kwa bei ghali na wizi unafanyika katika Halmashauri zetu na utakuta kwamba asilimia kubwa ya fedha za maendeleo katika nchi yetu zinaishia mikononi mwa watu. Kwa hiyo, ni vizuri zaidi Serikali ikaangalia namna gani ya kudhibiti hiyo Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hali kadhalika nashauri kwamba, mashangingi makubwa ambayo yanatumiwa na watumishi wa Serikali yanaifilisi Serikali, ni vizuri tukabana matumizi. Tuangalie nchi ya Kenya wanatumia magari ya kawaida hata kama ni Mawaziri, hata kama ni Wakurugenzi, hii itasaidia sana kupunguza matumizi ya Serikali kama Waziri alivyowasilisha katika bajeti yake amesema kwamba ni bajeti ya kubana matumizi, tuanze kubana matumizi kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naungana na wale wote waliojiuliza kwamba tuna rasilimali nyingi katika nchi yetu. Tuna mito, bahari, maziwa, Hifadhi ya Taifa, gesi, madini, misitu, milima, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika. Nataka nifahamu nafasi ya hii asilimali katika kuchangia pato la nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusishabikie kwenda kufungua shule au madarasa ambayo yanajengwa na wawekezaji, lakini wakati huo huo wawekezaji hao wanaifilisi nchi. Lazima tuwe wazalendo wote tujue kabisa kwamba hii nchi iko mikononi mwetu lazima tutetee kwa hali na mali. Wawekezaji sio waaminifu, ni wezi wanaifilisi nchi yetu ya Tanzania ,halafu vilevile hawalipi kodi. Naomba hili tulifahamu na tulizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niisemee Tume ya Mipango, Waziri anayehusika na Mipango amewasilisha kwa kusema kwamba kufikia mwaka 2025 Tanzania itakuwa na kipato cha kati cha Dola 3,000. Dola 3,000 ni shilingi milioni tano kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha wa sasa hivi. Lakini sasa hivi najiuliza kwamba je, hiyo kweli itafikia kama sasa hivi tangu tuanze huo mpango miaka minne imeshapita tuna Dola 700. Dola 700 kwa muda wa miaka minne tutoke twende mpaka Dola 3000 itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, cha kwanza kabisa, tuhakikishe kwamba tunamwezesha mkulima, mkulima akiwezeshwa akalima mazao ambayo yatatafutiwa soko na Serikali. Mkulima alime kilimo cha kisasa, mkulima apewe mbolea ya kisasa ambayo itamudu katika uzalishaji wa mazao yake, badala ya kilimo cha ujima, naamini kwamba tunaweza

tukajivuna kwamba hiyo ndoto tutaweza tukaifikia, lakini tusipofanya hayo hatuwezi tukafikia hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi na cha maana, nauliza kwamba kilimo kimewekwa katika Matokeo Makubwa Sasa bila ya kuweka ardhi, hivi kweli tutakuwa tunafikiri vizuri? Hapo kuna matatizo katika uwezo wa kufikiri katika hiyo Tume ya Mipango. Nafikiri kwamba ardhi iwe ndiyo msingi wa maendeleo kuwekewa katika Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nasisitiza utafiti ufanyike kwamba uchumi unakua kwa asilimia saba, lakini ukienda vijijini hali inatisha, maisha ni magumu, wengine wanasema afadhali ya jana kuliko leo. Hali hii inatishia sana na tujue ni kwa nini uchumi unakua kwa asilimia saba, lakini Watanzania hawana fedha mfukoni, matokeo yake tunajenga matabaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakapofika mwaka 2025 hali ya tabaka inatisha katika nchi yetu na tabaka la wenye nacho wataendelea kuwa nacho na lile tabaka la maskini litabaki kuwa maskini wa kutupwa. Ni vizuri zaidi utafiti ufanyike tuna uwezo wa kufikiri na tufikiri zaidi ili tuweze kuona namna gani ya kuleta maisha nafuu kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napendekeza Serikali ifanye utafiti kwamba, Watanzania walio wengi hawafanyi kazi, matokeo yake wamekaa tu kulalamika, matokeo yake ni kupiga soga tu maofisini, matokeo yake wanalewa tangu asubuhi mpaka jioni. Nataka nijue nafasi ya sisi viongozi wenyewe kuanzia Waziri Mkuu, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Watendaji wa Halmashauri, sisi Wabunge wengine, Madiwani, Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa kwamba wanasaidiaje wananchi wetu wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukaendelea kama hatufanyi kazi, tukafikiri kwamba tutapata maendeleo, sio rahisi. Tujifunze katika nchi za wenzetu, tujifunze katika nchi kama China, watu wanachapa kazi tangu asubuhi mpaka jioni. Hata Kenya ukienda, mimi ni jirani na Kenya kule, watu wanafanya kazi tangu asubuhi mpaka jioni, lakini sisi tumekaa tu ni soga tu tangu asubuhi mpaka jioni, hatuwezi kuendelea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nisisitize kwa wale waliogusia kwamba, Serikali ifanye kila linalowezekana ili iweze kupunguza deni la Taifa au isiendelee kukopa zaidi kwa sababu ni aibu kuendelea kukopa kila kukicha, lakini hali ya Watanzania ni maskini sana na hilo kwa kweli tulifanyie utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba niongelee Sekta ya Elimu kwamba, ili tuweze kutatua matatizo yanayoiandama elimu katika nchi yetu ya Tanzania tulipitisha Sera ya Elimu tulijadili mwaka uliopita hiyo sera ije ifanye kazi mapema. Halikadhalika kuanzishwe Mfuko wa Elimu na tutumie rasilimali zetu kugharamia huo Mfuko wa Elimu. Mfuko wa Elimu utasaidia kutatua matatizo na huo Mfuko wa Elimu utasaidia kutoa elimu ambayo itakuwa bora ambayo itafanya Watanzania watafikiri fikra sahihi na kwa muda muafaka watachukua majukumu ya kuitetea na kuipenda nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi, naomba kuunda mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana.

TAARIFA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpatie taarifa mzungumzaji, nilitaka nimuache amalize, nisimtoe kwenye reli. Ukienda tu kwenye *simple* tu *google,* uki-*google* ukiandika *countries with least IQ, lowest IQ* utaikuta pale, zimeandikwa nchi nyingi Sierra Leone, Ghana na nyingine, zote zimeandikwa na nchi zenye *IQ* kubwa. Sasa Tanzania ni miongoni.

Sasa jukumu la Serikali, mtuambie sijui kama unanielewa. Kwa nini watu wana *IQ* ndogo, kwa nini mmeshindwa kuhakikisha watu wamekuwa na *IQ* kubwa. Sasa hii imeelezwa kwenye kila kona.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba a-*google* kwa sababu mwandishi wa vitabu kama huyu hajui mambo ya mitandao...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde. Taarifa hiyo Mheshimiwa Nyangwine nitakupa nafasi kama unaikubali au vipi. Mheshimiwa Lucy ulisimama?

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba Mwongozo wako msemaji aliyepita amesema wawekezaji ni wezi. Naomba athibitishe ina maana Serikali inashirikiana na wezi. Naomba uthibitisho wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chacha Mariba Nyangwine, yote mawili taarifa hizo zinakulenga unasemaje kuhusu haya?

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, unajua hatuwezi kufanyia kazi kwenye mitandao. Mheshimiwa Silinde namheshimu sana na hiyo *google* inawezekana ikawa hata ya matapeli na ndiyo maana nasema kwamba lazima tusome. Unajua kitu kikishaandikwa kwenye vitabu na ikathibitishwa hicho kitakuwa na ukweli zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapo-*google* kuna mtu mwingine anaweza kuwa na ulevi wake tu, akaamka tu akaamua kuandika, akatoa mambo mengine tena Wazungu wana chuki sana na nchi za Afrika, wanatoa taarifa ambazo ni za uongo. Kwa hiyo, naomba kwamba uende utafakari sana na hilo ulione.

Mheshimiwa Owenya, usipotoshe mambo nimesema kwamba, wawekezaji wasiofuatiliwa baadhi yao ni wezi na hilo lazima mlifanyie utafiti kwa sababu kuna baadhi ya vitu ambavyo wawekezaji wanavisimamia hasa katika kulipa kodi tumeweza kuwabana. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Tarime sasa hivi wameanza kufanya mambo ambayo yanaonekana dhahiri, lakini zamani walikuwa hawafanyi.

Kwa hiyo, nasema kwamba, ni vizuri zaidi tukalifanyia utafiti wa kutosha na si kwamba nimesema ni wezi, lakini nasema kwamba, baadhi ya wawekezaji sio waaminifu hasa katika hoteli na katika maliasili zingine tulizonazo na hata Watanzania wenyewe baadhi yao ni wezi, sio wawekezaji wageni tu, hata wawekezaji wengine wa Kitanzania wengine ni wezi, ambao wanakwepa kodi na vitu vingine. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumeanza mjadala wetu uko moto kidogo. Tumeanza vizuri tunawashukuruni sana na taarifa ambazo zimetolewa zingine zinastusha. Mheshimiwa James Mbatia ametuambia kule Rombo hali mbaya sana. Kwa hiyo, watu wakitoka Rombo kuja kuoa

Kongwa kule itabidi tuangalie mara mbili mbili kama tuwakubalie au vipi, maana yake viwango vyao vinataka kufanana na vya Ufaransa na nchi zingine za Ulaya huko ambayo wana matatizo hayo.

Pia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Andrew Chenge akatukumbusha kuhusu wale vijana waliojaa Uwanja wa Taifa pale 10,816 wakitafuta ajira 70. Nilikuwa na Mwalimu wangu mmoja wa Kirusi zamani shuleni anasema *difficult to imagine*. Sasa unaweza ukafikiri kitu ambacho *it is difficult even to imagine*. Kwa sababu watu 10,000 sijui hata usaili wake utaratibu wake ulikuwaje kutafuta hawa watu 70, sijui *elimination process* inakwendaje.

Lakini *message* tunayopata ni kwamba watumishi wa Serikali wale ambao wanazembea wanapaswa kujua kwamba wako vijana *talented* wengi sana wenye sifa kubwa, huenda wenye vyeti bora sana kuliko hao walioko ofisini leo.

Kwa hiyo, Serikali leo kuhangaika hangaika na watumishi wazembe na zile sheria ambazo zinalinda watumishi wazembe hakuna sababu. Tunayo *work force* huko unaweza ukabadilisha watumishi ukachukua *set* mpya ukabandika Serikalini ili mambo yako yaweze kwenda. Yaani tuna watumishi wa kila kada sasa hivi nchi hii.

Kwa hiyo, nchi hii inakwenda, wanaosema nchi hii haina maendeleo nawashangaa kweli hii ni dalili moja ya kwamba tunasogea kwa haraka sana. *(Makofi)*

Kama alivyosema Mheshimiwa Silinde tunatoa *graduates* 40,000 kwa mwaka mmoja, hiyo ni shughuli nzito, ushindani ni mkubwa. Kwa hiyo wale wazembe ofisini kwa kweli eeh!! eeh!! Lazima wajue vijana wanaokuja huko shughuli kubwa.

Tangazo moja ili tuweze kuondoka kwa vile muda wetu hauruhusu linatoka Ofisi ya Bunge na lenyewe linawatangazieni kwamba yale Maonyesho ya kila mwaka ya Asasi ya Kiraia yanaanza leo yatakuwepo leo Jumatatu, kesho Jumanne na Jumatano, pale nyuma ya lile jengo letu la Utawala Asasi za Kiraia wameleta maonyesho yao ya asasi zipatazo 65.

Kwa hiyo, ni nyingi kwa kweli. Kwa ajili yenu Waheshimiwa Wabunge kuweza kuona na wananchi ambao wako hapa Dodoma.

Wanaonyesha shughuli zao mbalimbali kama nilivyosema kati ya leo na tarehe 18. Aidha, kesho tarehe 17 Asasi za Kiraia wanatualika Wabunge wote kwenye semina inayohusu Hali ya Afrika Mashariki Kiuchumi na Kimaendeleo ya Huduma za Kijamii kwenye ukumbi wa Msekwa. Semina ile itaanza saa 7.00 kamili mchana baada ya kuahirisha shughuli zetu kesho pale ukumbi wa Msekwa.

Kwa hiyo tunawaalika mfike pale kuona Maonyesho ya Asasi za Kiraia, lakini vilevile tunawaomba mhudhurie kesho semina itakayoanzia saa 7.00. Sasa msiniulize Waheshimiwa kuhusu utaratibu wa hiyo semina.

Jioni saa 11.00 kamili tutakaporudi mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Agripina Buyogera na Waheshmiwa wengine watafuatia.

Kwa hatua hiyo sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi leo saa 11.00 jioni. Ahsanteni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na majadiliano kama tulivyokwishaanza asubuhi kuhusiana na hoja mbili zilizo mbele yetu, moja ikiwa ni moja ya hoja ambayo inahusiana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na ya pili ni kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa maana ya bajeti ya mwaka 2014/2015.

Sasa kuna watu niliwataja pale asubuhi karibu wote siwaoni ambao nilisema tungeanza nao basi lakini tuanze na Mheshimiwa Agripina Buyogera, halafu na wengine watafuata. Mheshimiwa Buyogera.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwe ni mchangiaji wa kwanza jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba niipongeze hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyosomwa na Mheshimiwa James Mbatia, Waziri Kivuli wa Fedha na Naibu wake, lakini pia ninaomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambao wamewasilisha hoja yao mezani na ushauri wao mkubwa kwa ajili ya au kwa niaba yetu.

Awali ya yote ninaomba niikumbushe Serikali kwamba kwenye Wizara ya Maji nilichangia kwa uchungu mkubwa sana na kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma hususani Jimbo la Kasulu Vijijini ninaloliwakilisha ninaomba tena niwakumbushe Serikali ili iweze kutufikiria katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya barabara ya Kidahu – Nyakanazi. Tangu tumeingia Bungeni kila Mbunge wa Mkoa wa Kigoma akisimama hapa anakumbushia ahadi hiyo, lakini mpaka leo tunamaliza miaka minne sasa barabara ya Kidahu – Nyakanazi haijajengwa pamoja na ahadi nyingi za viongozi mbalimbali.

Tunaomba barabara hii muitengee fedha, lakini siyo hilo tu kila mwaka mnaitengea fedha kidogo ukilinganisha na mikoa mingine ambayo tayari kuna barabara ya lami lakini bado wanapata bajeti kubwa kuliko barabara hii ambayo ni ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niikumbushe Serikali tena kwenye miradi ya maji ya Kijiji cha Nyarugusu, Kasangezi ilitakiwa iwe imekamilika tangu mwaka jana, lakini mpaka leo miradi hii haijakamilika. Niwakumbushe wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini hasa Baba zangu Mabalozi wa Chama cha Mapinduzi, Wenyeviti wa Kata na viongozi mbalimbali katika Jimbo langu wanaotoka Chama cha Mapinduzi waililie Serikali yao ambayo kila siku tunaambiwa kuwa ni Serikali sikivu, ni kwa nini kila siku Mbunge wao ninalalamika Bunge hapa? Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwa nini hamsikii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bajeti ya maji nilitaja vijiji mbalimbali kikiwemo Kijiji cha Nyarugusu, Kasangezi, Asante Nyerere, Sogeeni, Shungulima, Titya Sekondari, Muzye na Mtala. Hivi ni vijiji mbavyo vilitegemewa kupata maji tangu mwaka jana, lakini bajeti iliyopangwa kwa ajili ya kukamilisha mradi wa Nyarugusu na Kasangezi ilikuwa ilikuwa ni shilingi bilioni moja na milioni mia mbili, cha kusikitisha katika fedha zote hizo fedha iliyopelekwa ni milioni 200 tu lakini nilikuwa ninapitia kitabu hapa cha Mpango wa Maendeleo ukurasa wa 30 kinaonyesha ni namna gani ambavyo Watanzania wenzetu maeneo mengine wameweza kupata maji kwa

miradi iliyokamilishwa ndani miezi sita tu. Sasa tunajiuliza kulikoni Jimbo la Kasulu Vijijini miradi ambayo ilitakiwa kukamilika mwaka jana mpaka leo hakuna hata kijiji kimoja kinachopata maji ni jambo la kusikitisha ndugu zangu.

Ninaomba niende kwenye Wizara ya Afya, nimekuwa nikizungumza hapa Bungeni. Kule Jimbo la Kasulu Vijijini kuna Vituo vya Afya ambavyo tayari vimeshaanza kujengwa mfano ni Kata ya Nyamidaho, Kata ya Makyele, Kata ya Nyachenda na Kata ya Rungwe Mpya kote huko kuna vituo ambavyo wananchi wameshawekeza nguvu zao na Serikali kwa kupitia Halmashauri imeshapeleka fedha kidogo ambapo Wizara inaelewa kwamba Kituo cha Afya ili kikamilike siyo chini ya shilingi milioni 400. Sasa unashangaa kituo kinapangiwa bajeti ya shilingi milioni 400 halafu mwaka jana mmetupelekea milioni 55 hivi huu ni utani au ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya kinajengwa kwa milioni 400, unapeleka milioni 55 kama siyo kuwahadaa Watanzania waendelee kuimba CCM sikivu, chama tawala wakati hakuna kitu mnachowasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niikumbushe Serikali na mmeona mfano hai wa Mkoa wa Kigoma mwaka huu waliipa likizo CCM ni sababu kama hizi! Kwa sababu haiwezekani mtu ambaye unamuambia kwamba Serikali ya chama ni sikivu, halafu unakwenda kuwahutubia wananchi unawaambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo yenye mamlaka ya kuleta maendeleo, halafu ahadi zote hakuna hata moja ambayo inakamilika, ninaiomba Serikali ituangalie kwa macho mawili. Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ni mama mwenzangu na unajua uchungu wa akinamama wanapopata shida kwa ajili ya maji, ninakuomba unipe kipaumbele kwenye bajeti hii katika miradi hii ya maji unipe fedha ndugu yangu, wewe ni rafiki yangu sina matatizo kabisa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye reli. Kuna jambo la kusikitisha sana kwenye Reli ya Kati, tumekuwa tukipiga kelele humu ndani hususani wananchi wanaotoka Mkoa wa Tabora, Kigoma, Mwanza, Katavi na Rukwa ambao tunategemea njia ya reli kwa kiwango kikubwa, lakini Serikali kwa makusudi kila siku mnatupa ahadi tu nzuri za kurekebisha njia ya reli lakini hakuna kitu kinachokamilika kwa mfano, reli imesitishwa kwa muda wa miezi sita, treni ilikuwa haifanyi kazi, wananchi wa mikoa hii wamenyanyasika sana, ndani ya miezi sita reli ikiwa inatengenezwa, reli inakarabatiwa, treni haifanyi kazi, matokeo yake miezi sita imekwisha reli imeanza kufanya kazi ndani ya siku mbili sijui tatu tunapewa taarifa tena kwamba treni imesitishwa kwa sababu kuna daraja bovu. Ni vitu ambavyo haviingii akilini. Hivi kweli kwenye Wizara muhimu kama hii hatuna kitengo maalum ambacho kinaweza kikawa na majukumu ya kukagua njia ya reli?

NAIBU SPIKA: Ahsante Kamishna malizia.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, mambo ni mengi lakini mengi nilishayazungumza na mengine nitapeleka kwa maandishi, ninakushukuru ahsante sana na Mungu akubariki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agripina Buyogera, Kamishna wa Tume ya Bunge. Sasa nimuombe Mheshimiwa Henry Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma. Tafadhali Mheshimiwa Henry.

MHE.HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mada hii na nianze kwa kumpongeza sana Wazari Mama, ameonyesha ujasiri mkubwa na uwezo mkubwa, tumpe moyo ninaamini atafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwapongeza pia wasaidizi wake na Naibu Mawaziri wake, wamefanya kazi nzuri katika kipindi kifupi wameweza kumshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua nafasi hii pia kuipongeza sana Kamati ya Bajeti, ukisoma hotuba ya Kamati ya Bajeti imezungumza mambo mengi ambayo yakipewa msisitizo yanaweza kutupeleka mbali, wajibu wa Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, wametamka vizuri na wameonyesha uwezo wa kuishauri na sasa tuende katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizungumzie mambo muhimu matatu, la kwanza nikizungumzia kuhusu bajeti kwa ujumla sioni sababu na pengine Waziri baadaye atuambie Kamati imelalamika kwamba hawapati ushirikiano katika kuchukua mawazo yao katika kuanzia vyanzo vingine vya mapato, hivi tatizo liko wapi hapa, mtu anakuja katika nyumba yako anakuambia bwana ukitaka utajirike fanya moja, mbili, tatu bado unamuogopa uchawi uko wapi?

Mimi ninashauri sana na tuliunda Kamati hii ya Bajeti kuisaidia Serikali, mwaka jana tulithubutu, tukajaribu kuongeza kodi ile ya simu kidogo ika *backfire* lakini bado imekuwa bado ni chanzo cha kuleta mapato. Sasa ninaomba Wizara izingatie hili na ikubaliane na sisi kama Bunge tufike mahala tuisimamie Serikali vizuri ili ishirikiane na Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nikijielekeza katika upande wa bajeti ya maendeleo au uchumi kwa ujumla. Kamati pia imezungumzia sana suala la kilimo na mchumi yeyote katika uchumi unaotegemea kilimo kama wetu, bila ya kuzingatia kilimo hatuwezi kwenda, ni ukweli kwamba kwa sasa hivi tumetoa *priority* katika yale mambo sita – BRN, lakini bado mimi sioni kilimo kilivyoangaliwa kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba tunahitaji kukipa kilimo umuhimu wa kwanza, kwa mfano wenzetu nchi kama Kenya wana uwezo mkubwa wa uchumi wao kwa sababu wameimarisha kilimo, sisi katika BRN ni kweli tumechagua wawekezaji wakubwa wachache, lakini huu ni utaratibu mpya, tungewasaidia wakulima wadogo wadogo, tukawawezesha kwa kuwapa pembejeo, tukaongeza utalaamu, tukawasaidia kwa kuhakikisha kwamba tunawapa mitaji, wakulima kama wale wa Lushoto ambao kwa kweli sisi hatuoni msaada tunaoupata katika Serikali hasa katika pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo letu sisi ni wakulima wadogo wadogo wa mboga na matunda, bila ya kutusaidia tupate dawa, mbolea sisi hatunufaiki na huu mpango wa pembejeo za kilimo. Kwa hiyo, wakulima wale wangesaidiwa, wakaweza kuzalisha pamoja na wakulima wengine katika maeneo mbalimbali, wakasaidiwa kuzalisha wakapewa uwezo, mimi nina uhakika tungesonga mbele kwa haraka sana.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ielekeze nguvu iwekeze katika kilimo, tusiseme kiutani. Sasa hivi mchango wa kilimo ni 4%; ni kweli tumepata faida ya mfumuko wa bei kwa maeneo mengine kwamba tumepunguza mfumuko wa bei. Lakini huu umepungua kutokana na vyanzo vile vikuuu kama madini, biashara hivi havimgusi mwananchi. Kwa hiyo utaona kuwa uchumi umekuwa lakini mwananchi wa kawaida hanufaiki, mwananchi wa kawaida angewezeshwa katika kilimo tungeweza kuona kuwa manufaa ya mchango wa kilimo itamfikia na umaskini utapungua, haiwezekani ukapunguza umaskini Tanzania bila ya kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sasa hivi tumekopesha, tumesaidia viwanda na bila ya viwanda hatuwezi kwenda na Kamati imependekeza viwanda vidogo vidogo, wakulima

hawa wangewezeshwa kuweza kuongeza thamani ya mazao yao, ni ukweli kwamba hali ingebadilika sana na tungeona matokeo mazuri kwa wananchi kuweza kuachana na umaskini.

Suala lingine ni ununuzi wa mazao. Leo ninazungumzia kilimo tu kwa sababu ninaamini kwa kupitia kilimo ndiyo tutaokoka na kwa nchi yetu kwa sababu tunategemea wakulima wadogo wadogo tusitegemee matokeo makubwa bila ya kuwawezesha hawa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana au mwaka huu tumefanikiwa sana katika mfumuko wa bei ni kwa sababu tumeweza kujiwezesha wenyewe katika vyakula. Tumekuwa na mahindi ya kutosha, tumekuwa na mchele wa kutosha na tumekuwa na maharage ya kutosha na hali hii ilitusaidia sana katika kupunguza mfumuko wa bei. Sasa asiyeamini na ajaribu kwa sababu mwaka uliopita kabla ya mwaka huu mfumuko wa bei ulipanda haraka sana mpaka kufikia 12% na kuendelea kwa sababu bei za vyakula zilikuwa zimepanda. Sasa tumeweza kudhibiti na mwaka jana tumenunua chakula kingi kutoka kwa wakulima. Tukiendelea na kuliwezesha Shirika au SGR ambayo ina nunua mazao nina uhakika mfumuko wa bei utaendelea kupungua na nchi itanawiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea sana uzalishaji wa ndani na siyo wa nje, kwa hiyo *effect* ya uchumi wetu ni kuimarisha uchumi wa ndani, tukijidai kuangalia sana nje hatutakwenda na tukiachia tu tupate njaa katika nchi mfumuko wa bei utafika 29% na nchi zote leo zenye kupata matatizo kwa sababu ndani hawajitoshelezi.

Kwa hiyo, ninaishauri sana Serikali ijitahidi kuwekeza katika kuzalisha ndani ili tuweze kupata faida za uchumi na umaskini upungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, ninaomba Sheria ya Bajeti ije ili mdhibitiwe vizuri na msichelewe, halafu ninaomba pia kufanya manunuzi kwa wakati, hili ni tatizo kubwa sana, kila siku Serikali ina ahidi tutafanya hili tuna aliangalia, mwaka unapita, mwaka wa pili, wa tatu kuna gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaiomba Serikali izingatie kufanya maamuzi kwa wakati. Utaratibu wa *cash budget* uangaliwe upya, mimi ninawashauri ikiwezekana tufike mahala Serikali izungumze na mabenki, kama tunatarajia kukusanya kiasi fulani tuweze kuchukua hela kutoka kwenye mabenki kiasi kile ili tuweze kuendelea na miradi kuliko kusubiri tumekusanya na miradi inakaa, kwa mfano juzi ndiyo tumetoa hela za maji, shilingi milioni 84, hela za simu. Sasa hii katika uchumi wa mwaka jana bajeti haikuwa na maana kwa sababu umewapa hela wana miezi miwili watatekelezaje bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri sana Serikali hii waliangalie, nimeshazungumzia ununuzi wa mazao utatusaidia sana kupunguza mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi niipongeze sana Serikali, tuendelee na jitihada za kupunguza kodi. Mismaha ina faida zake na ina hasara zake tuangalie maeneo yale ambayo kwa kweli hayatupi faida tuondoe misamaha.

NAIBU SPIKA: Ahsante, malizia Mheshimiwa Shekifu tayari muda wako.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe na ninasema ninaunga mkono hoja, hii hoja ni muhimu na tusipokubaliana nayo ina maana tusipate fedha tutakwenda wapi, mimi ninakubaliana kuwa juhudi ziendelee, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Henry Shekifu. Mheshimiwa Riziki Omar Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika bajeti hii ambayo itatuwezesha kufikia malengo pindi bajeti hii ingekuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba nguvu zangu nizielekeze kwanza moja kwa moja kwenye bajeti yenyewe. Bajeti hii ambayo tunaizungumzia tofauti yake na bajeti ya mwaka ambao unaishia ni ndogo sana na pamoja na udogo wake basi matumizi ya gharama za maisha yameongezeka kwa maana hiyo ongezeko la bajeti hii haijafua dafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba bajeti yetu mara nyingi tunalenga zaidi matumizi ya kawaida kuipa fedha nyingi kuliko matumizi ya maendeleo. Maendeleo ni muhimu na nchi haiwezi kusema imeendelea bila ya kuwa na maendeleo na fedha za maendeleo ndiyo zinazotegemewa kwenda kwenye miradi mbalimbali ya Taifa hili, ili wananchi waweze kujikomboa katika hali mbalimbali. Kwa mfano miradi ya umeme, maji, elimu, sekta ya afya, yote hiyo inategemeana na fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo fedha za maendeleo zilizotengwa ni ndogo sana kwa hiyo, bajeti hii bado haijamkomboa Mtanzania na haijamkomboa maskini wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Taifa tunaambiwa umeukua, Pato la Taifa limeoongezeka lakini mwananchi wa kawaida ukimwambia uchumi umeongezeka au uchumi umekuwa haelewi kwa sababu bado Mtanzania wa kawaida anaendelea kulala na njaa, kupata shida ya matibabu, shida ya kumsomesha mtoto, anaendelea kutafuta maji vijijini huko, kutafuta kuni, anaendelea kufanya shughuli mbalimbali katika hali duni sana. Kwa hiyo, kuzungumzia suala kwamba uchumi umekuwa mwananchi wa kawaida bado haelewi na tunapaswa kufanya juhudi za kutosha kuhakikisha kwamba tunamkomboa Mtanzania ili aondokane na umaskini wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo linatutatiza nadhani tunategemea zaidi kwamba tukusanye mapato ili yaweze kutusaidia kuendeleza maisha. Lakini makusanyo yetu ambayo tunayategemea hatufikii malengo siku zote na makusanyo haya ni kwamba inawezekana makusanyo haya yanakusanywa lakini yanavuja kwa upande mwingine. Kwa hiyo, hofu yangu ni kwamba hatujaweka mikakati vizuri ya kudhibiti makusanyo yetu pamoja na kwamba tuna vyanzo ambavyo vimeainishwa havitoshi lakini pia na hata makusanyo hayatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vyanzo vingi ambavyo tungeweza kuvitumia na vikaweza kutusaidia. Katika nchi hii tuna viwanda vingi tu, lakini vinaonekana kufa siku hadi siku, ni mapato hayo ambayo tungeweza kuingiza. Tuna wakulima ambao wanazalisha mazao mbalimbali yanahitaji mazao yale kutafutiwa viwanda vya usindikaji, leo wananchi wa nchi hii, akinamama maskini wajasiriamali, badala ya wao kutoa bidhaa hapa kwetu wakasafirisha nje wanaenda wakichukua bidhaa hapo Uganda, wakileta hapa kushusha hadhi na thamani ya fedha yetu. Hapo Serikali ingejikita zaidi ili tukaweza kuongeza hadhi ya sarafu yetu.

Kwa hiyo, naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ananisikia kwa hiyo, naomba aliangalie kwa umakini hili, ili tuweze kumkomboa Mtanzania wa kawaida naye aweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kidogo kwenye suala la vipaumbele. Vipaumbele ambavyo naviona kwenye hotuba ya Mheshimiwa kwanza ni elimu, pili, ni miundombinu lakini tatu ni afya na vingine vinaendelea.

Mimi mara nyingi sana nikisimama hapa huwa napingana sana na kwamba Wizara ya Afya ni Wizara muhimu sana, ni Wizara nyeti sana, ni Wizara ambayo inaweza ikamkomboa Mtanzania yeyote tukiwemo sisi wenyewe tuliomo humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukabeba mambo yote kwa wakati mmoja na mara nyingi huwa natoa rai hiyo. Ni kweli mambo yote ni muhimu sana, elimu ni muhimu, kilimo ni muhimu, miundombinu ni muhimu na mambo yote ni muhimu, lakini lazima tutafute dawa ya ku-*stick* kwanza mwaka huu tuseme *lump sum* kubwa hii tuipeleke kwenye Wizara ya Afya. Halafu mwaka unaofuata siyo kama Wizara nyingine tunaziacha, *no,* tunaendelea nazo lakini pato kubwa tunalipeleka kwenye Wizara ya Afya ili kuweza kuwakomboa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya tuna tatizo kubwa sana. Afya ni uhai, ni elimu, ni kilimo na ni kila kitu na zamani walikuwa wakiimba wakituambia kwamba afya ni uhai na walikuwa wanatuambia kuleni kuku, mayai, mboga samaki, maziwa. *(Makofi/Kicheko)*

Leo yule mtu ambaye ana ng'ombe basi hadiriki kunywa maziwa, anaenda kuuza maziwa ili apate fedha aweze kumsomesha mtoto wake, aweze kupata chakula, kupata nguo, matibabu, hawezi kunywa maziwa. Ni Watanzania wangapi leo wanaokunywa maziwa?

MBUNGE FULANI: Mpaka uwe mgonjwa.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Ukilazwa hospitali ndiyo watu wanakuchemshia yai wakuletee. Unaumwa sasa huko hospitali tena unakaribia kufa ndiyo unaletewa yai, huwezi kula. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana Wizara ya Afya tuiangalie kwa umakini. Tangu juzi nasoma kwenye mitandao fulani, nakuta kwamba dawa za UKIMWI wale wagonjwa ambao wameathirika na virusi vya UKIMWI hamna. Zimekwisha na hizo hospitali ambazo wanakwenda wengine wakitibiwa wamebadilishiwa dawa ambazo sio stahiki yao, kwa hiyo, ina maana tunawaangamiza zaidi. Wanaoathirika zaidi katika hili ni akinamama wajawazito ambao wameathirika na virusi vya UKIMWI. Sasa na watoto wao je, watakuwaje wakati wao dawa ya kuwakinga wale watoto haipo, wanapewa dawa nyingine, wale watoto tunawasaidiaje na sisi kila siku tunapiga kelele tunasema kwamba lazima tumsaidie mama mjamzito na mtoto mchanga ili tuweze kuokoa maisha yake na kuweza kupunguza vifo. Leo vifo tunavipunguza, tunaviongeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposemea Wizara ya Afya nina maana kubwa kwamba hali tuliyonayo ni mbaya. Nenda hospitali ya *Ocean Road*, kuna matatizo tele, nenda Muhimbili kuna matatizo tele na hospitali nyingine, sijakwambia huko vijijini hizi ni hospitali ambazo zipo Dar es Salaam ambazo tunasema labda ni Hospitali za Rufaa. Nenda vijijini kaangalie *situation* iliyopo ni mbaya sana, kiafya watu wetu wana tatizo la matibabu, hawana uwezo, hawana fedha, hawawezi kujitibu wenyewe wala watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipato chao ni kidogo sana, hawawezi kumtibu mtoto wala kujitibu yeye mwenyewe na ndiyo maana wengine wanafikia hadi kujinyonga kwa sababu wameshindwa na maisha. Hali ni mbaya sana na naomba sana Serikali iliangalie kwa umakini, vipaumbele lazima tuchague kimoja, tu-*stick* kwa mwaka huu tuseme tunachukua hili fungu tunalipeleka kwenye Wizara ya Afya, tunajifunga mkanda huku tunapeleka dogo, huku kwenye Wizara ya Afya tunapeleka kubwa *then* mwaka ujao tunatafuta namna nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda hivyo tutaweza kuwakomboa Watanzania kwa sababu afya ni muhimu sana na bila ya afya hatuwezi kufanya chochote. Sote tukiumwa hapa tunakimbilia kwenye hospitali kubwa kubwa, tunaenda kutafuta matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie sasa upatikanaji wa hizo fedha! Tatizo kubwa linalotuathiri ni kwamba upatikanaji wa fedha hazitolewi kwa wakati. Mpaka sasa hivi ninazungumzia hapa, fedha za bajeti za mwaka uliopita unaoishia tarehe 30 Juni hadi sasa hazijafikiwa, tutafikaje kwenye hayo maendeleo tunayotegemea? Je, mwaka huu tutaweza? Sidhani kama tutaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Omar Juma kwa mchango wako. Kama nilivyosema badala yako ni Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya na Mheshimiwa Deo Sanga, ajiandae.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo ambayo sauti yangu inasikika pia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliotangulia wamechangia vizuri sana. Lakini nilikuwa naomba pia niweze kuongeza haya machache kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia upande wa ukurasa wa 37 kuhusu Serikali kujitahidi kuendelea kuiwezesha polisi. Hali ya nyumba za askari wetu hasa polisi siyo nzuri kabisa kwenye maeneo tunayotoka. Nimejaribu kutathmini pamoja na mikakati yote tunayozungumza, suala la ulinzi, suala la kuhakikisha sheria za nchi zinatekelezwa, suala la kushika wahalifu, lote hilo linakabili idara hii ya polisi. Lakini mazingira yao ni magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri kwa kuwa polisi pia wanahusika katika kukusanya maduhuli ya aina mbalimbali, pengine ifike wakati sasa tungewawekea kama utaratibu katika kile kinachokusanywa asilimia kubwa iende katika kuboresha haya mazingira yao na asilimia nyingine iende hata kama ni nusu kwa nusu. Mimi naamini kwa kufanya hivyo polisi watapata motisha kubwa kwa sababu watajua wanafaidika moja kwa moja na kuona kwamba wajitahidi kukusanya maduhuli hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa katika hilo pia kuna mahali nilimsikia kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anawasilisha bajeti yake akizungumzia juu ya maduhuli yote kukusanywa na TRA na kuwekwa kwenye mfuko wa pamoja. Sasa kama ni sawa nilivyomuelewa, mimi naomba nitoe angalizo kwa sababu kuna ugumu au uchelewashaji katika kurudisha *retention* kwa wale wanaokusanya, hiyo inaweza ikasababisha baadhi ya taasisi zikashindwa kufikia malengo yake. Ni vyema basi kama kuna taasisi zinaonekana zinakusanya sana na zinatumia sasa kupita kiasi kile ambacho kilitegemewa kwa sababu wana makusanyo mengi, basi ni vyema tupandishe kile wanachotakiwa kukirudisha kwenye Serikali badala ya kunyang'anya ile kazi waliyokuwa wanaifanya na kuihamishia kwa TRA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tuliamua kwa hiari yetu kufanya masuala yanayohusisha *decentralization* tukasema sasa tushuke chini. Sasa tukianza tena kurudisha kila kazi kwenye *centre* hilo mimi naona ni tatizo. Ni vyema shughuli ziende katika maeneo yote mpaka huko chini na kila mmoja awajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hilo pia nilikuwa naomba nisisitize juu ya suala la *strategic investment*. Katika ukurasa wa 52, Mheshimiwa Waziri amependekeza *investor* ambaye ni *investor* mahiri *(strategic investor)* afikie sasa kuwa kiwango cha kuweza kupewa kodi iwe ni dola milioni 50, huyo ni kwa mgeni na kwa Mtanzania iwe ni dola milioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kwamba ni sawa, lakini kwa upande wa Mtanzania nadhani tuangalie zaidi na hata kama ni kwa mgeni, je, ni aina gani ya *investment* na anaenda kuwekeza wapi? Kwa sababu tuliangalia mtaji peke yake bila kuangalia mazingira ya uwekezaji tutakuwa bado hatujafanya sawa sawa. Kuna vivutio vingi vipo mbali na maeneo yaliyozoeleka. Tunaipongeza sana Serikali sasa hivi imefungua barabara, inasambaza maji, lakini na umeme unaenda maeneo mengi mpaka vijijini. Kuna vivutio vingi na rasilimali nyingi zipo katika maeneo hasa yale yaliyokuwa yamesahaulika, sasa nani ataanza kuwekeza huko ambako soko lake bado halijawa bayana?

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba kigezo kingine kiwe ni eneo gani huyu mtu anaenda kuwekeza. Lakini vilevile kwa mwekezaji wa ndani ambaye mimi namchukulia hata *micro-entrepreneur* ni mwekezaji, hata kama ana mtaji wake wa milioni tano ni mwekezaji, ndiye anayeanza kufungua. Tumegundua kwamba hawa wakifungua biashara ndiyo wakubwa wanakuja, hao ndiyo wanaovutia na jicho la kusema mahali fulani pana *potential.*

Sasa watu kama hao wanastahili kusaidiwa, wapewe *incentive* ikiwezekana hata kama ni miaka miwili ya mwanzo anapothubutu kwenda kuwekeza sehemu ambayo hapajawa na kitu kabisa kama kule *Kalambo falls,* Nyasa, Liuli, Lipalamba basi aweze kupewa kivutio angalau miaka miwili asilipe kodi ili aweze kufanya biashara yake na hiyo tutafungua ajira kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema hilo kwa uchungu mkubwa kwa sababu uwekezaji huu na nimeshasema si zaidi chini ya mara moja, umeegemea zaidi kwenye maeneo ambayo tayari kuna uwekezaji na ndiyo maana watu wengi wanahamia mjini, tunabomoa barabara, tunajenga *flyovers,* tunajenga mambo chungu mbovu watu wanashindwa kukaa kule vijijini. Kwa hiyo, lazima tufanye maamuzi ya makusudi ya kuwekeza maeneo yale ambayo yapo pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo niliyozungumzia nilitaka pia nirudi katika upande wa hawa ambao wanaojiajiri wenyewe zaidi ya asilimia 70 ambayo ni wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo. Ukweli ni kwamba tatizo la kilimo siyo kupeleka matrekta 200 kila Kata kama alivyosema kiongozi wangu aliyewasilisha upande wa upinzani peke yake. Mimi nadhani tatizo kubwa lipo kwenye soko, mtu akishaona soko lipo, mazao yake yananunuliwa hata kama anakopa anajua kwamba ataweza kurudisha mtaji wake. Sasa hivi kwa hali iliyopo watu wamelima, anayenunua NFRA ndiye mnunuzi mkuu na NFRA anakatwa, anapewa fedha isiyotosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tuone Waheshimiwa Wabunge tuacheni unafiki, sisi hatujaamua kuwasaidia wakulima na hilo nasema wazi kwa sababu kama sisi tusingekuwa wanafiki tungetoa mfano kwa mikoa ile ambayo inalima. Mkoa kama Rukwa, Ruvuma tunalima lakini hata tu kwenye bajeti kupewa *cess* ambayo tayari ni fedha ambayo ilikuwepo katika usimamizi wa kilimo haiendi, Halmashauri yenyewe haipewi sembuse huyo mkulima! Halafu hapa tunasema kwamba mkulima, mkulima sisi waongo!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli ni kwamba bajeti inapo-*fail*, Wabunge ndiyo wakulaumiwa sisi, kwa sababu Serikali inakuwa imeleta bajeti, sisi tunajaribu kuirekebisha kadri tunavyoona inafaa, halafu ikifika huko haijatekelezeka sisi tunakaa pembeni tunasema Serikali, hapana! Wote lazima tuwajibike.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu na ombi langu ni kwamba lazima tukae wote katika sura ya kushirikiana na kuweza kuleta mabadiliko yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa pia naomba suala la afya hasa kwa upande wa vijijini, ukiangalia kule Mpepo, Kihagara kule Wilaya ya Nyasa kote huko kuna tatizo, akinamama wanakufa! Nenda kule Wampembe, Kala watu wanakufa. Jamani tusione tumekaa hapa wenzetu wanapata shida. Zahanati za maeneo hayo unakuta hazipo kwenye kiwango. Mimi najiuliza kila siku hivi huyu mwananchi ambaye anakaa kijijini, yeye damu yake haiumi, kifo chake kinakuwa chepesi kiasi kwamba hata kama akiwa na kizahanati cha ilimradi anaweza akatibiwa tu. Sisi tuliokaa mijini ndiyo tunataka tuwe na hospitali nzuri zenye malumalu, umeme na zenye kila kitu, hapana, lazima tu-*reverse style* yetu ya kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, umeme sasa unaenda kila kijiji, yaani kule Rukwa kwa kweli wanaraha, kule Mbinga, Ruvuma, Nyasa wana raha kama kweli atatekeleza siyo yale makaratasi kama utatekeleza, hayo ndiyo mapinduzi tunayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji imesambaa sasa hivi maeneo mengi na yanatekelezeka tunashukuru hayo ndiyo mapinduzi tunayotaka. Tufikie sasa kumuona huyu mwananchi ambaye yupo kijijini na aweze kusaidiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kutoka mwisho ni suala la SADC. Tanzania inasaidia vipi kuhakikisha kwamba SADC inakuwa Bunge kamili?

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Stella malizia sasa.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tushirikiane. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana, Mheshimiwa Stella Martin Manyanya. Muongozo Mheshimiwa Rajab!

MUONGOZO

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mchangiaji ambaye amepita alisema kwamba Wabunge ni wanafiki, waongo katika suala la kilimo. Sasa sijui maneno haya anayesema kwa jeuri tu kwamba yeye ni Mkuu wa Mkoa, hayupo tena katika nafasi ya Ubunge ama vipi?

Tunaomba muongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika kutokana na kauli kama hizi ambazo nzito alizozingumzia, kwa kweli zinatudhalilisha ambazo amezungumza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa.

NAIBU SPIKA: Hiyo wala siyo muongozo bali taarifa kwa Mheshimiwa Manyanya. Mheshimiwa Manyanya taarifa hiyo unapokea au unasemaje?

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza atambue kweli mimi ni Mkuu wa Mkoa na naongea pia upande mmoja kama Serikali. Lakini asisahau mimi ni Mbunge, tena Mbunge sahihi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyosema kwamba sisi Wabunge ni wanafiki, nasema ni ukweli sisi Wabunge wanafiki, kwa sababu kama sisi siyo wanafiki tuone sasa tukijielekeza nguvu katika kupanga bajeti yetu kwenda kwa hawa wananchi, tusiilaumu Serikali peke yake. Sasa wewe unakasirika nini wakati na wewe unalalamika bajeti haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, lakini nilijua pia huwa ni raha yake kunishtua ninapoongea. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, hilo limeisha.

Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii ya kukushukuru kunipa nami nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na wenzangu kwa kutoa pongezi kubwa kwa Waziri wa Fedha pamoja na wanaomsaidia Naibu Mawaziri, Makamishna wa TRA pamoja na uongozi mzima kwa kazi nzuri walioifanya juu ya bajeti hii ambayo tunaijadili hapa. *(Makofi)*

Lakini pia nimpongeze Waziri Mheshimiwa Wasira aliyewasilisha juu ya Mpango wa muda mrefu, nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo wamejipangia juu ya Serikali kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapa mwaka jana na nirudie tena kwamba ombi langu mwaka jana nilisema namna ambavyo tunakaa hapa, tunajadili kupitisha bajeti na fedha zinakuwa hazifiki kwa wakati kwenye Halmashauri ili kutekeleza miradi, nilisema ambapo Kamati ya Bajeti imelisema leo hapa naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema ni vizuri wakati wanaendelea kukusanya maduhuli ni vizuri Serikali ikakopa fedha Benki Kuu awamu kwa awamu ili ziwe zinakwenda kwa waakti kwenda kutekeleza miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia hasa mambo yanayotokana na Jimbo la Njombe Kaskazini. Tuna mradi wa maji pale Makambako, naishukuru Serikali ilitupa fedha. Niombe sana Serikali itupe fedha ili mradi huu uweze kukamilika ili wananchi waendelee kunufaika na maji pale Makambako hasa mwezi wa 9, 10, 11 na 12 tunakuwa na tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi pia ambao uko Image unaokwenda Lupembe kule kwenye vijiji karibu 9, 10, mradi huu Serikali ilitupa fedha na niombe sana Serikali itoe fedha kumalizia ili miradi hii iweze kuwasaidia wananchi wanaoishi maeneo ya kule Lupembe. *(Makofi)*

Nizungumzie mambo ya barabara, niombe sana Serikali itupe fedha kwa ajili ya barabara ambayo ilifanyiwa upembuzi na tayari imeshatengwa kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha lami kutoka pale Kibena kwenda kule Lupembe. Ni vizuri Serikali ikatupa fedha ili mradi huo uweze kuanza mwaka huu wa 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mambo ya umeme wenzangu wamezungumzia na mimi niungane na mradi ambao tulipewa tangu mwaka jana mwaka juzi kwamba umeme utatoka pale Makambako kupitia vijiji vya Lyamkena, Kiumba, Itipinyi mpaka kwenda kule Lupembe na kwenda mpaka Songea. Tuombe mradi huu sasa mkandarasi tulipata taarifa

alikwishatangazwa, ni vizuri Serikali ikatoa fedha kwa mkandarasi huyu ili shughuli hizi mwaka huu zianze ili ziwanufaishe wananchi wa vijiji vinavyopitiwa na umeme huu. *(Makofi)*

Lakini niombe kuna baadhi ya vijiji ambavyo vinaingia awamu ya pili, kwa mfano pale Muloa, Kifumbe, Ibatu, Kitandililo, Ikwete, Manga, Mawande, Idamba, Mfiriga napo pia ni vizuri Serikali ikatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha vijiji hivi kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la elimu. Niipongeze Serikali kwa mpango mzuri ambao wametenga fedha kwa ajili ya kujenga maabara, kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu, basi ni vizuri sasa Serikali ikatupa fedha hizi kwa wakati ili tuweze kukamilisha shughuli hii ambayo ipo mbele yetu.

Lakini niiombe tena Serikali kuna shule nyingi za watu binafsi, niombe Serikali kama Serikali inatoa ruzuku kwenye hospitali za watu binafsi kwa nini isitoe ruzuku kwenye shule za watu binafsi ambazo wanafanya kazi ile ile ambayo Serikali inaifanya. Kwa mfano pale Makambako na hala pengine tuna shule ya Naboti sekondari ni shule moja mzuri sana, inafanya kazi vizuri. Sasa ni vizuri Serikali ikasaidia kwa watu binafsi kuchangia kutoa ruzuku kama ambavyo inafanya kwenye hospitali za watu binafsi, itakuwa ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pale Makambako juu ya hospitali. Tunaishukuru Serikali ilipandisha hadhi Kituo cha Afya na kuwa hospitali. Niombe sasa baada ya kupandishwa hadhi kuwa hospitali tuombe mtupe fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya kufanyiwa upasuaji pale, shughuli zinakwenda vizuri. Niombe Serikali iweze kukamilisha suala hilo la kupata vifaa tiba ili watu waweze kufanyiwa shughuli za upasuaji pale badala ya kwenda mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia hapa inazungumzia habari ya magari ya miaka kumi sasa kushushwa kuwa magari yaingizwe nchini ya miaka nane.

Ndugu zangu Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ni maskini sana, gari lenye umri wa miaka kumi kwa Tanzania gari hili bado ni jipya kabisa, bado ni jipya kabisa. Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali mnaposema gari la miaka kumi linaharibu mazingira, hebu tupe *data* ni mazingira gani hayo ambayo yameharibiwa kupitia gari hilo la miaka kumi? Gari hili bado ni zuri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sanga akisema hivyo anazungumzia kutoka kwenye *point* ya uzoefu. Kwa hiyo, hazungumzi tu.

Mheshimiwa Sanga endelea.

MHE. DEO K. SANGA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo gari hili, gari kwa mfano la kutoka mwaka 2004/2006 lina miaka tisa, kumi, gari hili bado ni jipya kabisa. Kwa hiyo niiombe sana Serikali irudishe gari za miaka kumi ziweze kuwasaidia wanyonge wa Tanzania ambao ndiyo wanaibuka kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya watu hapa wamechangia wakisema Serikali hii haijafanya kitu, mimi naogopa sana. Hivi kweli Serikali hii hakuna mambo yaliyofanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi niwaombe ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kwanza unaposema Serikali hii ya CCM haijafanya kitu hebu jitathmini wewe

mwenyewe umeifanyia nini Serikali hii halafu ndiyo useme Serikali ya CCM haijafanya kitu. Serikali ya Jakaya Mrisho Kikwete imefanya kazi kubwa sana, lazima tuipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upungufu tunakubali, lakini Serikali imefanya kazi kubwa sana. Hata unaposema Serikali haijafanya nini, hapa unatoka leo hapa unakwenda Manyoni, unakwenda Kondoa, unakwenda wapi, unakwenda wapi, unataka Serikali ifanye nini sasa? Ni lazima tuseme ukweli, Serikali ya Jakaya Mrisho Kikwete imefanya kazi kubwa, haijapata kutokea na lazima tuipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sanga nikuhakikishie hata Mheshimiwa Tundu Lissu anatikisa kichwa kukubali. Endelea Mheshimiwa Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Ni kweli, Serikali imefanya kazi nzuri, lazima tupongezane, upo upungufu, tunakubali. Lakini Serikali imefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la minara. Napongeza wakati tunajadili Bajeti ya Mawasiliano, niiombe Serikali sasa kwa sababu hawa watu wenye makampuni ya minara wanashindwa kutekeleza na Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya mawasiliano.

Niombe sana Serikali ipeleke fedha hizi kwa wakati ili minara katika maeneo yetu ili wananchi wetu waweze kupata mawasiliano ya uhakika na waweze kufanya biashara zao za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niiombe Serikali juu ya kilimo namna ambavyo Serikali imejipanga kununua mazao mbalimbali kwa wakulima. Niiombe fedha hizi zitengwe kwa wakati ili mkulima asikopwe, anapouza mazao yake anauza kwa sababu atatue matatizo aliyonayo. Kwa hiyo niombe Serikali…

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, malizia Mheshimiwa.

MHE. DEO K. SANGA: Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Serikali kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, nakushukuru.

Sasa anayefuata ni Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe.

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi kwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia naomba nitoe pongezi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Wasira kwa kazi anayoifanya na tatu naomba nitoe pongezi kwa Kamati ya Fedha.

Kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali yangu kwa mambo mazuri inayofanya. Kila mmoja aliye hapa anajua kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne inafanya mambo mazuri kwenye Jimbo lake na kwenye Halmashauri yetu. Kila Mbunge aliye hapa anafahamu kwamba miradi ya maendeleo inayoendelea kwenye jimbo lake. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa mambo yote inayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tulipo kwanza kabisa naishukuru Wizara ya Nishati. Umeme REA wamefanya mambo mazuri, kila mmoja kwenye jimbo lake kwa wastani amepata vijiji mbalimbali ambavyo vinategemea kupata umeme, kwa hiyo, tunaishukuru sana. Kila jimbo kwa wastani imepata vijiji ambavyo inategemea kupata maji na mpaka sasa hivi maji kwenye vijiji vingine yanatoka. Kwa hiyo, Serikali yetu inafanya mambo mazuri na naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete iendelee na idumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya mwaka 2014/2015 vimelenga kwenye miradi ya BRN. Miradi ya BRN tunaifahamu kuwa ni elimu, kilimo, nishati, maji, uchukuzi na ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua mambo haya ni lazima sana tuwekeze kwenye mambo haya, kwa sababu mambo haya kabisa yanamlenga Mtanzania na hasa yanamlenga Mtanzania yule aliye kijijini na hasa nikiongelea kwenye upande wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilenga sana bajeti yetu kwenye mambo ya kilimo asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini na hawa wa vijijini wanategemea uchumi wao kutoka kwenye kilimo. Kwa hiyo, naishukuru naiona hii Bajeti kama itatekelezwa vizuri ipasavyo itafanya vizuri na kwa hiyo naishukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu uchumi. Uchumi wetu tunaona unakuwa, ni kweli Tanzania inafanya vizuri kwenye uchumi na umekuwa mpaka asilimia saba. Naamini kwamba uchumi kama tutasimamia vizuri utaendelea kukua zaidi ya asilimia saba kama Kamati hii ya Bajeti ilivyosema kuwa inalenga angalau uchumi uendelee kukua mpaka kwenye asilimia nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato. Naamini kuwa ukusanyaji wa mapato na hasa tukisimamia vyanzo tulivyo navyo sasa ukusanyaji utakuwa nzuri. Jambo la maana ni usimamizi. Nilikuwa nashauri kuwa usimamizi wa mapato, ukusanyaji wa mapato, usimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa nashauri kuwa viangaliwe vyanzo vipya vya mapato kama utalii pamoja na uvuvi wa baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naamini kuwa mapato yakisimamiwa yanaweza kukua na kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuwe na tabia ya kudai risiti mara tunaponunua bidhaa madukani, Watanzania wengi hawana tabia hiyo. Nawaomba hata Waheshimiwa Wabunge huko madukani mnakokwenda kununua vitu vyenu muweze kuomba risiti kusudi tuweze kukuza pato letu na hasa nawaasa pia wafanyabiashara wawe na tabia ya kutoa risiti kwa sababu umefika wakati, wakati mwingine nawaambia nipatie risiti, mfanyabiashara anasema kwani unahitaji risiti. Kwa hiyo, naomba iwe ni lazima na ieleweke kuwa tutoe risiti na tuombe risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kuwa Watanzania wengi wanalalamika kuwa hawana kazi, kazi ipo na kazi imejaa. Watanzania hawana nidhamu au maadili ya kufanya kazi, Watanzania wengi hawatumii muda wao kwa kufanya kazi, ni kupiga porojo tu, kama hivi tunavyofanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wafanyakazi, nimesema wafanyakazi sikusema ninyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana wafanyakazi waweze kutumia nafasi yao vizuri pamoja na wakulima kwenye kufanya kazi yao vizuri. Waache kukaa kwenye *pool* au kufanya kazi zingine ambazo hazionekani. Vijana nawaasa, kazi ya kwanza ni kilimo. Vijana wengi tumewaona wahitimu baadhi yao, kutoka SUA, kutoka vyuo vingine, hata *Tumaini University* wamejiunga kwenye vikundi mpaka sasa hivi wanafanya kazi ya kulima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba sana vijana wanaomaliza vyuo vikuu, njooni huku mikoani, njoo kwa Wakurugenzi, nafasi ipo, tutawatafutia ardhi. Mtaanza kilimo na tutashirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 mpaka 12 hasa kwenye mishahara ya wafanyakazi mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ananisikia naongea kwa unyenyekevu, naona kuwa kwa kweli ni kidogo sana. Nawatetea wafanyakazi, asilimia moja hiyo iliyopungua ni kidogo mno. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na ninashauri hiyo muiangalie kusudi kuwapatia unafuu wafanyakazi na wenyewe wakajiona angalau wamefaidi kwenye bajeti hii ya mwaka huu 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yangu kwa kutenga bajeti ili kulipa madeni ya wazabuni na makandarasi. Ukweli uliopo ni kweli walikuwa wanatusumbua sana maofisini, wapi, wakiomba hela zao. Kwa hiyo nashukuru sana bajeti hii ambayo imeona kuwa wakandarasi na wazabuni waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri kuwa hata yale madeni mengine ya taasisi zingine ambayo yameorodheshwa naomba pia myaangalie kusudi muweze kuwalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwanadamu anahitaji maji mwilini mwake, naishukuru Serikali yangu kuona kuwa bidhaa zinazozalishwa kwenye maji yaliyo hapa Tanzania viwandani hayatatozwa ushuru, pia na *juice*. Naamini kuwa kwa upande wa lishe tunahitaji vitamini mwilini mwetu. Kwa hiyo, nafurahi sana kuona *juice* zinazozalishwa kutoka kwenye matunda ambayo yanazalishwa hapa nchini hayatatozwa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za maendeleo, nilikuwa nashauri kuwa mara kwa mara unakuta hela za maendeleo tunategemea fedha za maendeleo kutoka nje. Lakini nilikuwa naomba sana hizi fedha za maendeleo iwekwe mikakati kusudi ziweze kufika zote na ziweze kufika kwa wakati ili miradi ya maendeleo iweze kutimilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tatizo ni kweli wakati mwingine unakuta miradi ya maji haitimiliki kwa wakati, unakuta miradi ya DADPS haitimiliki kwa wakati kwa sababu fedha za maendeleo zinachelewa. Lakini kwa Serikali yangu sikivu naamini kuwa itajitahidi litafuta hizi fedha kusudi miradi iweze kutimilika kwa wakati na hata wananchi waweze kupunguziwa hali ya umaskini walionayo huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba sana Watanzania tuwe na tabia ya kufanya kazi. Naamini kuwa tukifanya kazi kila mmoja kazi aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kila mmoja kazi aliyo nayo hatutakuwa tunalalamika kuwa kuna umaskini hapa Tanzania na ninarudia kusema kuwa kazi ya kwanza ni kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana, Watanzania tufanye kazi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, sasa tumsikilize Dkt. Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Joseph Selasini ajiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi zilizopo hapa mbele yetu.

Kwanza kabisa napenda niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jitihada zake zote inazofanya kuhakikisha mwananchi wa kawaida hasa wa kijijini, nikiungana na ndugu yangu Injinia Stella Manyanya kwamba, sasa wanaanza kuona matokeo ya kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niende moja kwa moja katika hoja. Kwanza kabisa napenda kuungana na Kamati ya Bajeti kwa mapendekezo yao yote ambayo wamekuwa wakiyatoa kila wanapokutana na toka imeanza pamoja na upya wake, lakini imeonekana kabisa Kamati hii ni msaada mkubwa sana katika upatikanaji wa fedha hasa katika Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi katika hili ni kwamba sasa ifike mahali Serikali ifanyie kazi mawazo yanayotolewa na Kamati, tena hasa kwa kuangalia vyanzo vipya kwa ajili ya kupata mapato ambavyo, vimeainishwa kwenye ile Ripoti ya Mheshimiwa *Chenge One* ambavyo vyanzo vingine amesema vya uvuvi, kupiga mnada, uwindaji wa kitalii, mawasiliano, kodi za majengo na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hivi kwa sababu mpaka sasa hivi kwa nini tunakuwa na kodi ya mapato ya ajira ya hali ya juu? Asilimia 13, leo tunaambiwa imepungua kwa 12%, ni punguzo dogo sana ukilinganisha na mshahara anaopata mtumishi wa Serikali, hasa wa kima cha kati au kima cha chini. Lazima tufike mahali sasa tumuonee huruma huyu mtumishi, yeye sio wa kubeba mzigo kwa ajili ya kutekeleza miradi. Ukiangalia kwenye fedha tunazotenga za maendeleo, fedha za maendeleo zinakuwa chache kuliko fedha za matumizi mengineyo. Sasa haya matumizi mengineyo tumesema yapunguzwe fedha ziende kwenye maendeleo, ili miradi iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana, sipendi kurudia yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti, napenda Serikali iangalie na myachukue, kuna kigugumizi gani kuchukua hayo? Mbona ni mapendekezo mazuri tu yanayoleta Serikali yetu kupata fedha za kutosha ili kutekeleza miradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niseme, kuna hili suala unakuta mafungu yanatengwa, yanapitishwa Bungeni, lakini hayaletwi kwa wakati, fedha haziletwi kwa wakati, ni hivi tu tunaambiwa hela zile bilioni 80 nukta ngapi zile ndio zimetoka majuzi kwa ajili ya miradi ya maji ambazo fedha hizo tuliidhinisha Bajeti ya mwaka jana. Sasa hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, inatuambia hata hii bajeti tutakayoidhinisha italipa madeni ya mwaka jana. Kwa maana kwamba na kwa lugha iliyo rahisi mnataka kutuambia hatuna bajeti ya mwaka huu na kwamba bajeti iliyopo tunalipa madeni ya nyuma. Sasa tuondokane na hiyo hali, sisi tunataka wananchi wawe na maendeleo mazuri na wayaone. Tunasema uchumi unakuwa kwa 7%, mwananchi wa Katavi kule anajua uchumi unakuwa kwa 7% jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, anataka aone ukimwambia uchumi umekua, treni inatembea, uchumi umekua barabara inapita barabara ya lpole, ile barabara kila siku naipigia kelele, naomba kwanza niulize kwa nini haikuwekwa kwenye kipaumbele? Naona katika vipaumbele

vyenu kuna barabara ya Tabora – Ipole mpaka Rungwa, sasa pale Ipole mnapapita, ili mje Koga, sasa mimi nataka kuuliza hata kama kuna mazungumzo yanaendelea, toka mwaka 2011/2012 mpaka leo haya mazungumzo yanaendelea mpaka lini? Maana hilo nalo ni la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi kule kila siku nasema toka 1961 hawajaona lami jamani. Mheshimiwa hapa na Mheshimiwa Said Nkumba shahidi yangu, dada yangu Uvinza kule Kasulu shahidi yangu, hizo barabara zinaenda lini na sisi ni wazalishaji wakubwa, kila siku nasema niambiwe kwa nini hii barabara haiwekwi kwenye kipaumbele? Ya kutoka Ipole – Koga mpaka Mpanda, mpaka Uvinza mpaka Kasulu? Na kwa nini hii barabara ya kwetu hapa Sumbawanga – Nyakanazi haziishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio ya msingi ndio atakwambia uchumi umekuwa, hawezi kukwambia uchumi umekuwa wakati haoni, lazima aone kwa macho. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Spika wewe ni shahidi, umesema umeenda Kigoma huko umeona nyumba zimebadilika na nini, sawa, sikatai. Hizi nyingine ni jitihada za wakulima wenyewe, anaona sasa atenge pato langu, leo niweke matofali ya kuchoma, kesho niweke mabati, kesho kutwa niweke *solar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunataka waone na wenyewe wafaidi, kama ni hizo barabara ziwekwe, lakini kuna hii miradi pia ya umeme toka 2011 mpaka 2015 ipo inasemwa, upembuzi yakinifu, mchakato, leo miaka minne. Kwa mfano huu mradi wa *Kv* 400 ambao umesemwa kwenye kitabu humu wa *North West Grid,* ni lini? Kila siku tunausikia na fedha zinatengwa, toka 2011 fedha zinatengwa, sasa hatuelewi zinafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ooh, tunasubiri *compensation,* tunasubiri, hapana jamani, tufike mahali tufanye kazi, kama Msemaji aliyepita, kila mtu kwa nafasi yake afanye kazi. Tena afanye kazi kwa bidii na kwa maarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee tena katika kuongea katika sekta ya fedha kuna hii ya kuanzisha taasisi itakayotoa mikopo ya nyumba. Mimi naomba nishauri badala ya kuanzisha hiyo taasisi ni vema mkashirikiana na Shirika la Nyumba na mkawapunguzia baadhi ya vifaa vyao vya ujenzi kodi ili waweze kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wananchi wa kawaida, hasa wa vijijini kama kule Mlele, sasa hivi wameanza, lakini ile nyumba itaenda si chini ya milioni 40. Sasa milioni 40 kwa mkupuo mtu kuinunua kwa kweli kwa mwananchi wa kijijini ni ngumu, hasa ukizingatia Mheshimiwa Sanga ametoka kusema hapa tusiwakope wananchi wetu mazao, sasa tunawakopa, lini atanunua hiyo nyumba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hili lingine katika hotuba ya Waziri ametenga bilioni 8.7 ujenzi na ukarabati wa hospitali za mikoa mipya, ikiwemo na mikoa mingine Kilimanjaro na wapi. Naomba tu mimi niombe kwanza hii fedha kwa hospitali hizo haitoshi, ni kutufurahisha tu masikioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Serikali kama tunaamua kujenga, kwa mfano Mkoa wa Katavi, Simiyu, Geita, ile ni mikoa mipya tuwe na mipnago ya mbele. Usiniambie sasa hivi unaenda kukarabati Hospitali ya Mpanda pale ambayo hata eneo la pembeni la ukuta hakuna, unakarabati wapi kuwa Hospitali ya Mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunataka sasa badala ya kujenga nyumba moja moja tujenge kwenda juu, tujenge maghorofa. Mimi nafikiri hospitali angalao zinaweza kuchukua watu wengi wakutosha na tunaweka barabara hizo ni kwamba wananchi wataingia na kutoka kwa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba tu niongelee hili la ufungaji wa umeme Biharamulo, Mpanda na Ngara. Wiki iliyopita nimepata *message* kutoka kwa Profesa Waziri wa Nishati kwamba jenereta hizo sasa zinatengenezwa, sijui zinatengenezwa ama zinakarabatiwa Ubelgiji, sijui zitafika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niwaambie nimesema Mpanda sasa hivi umeme ni tatizo na nimeweza kufanya mawasiliano na Katibu na Wizara, nawaambia wananchi wa Mpanda Mjini sasa kuanzia mwisho wa mwezi huu jenereta mpya tutapata wakati tunasubiri hizo za Ubelgiji, ili muweze ku-*enjoy* na ninyi kuangalia Kombe la Dunia na muweze kufanya biashara zenu zinazowaletea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba tena nitoe katika hili suala la wastaafu limeongelewa humu. Mheshimiwa ile shilingi 50,000/= kwa mwezi haitoshi, naomba vyanzo hivi muviangalie upya.

Kuna Mifuko ya Jamii, ili iweze kujiendesha na kuogopa kupata hasara sasa ifike mahali hii mifuko pia ya jamii iwekeze kwenye miradi ambayo faida yake itarudi kwa haraka ili iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Serikali ijenge kuondokana na huu uchakavu, tunasema tuingize magari ya miaka kumi, nane, ngapi, hebu iangalie mfumo rafiki ambao utaweza kumwezesha mwananchi wa kawaida kuhusu kupunguza ushuru wa bidhaa. Ushuru wa bidhaa ndio unaongeza hayo madubwasha yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uweze kupunguza, jenga mfumo rafiki ili huyu mwananchi sasa badala ya kununua *second-hand* aanze kufikiria kununua gari mpya, ndipo tutakapoweza kupunguza haya matatizo yote. Kwa hiyo, tuangalie upya mfumo wa kupunguza ushuru wa bidhaa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu waambie wananchi wa Mpanda Mjini ambako ndiko ninakotoka kwamba tupo pamoja na tunahangaika nao kuhakikisha kwamba, tunapata maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Dkt. Pudenciana Kikwembe kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia mabenchi mengi yana watu wachache wachache, lakini ukiangalia benchi moja limetia fora, lile ambalo yuko Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Peter Serukamba, lile ni benchi la mfano. Sasa naomba na mabenchi mengine yawe yanajaa hivyo hivyo. *(Makofi)*

Benchi namba mbili katika utafiti wangu ni la Mheshimiwa Ally Kessy na wenzake pale nalo linapendeza kwa kweli. Kwa hiyo na wengine igeni mfano huo. *(Makofi)*

Sasa katika uchangiaji tunaendelea, mchangiaji anayefata ni Mheshimiwa Joseph Selasini, asubuhi ilisemekana Jimbo lake majogoo hamna kitu kule.

Mheshimiwa Joseph Selasini karibu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii na ningeanza na hilo ulilolisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi kuna hoja ilisemwa hapa kwamba watu wangu wana shida, majogoo hayapandi mtungi. Sasa kwanza nataka niwathibitishie kwamba hiyo shida hatuna, tupo sawasawa na wale wote ambao mngependa tuwe wakwe zenu karibuni Rombo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ningependa kusema tu kwamba jambo hilo limezungumzwa kwa sababu kisayansi unywaji uliopindukia wa pombe unaathiri uwezo wa wanaume katika eneo hilo na kwa sababu hiyo sio Rombo peke yake ni nchini kwa ujumla na ndio maana ningependa kuishauri Serikali iachane na hii tabia ya kila mwaka ya kupandisha kodi kwenye vinywaji kwa sababu inasababisha wananchi wetu kwa ujumla, nchi nzima sio Rombo peke yake kujiingiza katika unywaji wa pombe ambazo zinaharibu afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ningependa pia kuchukua nafasi hii kuwaomba Watanzania waangalie sana jambo hili, unywaji uliopindukia unaharibu afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba ninaunga mkono 100/100 taarifa ya Kamati yetu ya Bajeti iliyosomwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na katika uchambuzi wetu kuna mambo mengi ambayo tuliyaangalia na kuyazingatia. Niseme tu moja kwa moja wakati tukijadili bajeti za Wizara mbalimbali, yapo mapungufu mengi sana tuliyoyaona katika kila Wizara na tumeishauri Serikali na tunafikiria kwamba Serikali italeta hapa Bungeni mrejesho wa ushauri wetu.

Mimi ningependa kusema Serikali ikubalianena ushauri wa Kamati ya Bajeti, kwa mfano, tumezungumza sana kuhusu matatizo ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi halina magari, Jeshi la Polisi halina vitendea kazi, Jeshi la Polisi limekosa morali ya kufanya kazi na ni Jeshi linalopigana kila siku, posho za Jeshi la Polisi zimekuwa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio jeshi hilo tu, Jeshi la Magereza ni hivyo hivyo. Imefikia mpaka sasa hivi wafungwa wanatembea hawana nguo, makalio yako nje katika Taifa hili na sisi sote kwa ujumla sheria inaweza ikatubana kwa namna moja au nyingine. Serikali lazima iangalie Jeshi lile na kulisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni majeshi yetu yote kwa ujumla, ni lazima yaangaliwe vizuri na Kamati ya Bajeti tumeshauri, tunaomba Serikali ielete hapa Wabunge wote kwa ujumla wetu tujadili na muone ni nini tulichoshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Manyanya amesema kuhusu *cess* ya mahindi pamoja na pamba. Kamati ya Bajeti tumeshauri na tumetoa mapendekezo yaje hapa Serikali ilete tuyaone.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni MSD. Bodi ya Dawa wamekaa na sisi wametuambia deni lao lisipolipwa mwezi wa nane ukifika nchi itakosa dawa. Serikali ilete ushauri wa Kamati ya Bajeti hapa muone tulichoshauri, upo ushauri wa kutosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Balozi zetu, inawezekana Wabunge hamjui, lakini nje ya nchi kuna aibu kubwa sana ambayo tunaipata. Ubalozi wa Zambia mti uliota ndani ya nyumba ya ubalozi mpaka ubalozi ukaanguka. Ubalozi wa Nigeria tumepata viwanja, vinataka kunyang'anywa. Ubalozi wa Uingereza tumepata viwanja, jengo limebomoka, tunataka kunyang'anywa na Ubalozi wa Marekani hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kenya, tulipewa kiwanja sambamba na sisi tuliwapa kiwanja hapa Msasani na wao wakatupa kiwanja kule, wao wameshajenga, sisi bado tunasuasua. Ubalozi wa Msumbiji ni matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti tumetoa ushauri, ni vizuri Serikali iangalie na sisi tumeshauri maeneo ambayo lazima tufunge mkanda yatatuliwe lazima tufunge mkanda, lazima tufunge mkanda MSD deni lilipwe wananchi wapate dawa, lazima tufunge mkanda Balozi zetu zishughulikiwe, lazima tufunge mkanda tuache kulalamika kwamba Polisi hawana maadili, Polisi wapate magari wasaidiwe, Magareza wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, cess Serikali iliagiza wananchi wauze mahindi yao. Halmashauri hazijapelekewa fedha zao mpaka leo, wakati tunalalmika Halmashauri zikusanye kodi na tumetoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu uchumi kwa ujumla. Bajeti hii isipoangaliwa inakwenda kuuwa uchumi, tusiwe na haraka ya kufikiria kwamba kupunguza misamaha au kuondoa misamaha ndio tunajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kipo kiwanda kimoja sasahivi wameamua baada ya kupandishiwa *excise duty* kutoka 10% kwenda 25% wameamua kuanzia Bajeti ilipotangazwa wanazalisha *24 hours* mpaka tarehe 31 Juni, baada ya hapo kiwanda hakifanyi kazi. Kwa hiyo, mimi ninachoshauri tuangalie tusiwe na haraka katika hili jambo kwa sababu wawekezaji wanaweza wakatukimbia. Matokeo yake kodi inayokusudiwa itakosekana, matokeo yake tuta-*create* tatizo kubwa zaidi la ajira hapa nchini na mtokeo yake bajeti hii itakuwa sasa sio kwa ajili ya kusaidia uchumi ni kwa ajili ya kuuwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwa nguvu zangu zote, tuwe makini, hata itakapokuja ile sheria tuiangalie kwa makini kwa sababu tukienda kwa pupa tutasababisha wawekezaji watukimbie nchi hii. Hapa Kilombero, kiwanda cha Kilombero watu wa Illovo walitaka wapanue eneo lao, ili waweze kuzalisha miwa kwa wingi. Tumesuasua kuwapa eneo Illovo, wameondoka wameendazao Zambia, sasa Zambia ni mzalishaji wa sukari wa pili Afrika kwa sababu tu ya sera zetu na labda ama hamaki zetu katika kutekeleza mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba ninaipokea hii bajeti kama ilivyo, lakini kwangu mimi ambaye nimeipitia kwa muda mrefu katika kipindi hiki ninaendelea kushangaa. Waziri labda atakapokuja kufanya majumuisho atuambie, kwa mfano tumepitisha hapa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi shilingi bilioni 550 na kitu hivi, lakini Wizara ya Ujenzi haijatuambia ukweli, inadaiwa karibu shilingi bilioni 800, hivi hizi fedha zitalipwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio matokeo yake zinachomolewa chomolewa baadaye kwenye *re-allocation* na matokeo yake nchi haiendi, bajeti inayumba. Twende kwenye suala la TANESCO, TANESCO ni dudu ambalo linakula fedha kila mwezi bilioni 800 hazipo kwenye bajeti, zitapatikana vipi? Waziri atuambie fedha za TANESCO watapata wapi za mafuta mazito, fedha za madeni makubwa kama madeni ya ujenzi atapata wapi, vinginevyo tunapitisha kitu ambacho hakitekelezeki. Matokeo yake mwaka ujao tutakutana hapa tunaanza kulalamika, fedha hazikwenda kwenye maji, fedha hazikwenda kwenye REA, fedha hazikwenda sijui wapi kwa sababu, tayari kuna vitu ambavyo lazima vilipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la ujenzi wakandarasi wanadai na tusipowalipa lazima tutawalipa na riba, kwa hiyo, lazima watalipa, watalipa kutika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na imekuwa ni desturi hawa Maafisa Masuuli hawalipi haya madeni. Fedha zinakwenda wanafanya wanavyotaka, sasa ifikie wakati Maafisa Masuuli wawajibishwe ili fedha zao, madeni yao yaonekane kwenye Bajeti na walipe kutokana na Bajeti yao. Vinginevyo sisi tutakuwa tunaletewa hapa tunafanya *rubber stamping,* mambo yanaisha, tunamaliza Mkutano wa Bunge wa Bajeti, biashara inakwisha. Safari hii Waheshimiwa Wabunge, mimi nawaomba lazima tumkatake Waziri atueleze haya madeni ambayo kila Wizara inayo yatalipwa namna gani na kutoka kwenye mafungu yapi ya fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo wananchi wetu wataendelea kuteseka kwa maji kwa sababu fedha hazitapelekwa, zinapelekwa dakika ya mwisho kama ilivyofanyika mwaka huu, fedha zimepelekwa mwishoni mwa mwezi wa tano. Mwishoni mwa mwezi wa tano hata taratibu za manunuzi zitakuwa zimepitiwa namna gani? Matokeo yake fedha zinaenda kuliwa huko Majimboni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kupata fursa ya kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuendelea kuwa mzima, buheri wa afya na kuweza kumudu majukumu yangu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo machache sana; sio mchumi kitaaluma, lakini ninayo mambo macheche ambayo nimeyaona ndani ya bajeti, ningependa kuyazungumza. La kwanza kabisa ni kuhusu ukuaji wa uchumi. Wenzangu wengi wamezungumza, lakini kwanza naipongeze Serikali kwa kutueleza kwamba uchumi wa Taifa unakua sasa na pato la Taifa linakua kwa asilimia saba. Lakini jambo la msingi, ni kuona namna gani ukuaji wa uchumi unavyoweza kuathiri maisha ya wananchi hasa wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya vijijini ukuaji wa uchumi ni kuwahakikishia makazi bora, miundombinu inayopitika wakati wote wa mvua na kiangazi na kuwahakikishia wananchi wa vijijini wanapata fursa ya kusomesha watoto wao. Hayo ndiyo mambo ambayo yanaashiria ukuaji wa uchumi kwa mwananchi wa kawaida wa kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza ukuaji wa uchumi, tunazungumzia pia Halmashauri zetu. Tumeleta bajeti mwaka 2013; Halmashauri yetu kwa mfano ya Wilaya ya Lindi iliomba Serikalini bilioni 18, lakini hadi tunafika mwaka 2014 tunajadili bajeti mpya, Halmashauri yangu imepata Shilingi bilioni 14. Maana yake ni kwamba, Shilingi bilioni nne ambazo hazijapelekwa, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu mwaka wa fedha haujaisha, fedha hizi ziende kwenye Halmashauri ya Lindi ili ziweze kufanya kazi ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu daraja la Mchinga gharama ya Shilingi milioni 380; ilitarajiwa fedha hizi, Shilingi bilioni nne ambazo hazijafika ndizo zingeweza kujenga daraja na kuwahakikishia wananchi wa Mchinga wanafanya mawasiliano yao vizuri hadi kijiweni. Lakini barabara ya Nangaru, fedha hizi Shilingi bilioni nne ambazo hazijaenda, urefu wa kilomita 30 kutoka Nanyanje hadi Nangaru, hizi Shilingi bilioni nne ndizo ambazo tulitarajia tuzipate na hatimaye tuboreshe miundombinu ili wananchi wa Tarafa ya Nangaru waweze kusafirisha ufuta wao kwenda kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia michango mbalimbali na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametueleza michango ambayo sekta mbalimbali zinavyochangia ukuaji wa uchumi. Sekta ya Mawasiliano, 22.8% imeachangia kwenye ukuaji wa uchumi; Sekta ya Fedha 12%, Viwanda na Ujenzi 8%, lakini inastaajabisha kuona kwamba Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inachangia ukuaji wa uchumi kwa kipindi kilichopita kwa asilimia nne tu. Hili jambo linafadhaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu asilimia 70 ya wananchi wanaoishi vijijini, Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo ndiyo sekta inayotegemea kuendesha maisha yao na kuinua uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo mbalimbali wanaojishughulisha na uvuvi ukienda Mchinga, ukienda Mafia, maana yake hapa inaonesha kabisa namna ambavyo hawawezi kunufaika na sekta hii. *(Makofi)*

Niliwahi kusema hapa ndani ya Bunge letu kwamba tunalo tatizo kubwa la ajira kwa vijana. Katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba hadi kufika Aprili, 2014 mwaka huu, jumla ya ajira mpya zilizozalishwa ni 630,000. Lakini ukiangalia takwimu zinaonyesha ajira hizo kwenye Sekta ya Elimu ni ajira 36,073; Sekta ya Afya, ajira 11,221 zilizalishwa, lakini bado inasikitisha Sekta ya Kilimo imeweza kuajiri watu 130,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya wananchi wanategemea kilimo, lakini ni namna gani Sekta ya Kilimo imeandaliwa ili kuweza kutoa ajira kwa vijana wanaoishi maeneo ya vijijini? Bado hatujafanya kazi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tuliona uwanja wa Taifa vijana wakifanyishwa *interview* ili kuweza kuteua Maafisa Wahamiaji 70. Wamekwenda vijana 10,000 na zaidi ili kuweza kupigania nafasi 70. Maana yake ni nini? Maana wengine tulifikiri kuna mechi pale, Taifa *Stars* wanacheza ma Msumbiji; lakini kumbe ilikuwa ni vijana kwenda kuangalia fursa ya ajira 70, vijana 10,000. Sasa hali ile…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtanda, wale 10,000 ni baada ya mchujo wa maombi 20,000. Maombi 20,000, mchujo ule ndiyo ukatoa 10,000, ndio hao unaowazungumzia. Endelea Mheshimiwa!

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana rafiki yangu. Ninachojaribu kusema hapa ni kwamba Sekta ya Kilimo ndiyo Sekta ambayo tukiimarisha, itatoa ajira kubwa kwa vijana wenye taaluma za kishule na vijana wale ambao hawakupata fursa ya kupata elimu iliyo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri jambo hili ni muhimu. Pia katika Sekta ya Kilimo, kwa mfano, wananchi wa Mchinga wanategemea sana zao la ufuta, sasa hivi Serikali imeshindwa kudhibiti soko na sasa hivi wananchi wanauza zao hilo la ufuta kilo moja Sh. 2,220/= wakati Soko la Dunia linataka sasa kilo moja Sh. 2,800/= hadi Sh. 3,000/=.

Kwa hiyo, tumewaachia Walanguzi sasa wanadhibiti soko la ufuta. Kwa hiyo, wananchi ambao kwa muda mrefu wanategemea zao la ufuta hawanufaiki nalo. Hili nililizungumza sana wakati nachangia bajeti ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu aliahidi kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Lindi ili kuona namna Serikali inavyoweza ku-*intervene* katika jambo hili na kuleta tija kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mikoa mingine ambayo wanajihusisha na kilimo cha zao la ufuta. Matumaini yangu ni kwamba Serikali itakuwa imechukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo niliona nilizungumze ni kuungana na Serikali na Wizara ya fedha kwamba ulipaji kodi kwa mfumo huu wa kielektroniki ni jambo bora, ni jambo ambalo litasaidia kukuza mapato ya nchi yetu, lakini ninaomba sana Wizara, kabla hawajaanza matumizi ya Elektroniki kama ilivyokuwa, ni vizuri wafanyabiashara hawa wakapata fursa ya kupata elimu juu ya matumizi ya hizo mashine za elektroniki kabla hazijaanza kutumika. Lakini pia gharama kubwa kwa ununuzi wa mashine hizi za kieletriniki.

Kwa hiyo, nafikiri ni jambo bora Mheshimiwa Waziri na timu yake kuona namna gani kwanza wananchi wetu wafanyabiashara waelewe matumizi sahihi ya mashine hizo ndipo sasa tuanze kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana mkono na Serikali, pale ambapo wamekuja na mifumo mbalimbali ambayo itachangia kuboresha ili tuweze kupata kodi kupitia maboresho ya sheria mbalimbali hasa Sheria ya Kodi ya Mapato sura 332 ambapo kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi 12. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwa sababu mishahara inayolipwa kwa wafanyakazi wetu inatozwa kodi kubwa, kwa hiyo, uamuzi huu utasaidia sana wafanyakazi wetu kupata kipato kutokana na mishahara yao ambayo ni jasho lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nashauri kwamba, ikiwezekana wale wafanyakazi wa kima cha chini, bado hii asilimia 12 ambayo Waziri amependekeza ni kubwa sana, Wafanyakazi wanaopata mishahara ya kima cha chini, basi kodi yao ingekuwa ni asilimia 10 badala ya asilimia 12 ambayo Serikali imeshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nashukuru pia kwa sababu Serikali imeona adha ambayo watumiaji wa Mabenki wanaipata kuhusu ushuru mkubwa unaotozwa katika kufanya *transactions* za kifedha *(money transfer)* au *transaction* kupitia simu. Kwa hiyo, tunashukuru kwa sababu ukurasa wa 46 wa hotuba hii Mheshimiwa Waziri ameahidi sasa kuliondoa jambo hilo ili kuweza kuleta tija kwa watumiaji wa shughuli hizi za kibenki kwa ajili ya kutuma fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Deo Sanga, *Jah People,* mtu wa watu, kwamba sasa hivi ushuru kwa magari yale bado tuache pale pale miaka kumi, tusirejeshe chini kwenda miaka nane kwa sababu sababu zilizotolewa na Wizara hapa, hazina mashiko. Kwa hiyo, nafikiri bado miaka kumi, inatosha; tukipunguza kwenda miaka nane tutawaondoa watu wengi kwenye biashara hii ya magari nchini. Lakini pia inatu-*limit* sisi wenyewe. Tunazo njia nyingi, tunaweza kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu riba kubwa zinazotozwa na Taasisi ndogo ndogo za kifedha…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Said Mtanda, muda hauko upande wako, malizia tu Mheshimiwa.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kuhusu riba kubwa zinazotozwa na Taasisi ndogo ndogo za kifedha. Ziko hizi Taasisi zinazotoa mikopo midogo midogo, ni jambo zuri, lakini ni lazima Sheria idhibiti Taasisi hizo kwa sababu wakati mwingine itoza riba hadi asilimia 100 na zaidi. Unakopa Shilingi milioni moja, unaambiwa urudishe Shilingi milioni mbili ndani ya mwezi mmoja. Kwa hiyo, nafikiri Sheria irekebishwe ili Taasisi hizi zidhibitiwe kwa mujibu wa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Saidi Mtanda, nakushukuru sana. Kama nilivyosema mwanzoni, sasa namwita Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa Vita Kawawa! Ametoka? Oh! Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na niweze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Watendaji wake wote kwa kuweza kuwasilisha bajeti yake hapa Bungeni. Vile vile nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Kamati yake yote kwa kuweza kutoa ushauri mzuri sana katika ripoti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze labda na kuzungumzia kuhusu hoja ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Esther, mama yangu, maana jina lake anaitwa Esther.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 18 amezungumzia kuhusu Sekta ya Elimu, lakini amesema eti Serikali kuwa msimamiaji wa ubora wa elimu na siyo mtoaji wa elimu. Kwa kweli kwa hapa mimi naomba nipingane naye kwa sababu katika dunia yote, lazima kunakuwa kuna *public school.* Sisi wenyewe wote humu ndani walio wengi tumesoma katika Shule hizi za Serikali. Labda kitu kikubwa ambacho angesemea pale ni kwamba maboresho yafanyike kwa hali ya juu kuhakikisha kwamba elimu yetu ya Shule za Serikali inapewa kipaumbele kwamba kuwepo na maabara, yaani watendewe haki. Kwa sababu hii imesababisha hata vijana wengi vijijini wa hali zote kupata elimu tofauti na zamani kulipokuwa kuna Shule nyingi sana za *Private,* unaona kwamba watu wengi sana hawakupata elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwamba pamoja na uchumi wetu kukua kila mwaka, lakini bado tunaona kwamba hali ya umaskini inazidi kuwa kubwa kwa wananchi wetu wa Tanzania kama ambavyo Sensa ya mwaka 2012 ilivyosema katika ripoti yake. Inaonyesha bajeti zetu tunazopitisha hapa Bungeni bado hazijaweza kumkomboa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipitisha bajeti katika Wizara zetu, lakini matokeo yake, unapofika mwisho wa mwaka wa fedha tunaona kwamba fedha haziendi kwa wakati. Utakuta kwamba nyingi sana, asilimia 20 mpaka 40 tu ndiyo zinaweza zikafikia mwisho wa bajeti kupitishwa. Hii inasababisha miradi mingi ya maendeleo kutokamilika kwa wakati. Miradi inakuwa inatumia gharama kubwa sana kwa kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wale wote waliosema kwamba tunaomba sasa Serikali yetu, Wazabuni na Wakandarasi walipwe kwa wakati; kwa sababu tumeona kwamba katika bajeti zote, Wizara zote zimekuwa na madeni makubwa sana kwa hawa wazabuni na hata wakandarasi kwenye Wizara ya Ujenzi, kwa sababu hawa Wazabuni wetu, walio wengi ni wafanyabiashara na wamekuwa wakichukua mikopo Benki; na kutolipwa kwao kunasababisha hata wakati mwingine kufilisiwa mali zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kweli nimeshukuru kwamba katika ripoti wamesema madeni yote yatahamishiwa Hazina. Sasa naomba usiwepo tena urasimu wa kuwalipa hawa wazabuni au wakandarasi ambao wanafanya kazi katika Wizara zetu au Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee sana kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, imefanya kazi kubwa sana na imezindua miradi mingi sana mwaka huu. Kwa hiyo,

naomba kwa kweli nategemea kwamba kama Wizara zetu zitapelekewa pesa kwa wakati, miradi mingi itakamilika na tutaendelea kuzindua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, amekuwa akifanya kazi kubwa na nimpongeze pia Katibu wetu wa Chama cha Mapinduzi ambaye amekuwa akipita katika maeneo mbalimbali kuhamasisha kazi za Waheshimiwa Wabunge wetu za maendeleo. Kwa kweli nampa pongezi sana Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, ni vigezo gani vinavyotumika katika kupeleka pesa hizi za maendeleo katika Halmashauri zetu. Kwa sababu utakuta kuna baadhi ya Halmashauri ambazo pesa hazipelekwi hata kwa kipindi cha miaka miwili, mitatu na kusababisha miradi mingi kutokamilika.

Nikichukulia tu mfano, kwa sababu mimi nipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, utakuta kuna miradi; kwa mfano, miradi ile ya umwagiliaji, kuna miradi miwili ambayo imekuwa ya muda mrefu sana. Kuna mradi mmoja wa Mkoga ambao upo katika Kata ya Isakalilo, mradi ule ulirithiwa kutoka kwenye Halmashauri ya vijijini kabla hawajahamishwa. Lakini mpaka wamehamishwa safari hii, bado pesa hazijapelekwa toka mwaka 2011 mpaka sasa hivi hawajapelekewa pesa yoyote ambazo zinahitajika kama Shilingi milioni 526.

Pia kuna ule mradi mwingine ambao upo Kitwiru *Irrigation Scheme* ambao na wenyewe upo katika Kata ya Kitwiru. Nao ni mradi wa muda mrefu sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii miradi, tunategemea kwamba, pamoja na kwamba ipo Mjini, kama ingekamilika kwa wakati, ingeweza kusaidia hata ajira kwa vijana wetu. Tunaona Halmashauri nyingi sana, kutokamilika kwa miradi kunasababisha vijana wengi kukimbilia katika Miji mikubwa kwa sababu wanafikiri labda kule kuna ajira nyingi za kutosha. Lakini kama miradi mingi ingekamilika kwenye Halmashauri zetu, basi vijana wengi sana wangeweza kukaa katika Halmashauri zao na kupata ajira pale walipo. Kwa hiyo, naomba Serikali ituambie vigezo gani inatumia ili tuweze kujua kwamba tufanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusiana na mradi ule wa daraja la Igumbilo, upo pale Iringa. Huu mradi kwa kweli ni wa muda mrefu. Serikali iliweza kutoa pesa mwaka 2009 na 2010. Kuna Shilingi milioni 172 ambazo ziko pale. Baada ya hapo, haijaweza kutoa tena pesa mpaka leo, na ule mradi kwa kweli ni hatarishi sana kwa wananchi wa Iringa. Kwa sababu lile daraja linasababisha kila mwaka vijana wanapoteza maisha.

Sasa labda Serikali ingesema, lile daraja ili liweze kukamilika, linahitaji kama Shilingi bilioni 1.1, lakini zimeletwa Shilingi milioni 172 tu toka mwaka 2009 na 2010.

Sasa ningeomba kwa kweli labda Serikali ingesema, *either* labda kitolewe kibali, zile pesa zilizopo, basi litengenezwe tu daraja *temporary* kuliko pesa zimekaa toka mwaka 2009 mpaka leo hii haijaweza kuongezewa kiasi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipojadili kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kuhusiana na ujenzi wa viwanja vya ndege; kuna viwanja vya ndege 11 ambavyo vipo katika upembuzi yakinifu.

Sasa nilikuwa naomba kusema kwamba pamoja na kuwa kiwanja chetu cha Nduli na chenyewe kipo katika upembuzi yakinifu, tunaomba basi itengewe pesa kwa sababu kuna matatizo ya matengenezo barabara ya kuruka, yaani *run way* ambayo imesababisha kuna wakati kama mara mbili ndege ilitaka kupata ajali; basi itengewe tengeo iweze kurekebishwa

na pia kufanywe uzio. Kwa sababu utaona kwamba wanyama wanakatiza katikati ya uwanja, inaweza ikasababisha ajali kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niendelee kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ya ujenzi wa Wodi ya Watoto ambayo ipo katika Hospitali kuu ya Mkoa. Kwa kweli niipongeze pia Serikali ya Italy, imeweza kutoa pesa nyingi kwa ajili ya ule ujenzi wa kisasa wa Wodi ya Watoto iliyopo katika Hospitali yetu ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifungua Hospitali ya Wilaya ya Mkoa kwa ajili ya kupunguza msongamano mkubwa sana ambao upo katika Hospitali yetu ya Mkoa; na mpaka sasa hivi imeweza kujenga Wodi ya akina mama nzuri sana ya kisasa, hongera na vilevile imeweza kujenga *theatre*. Lakini sasa kuna msongamano mkubwa sana wa *theatre* katika hospitali yetu ya Mkoa. Tunaomba sasa viletwe vifaa vya kutosha ili ile *theatre* ya Wilaya iweze kufanya kazi na kuondoa ule msongamano ambao upo wa operesheni ili kunusuru vifo vya akina mama na watoto katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli nakipongeza sana Chama changu na naipongeza Serikali yetu na ninaomba…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RITTA E. KABATI: Naunga mkono hoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ritta.

MHE. ESTER N. MATIKO: Taarifa!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Nakushukuru sana kwa mchango wako na kuwasemea kweli kweli wananchi wa Iringa.

Taarifa hiyo inatolewa na nani?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Esther Matiko!

NAIBU SPIKA: Ooh! Samahani Mheshimiwa Esther! Endelea Mheshimiwa Esther!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ningependa tu kumpa binti yangu taarifa kwamba nafikiri hajanielewa vizuri. Sijasema kwamba *public schools* ziondolewe, ila nili-*suggest* kwamba kiundwe chombo, *Regulatory Authority* ambayo itakuwa ina-*control* kuweza kusaidia mfumo wetu wa elimu uwe bora zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kwa sababu ni binti yangu, nitamweleza zaidi tukiwa nyumbani kuliko kula muda wako. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, natumaini taarifa hiyo umeisikia.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami namshukuru sana mama yangu kwa kweli, nafikiri wote tunajenga nyumba moja na maboresho yatafanyika kuhakikisha kwamba hizi *public schools* zinapewa kipaumbele. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Esther Matiko.

Nilimtaja Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige na atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe. Mheshimiwa Ezekiel Maige!

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Kipekee naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Niseme, kwa hakika nilikuwa sijawahi kumwona Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hotuba yake na nilivyomwona kwa kweli alinifurahisha sana. Amekidhi vigezo, nakupongeza sana mama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi ambazo nimezitoa, naomba pia nitoe pongezi nyingi kwa Serikali kwa ujumla wake. Kusema ukweli kwa kazi za kimaendeleo zinazofanyika sasa hivi, hazina mfano. Ukifika kwenye Jimbo langu ukaangalia maendeleo yaliyofanyika katika kipindi cha miaka minane hii ambayo nimekuwa Mbunge na miaka hii minane ambayo Mheshimiwa Dkt. Kikwete amekuwa Rais wetu, kwa kweli mambo mengi sana ya kimaendeleo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna maji kwenye Miji mikubwa mikubwa au *center* kubwa kubwa ya maji ya bomba, tuna umeme karibia kwenye vijiji vingi unapelekwa, pamoja na miradi mingi ya kimaendeleo; na kubwa zaidi kufungua mawasiliano ya barabara. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba haya yanafanyika kwa kukusanya fedha na kwa maana hiyo malengo ya makusanyo ya kifedha ni ya muhimu sana. Nakubaliana na mengi ambayo yamependekezwa kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba yafanyike. Hata hivyo, nilikuwa na maeneo machache ambayo nilikuwa nataka sana kuiomba Serikali iyatizame kwa mara nyingine. Eneo la kwanza ambalo naona linahitaji kutazamwa zaidi, ni eneo hili la kupunguza au kuondoa kabisa misamaha kwenye baadhi ya maeneo.

Kwa mfano, kuna eneo moja ambalo nadhani linastahili sana; pamoja na kwamba sasa hivi linatozwa kodi; *VAT* kwenye nyumba za bei nafuu, kuna *Watumishi Housing Company* pamoja na *NHC* wanajenga nyumba kwa ajili ya kuboresha makazi ya watumishi lakini pia ya wananchi wa kawaida. Nyumba hizo ambazo zinalengwa ziwe na bei nafuu, zinaongezeka bei kwa sababu ya *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wamekuwa wakiwasiliana viongozi wa Taasisi hizi pamoja na Wizara ya Fedha kuhusu uwezekano wa kuondoa kodi kwenye nyumba hizo; bado uamuzi haujafikiwa. Naiomba sana Serikali, eneo hili litazamwe. Najua lina athari kimapato, lakini kijamii na kiuchumi ni jambo la muhimu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba eneo hilo litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, limeshazungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengine ni eneo la kurekebisha umri wa magari au mitumba kutoka miaka kumi hadi miaka minane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana sana na Waheshimiwa Wabunge walivyozungumza. Mimi naamini Watanzania wengi wanapenda kutumia magari ya mitumba, siyo kwamba hawapendi kuwa na magari mazuri yenye *AC* au yenye vitu vyote vinafanya kazi; ni kwa sababu ya hali ya uchumi. Kwa ujumla, gari la miaka minane, au gari la miaka kumi kwa hapa kwetu bado ni gari lenye hali nzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizotolewa kwamba yanasababisha ajali, sidhani kama uchambuzi wa kina umefanyika, kwa sababu mimi naamini ajali zinasababishwa na vitu

vingi; kuna hali ya madereva, hali ya barabara, pamoja na hali ya magari yenyewe kwa maana ya kufanyiwa *service*. Kwa hiyo, nadhani kwamba magari yaendelee kutumika hadi umri wa hiyo miaka kumi ndiyo huo msamaha wa asilimia 25 kwa magari chakavu uweze kuendelea kutolewa kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo moja ambalo mimi naliona ni la muhimu sana, na sijui kwa vipi wenzangu hawajalitazama hivyo. Kuna moja ya pendekezo limewekwa kwenye ule ukurasa wa 47 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unazungumzia ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu na wote tunafahamu kwamba nimewahi kuhudumu kwenye Sekta hii ya Maliasili na hasa kwenye misitu. Mwaka 2012 mahitaji yetu ya mbao yalikuwa ni *cubic meter* milioni tano; uzalishaji uliokuwa ukifanyika kwenye mashamba ya Serikali ulikuwa ni *cubic meter* milioni 1,200,000. Tuna mashamba 16; *Sao Hill* pamoja na mengine. Kiasi cha *cubic miter* 300,000 zilikuwa zinatoka kwenye misitu ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii najua wamefanya utafiti kupitia ile *agency* ya *NAFOMA*; wanaita mradi wa *NAFOMA* ambao umeonyesha kwamba hivi sasa huwezi ukapata mninga, mtundu, mkola, mvule, mti wa mbao au mbao za aina hiyo kutoka kwenye *general land*, yaani kutoka kwenye maeneo yasiyohifadhiwa. Kwa lugha rahisi ni kwamba, kwa kiasi kikubwa sana miti imekwisha kwenye maeneo yasiyohifadhiwa, na kwa maana hiyo uzalishaji wetu wa mbao ni mdogo sana.

Kwa hiyo, ukiweka ushuru kwenye thamani zinazotoka nje, kwa lugha rahisi kabisa, unatangaza kiama kwa misitu. Nilikuwa naiomba sana Serikali, hii sera; *policy approach* ya kulenga zaidi kwenye uvunaji badala ya kulenga zaidi kwenye uzalishaji, ijaribu kubadilishwa. Kuna maeneo mengi ambayo ni ya misitu kwa maana ya sheria, lakini misitu imekwisha. Ukiangalia maeneo ya misitu kama *Ruvu North, Ruvu South*, Masanganya, Kazimzumbwi, Mufindi; maeneo mengi yamebaki hifadhi kwenye karatasi au hifadhi kwenye kumbukumbu za kisheria, lakini *on the ground* ni vichaka na nyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, kabla ya kuweka ushuru kwenye samani zinazotoka nje, bado tuendee kuruhusu samani kutoka nje ili kuoa misitu yetu na tuweke nguvu zaidi katika kuhimiza upandaji wa miti. *(Makofi)*

Hivi sasa asilimia 95 ya mbao zinatoka kwenye mazao au kwenye mashamba ya Serikali, kwenye nchi ambazo uchumi wake unatokana na misitu. Kwa mfano, nchi kama Finland, New Zealand; zaidi ya asilimia 75 ya mazao ya misitu yanatoka kwenye mashamba binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi hapa ni asilimia tano tu ya mbao inatoka kwenye mashamba binafsi maeneo ya Njombe pamoja na maeneo mengine ya Mkoa wa Iringa.

Naamini kwamba Serikali ikiweka nguvu kwenye eneo hili, tukahimiza zaidi upandaji wa miti, *commercial plantations* na hapa ni eneo muhimu sana la kutumia hii *PPP*, kwa maana ya *Private, Public Partnership* kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kupanda miti kwenye maeneo ambayo yalikuwa *forest reserves* lakini kwa sasa hivi zimekuwa *depleted* kiasi cha kwamba siyo misitu, siyo hifadhi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, tutakuwa tumeongeza uzalishaji na kwa kufanya hivyo, itawezekana sasa baadaye kuja kuweka huo ushuru.

Hivi sasa tunazalisha magunia milioni 36 kwa mwaka ambayo ufyekaji wake ni zaidi ya hekta 400,000 kwa mwaka. Ukiweka ushuru kwa mbao zinazoagizwa nje au samani zinazoagizwa nje, ninaamini kabisa kwamba *deforestation* itakuwa ni kubwa kuliko kiwango kilivyo hivi sasa.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuishauri Serikali kwamba kwa kuanzia, tuweke nguvu katika kuhimiza sekta binafsi ishiriki katika upandaji wa miti *tax incentives* ziweze kutolewa kwenye eneo hilo na *PPP* itumike kwa kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kupanda miti kwenye maeneo ambayo ni hifadhi, lakini hayana miti, tuweze kuongeza uzalishaji na *potential* yetu ni kubwa sana. Naamini tukifanya hivyo tutaweza kufanikiwa kuliko kupata haya mafanikio ya muda mfupi ambayo athari zake kwa muda mrefu ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba nimalizie tu kuiomba Serikali. Kule kwetu tunavutana sana na watu wa migodi kuhusu ushuru wa huduma, wao wenyewe pamoja na *sub-contractors* wanaofanya kazi kwenye migodi hiyo.

Naiomba Serikali, kama sehemu ya kuongeza mapato kwenye Halmashauri, najua mazungumzo yamefanyika na yamefikia hatua nzuri, lakini naomba sana Serikali iongeze mkazo katika mazungumzo ili migodi ianze kulipa ushuru wa huduma, yaani *service levy* kwenye Halmashauri kama ambavyo inatarajiwa. Lakini kubwa zaidi, *sub-contractors* wanaofanya kazi kwenye migodi waweze kubanwa iwezekanavyo ili waweze kutoa ushuru kwenye Halmashauri.

Kwa sisi Halmashauri yetu ya Msalala kwa mfano, *service levy* inayoweza kutoka kwenye mgodi wa Bulyankhulu ni zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 2.4 kwa mwaka. Kwa sababu tu mbalimbali za kisheria na za kimkataba ambazo zipo baina ya mwekezaji na Serikali, ushuru huo haukusanywi zaidi. Inayokusanywa ni Dola 200,000 ambazo hazisaidii chochote. Kwa hiyo, naiomba Serikali, eneo hilo ni la umuhimu, lizidi kutazamwa na ninaamini linaweza likasaidia sana kuongeza mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba niishie hapo, nashukuru sana, lakini kimsingi, naunga mkono sana hotuba na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magoliyo kwa hotuba yako nzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Freeman Mbowe, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo mawazo katika hoja inayoendelea mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji kadhaa waliotangulia kuzungumza mahali hapa, wamezungumzia tatizo la ajira, lakini sina imani kabisa kwamba Serikali inaona *seriousness* ya tatizo hili. Tunapozungumza habari ya watu ambao walikwenda uwanja wa Taifa vijana 11,000 kutafuta ajira 70 tunalifanya kama jambo la mzaha, hatuoni kama ni janga la Taifa. Sasa Wabunge wamelizungumza, nami naomba nilitie mkazo jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma kidogo, watu wengi wamezungumza jambo hili akiwemo Kiongozi mmoja mwandamizi sana ndani ya Chama cha Mapinduzi, lakini akapondwa kwamba anazungumza mambo kwa kuzua, hajaona kwamba Serikali inatekeleza mikakati ya kutoa ajira za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba ajira ni mkakati na ajira siyo jambo la kufumania kwamba litazuka lenyewe. Ukiangalia taarifa ambazo Serikali inatoa, unaona hakuna mpango ambao unaratibiwa kuanzia katika ngazi ya chini kabisa ya wananchi kuja

mpaka ngazi ya Taifa kutengeneza ajira katika Taifa hili. Kila kitu tumekilundika katika Serikali Kuu kwamba *Central Government* ndiyo inatakiwa ifikirie kwa niaba ya Watanzania wengine wote namna ya kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu 133 hazina mkakati wowote wa kutengeneza ajira katika maeneo yao na Serikali Kuu haizisukumi Halmashauri za Wilaya zitengeneze ajira miongoni mwao. Halmashauri inakaa inafanya mipango yake na bajeti yake ya mwaka, hakuna mkakati wowote unaoelezea kwamba Halmashauri hii mwaka huu itatengeneza ajira 1000, 2000 ama 3000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, hili Gazeti la Mwananchi lilitoa picha nzuri sana, nami napenda sana kuwapongeza Gazeti la Mwananchi. Katika ukurasa wa tatu, hii hali ni hali ya aibu! Kama Serikali yoyote iko makini, hali kama hii ingestahili kwamba hii hoja ya ajira iwe ni hoja maalum ndani ya Bunge hili, iwe ni hoja maalum ndani ya Serikali, iwe ni hoja maalum ndani ya Baraza la Mawaziri, iwe ni hoja maalum ndani ya Halmashauri za Wilaya, kwa sababu this the *National tragedy*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna watoto 11,000 wanatafuta ajira 70 na kila mwaka tunaingiza vijana zaidi ya 500,000 wanaotoka aidha Kidato cha Sita, katika Vyuo na katika Vyuo Vikuu katika soko la ajira. Lakini mkakati wa kitaifa wa kupambana na hili tatizo la ajira, haupo! Hata kama upo, upo katika *Central Government,* haupo katika *Local Government*! Mimi nashauri hivi, hatuna sababu ya kuwa na Wakurugenzi wa Wilaya na wataalam wachumi katika Wilaya kama hawawezi kubuni miradi ya kuweza kujenga ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya ku-*stimulate* uchumi katika Halmashauri zetu na hili linawezekana. Nami nitawaeleza hapa namna ya kupata Shilingi bilioni 500 kila mwaka mpaka Shilingi bilioni 800 pesa ambazo mnaweza mkazipeleka katika Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Wilaya zikaanza miradi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukajenga *industrial pack* katika viwanda vyetu katika Wilaya zetu. Tusizungumze tu ajira ambazo labda kuna wawekezaji binafsi wamekuja ama wako kwenye madini wakapata ajira, lazima tutengeneze ajira sisi kama viongozi, sisi kama Wabunge, sisi kama Serikali, ni lazima tuweke mikakati ya makusudi kabisa ya kuhakikisha kwamba ajira zinatengenezwa kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kutengeneza ajira kupitia miradi mbalimbali itakayobuniwa kuanzia ngazi za Halmashauri ya Wilaya na iwe ni lazima, iwe ni elekezo la Serikali Kuu! Kama nyie hamwezi, mtusubiri tuingie Serikalini mwaka ujao tutoe maelekezo haya. Sisi tunawasaidia ushauri ili iwasaidie na iwasaidie Watanzania. Lakini nyie hamtaki kuchukua ushauri, mnaona labda ni utani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema ni hivi, tunaitaka Serikali itoe agizo kwa Halmashauri zote za Wilaya. Kila Halmashauri ya Wilaya ibuni miradi katika Wilaya ambayo inaweza ika-*absorb* ajira ya vijana kati ya 5,000 mpaka 10,000. Haya mambo yanawezekana, wala siyo mambo ya kufirika, kunahitajika mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ambazo zitakwenda kuwezesha miradi kufanyika, zitakuwa zinashindaniwa kwa Wilaya ambazo zina miradi ambayo ni *more competitive* ambayo inaonekana kwamba kweli inaweza ika-*generate* fedha na vilevile inaweza ikatoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii miradi isiwe miradi ya Umma, iwe ni miradi ya Umma ambayo inashirikisha sekta binafsi kwa maana ya *PPP* kwa sababu ya kuweka ile *discipline* ya

management katika miradi hii. Kila Wilaya ina utaratibu na mazingira tofauti ya uwekezaji, na kwa kupitia uwekezaji huo, inaweza ikazalisha ajira za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kila Halmashauri tukailazimisha kutengeneza ajira 5,000 kwa mwaka, maana yake nini? Tuna uwezo wa kutengeneza ajira 665,000 kwa mwaka katika Halmashauri za Wilaya.

Kama Wilaya fulani fulani zitaweza kupeleka mpaka vijana 10,000 wakapata ajira kwa miradi mbalimbali ambayo iko ndani ya Wilaya, ina maana tunazungumza ajira milioni 1.3 kwa vijana ama wakulima wetu katika nchi nzima. Kwa utaratibu huu tutapunguza ule mkakati ambao unaonekana sasa kwamba watu wote wanahama vijijini, wanaonekana kuhamia mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanakimbilia Mjini kwa sababu wanaona sasa fursa iliyobakia katika Taifa, vijijini hakuna fursa. Hao wafadhili wetu wa mambo ya maendeleo wanalalamika kwamba kweli uchumi wa Taifa unakua; lakini uchumi wa Taifa unaokua hau-*reflect* kwenye maisha ya kawaida ya wananchi ila ni kwamba ni kipato cha uchumi kinakua kwa kundi fulani la watu wachache ambao pengine na wana fursa zaidi. Lakini kwa Watanzania walio wengi ambao hasa wako katika *rural area,* hatujaweka mkakati wa kutosha katika kuhakikisha kwamba tuna-*stimulate rural growth* na hili ndilo jambo ambalo nalizungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaeleze, mtapataje hizi hela? Tumependekeza mara nyingi katika Kambi ya Upinzani kwamba, angalieni *construction industry* ambayo inaweza ika-*generate* pato kubwa sana kwa Taifa hili. Tumependekeza mara nyingi anzisheni *Really Estate Regulatory Authority*, m-*consolidate* kodi mbalimbali zinazotokana na majengo kwa maana ya *property tax* pamoja na *land rent*. *RERA* isimamie *land rent* pamoja na *property tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu Wilaya kama ya Kinondoni, Ilala ambayo ina ile *CBD*, yaani *Central Business District* ya Dar es Salaam, kwamba ni Wilaya ambayo nayo inangoja *subsidy* kutoka Serikali Kuu wakati kutokana na *property* ambazo ziko kwenye *CBD*, Halmashauri ya Wilaya ya Ilala ingeweza ikajenga Dar es Salaam nzima. Halmashauri ya Kinondoni, haihitaji kupata *subsidy*. Tumeweka Viongozi katika Halmashauri ambao hawafikiri, wanangojea kupelekewa kila kitu *from the Central Government* na ni kwa sababu ninyi mmeendekeza hali hiyo. Ndiyo sababu tunasema m-*decentralize*, mruhusu Halmashauri za Wilaya ziweze kutengeneza mikakati ya kukusanya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkiweza kutengeneza *RERA*, maeneo kama ya *Oysterbay* ni *category number one*; maeneo kama ya Masaki, Dar es Salaam ile ni *category namber one*. *Property* za kule mahali zina uwezo wa ku-*generate* fedha za kutosha. Watu wanajenga majumba makubwa, wanapata pesa ham-*collect taxes*, wala hakuna mkakati wa ku-*collect taxes*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema kwa kupitia *RERA* mna uwezo mkubwa. Kama mnataka *idea,* njooni wala msione aibu, tuwape mawazo nzuri ya namna ya kutengeneza fedha hizi muweze kwenda mbele. Yako mambo mazuri mnaweza kufanya na nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu ananisikia vizuri, huu tunatoa ushauri wa bure tu. Naomba niendelee mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikiliza hotuba za Waheshimiwa Viongozi Mawaziri wetu katika mambo ya deni la Taifa, tuna madeni mengi sana ya kujitakia. Kuna madeni ambayo ni *realistic*, lakini kuna madeni ambayo tungeweza tukaya-*avoid,* lakini hatuya-*avoid*, matokeo yake tunajipa mzigo mkubwa kweli kweli wa madeni. Nami nitatoa mfano rahisi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza mara nyingi kwamba miradi yoyote ile inakuwa na *value for money,* inakuwa na thamani yake kwa fedha kama itatekelezwa kwa wakati tutaokoa fedha nyingi sana ambazo zinapotea bure. *(Makofi)*

Sasa sikilizeni niwape mfano mmoja rahisi, nina mfano ambao ni *latest*. Mwaka huu katika bajeti tunazungumza kwamba tumetenga Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuwasaidia vijana nchi nzima, lakini ni mwaka huu wa 2014 kupitia mradi wa *Kinyerezi One,* Serikali itapata hasara ya Shilingi bilioni tano kwa sababu ya kuchewelesha malipo ya kumlipa Mkandarasi wa Jacobson ambaye anajenga Mradi wa Kinyerezi. Nitawapa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni barua imetoka kwa watu wa Jacobson, barua ya tarehe 5/6/2014 inakwenda kwa *TANESCO* kwamba kuna *arrears* ya malipo ya Shilingi dola milioni 48 hayajalipwa na Wizara ya Fedha imeahidi kuwalipa, haijawalipa. Hawa jamaa wanataka kusimamisha mradi na kwa ucheleweshaji wa malipo ya mradi huu, kwa muda wa miezi sita, kwa sababu kila mwezi Serikali mlistahili kulipa Dola milioni 12.5, hamjalipa pesa hizo Januari, hamkulipa *installment* ya Februari, hamkulipa ya Machi, hamkulipa ya Aprili, hamkulipa ya Mei. Mmelipa *installment* mbili tu za mwezi Novemba 2013. Matokeo yake mmeandikiwa barua mnadaiwa sasa kwa mujibu wa mkataba, dola za Marekani milioni 3.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hela ya Tanzania kwa *exchange rate* ya Dola moja ni Sh. 1,800/= *to* Sh. 1,900/= kwa *rate* ambayo inakwenda sasa hivi, hii ni *5.1 billion Tanzanian Shillings*. Sasa huu ni mradi mmoja, tunapoteza fedha za bure! Hizi fedha mngeweza mkaziokoa.

Sasa ninachosema, tunaiomba Serikali hii, tunaishauri Serikali hii hebu chagueni miradi ambayo ni *priority*. Hiyo ni *money management*. Chagueni miradi ambayo ni *priority,* muitekeleze kwa ukamilifu, msituingize kwenye hasara za bure! Mnaliingiza Taifa kwenye hasara za bure! Kila mradi wa barabara ni fedha! *(Makofi)*

Mimi kuna mradi wangu mmoja uko Hai, mradi wa mwaka 2009 umechukua miaka sita, kilometa 12 za barabara mpaka Rais amezundua. Ni mambo ya aibu, lakini mkandarasi anakusanya fedha. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Ya kwanza hiyo!

NAIBU SPIKA: Ya pili. Malizia tu Mheshimiwa! Nakushukuru sana. Dakika moja.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa hiyo, kwa kumalizia kabisa, nitoe hoja moja tu ya mwisho kabisa kuhusu *withholding tax* ambazo mnakusudia kui-*introduce* kwa watu ambao wanakodisha ndege kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi, niwaambie Serikali; nchi hii katika ndege zinazoruka katika anga ya Tanzania, ndege ambazo zimenunuliwa na Watanzania hazifiki 5% ya ndege zinazoruka nchi hii. Ndege zote zinatoka nchi za nje. *Air fair* katika nchi hii ni kubwa sana! Leo tunakwenda Kenya kwa nauli ambayo ingetupeleka Dubai au *South Africa* kwa sababu hatuna *Air line* yetu, hatuna ndege zetu na bado tunataka kui-*introduce withholding tax*. Hiyo Kodi itahamishwa kwa mwenye Ndege, itarudishwa kwa mtumiaji wa ndege ambao ni sisi Watanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tayari *air fair* ni *prohibitive* kwa nchi yetu, iko juu sana. *Air fair* ziko juu sana! Mtaua Utalii katika nchi hii kama mtaingiza kodi za namna hii, na utalii ni chanzo kikubwa sana cha mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali chonde chonde, hii kodi ambayo mnataka kuianzisha kwa upande wa kutoza *withholding tax* kwa ajili ya ndege zinazotoka nje, hiki kitu acheni, mtaua *tourism* katika nchi hii, hatuna ndege za ndani. Ina maana mta-*impose* kwa ndege za *Precision,* kwa ndege za *Air Tanzania* yenyewe ambayo ni Shirika la Umma, hizi ndege zimekuwa *leased* na nyingine zitaendelea kuwa *leased*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye makosa ya kufikiri tu kwamba kila biashara inyongwe kwa kodi! Tunakwenda kuua *economy* muhimu sana kwa mambo ya *tourism*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa upendeleo maalum. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Freeman Mbowe. Katika siku ambayo siwezi kukubaliana na wewe zaidi ni leo, hasa kwenye suala la ajira.

Tunaishukuru sana Serikali ya awamu ya nne kwa kusambaza umeme vijijini. Huo ni mtaji mkubwa sana wa *creation* ya ajira popote pale nchini na maji. Lakini niseme…*(Kicheko/Makofi)*

Mnisikilize vizuri, Nina nia njema kwa sababu nakubaliana kabisa na aliyosema Mheshimiwa Mbowe. Suala la ajira, hilo ni tatizo kubwa ambalo ni lazima lishughulikiwe.

Kuna vijana ambao hawaendi shule na ni maelfu lazima watazamwe; kuna vijana katika Shule ya Msingi ambao ni *droppers* hawafiki Darasa la Saba, na wenyewe hawa wanaweza wakawa ni mamilioni; kuna wanaomaliza Darasa la Saba, kuna wanaomaliza *Form Four*, kuna wanaomaliza *Form Six*, wanaomaliza Vyuo vya Kati, wanaomaliza Vyuo Vikuu; Ukichukua hiyo *group* yote na ukubwa wake, ni *millions of people*.

Sasa ndiyo maana nikasema, kwa uwekezaji huu wa Serikali ya awamu ya nne wa maji, umeme vijijini na kadhalika unaondelea, ni mahali pazuri sana pa kuanzia.

Waheshimiwa Wabunge, ni kwa nini nimesimama niseme; nilitaka kusema tu kwamba, kwa sababu ni dakika za mwisho za awamu ya nne, wale wanaojipanga kwa awamu ya tano, kama hukuongelea ajira, basi andika umeumia. Ajira ndiyo hoja inayokuja. *I am talking* yaani kutoka moyoni kabisa. Tuna maelfu ya vijana na ndiyo *voters* ambao lazima tuwatazame. Watoto wetu, ndugu zetu hawana ajira nchi hii, na ni jambo kubwa sana. Kila mtu ambaye ni *serious,* lazima afikirie suala la ajira kwa vijana. (*Makofi*)

Sasa nimwite Mheshimiwa Vita Kawawa! *(Makofi)*

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Mao Tse Tung alisema, kwamba ukiona adui yako anakusifia sana katika jambo fulani, jambo hilo liangalie kwa makini. Lakini ukiona mtu jambo unalolifanya wewe unaamini ni sawa sawa, halafu yeye analibeza analichukia, anakushauri vinginevyo, kazana nalo. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuhusu suala la vyanzo vya mapato walivyoviona vinafaa, kazaneni navyo hivyo hivyo. Kazaneni navyo! Hizo *withholding tax* kwenye ndege, kazaneni nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani leo hii Kamati ya Bajeti leo hapa asubuhi, imetueleza kwamba Serikali imeonekana kama haina utayari wa kupokea vyazo vya mapato. Sasa leo Serikali inaanzisha Serikali vyanzo vya mapato, tunaambiwa tusitoze *withholding tax* kwenye eneo hilo. Endeleeni! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili naomba nianze kwa kuwapongeza wenzangu, Mawaziri wote kwa kutoa *presentation* yao vizuri. Nawapongeza pia na Manaibu Waziri kupata nafasi hii katika Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nianze katika eneo moja la msamaha wa kodi. Msamaha wa kodi ya *VAT*, kuna sheria tumeletewa hapa tumeanza kupitia, na Mheshimiwa Spika alisema tuipitie na kama kuna mtu ana wazo lolote la *schedule of amendments* basi apeleke kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo hili ambalo liko katika ukurasa wa 170 katika Jedwali la Muswada huu ambao unazungumzia ku-*exempt imports* za wanyama, kutoa kodi ya ongezeko la thamani kwa wanyama hai. Kwa mfano, ng'ombe, shwaini ambaye ni nguruwe, *sheep,* kondoo, kuna mbuzi mpaka kuku. Muswada huu unaeleza kwamba wapate msamaha wa kodi wa ongezeko la thamani.

Pia, kuna mpaka *unprocessed* tumbaku humu ndani, ipo. Sasa mimi sikubaliani na hili kwa sababu leo tuna ng'ombe wengi hapa, tuna mbuzi wengi ambao wanatakiwa wapate masoko. Sasa tunataka turuhusu tuwape nguvu au tuwape *incentives* ya ku-*import* ng'ombe wazima hapa, mbuzi wazima hapa humu ndani; ng'ombe wetu hawa watakwenda wapi? Kwa hiyo, nashauri na *discourage* hii na nia ya kuleta *schedule of amendment* kubadilisha Muswada katika vifugu hivi. Naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lingine ambao watu wengi wamezungumza, lakini nami naomba nizungumzie kuhusu uchumi wetu ambao unakua kwa 7%. Lakini ni lazima tutekeleze kwa vitendo kuwafikia wananchi wetu hasa vijana na wanawake ambao hawana ajira. Kuna maeneo mengi ya kufanya, lakini pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, juzi alitusomea kwamba mapato ya Halmashauri zetu kwa ujumla wake, mapato ya ndani yatakuwa zaidi ya Shilingi bilioni 858. Katika sheria zetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia, imeelekeza kwamba asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri zetu yaelekezwe katika miradi ya vijana na akina mama.

Kwa hiyo, ukichukua kwa haraka haraka, asilimia 10 hii ni zaidi ya Shilingi bilioni 45. Kwa hiyo, naomba tusimamie vizuri eneo hili la *Local Government* ili kuhakikisha hizi asilimia 10 kweli Wakurugenzi wanasimamia vizuri, zinaenda kwa vijana na akina mama. Itatusaidia sana uchumi wetu huu tunaojidai nao kuwafikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna malalamiko katika eneo lingine la wastaafu. Wanalalamika sana kuhusu *pension,* hasa Maafisa wa Majeshi, kwamba, wamebaguliwa katika maeneo mawili. Kuna wanaopewa *pension* zao na Hazina na kuna wanaopewa na *GEPF*. Kwa hiyo, hawa wanaopewa na Hazina wao wanasema wanapata kidogo. Kwa hiyo, wanalalamika kwamba ni lini Serikali itawapeleka katika mfumo huu wa *GEPF* na wanaomba sana Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri, yeyote atakayekuja kufanya majumuisho, basi watoe maelezo ili waweze kulielewa jambo hili na waweze kupata faida nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vya mapato, nilikuwa nashauri tusiache wala kudharau mapendekezo ya vyanzo vya mapato yanayobuniwa na kutolewa ushauri wa vyanzo

hivi vipya ambavyo viko vingi sana. Tuyaangalie vizuri maeneo ambayo tunapata mapato au watu wanabuni mapato; tuwa- *encourage* wanaobuni vyanzo vya mapato katika sekta zote.

Pia wale ambao wako katika mpango wa *retention,* kwa mfano, kuna Taasisi zilizoko katika mpango wa *retention* ambao wanakusanya mapato yao, halafu Serikali inawaambia, asilimia kadhaa Hazina mbakinazo au wanapewa na Hazina. Taasisi hasa zilizo chini ya Wizara ya mambo ya Ndani, nitatoa mfano; Zimamoto na Uhamiaji, *retention* yao ilikuwa asilimia 70. Leo imepunguzwa mpaka 49. Lakini wao makusanyo yao huwa yanazidi *target* ambayo wanapewa na Hazina.

Sasa Hazina inafanya *calculation* yake kwa ile *target* iliyowapa tu, ile *surplus* ambayo wao wanapata, haifanyiwi *calculation*, inazama kwenye Mfuko Mkuu. Kwa hiyo, mnawa-*discourage* hawa! Kwa hiyo, tunaomba sana, Hazina iangalie sana katika maeneo haya ambapo hawa wanaokusanya mapato na *retention* zao na wameonyesha kabisa kwamba, zile *retention* zinafanya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna taasisi ambazo zinakuwa na mpango wa kupata vyanzo vipya vya mapato. Nitazungumzia eneo lingine la Tumbaku. Tumbaku ni eneo ambalo linazalisha fedha nyingi ya mapato katika nchi hii. Kwa mfano, tu rahisi ni kwamba Bodi ya Tumbaku peke yake au Serikali kwa ujumla unafanya kazi ya *crop surveying*, inafanya kazi ya ku-*grade* au *classification* ya mazao yale ya Tumbaku.

Pia, inasimamia masoko, tena soko la zaidi ya dola milioni 250 na kazi hizi zote inafanya bure, hakuna *service levy*. Sasa hii Bodi ilipendekeza huko nyuma kwamba ili kupunguza mzingo kwa Serikali, basi angalau watoze ile *service levy* kwa sababu kufanya kazi ya *crop surveying* nchi nzima bure, unawafanyia hawa wananuzi wa nje, unafanyia uteuzi, unawasimamia soko lao bure, halafu wao wananunua yale mazao wana *export without export levy,* yaani wao wana *process,* wana *export*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Tumbaku ilitoa mawazo huko nyuma kwamba angalau basi watoze *service levy* ya kazi hii ili kupunguza mzigo kwa Serikali kuhudumia hilo. Walisema kwamba kama watapata kazi *Service levy* hii, itasaidia kuongeza uzalishaji na kusimamia, kwa sababu wamesimamia katika mpango mkakati, wamefikia zaidi ya tani 130,00 ya uzalishaji kutoka tani 60,000 na mauzo yake yalifikia Dola milioni 350.

Sasa uzalishaji ulikua, wafanyakazi walikuwa wachache, anashindwa kusimamia; sasa uzalishaji umepungua kwa sababu wafanyakazi wameshindwa kisimamia maeneo yale yote ya tumbaku nchini. Kwa sababu uzalishaji ni mkubwa, *human resource* iko ndogo na tuliomba kwamba lazima tupate wateuzi wa kutosha kwenda kusimamia, matokeo yake ni kwamba uzalishaji umepungua kwa sababu ya kukosa wafanyakazi. Sasa Serikali lazima itambue hili pia, kwamba tuongeze watumishi katika eneo hili ili waweze kutupatia fedha za kutosha. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kawawa malizia!

MHE. VITA R. M. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niseme kwamba, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na suala la ripoti ya ubadhirifu Wilaya ya Namtumbo iliyotokana na watu walioshirikiana kuwaibia wakulima wa tumbaku.

Pia kwa sababu hili ni suala la uchumi wa wananchi wa Namtumbo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba walifanyie kazi, Serikali ije na majibu hapa, ripoti hiyo imesema nini ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa sababu wakulima hawa mwaka 2013 hawakulipwa fedha zao mpaka leo. Ni kwamba wameibiwa fedha zao na kundi la watu walioshirikiana na Benki katika mpango wa mikopo. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ije na kauli kuhusiana na ripoti hiyo iliyodhulumu wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa kwa mchango wako. Mheshimiwa Kidawa Hamed Saleh, atafutiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha.

MHE. KIDAWA HAMED SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naanza kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake wawili vijana mahiri, wachapa kazi, wenye elimu ya kutosha kwa kazi nzuri waliyoifanya wakiwa katika nafasi zao kwa muda mfupi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono taarifa ya Kamati ya Bajeti, nami ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Fedha kwa kuonyesha dhamira sahihi ya usimamizi na udhibiti na matumizi ya Serikali kwa kutaka kuleta Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili jambo lifanyike kweli katika mwaka huu wa fedha kwa sababu limeanza kuzungumzwa zaidi ya miaka minne nyuma na halijaletwa. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba mwaka huu wa fedha hii sheria iletwe.

Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendeleza lile jambo ambalo alifufua Marehemu Mheshimiwa Mgimwa la kuwa na *pre-budget consultation* baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kitu ambacho kikiendelezwa kitapunguza malalamiko ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja kwamba bajeti yetu ya mwaka ujao wa fedha ni ngumu sana kutokana na kuwa imebeba pengo kubwa ambalo halikutimiziwa na bajeti ya mwaka huu inayomalizika ya Shilingi trilioni mbili na ile nyongeza ya Shilingi trilioni 1.6. Kwa hiyo, hapa pana ugumu kidogo, hasa ukingalia vyanzo vya mapato vimekuwa vinasuasua kidogo.

Mwaka 2011/2012 au 2012/2013 kianzio chetu cha mapato cha *TRA* kilikusanya karibu asilimia 104 ya malengo yake. Kwa hiyo, kilifanya vizuri. Lakini kwa mwaka huu unaomalizika hadi Aprili ni asilimia 75 tu. Kwa hiyo, hii inatia mashaka kidogo. Zile changamoto ambazo zilizungumzwa zimeleelezewa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuwa ndizo zilizosababisha kutokufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Sitegemei kama zitamalizika zote kwa mwaka huu wa fedha ujao. Zikimalizika, ndiyo tunavyoomba, mapato yawe vizuri. Lakini kama hawakujitahidi, zile changamoto zikaendelea kuwepo kwa maana hiyo na mapato yataendelea kuwa madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa sababu hili ni jambo la nchi, siyo jambo la Serikali peke yake, wala siyo jambo la viongozi peke yao; nadhani kunahitajika jitahada ya pamoja ya wadau wote wa nchi hii, ikiwemo Serikali na Taasisi zake, wakiwemo walipa kodi wenyewe, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani kushirikiana na Serikali yao kuchukua agenda ya ukusanyaji wa kodi na ulipaji wa kodi kuwa ni agenda yetu sote kama

Watanzania. Mbunge, Mwakilishi, Diwani na Viongozi wa Vyama wa Upinzani, wote tunahitaji mapato, kwa sababu wote tunatumia mapato hayo ndani ya nchi yetu kwa manufaa yetu.

Kwa hiyo, kila tunapokwenda kufanya Mikutano yetu *whether* ikiwa ya hadhara au ya ndani, kila mmoja akijipa jukumu la kutoa elimu inayohusiana na kodi, basi nadhani tutasonga mbele vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ningependekeza kwamba somo la kodi lianzishwe kuanzia shule za *primary*, Darasa la Sita na la Saba, pale tayari wameshakuwa na akili nzuri. Likianza kusomeshwa mle, hadi Vyuo Vikuu, vijana wetu watakuwa wakiwa na mabadiliko ya kimawazo, wanajua nini kodi, nini manufaa ya kudai risti na nini manufaa ya kodi ndani ya nchi yao. Nadhani Taifa letu litabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, nimeshazungumza, lakini mapato yasiyokuwa ya kodi, haya ni mapato yanayokusanywa na Wizara na Taasisi zake, zimekuwa hazifanyi vizuri.

Takwimu zinaonyesha, makusanyo yamefikia asilimia 57 na haya ni maduhuli. Lakini kinachoshangaza, ni kuwa Wizara zinataka mapato ya nyongeza yatoke Hazina, wakati wao wenyewe maduhuli wamekusanya chini ya asilimia 50. Hili siyo jambo jema! Hili lichukuliwe kama ni jukumu letu sote, changia wewe, kusanya mapato, simamia mapato yako ya *portfolio* yako, fikia asilimia 100 na zaidi, *then* laumu Hazina kwa nini hawakutupatia mapato. Kwa sababu katika lile kapu zima la Hazina, linategemea mapato kutoka vianzio vyote; ya kodi na yasiyokuwa ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na *retentions scheme*. Kuna Taasisi kweli, wameruhusiwa kukusanya na bajeti ya Taasisi zile, wanaiandaa wenyewe, wanaji-*commit* Serikalini, kwamba katika mwaka huu wa fedha nitakusanya *X billion Shillings.* Lakini inafika hadi wanakusanya labda *20%.* Halafu katika ile *20%,* wanaambiwa, utapata *retention* ya *49%* au *70% and above*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale kama mtu mwingine yeyote, angejitahidi, akakusanya yale mapato, yakafikia ile bajeti aliyoiweka mwenyewe, au zaidi, halafu ile asilimia ya *retention*, ikamfaa kutumia katika mambo yake ya maendeleo. Lakini watu hawakusanyi! Wanakuja wanalalamika waongezewe mapato, watatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumeyaona. Wanakuja wanalalamika tuongezeeni, tuongezeeni! Ongeza ukusanyaji! Umeshapewa nafasi wewe ya asilimia ku-*retain* na kutumia kwa mambo yako, kwa nini hufanyi jitihada? Kwa nini hiyo isiwe ni motisha ya kukufanya wewe kukusanye zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo. *Mentality*, *mind sets* za watu bado hazijabadilika *towards* ukusanyaji wa mapato. Lazima tubadilike kuisaidia Serikali ya nchi hii, kuwasaidia Watanzania wote. Tukikusanya mapato, Watanzania wote wanafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hili lililozingumzwa. Serikali iwe tayari kuchukua ushauri wa vianzio vipya vya mapato. Imekuwa ikihemea kwenye vianzio vilevile tu ambavyo ni *traditional*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Pay As You Earn,* kwa kuwa ni rahisi kukusanya, hapa Serikali inasema imepunguza kwa asilimia moja, *what is* asimia moja? Asilimia moja siyo kitu! Tunataka

Serikali ipunguze kodi hii ya wafanyakazi mpaka ifikie *single digit*. Mheshimiwa Waziri amesema, lakini bado haijafikiwa, eti tunaanza kwa asilimia moja!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bado kabisa! Tunakwenda kuwa-*charge* wafanyabiashara ndogo ndogo, tunawaongezea kodi, wao wenyewe shida tupu! Mitaji yao midogo, bado tunawakata zaidi! Hii hatuwasaidii! Tunataka Serikali itengeneze mazingira ya kuwafanya wafanyabishara ndogo ndogo, wafanye shughuli zao vizuri, wavutike na tuwaingeze kwenye wigo taratibu taratibu kwa sababu kuna motisha, hawatakimbia. Lakini ukiwawekea kodi kubwa, watakwepa tu kulipa kodi hawa. Kile kinachotakiwa kipatikane hakitapatikana milele, watajaribu kutafuta mbinu za kukwepa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ni haya madeni ya Wazabuni na wafanyakazi. Serikali inapunguza *morally* ya wafanyakazi, deni la wafanyakazi linakaa tangu mwaka 2009 mpaka leo hawajalipwa. Amekwenda likizo, hakupewa kitu, matibabu halipwi, mambo mengine mengine, mshahara halipwi, *I mean* nyongeza ya mshahara wake hata kama cheo kimepanda, halipwi. Tutafika wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni watu, binadamu kama sisi; wana watoto, wana familia zao; wanahitaji kile wanachokitumia warudishiwe ili wapandishe *morally* ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Wazabuni. Serikali wakati mwingine imekuwa inacheza mchezo wa kitapeli. Wanawaita Wazabuni, wana- *supply* bidhaa na huduma, ikiwa umeshapita muda mrefu hawajawalipa, wanawakimbia, wanatafuta mzabuni mwingine, analetwa. Sasa yule umeshamuua! Wengine wanakwenda kukopa benki! Wanaweka *collateral* nyumba zao za kuishi wao na watoto wao, wanafilisiwa, kwa kuwa hawalipi benki. Kwa nini hawalipi? Serikali haiwalipi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo baya, siyo jambo la ubinadamu kabisa, Serikali inachangia kuleta umasikini wa hawa Wazabuni; watafanya nini? Wamekopa! *(Makofi)*

Hatimaye watoto wanaingia barabarani, wanakuwa ombaomba! Kwa nini? Wazazi wao wamefilisiwa na Serikali kwa kutokuwalipa, Benki imechukua nyumba, hawana pa kuishi. Siyo jambo jema.

Mheshimiwa Waziri, naomba uwekwe mkakati wa mahususi na muhimu; katika mwaka huu wa fedha, *quarter* ile ya mwanzo, uangazie jambo la mwanzo la kuwalipa Wazabuni na Wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *TBC* inaidai Serikali mabilioni ya fedha. Inapeleka matangazo yake, hawawalipi, halafu watu wanalalamika usikivu haupatikani. Watapata wapi? Mnajikopesha, mnajikopesha, hamwalipi! Walipeni mwone kweli kama *TBC* haitasikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KIDAWA HAMED SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kidawa Saleh, ahsante sana, nakushukuru sana. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, ajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini vilevile lazima tukubali kupanga ni kuchagua na kuchagua ni kupanga. Kwa maana hiyo, naungana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake wawili, kwamba hapo tulipofika, kwanza tutekeleze hayo na tusimamie hayo. Mara kwa mara tumekuwa sisi ni watu wa mipango mingi, lakini inapokuja kwenye utekelezaji tuna-*fail*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusizidishe zaidi ya hayo ambayo umeyaleta, tuhakikishe hayo mliyoyaleta leo, tunayasimamia hasa katika suala la ukusanyaji wa mapato, malengo yakamilike. Vilevile kusimamia matumizi kwa uadilifu mkubwa. Kwa maana hiyo, Mawaziri wote walioko hapo ni wapya, tuna imani na nyinyi, tunawategemea. Lakini ni lazima tuwe na uzalendo. Ukiona jambo limekuwa kubwa, labda kwa mashinikizo fulani, kama wewe ni mzalendo, una-*resign* mwenyewe, hata kama hujaona kosa lako. Siyo lazima watu waseme! Huo ni uzalendo kuonyesha *commitment* na mawazo yako kwa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumie suala la Serikali kuchelea kulipa madeni na hasa madeni ya Halmshauri, hasa kwa Mikoa inayotegemea *Cess* kwa maana ya Mkoa wa Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa. Halmashauri za Mikoa hii zinategemea *Cess* kwa kiwango kikubwa, lakini Serikali mpaka sasa inadaiwa karibu Shilingi bilioni 5.2 haijazipa Halmashauri. Maana yake mnaambukiza Halmashauri ziendelee kudhoofika, kutoka huku juu tudhoofike na kule chini wadhoofike, jambo ambalo siyo jema. Acheni tuwatafutie sababu nyingine, tusisaidie kuwadhoofisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Mkoa wa Rukwa peke yake unadai karibu Shilingi bilioni 1.8, ni fedha nyingi! Katika fedha hizo hizo, maana yake asilimia 20, ingepatikana, ingekwenda kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji, 5% ya akina mama na vijana. Kwa maana kama haijaenda, bado mnadhoofisha hata malengo yale wasiweze kufikia! Kwa hiyo, tunaishauri Serikali iweze kuchukua hatua za haraka kuhakikisha inalipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuiomba Serikali kuharakisha kupeleka umeme maeneo ambayo yana uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana na *nature* iliyoko katika maeneo yale. Kuacha kupeleka umeme mapema ni kuharibu vyanzo vya mapato, au ni kuharibu rasilimali au ni kubomoa uchimi wa nchi hii kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukanda wa Ziwa Rukwa, Ziwa Rukwa linaweza likakauka wakati wowote kwa sababu ya uharibifu wa mazingira. Mazingira yale yanatokana na *nature* yenyewe, limezungukwa na mlima, na mlima ule una miti. Wananchi wanatumia fursa hiyo kukata miti, kama kuni, kutengeneza mkaa. Sasa matokeo yake ziwa litakauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alione hilo. Mnapopanga jambo, mjaribu kuangalia na thari nyingine ambazo zinaweza kuwa kubwa zaidi kwa Taifa. Siyo kupeleka tu bora mnapeleka! Hebu jaribuni kuharakisha umeme katika ukanda wa Ziwa Rukwa kwa maana ya Kata za Mfinga, Mhuze, Mto Wisa, Milepa, Kaoze, Kipeta na Kijamatundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na ulipofika, hukufika katika maeneo yale. Hebu jaribu kwenda wewe mwenyewe, utavutika, utaona huruma, kwamba nchi hii inaharibiwa kutokana na mazingira.

Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwa Serikali kuharakisha umeme katika maeneo ambayo yana uharibifu mkubwa sana wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni soko la mazao. Wananchi wetu wamekuwa wakihangaika siku hadi siku, maana yake kutokaa na sababu hiyo, wamekuwa na utaratibu wa kubadilisha badilisha, leo alime mahindi, kesho alime alizeti, inabadilika bei, alime ufuta, bei inabadilika; yaani wanakuwa kigeugeu. Serikali inawayumbisha! Hakuna masimamo dhahiri wa kuwadhihirishia kwamba wanachokilima hiki, Serikali itanunua; jambo ambalo ni hatari! Wananchi wakimbilie wapi? *(Makofi)*

Kwa mfano, toka mwaka 2013 wananchi wamekuwa wakipiga kelele, wameshindwa pa kuuza mpunga, hata mwaka huu bado wanauza kwa bei ya hasara, lakini Serikali haijatamka inafanya nini? Mahindi vilevile toka mwaka 2013, mlinunua kiasi kidogo, hamkununua yote na mwaka huu mmerudisha lengo nyuma, badala ya tani 50 mmesema tani 40, maana yake mnataka kuendelea kuwasumbua wananchi. Hebu Serikali jaribuni kusimamia mambo ambayo ni ya msingi. Sisi tumesema kwamba katika nchi hii, sehemu kubwa ya Watanzania karibu asilimia 80 ni wakulima. Sasa hebu, pelekeni nguvu angalau katika eneo hilo kwa kiasi kikubwa, matokeo yatajionyesha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwabeba hawa watu, itaonekana kwamba Serikali imewajali na malalamiko yatapungua. Sehemu kubwa ya wananchi wako vijijini. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali, kama mnaamua kununua mazao, pelekeni fedha kulingana na makisio yaliyopo katika maeneo husika, kulingana na uzalishaji. Naishauri Serikali iweze kuliangalia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kulipa madeni ya wafanyabishara, mawakala na wasafirishaji. Hawa watu, vilevile ndio wanabeba watu wa chini katika kutoa ajira ndogo ndogo; na wanachukua mikopo benki. Ukiwasaidia hawa, maana yake umeshawabeba hata wale wa chini, kwa sababu hawa hawawezi kufanya kazi peke yao, lazima kuna watu nyuma; na watu ni wale watu wa chini, wakulima wadogo wadogo na vijana wetu ambao wanakuwa vijiweni, wanawabeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, usipowalipa hawa, umedhoofisha uchumi wa watu wengi, halafu mnawafanya hata wale ambao wamepiga hatua angalau kidogo, warudi nyuma tena, kuwa masikini, kwa kufilisiwa na mabenki.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Mawakala, hasa wa pembejeo, ma-*transporters*, waweze kulipwa na Serikali kadri inavyowezekana. Hii ni biashara bwana, tusiwacheleweshe! Unakaa mtu miezi sita, saba hujamlipa! Maana yake nini? Halafu mabenki yanachukua nyumba yake, na wewe Serikali sasa, hata unapolipa hutoi hata riba, unamwacha kama alivyo, kama siyo kudhoofisha wananchi wetu! Nilikuwa nashauri iweze kuliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Serikali kuchelewa kupeleka fedha za miradi katika Halmashauri zetu. Serikali imekuwa ikipanga yenyewe na Halmashauri zinapitishiwa bajeti yake. Cha ajabu, fedha haziendi. Kwa mfano, nichukulie msimu wa mwaka 2013/2014, nikichukulia mfano wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Sumbawanga, Serikali ilipitisha kwamba itapewa karibu Sh. 4,800,000,000/= lakini mpaka sasa, imepewa Sh. 1,700,000,000/=, sawa na asilimia 36. Sasa hivi mwaka unaisha, sasa sina hakika, zile nyingine zitapelekwa lini? Katika fedha hiyo hiyo, kuna miradi ya elimu, miradi ya afya, miradi ya umwagiliaji, miradi ya barabara na miradi ya maji. Kwa maana miradi ile imesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshangaa, siku moja Serikali ilisimama hapa ikatoa agizo kwamba kwa miradi yote, ambayo imepitishwa, hebu Halmashauri tangazeni kwa Wakandarasi. Halmashauri zimefanya hivyo, Wakandarasi wameanza kazi. Sasa cha ajabu, Halmashauri zimeshasimama, zinashangaa, nini kinatokea? Serikali ilishatoa tamko hapa, hebu pelekeni zile fedha haraka ili Halmashauri ziweze kumalizia ile miradi ambao imebakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, mimi nasisitiza bajeti hii ambayo Waziri wa Fedha ameleta na Manaibu wake, tuisimamie katika kukusanya mapato, tuisimamie kwa nidhamu ya hali ya juu katika matumizi.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: ahsante sana Mheshimiwa Agnas Aloyce Malocha kwa mchango wako. Mheshimiwa Sara Msafiri, mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti. Naomba kuungana na wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana na vilevile niwapongeze Manaibu Waziri wa Fedha wawili, kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana na kwa kuendelea kusisitiza kwamba Serikali lazima iangalie mapendekezo ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza kwanza Serikali kwa kutoa msamaha wa kodi kwenye ushuru wa forodha, hasa kwenye mashine za kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu jukumu la kukusanya kodi ni jukumu la Serikali, ndiyo inasimamia masuala ya ukusanyaji wa kodi, lakini tumeona kwamba hizi mashine za kielektroniki sasa wamepewa wajibu, jukumu, wafanyabishara wote, waweze kuzinunua na waweze kukusanya kodi. Kwa hiyo, naipongeza kwanza Serikali kwa kutoa ushuru huu wa forodha kwenye hizi mashine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee kuiomba Serikali tena, kwa sababu ndiyo jukumu lake la msingi la kukusanya kodi, ikae iangalie kwa njia yoyote ile kushusha gharama za hizi mashine ili kila mfanyabishara aone umuhimu wa kuwa na hii mashine na kuweza kusimamia kazi ya kukusanya kodi, ambayo kimsingi ni kazi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kupitia taarifa yake ya utekelezaji wa mipango, ambapo asilimia 92 ya miradi *ya Big Results Now* imetolewa fedha. Hii ni hatua nzuri sana kwa Serikali, kwamba vipaumbele vile tulivyotoa kwenye maji vijijini, elimu, nishati, uchukuzi na kilimo, fedha imetoka kwa asilimia 92.

Naiomba Serikali, mwaka huu wa fedha unaoanza, yasije yakatokea yale yaliyotokea kwenye mwaka uliokwisha. Fedha zipelekwe kwa wakati kwenye miradi ili kusaidia hii miradi iweze kutekelezeka kwa wakati. Wote ni mashahidi, fedha za maji, za umeme, zimetolewa kwenye kipindi hiki ambapo tunaanza bajeti, fedha za mwaka uliokwisha.

Kwa hiyo, napenda sana kuiomba Serikali ihakikishe kwamba, fedha zote zilizowekewa kipaumbele kwenye miradi, itoke kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukisoma taarifa ya Kamati ya Bajeti, unaona kwamba wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi, kilimo na ufugaji, ndiyo wananchi masikini kabisa kwenye nchi hii na kwenye Sekta ya Kilimo, ndiyo ya mwisho katika kukua kwenye pato la Taifa.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu, tunaposema kwamba uchumi unakua kwa asilimia saba, lazima tuangalie kwenye Sekta ya Kilimo, Sekta ya Uvuvi na Sekta ya Ufugaji

ambazo ndiyo asilimia 75 ya Watanzania wanafanya shughuli hizo, ili uchumi unapokua, tuone kwamba ina *reflection* ya wananchi na shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusijikite tu kwenye masuala ya masuala ya mawasiliano, huduma za fedha, ambazo sekta yote hii iko maeneo ya Mijini tu, ambapo wananchi wenyewe ambao ni asilimia 75 ya Watanzania huko vijijini, wanaofanya kazi za uvuvi, kilimo na ufugaji, uchumi wao ni wa chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua mpango wa dira ya mwaka 2025, kwamba, tutoke kwenye pato la chini, twende kwenye pato la kati. Hapa tunaongelea hawa Watanzania asilimia 75 ambao ni wakulima, wako vijijini. Sasa uchumi unaopaa Mijini tu, tutashindwa kufikia dira ya maendeleo ya 2025, tusipokuwa na mikakati ya pamoja ya kuhakikisha kwamba kilimo, uvuvi na ufugaji unakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti, tunaona kwamba kwenye vyanzo vya mapato ambavyo vimependekezwa, kwenye masuala ya uvuvi, tunapoteza fedha zaidi ya Shilingi bilioni 372, ambazo hizi ni fedha nyingi sana.

Kamati ya bajeti imejaribu kushauri mwaka jana na mwaka huu imeendelea kushauri, kwamba fedha hizi ni nyingi sana, kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kuwekeza kwenye Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nasema kwamba, kati ya sekta ambayo ni rahisi sana kwenye uvunaji na kupata fedha, ni Sekta ya Uvuvi. Kwa sababu ni suala la kuweka nyavu, kuvuta kokolo, unapata samaki unauza. Lakini nashangaa kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kuwekeza kwenye Sekta ya Uvuvi, na hapa ndiyo vijana watakapopata ajira.

Serikali inasema mpaka ijenge bandari, sijui ya uvuvi; mimi najiuliza, hawa wanaofanya *illegal business* kwenye biashara ya uvuvi, wao wanavuna tu, hawana bandari. Sasa Serikali wao mpaka wajenge Bandari ndiyo wavune, mimi naona kwamba hapa, lazima tukae tuangalie namna. Haiwezekani watu wavune samaki, wanavuna mazao baharini, halafu sisi tunasema mpaka Serikali ijenge bandari ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikubaliki! Hizi fedha ni nyingi sana! Watu wanafanya *illegal business,* wanavua, meli zinakamatwa, mbona hawana bandari? Kwa nini sisi mpaka tujenge! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna nia ya msingi kwenye kujenga bandari ya uvuvi, tunaona kuna bandari ya Dar es Salaam, na sasa tuna bandari ya Bagamoyo, kwa sababu ni kilomita chache kutoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo; kwa nini tusiamue kwa dhati sasa kwamba tuelekeze nguvu kwenye Bandari hiyo ya Uvuvi wanayoitaka Serikali, ili tupate hizi fedha? Kwa sababu ni kilomita chache sana ukiangalia bandari ya Dar es Salaam na Bagamoyo! Kwa hiyo, ni lazima tuangalie na vipaumbele vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee masuala ya ajira kwa vijana. Wenzangu wameongea sana, lakini mimi ni Mbunge wa Vijana lazima niongee zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali ni mbaya sana! Kama wanafunzi 20,000, wanakwenda kufanya *interview* ya nafasi 70, hapo kwa kweli lazima tukae tujiulize. Tuwe na mkakati wa kitaifa wa kusaidia vijana kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna Mfuko wa Vijana, lakini umetengewa Shilingi bilioni nne tu! Vijana ni asilimia 67 ya *population* ya Watanzania, ambayo ndiyo nguvukazi. Sasa tunatenga bilioni nne, lakini tunaona kwamba kuna *program* ya kukuza ajira kwa vijana,

kuwasaidia elimu za ujasiliamali, imetengewa Shilingi bilioni tatu. Hii fedha ni ndogo sana! Kwa sababu kila mwaka tuna vijana zaidi ya 40,000, hao ni ma-*graduates*, lakini tuna vijana wengi sana kwenye Vyuo hivi vya Ufundi vya kawaida na vijana waliojiajiri wenyewe ambao hawana elimu. Kwa hiyo, tukitegemea hii mifumo ya Shilingi bilioni nne, Shilingi bilion tatu, hatutaweza kuwasaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema mwaka 2013 na kwenye hotuba yake aliziagiza Halmashauri zote kupitia Wakuu wa Wilaya, kwamba watenge maeneo kwa ajili ya kilimo kwa vijana. Hili ni jambo jema, lakini lazima tuangalie namna, kama siyo kuwasaidia vitendea kazi hawa vijana, tusijikite kwenye fedha tu, tuangalie namna ya kuwapa vitendea kazi; Matrekta, pembejeo, tuwape zana za kilimo waweze kufanya kazi, kwa kuwakopesha kwa bei nafuu, kuliko kutenga Shilingi bilioni nne kwa vijana asilimia 67 ambao ni Watanzania wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali iwe na mikakati ya kudumu ya kuhakikisha kwamba vijana wanajikomboa kutoka kwenye wimbi la kutokuwa na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sara Msafiri.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwashukuru sana Waheshimiwa wote ambao mmepata nafasi ya kuchangia hotuba hizi mbili. Hotuba ya mipango na hotuba ya bajeti ya Taifa na tutaendelea na uchangiaji wetu kesho.

Kwa hatua hii kama tulivyokubaliana, ratiba yetu itakavyokuwa, basi naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.44 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 17 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)